Ufafanuzi Wa Agano Jipya

Tito - Yakobo

Na Dorothy Almond

mwisho na Askofu Francis Ntiruka

www.africanpastors.org

Ufafanuzi Wa
Agano Jipya

African Pastors Fellowship

Tito - Yakobo

Dorothy Almond

© African Pastors Fellowship 2010

Kimetolewa na:
AFRICAN PASTORS FELLOWSHIP
Station House, Station Approach, Adisham
Canterbury, Kent CT3 3JE
United Kingdom

www.africanpastors.org

WARAKA KWA TITO

YALIYOMO

UTANGULIZI

a) Sababu
b) Shabaha
c) Mwandishi

} Tazama utangulizi wa kitabucha 1 kwa Timotheo

d) Tarehe ya kuandikwa
Paulo alikuwa Rumi akitazamia kufa (2 Tim.4:6) naye alitaka Timotheo aje kwake bila kukawia kabla ya wakati wa baridi. (2 Tim.4:21). Tito alikuwa ameondoka Krete na kwenda Dalmatia.

UFAFANUZI

1: 1-4 Salaam
5-9 Sifa na tabia za Viongozi wa Kanisa
10-16 Maonyo juu ya Waalimu wa uongo

2: 1-10 Uchungaji wa watu wa marika mbalimbali
11-15 Neema ya Kristo yatawaelimisha katika maadili

3: 1-8 Wakristo waishije mbele ya watu wa nje?
9-11 Maonyo juu ya Waalimu wa uongo na mafundisho yao
12-15 Maagizo kwa Tito na Salaam za kuagana

U F A F A N U Z I

1:1-4 Salaam

Salaam hizo kwa Tito ni ndefu kuliko zile kwa Timotheo. Paulo alijiita “mtumwa wa Mungu”. Ni hapo tu Paulo alitumia maneno hayo. Katika Waraka kwa Warumi na Waraka kwa Wafilipi alijitaja “mtumwa wa Yesu Kristo”. Maana yake alikuwa amejitoa kabisa kuwa mali ya bwana wake Mungu bila kuwa na haki yoyote ya kuamua juu ya maisha yake mwenyewe. Alikuwa amejitoa kabisa kufanya mapenzi ya Mungu bila kujiwekea nafasi kwa mambo yake mwenyewe. Pamoja na hayo alijiita Mtume wa Yesu Kristo, maana yake hakujiweka mwenyewe na kukata shauri mwenyewe kuwa mtumishi wa Kristo, bali alichaguliwa na kutumwa na Yesu Kristo. Hivyo alishiriki mamlaka ya Yule aliyemtuma. Hilo lilikuwa neno kubwa kuhusu Waraka huo, Wakrete wafahamu kwamba mambo yaliyomo yaliandikwa kwa mamlaka ya KiMitume.

k.1b Alipotafakari juu ya Utume wake Paulo aliona kwamba yeye ni Mtume “kwa ajili ya imani ya wateule wa Mungu” kwa hiyo ilikuwa wajibu wake kuleta watu kumwamini Kristo ili wawe Watu wa Mungu, wateule wake kama Israeli ya Zamani walivyoteuliwa kuwa watu wake. Ni Mungu anayewachagua watu kuwa wake. Lugha hiyo ni ya Agano la Kale, pengine Paulo alitumia lugha hiyo kwa ajili ya wengine wa pale Krete waliokuwa Wayahudi kwa asili au waliokuwa na mtindo wa kuwaza kama Wayahudi (1:10,14; 3:8-9).

Pamoja na hayo Paulo alikuwa Mtume “kwa ajili ya ujuzi wa kweli (yaani Injili) iletayo utauwa”. Katika Utume wake apaswa kujenga imani ya watu katika Injili ambayo tunda lake ni maisha matakatifu. Ni ukumbusho kwamba Imani si masharti fulani ya kushikwa kichwani, bali hasa ni kujikabidhi kwake Kristo na kushirikiana naye kibinafsi na tokeo la ushirika huo wa kumjua Kristo ni kuishi maisha yampendezayo Mungu.

k.2 Ndipo Pauo aliendelea kwa maneno “katika tumaini la uzima wa milele”. Utume wa Paulo haukuhusu maisha ya hapa duniani tu bali ulijengwa juu ya tumaini la uzima wa milele. Msingi wa tumaini hilo ni katika Mungu asemaye kweli, Mungu asiyeweza kusema uongo, Mungu aliyetoa ahadi ya uzima wa milele, tena ahadi hiyo aliitoa hata kabla ya kuumbwa kwa kitu chochote. Mungu aliiamua katika mashauri yake ya umilele. Ndipo ahadi hiyo ilidhihirika kwa njia ya Injili kutangazwa. Kwa hiyo Mtume Paulo aliwekewa amana Ujumbe wa Injili, ulio na ahadi ya uzima wa milele ndani yake, tena aliwekewa kwa amri ya Mwokozi wetu Mungu.

Kwa nini Paulo alisema hayo yote na kutilia mkazo kuwekwa kwake “kwa amri ya Mwokozi wetu Mungu”. Sababu ni kwamba pale Krete walikuwa wametokea waalimu wa uongo, watu wasiotumwa na Mungu. Hao waalimu wa uongo walifundisha yasiyo kweli na mafundisho yao yalisababisha watu kuishi maisha yasiyompendeza Mungu.

“Mwokozi wetu Mungu” maneno hayo yaonyesha kwamba ni makusudi ya Mungu tangu milele kuwaokoa wanadamu, kama Paulo alivyomwandikia Timotheo “Mungu hutaka watu wote waokolewe na kupata kujua yaliyo kweli” (1 Tim.2:4).

k.4 Paulo alimwita Tito “mwanangu hasa katika imani tuishirikiyo”. Tito alikuwa Myunani, hakutahiriwa (Gal.2:3) tofauti na Timotheo ambaye baba yake alikuwa Myunani na mama yake alikuwa Myahudi (Mdo.16).

Wakati fulani baada ya Paulo kuokolewa Tito alikwenda pamoja naye mpaka Yerusalemu (Gal.2:3). Baadaye Paulo alimtuma Korintho wakati wa shida kubwa kutokea katika Kanisa la Korintho. Inaonekana Tito aliweza kutoa msaada kwao (2 Kor.2:13; 8:23; 12:18).

Katika safari zilizotajwa katika Matendo ya Mitume hatuna habari ya Paulo kuhubiri katika kisiwa cha Krete, ila inaonekana alipofunguliwa gerezani alielekea sehemu za Mashariki na kufika Krete pamoja na Tito. Katika Waraka kwa Tito picha ni kwamba baada ya kuhubiri na kupata waumini walio wenyeji Paulo aliondoka na kumwacha Tito pale. Kwa hiyo ni wazi kwamba Paulo alimthamini sana kama mjoli wa kazi za Injili, akimwita “mwanangu hasa”, wote wawili, Paulo Myahudi na Tito Myunani waliishiriki Imani moja pamoja na waumini wote wa kweli.

Kufunga salaam hizo ndefu Paulo alitumia salaam zake za kawaida, neema na amani.

1:5-9 Sifa na tabia za Viongozi wa Kanisa

Twajua Wakrete walikuwepo pale Yerusalemu Sikukuu ya Pentekoste Roho Mtakatifu aliposhuka kwa Mitume na wengine (Mdo.2:11). Paulo alikuwa pale kwa muda mfupi wakati wa safari yake kwenda Rumi kuhukumiwa, merikebu ilipigwa sana na dhoruba kali wakati wa kuizungukia pwani ya Krete. Hatujui kama wahubiri wengine walikuwa wamefika pale (Mdo.27:8ku.).

k.5 Inaonekana Paulo alifika pale pamoja na Tito baada ya kufunguliwa gerezani mara ya kwanza. Wenyeji wengi waliamini na Paulo alimwacha Tito pale ili alisaidie Kanisa la pale kuimarika kwa kuwekewa viongozi katika masharika ambao watawasaidia waumini wenzao katika Imani ya kweli. Kwa kulingana na Kanisa la Efeso Kanisa la Krete halikuwa na historia ndefu. Hivyo, ilikuwa kazi ya Tito kutengeneza yaliyopunguka, mambo ambayo Paulo hakuwa na nafasi ya kufanya, na hasa kuwaweka wazee katika kila mji.

k.6 Tukumbuke ya kuwa watu wa namna hiyo hawakupelekwa kusoma katika Chuo cha Theologia au Shule ya Biblia, kwa sababu hazikuwapo. Hasa walichaguliwa kufuatana na tabia zao nzuri. Kama ambavyo tuliona katika

Waraka kwa Timotheo (1 Tim.3: 2,7,10) yalimpasa mzee awe mtu asiyeshtakiwa neno, yaani awe amekubalika katika jamii ya watu kuwa mtu mwenye maisha safi. Hasa maisha ya nyumbani yalikuwa ishara thabiti ya uwezo wa mtu kuwaongoza wengine ikiwa kwanza alikuwa amefaulu kuongoza familia yake vizuri, hasa kwa kujitawala mwenyewe kwa kutulia na mke mmoja pamoja na kuwalea watoto katika imani ya kweli. Jirani na watu wa nje walifahamu vizuri jinsi alivyoishi nyumbani na kazini.

k.7 “askofu/mwangalizi” si wazi kama huyo alikuwa tofauti na wazee, yawezekana alikuwa mzee. Katika 1 Tim.3:2 na Tit.1:9 askofu ni mwalimu na katika 1 Tim.5:17 waalimu walikuwa wazee pia, ila huenda si wazee wote waliokuwa maaskofu. Hatujui ni wazee wangapi waliowekwa katika shirika moja lakini kufuatana na Flp.1:1 neno ni maaskofu kwa hiyo si vizuri kufikiri kwamba askofu alikuwa mmoja kati ya wazee wengi, ila baadaye katika karne ya pili ilitokea hivyo. Katika k.7 Paulo alitoa sababu ya askofu/mzee kuwa mtu asiyeshtakiwa neno. Hasa kwa sababu yeye ni wakili wa Mungu, kama maneja katika nyumba ya Mungu, nyumba ambayo ni mali ya Mungu, si mali ya Kanisa, wala yeye si mali ya Kanisa bali ni maneja aliyewekwa na Mungu.

Halafu Paulo aliendelea kutaja tabia zingine. “asiwe mtu wa kujipendeza nafsi yake” awe tayari kunyenyekea na kutumika badala ya kusukuma matakwa yake mwenyewe. “asiwe mwepesi wa hasira”, awe mpole, mwepesi wa kushauriwa na kusikiliza watu bila kukasirika ikiwa watu waliona tofauti na yeye. “asiwe mlevi wala mgomvi” Yawezekana hizo zilikuwa tabia za kawaida ya Wakrete wengi (Tito.1:10-12); watumishi wa Kikristo lazima waachane na tabia mbaya na kuwa tayari kutofautiana na wenzao.

“asiwe mpenda mapato ya aibu”; maaskofu/wazee lazima waepukane na jaribio la kutamani fedha kwa kazi zao, wasifuate mfano wa waalimu wa uongo waliotafuta kujifaidi, pengine kwa kutoza ada kwa mafundisho yao n.k.

k.8 Baada ya kutaja tabia zisizokubalika Paulo alitaja tabia zilizotakiwa. “awe mkaribishaje” mtu awe tayari kupokea watu nyumbani na kuangalia mahitaji ya watu. “mpenda mema, mwenye kiasi, mwenye haki, mtakatifu, mwenye kudhabiti nafsi yake” kwa jumla awe mtu aliyekaza nia yake kuishi maisha ya kumpendeza Mungu na kuwasaidia watu.

k.9 Kwa upande wa imani, askofu/mzee awe mtu wa kushikilia yale aliyofundishwa ili asiyumbishwe na waalimu wa uongo na mafundisho yao. Kwa njia hii atawasaidia wengine, ili hao nao wawe na msimamo mzuri. Awaonye na kuwarekibisha wale walioanza kuteleza na kuwashinda wapinzani wa Imani ya kweli. Kwa hiyo twaona ya kuwa waangalizi/wazee walipewa wajibu uliofanana na ule aliopewa Timotheo katika Waraka wa kwanza pia katika 2 Tim.4:2.

1:10-16 Maonyo juu ya waalimu wa uongo

Katika 1:5-9 Tito aliambiwa kuweka wazee/waangalizi waliostahili ili waonye watu kwa mafundisho yenye uzima na kuwashinda wenye kupinga.

Kuanzia k.10 twapewa maelezo zaidi juu ya hao wapinzani. Katika Nyaraka kwa Timotheo tulipata habari za watu wa namna hiyo kuwepo katika Kanisa la Efeso na hata kabla ya hapo Kanisa la Kolosai lilisumbuliwa na watu kama hao, kwa hiyo si jambo la pale Krete tu. (Kol.2:16-23).

Huko Krete inaonekana ni Wakristo wa Kiyahudi walioendesha upinzani huo - taz.k.10 - wale wa tohara na k.14-16 walitoa maagizo yao ya kibinadamu juu ya vitendo kadha vya dini, huenda miiko juu ya chakula kadha; pamoja na kufundisha hadithi zisizo za maana.

Katika sehemu hiyo Paulo alionyesha mzigo juu ya mambo mawili hasa; jambo moja lilihusu maisha na matendo yao mabaya, na jambo jingine lilikuwa mafundisho yao yasiyo sawa, yaliyosababisha maisha yao kuwa mabaya.

k.10 Hao wapinzani walikuwa wengi, nao hawakuwa tayari kukubali na kufuata mafundisho ya Kanisa. Walipenda kusemasema bila kutenda, na yale waliyosema yalikuwa upuuzi, hayakuwa na faida kwa wasikilizaji wao na kwa waumini. Kwa mafundisho yao waliwadanganya watu, huko wamedanganyika, kwa sababu hawakujitia chini ya kweli. Hasa walioleta shida walikuwa “wale wa tohara” kwa hiyo ni watu wa Kiyahudi.

Wajibu wa Tito ni “kuziba vinywa vyao” wasipate nafasi ya kusema na kufundisha mambo yao. Inaonekana Kanisa la pale Krete lilikuwa changa na bado halijakamilisha mipango yake na kwa sababu hiyo bila shaka mafundisho mengi yalitolewa na watu ambao hawakushika sawasawa Imani ya kweli, na kwa sababu mafundisho yalitolewa manyumbani ilikuwa vigumu kuwaangalia. Ndiyo sababu Paulo alimwagiza Timotheo kuchagua na kuweka wazee katika kila mji. Bila uangalizi wa kutosha hao watu walipata nafasi. Picha ni kwamba wamefaulu kukamata usikivu wa mtu mmoja mmoja katika nyumba ndipo kunasa nyumba nzima.

Kwa kuweka wazee wazuri, wenye uwezo wa kufundisha, hali hiyo itarekebishwa.

k.11 Waalimu wa uongo walilenga faida yao ya kimwili, hawakuwa na mzigo juu ya kweli, wala usafi wa maisha, wala Utukufu wa Mungu, walifanya kwa mapato tu. (k.7). “Mapato ya aibu” maana yake ni nini? ina maana kwamba ni aibu kutumia dini kuwa njia ya mapato.

k.12-13 Lakini hali ya hao watu ilifanana na tabia ya Wakrete kwa jumla. Walijulikana kuwa waongo, na wenye choyo, wavivu na wenye tamaa nyingi. Hata mwandishi wao mmoja aliandika hivyo. Huenda Paulo hakuwa na shabaha ya kuwalaumu Wakrete wote, ila hao wapinzani walifanana na baadhi yao, ni kama onyo kwa Tito ajue hilo. Paulo aliunga mkono mawazo ya huyo mwandishi. Kwa sababu Paulo aliingiza maneno hayo twaelekezwa kufikiri kwamba barua hiyo ni kwa Tito mwenyewe si barua ya kushirikishwa kwa waumini wote wa pale.

Tito aliambiwa na Paulo “uwakemee kwa ukali” Ni hapo tu Tito ameshauriwa kuchukua hatua juu ya waalimu wa uongo. Katika k.9 tumeona ni wazee/waangalizi waliopewa wajibu wa kuwaonya. Shabaha ya kuwakemea kwa ukali ni kuwafanya wajihoji na kujirekebisha ili wapate kuwa wazima katika Imani. Paulo hajakata tamaa juu yao. Kwa njia hiyo hata waumini wengine watasaidiwa na kujengwa kuwa thabiti katika Imani.

k.14 Hatua ya kwanza ni kwa hao watu kuacha kusikiliza hadithi za Kiyahudi (1 Tim.1:4; 4:7). Hatua ya pili wasiyapokee maagizo ya watu ambao wamekataa kuiamini Injili ambayo ni Habari Njema ya kuokolewa kwa neema si kwa sheria (Isa.29:13; Mk.7:7; Mt.15:9; Kol.2:22). Ni tabia ya wanadamu kutaka kufanya jambo na kuchanga kitu ili wapate wokovu, lakini katika kuokolewa bure, kwa neema, hali hiyo haina nafasi.

k.15-16 “maagizo ya watu” yalikuwa maagizo gani? Inaonekana yalihusu chakula, kwa maagizo hayo chakula fulani kilipigwa marufuku. (1 Tim.4:3; Kol.2:16-23). “vitu vyote ni safi kwa hao walio safi” Ndivyo alivyosema Paulo (Rum.14:20) akifuata mafundisho ya Bwana Yesu (Mk.7). Kwa sababu chakula kilicholiwa na mtu hakiwezi kumtia unajisi, hamna chakula chochote kilicho najisi. Imani katika Kristo hutakasa vyakula vyote. Kwa mawazo ya Kiyahudi mtu mnajisi hunajisi kila anachogusa, kwa hiyo waliweka “miiko” chakula kingine ili waulinde usafi wao. Kwa njia hiyo walijishuhudia kwamba wamepotoka katika mafundisho ya Injili kwa sababu hawamwamini Kristo wala hawakuweka tumaini lao Kwake. Shida yao si katika mambo ya nje kama chakula bali ni katika mambo ya ndani, katika akili na dhamiri zao. Kosa lao lilizidi kwa sababu walithubutu kuwafundisha wengine ubatili huo hata kuwaagiza juu ya chakula cha kula na kutokula n.k. Usafi wa kweli ni katika maisha ya kiroho.

k.16 Ndipo Paulo aliwashtaki kwamba iwapo walidai kuwa wanamjua Mungu, walimkana kwa matendo yao. Wayahudi walijivunia kwamba ni wao wanaomjua Mungu wa kweli, aliye Mmoja, tofauti na WaMataifa waliokuwa na miungu mingi. Kwa kudai kumjua Mungu walikuwa wakijitanguliza mbele kuwa viongozi waliostahili kuwasaidia wengine kumjua Mungu.

Lakini kweli iliyopo ni kwamba hawakumjua Mungu wala kweli zake na maisha yao yalithibitisha hayo. Paulo aliendelea kuwalaumu kuwa waasi na wenye machukizo, walimchukiza Mungu kwa kutii maagizo ya wanadamu na kutokutii maagizo ya Mungu. Kwa sababu hiyo hawakufaa kwa kila tendo jema, tofauti na Wakristo wa kweli waliompokea Yesu na wokovu wake na kuushuhudia wokovu wao kwa kutenda matendo mema (Efe.2:8-10).

2:1-10 <u>Uchungaji wa watu wa marika mbalimbali</u>
Ni vizuri kulinganisha na Waraka kwa Timotheo 1 Tim.5:1-2; 3:1-13; 2:9-15; 6:1-2.

k.1 Paulo alisema na Tito juu ya kutoa mwongozo wa maisha kwa waumini. Tofauti na hao waalimu wa uongo waliosemwa katika 1:1-16 yalimpasa Tito azungumzie mambo kuhusu mafundisho yenye uzima, yaani mafundisho ya kuleta afya ya kiroho na maisha mema, ili watu wenyewe waishi tofauti na waalimu wa uongo na wafuasi wao. Dawa kubwa ya kuutibu uongo ni kweli.

k.2 Wazee wa kiume
Hao wazee ni watu ambao kwa kuishi muda mrefu walikuwa wamejifunza mengi. Iliwapasa kuishi kwa busara na kwa kujiheshimu, na kwa kujitawala, hali wakitambua umuhimu wa kuishi kwa shabaha ya kumpendeza Mungu. Wawe watu waliohitimu maisha ya Kikristo wakiwa wazima katika mambo makuu ya Imani, katika upendo, subira na imani ili watoe kielelezo chema katika mashirika yao.

k.3 Wazee wa kike
Ni dhahiri kwamba hao walithamaniwa katika Kanisa, iliwapasa waishi kama watu waliojiweka wakfu kwa Mungu na kumtumikia katika maisha ya kila siku nyumbani. Wajihadhari na tabia ya kusengenya. Pia wasitumie mvinyo nyingi. Huenda pale Krete wanawake wengi walishikwa na tabia hizo mbaya. Wao wawe tofauti na hao.

Kazi yao moja ilikuwa kufundisha mema, siyo kusema kwamba walitoa mafundisho rasmi kanisani ila kwa kielelezo chao chema cha maisha ya nyumbani wengine waliweza kujifunza kwao. Hasa wakijihusisha na wanawake vijana na kuwasaidia.

k. 4-5 Wanawake vijana
Hao watajifunza mengi kutoka kwa wanawake wazee ili wawe na “akili” kuhusu maisha yao ya Kikristo. Neno kubwa la kwanza ni kuwapenda waume zao na watoto wao. Yawezekana katika nyumba zingine wale waalimu wa uongo walijiingiza na kuleta shida kati ya familia. Tena mwanamke kijana awe na kiasi, ajitawale maisha yake, asipelekwe huko na huko katika mawazo yake. Awe na maisha safi akiishi vizuri na mumewe bila kuwaka tamaa. Hasa watulie nyumbani wakitimiza wajibu zao kwa mume na watoto na kuwafanyia mema

jirani zao. Kwa njia hizo walitoa ushuhuda mzuri kwa wanawake wengine walioyumbayumba katika maisha yao wakijiingiza katika nyumba za watu (2 Tim.3:6). Kama ambavyo tumeona mara nyingi Paulo alikuwa na mzigo juu ya Injili na Wakristo kuwazwa vizuri na watu wa nje, kwa hiyo ilikuwa jambo muhimu kwa wanawake vijana kuishi vizuri kupatana na Imani yao ili Injili ieleweke vema katika jamii.

k. 6-8 Vijane Wanaume
Tito aliweza kujihusisha nao bila watu kumwonea mashaka. Badala ya kusema "fanya hivi, fanya hivi" Tito mwenyewe aliweza kutoa kielelezo kizuri kwao kwa matendo yake mema na kwa mafundisho aliyowafundisha. Wamwone Kristo na uwezo wake katika maisha ya Tito. Anapofundisha afanye kwa uzito wa hali na kwa kujimudu ili awavute kujali mafundisho yaliyotolewa. Mafundisho yenyewe ni mafundisho yaletayo afya rohoni, tena ni ya kweli, hayana makosa. Kwa maisha yake mazuri na kwa mafundisho yake mazuri aliyethubutu kupinga atasikia aibu kwa sababu atakosa kupata neno baya la kumshtaki Tito, hata Paulo, hata waumini. Daima macho ya watu huangalia Wakristo na mienendo yao wakitafuta kupata neno la kuwalaumu au kuwashtaki.

k.9-10 Watumwa
Walikuwepo watumwa wengi katika ulimwengu wa zamani. Katika hao wengi walivutwa kumwamini Kristo wakitumainishwa na upendo wa Kristo. Kanisa liliwapokea sawa na wengine wote, wakiwabatiza bila ubaguzi. Ila Kanisa halikuchukua hatua zozote za kuuondoa utumwa maana kwa wakati ule kufanya hivyo na kuleta mageuzi makubwa katika jamii fujo nyingi zingalitokea. Ila kwa mafundisho ya Kanisa juu ya usawa wa wanadamu wote mbele za Mungu, na usawa wao katika wokovu, ilitazamiwa kwamba polepole nafuu
itapatikana katika maisha ya watu. Huku watumwa wenyewe walifarijika kwa tazamio la uzima wa milele baada ya shida za hapo duniani.

Hatujui kama hao mabwana walikuwa Wakristo au siyo, ila watumwa wao waliwajibika kuwatii na kuwapendeza katika yote, wakiwatumikia kwa moyo mzuri iwapo maisha yao yalikuwa magumu, kwa neema ya Kristo waliwezeshwa kufanya hivyo. Tena iliwapasa wasihojiane nao, wala wasiibe vitu vya mabwana wao. Bila shaka mambo hayo mawili yalitajwa kama ni tabia ya kawaida ya watumwa wengi. Wawe waaminifu kikazi na kwa mali.

Lengo lilikuwa wayapambe mafundisho ya Kikristo na kuudhihirisha uzuri wake, ili Injili ipate sifa na kibali kati ya watu wa nje. Bila shaka mashauri hayo yote kuanzia neno kwa wazee yalilenga mapambo hayo.

2:11-15 Neema ya Kristo yatawaelimisha katika maadili
k.11 Neno "maana" mwanzoni mwa sehemu hii ni daraja kati ya yaliyotangulia na yanayofuata. Katika sehemu iliyotangulia Tito alitoa mwongozo kwa vikundi

mbalimbali katika mashirika ya Kikristo akimaliza na maneno “wayapambe mafundisho ya Mwokozi wetu Mungu katika mambo yote”(k9) Lakini haiwezekani mtu aishi Kikristo kwa nguvu yake mwenyewe, maadili yamefungamana kabisa na Imani ya kweli. Imani na maadili huenda pamoja kama mizizi na matunda ya mti. Kwa sababu hiyo katika k.11 Paulo alisema neema imefunuliwa, neema iwaokoayo wanadamu wote. Nje ya neema ya Mungu hamna wokovu, hakuna mwanadamu awaye yote atakayepona na dhambi bila neema hiyo. Na wokovu huo ni kwa wote, yaani kwa kila aina ya watu, watumwa kwa wahuru, waume kwa wake, Wayahudi kwa WaMataifa, matajiri kwa maskini n.k. Ndiyo sababu Paulo alitaka Wakristo “wayapambe” mafundisho ya kweli, ya wokovu, ya Mwokozi wetu Mungu k.9 ili maisha yao yawe na uvutiko mkali kwa watu wa nje. Ni kuendeleza mafundisho ya Paulo katika 1 Tim.2:3-6 “Mungu hutaka watu wote waokolewe”.

k.12 Ni neema hii inayotufundisha namna ya kuishi. Watu wa Mungu waishije? Wapaswa kusema “la” kwa mabaya, yaani maasi (neno ni sawa na lile la Rum.1:18) na kwa tamaa za dunia kwa sababu Kristo ametukomboa na maasi yote (k.14).
Pamoja na kusema “la” Wakristo wapaswa kusema “ndiyo” kwa maisha ya kiasi, ya kujitawala, na kwa kufanya iliyo sawa na kumcha Mungu katika ulimwengu huu wa sasa, kwa sababu Kristo alitukomboa ili ajisafishie watu wawe milki yake k.14.

k.13 Iwapo Wakristo wanaishi katika ulimwengu huu wa sasa, matazamio yao ni katika ulimwengu ujao, wakingojea jambo kubwa sana, kule Kufunuliwa kwa Yesu Kristo katika utukufu wa ajabu. Ataonekana kama alivyo, Mungu Mkuu na Mwokozi. Tumaini hilo limejaa baraka nyingi kwa waumini. Ni hapo tu Yesu Kristo ameitwa Mungu Mkuu. Kwa sababu ya tumaini hilo Wakristo hupenda sana kujiandaa kwa kuishi maisha mema na kufanya mapenzi ya Mungu.

k.14 Ndipo Paulo alisema neno juu ya wokovu akitaja jinsi wokovu ulivyopatikana kwa njia ya Yesu Kristo kutoa nafsi yake pale Msalabani. Twakumbushwa maneno ya Marko 10:45 juu ya Yesu kuwa fidia. Yesu alijitoa kufa kwa ajili yetu kwa sababu gani? Kwanza, ili “atukomboe na maasi yote”(Gal.1:4) na ndiyo sababu twaitwa kukataa maasi na tamaa za dunia hii. Pili, ili tuwe watu wake, mali yake safi, tuliotakaswa na damu yake ili tutende mema kwa moyo wa kutaka na kwa bidii (Efe.2:8-10). Matendo mema ni itikio lifaalo kwa neema ya Mungu iliyofunuliwa katika Kuja kwake Yesu Kristo na Kufa Kwake. Yesu hutaka kumiliki maisha yetu, tu tunu yake ya kazi ya ukombozi wake.

k.15 Paulo alimsihi Tito anene mambo hayo na kuyasema wazi, akiwaonya na kuwasihi wengine na kuwakaripia wengine walio wakaidi. Afanye kwa mamlaka kwa sababu Tito ni mshiriki wa Paulo na mamlaka yake ya KiMitume.

“asikudharau mtu awaye yote” maneno hayo yafanana na 1 Tim.4:12 bila maneno ya “ujana wako”, kwa hiyo, inaonekana Tito alizidi Timotheo kwa umri.

3:1-8 Wakristo waishije mbele ya watu wa nje?

Katika Waraka huo Paulo alikuwa amekaza sana wajibu wa Wakristo kutenda matendo mema. Katika sehemu hiyo aliendelea na hoja hiyo akiwaza uhusiano wao na watawala na viongozi katika jamii.

k.1 “uwakumbushe” Paulo alitazamia ya kuwa waumini wa Krete wamekwisha kuelewa wajibu wao. Kwanza iliwapasa kunyenyekea na kuwatii wale waliokuwa na mamlaka katika miji na katika serikali. Kwa tabia yao Wakrete walikuwa wakaidi na wabishi na Paulo aliogopa kwamba huenda hata Wakristo watavutwa kupinga wenye mamlaka. (1 Tim.2:2).

Pamoja na kuwa watiifu wawe tayari kufanya kila kazi njema, wajihusishe na maisha na mahitaji ya watu nje ya Kanisa.

k.2 Halafu Tito awakumbushe wasiwe watu wa kuwatukana na kugombana na watu, afadhali wawe wafadhili na wapole, na wenye adabu kwa watu wote. Ilihitaji neema nyingi kutokusema neno baya juu ya mtu na kuwa na tabia hizo njema hasa tukikumbuka jinsi Paulo alivyosema juu ya Wakrete na tabia yao (Tit.1:12). Kwa kusema “wote” inaonekana Paulo alifikiri kwamba kwa matendo yao mema na tabia zao njema watavuta wengi kumwamini Kristo.

k:3 “sisi nasi” Hapo Paulo alijiunga na waumini wengine wote na kukiri kwamba kabla ya kumwamini Kristo walikuwa wajinga, yaani walikosa ufahamu wa kiroho, walikuwa waasi, watu wasiomtii Mungu, watu waliodanganywa, walitawaliwa na tamaa na anasa za dunia hii, watu ambao hawakupenda jirani zao, walioshindwa kuishi nao vizuri - kwa jumla, walikuwa wenye dhambi. Kwa orodha ya madhambi hayo Paulo alikuwa akifafanua ANGUKO LA WANADAMU ambalo yeye pamoja nao, pamoja na wanadamu wote hulishiriki (Rum.1:29-31, Gal.5:19-21; Efe. 4:17-24; 1 Kor.6:9-11).

k.4-7 Jibu la Mungu kwa Anguko hilo la wanadamu na kwa madhambi yao lilikuwa kumtuma Yesu Kristo kwa kusudi la kuwaokoa, ishara thabiti ya Wema na Upendo wa Mungu kwa wanadamu wote. Walipompokea Kristo na wokovu wake walioshwa dhambi zao, ubatizo ukiwa ishara yake, walizaliwa kwa pili, kwa Roho Mtakatifu aliyewabadili na kuwafanya upya kwa ndani. (Yoh.3:1ku. 2 Kor.5:17). Hayo yote yalitokana na rehema za Mungu, wala hayakutegemea matendo yao mazuri. Walihesabiwa haki, yaani walivikwa haki ya Kristo, huko Kristo alivikwa dhambi zao Msalabani na kufa kwa ajili yake. Walipatanishwa na kusamehewa dhambi zao na kwa njia hiyo waliletwa katika uhusiano mwema na Mungu, wakiishi katika tumaini la uzima wa milele. Kwa kifupi twaweza kujumlisha hivi: Twaoshwa dhambi zetu, na kusamehewa.

Twahuishwa na kupewa uzima wa Mungu na kushirikiana kibinafsi na Kristo aliye Hai. Twashirikishwa Roho Mtakatifu na uwezo wake, tena bila kipimo, kwa wingi wa ukarimu wake. Twafanywa kuwa watoto wa Mungu watakaorithi uzima wa milele (Gal.4:4-7; Rum.8:14ku.).

k.8 Mambo hayo ni “neno la kuaminiwa” maneno hayo tumeisha kukuta katika 1 Tim.1:15; 3:1; 4:9; 2 Tim.2:11. Mambo hayo ni mazuri yenye faida kwa wanadamu. Kwa hiyo Paulo alimsisitiza Tito awakumbushe waumini wa pale Krete waendelee kutenda mema kama itikio lifaalo kwa tendo kuu la Mungu katika kuwaokoa. Kwa maneno hayo Paulo alikuwa akiyaelekeza mawazo yao kujua kwa hakika kwamba Mungu aweza kubadili maisha ya Wakrete wengine, ili wavute watu kuamini.

3:9-11 Maonyo juu ya Waalimu wa uongo na mafundisho yao

Halafu Paulo alisema tena kwa Tito juu ya waalimu wa uongo na mafundisho yao (Tito 1:10-16). Budi ajitenge mbali na mafundisho yao kwa sababu yalikuwa bure, yaliamsha maswali yasiyo na maana wala faida (ling. k.8 juu ya mafundisho ya faida). Yalisababisha magomvi na mashindano juu ya sheria. Hayo yote yalikuwa tofauti na Injili, mafundisho yenye uzima, iliyoleta amani na ufahamu mzuri na faida kwa roho na maisha ya watu.

k.10 Mzushi, neno hilo wakati ule lilitumika kueleza mtu aliyeleta mafarakano katika watu na kusababisha vikundi kutokea. (Baadaye neno hilo lilitumika kueleza mtu aliyeamini mafundisho yasiyokubalika kuwa sawa). Paulo alisema kwamba mzushi aliyepotoka aonywe ili ajirekebishe, akikosa kujirekebisha aonywe kwa mara ya pili. Bila shaka kwa kutoa nafasi mbili ilitazamiwa kwamba wengine watakubali kujirekebisha. Kama mtu ataendelea kukataa, basi, wajitenge naye, kwa kuwa mwenyewe amejishuhudia ukaidi wake.

3:12-15 Maagizo kwa Tito na Salaam za kuagana

k.12 Paulo alimwomba Tito afanye bidii kuja kwake mara baada ya kuipokea barua hiyo. Atamkuta Nikapoli kwa sababu Paulo alitazamia kufika pale na kukaa pale wakati wa baridi, bila shaka kwa sababu ya ugumu wa usafiri. Kwa hiyo ni wazi kwamba Paulo alikuwa bado angali katika nchi za mashariki.
Paulo alikuwa hajakata shauri juu ya nani atakayemshikia Tito pale Krete. Yawezekana itakuwa Artema, mtu asiyetajwa mahali pengine katika Agano Jipya; Kama si yeye itakuwa Tikiko ambaye ametajwa katika Mdo.20:4 Kol.4:7; Efe.6:21. Kutokana na 2 Tim.4:10 twajua kwamba baadaye Paulo alimtuma Tikiko Efeso ili amshikie Timotheo. Tukumbuke ya kuwa Paulo alikuwa hajakamatwa bado kwa mara ya pili, na Waraka kwa Tito uliandikwa kabla ya Waraka wa Pili kwa Timotheo. Pia twajua kwamba Tito alitumwa Dalmatia, sehemu iliyo kaskazini ya Nikapoli (2 Tim.4:10) kwa hiyo inaonekana ni Artema aliyekwenda Krete.

k.13 Inaonekana Zena na Apolo walikuwa pamoja na Paulo na alipofahamu watasafiri mpaka Krete alituma Waraka huo kwa mikono yao. Paulo alimkumbusha Tito wajibu wake wa Kikristo kuwatunza hao wawili vizuri na kuwapatia mahitaji yao ya kusafiri mbele. (Mdo.15:3; 21:5; Rum.15:24; 1Kor.16:6,11; 2 Kor.1:16; 3 Yoh.6).

Hatuna habari juu ya Zena ila kama huyo Apolo ni yule aliyetajwa katika Mdo.18:24ku. 1 Kor.1:12; 3:4ku. 16:12 basi tunazo habari nyingi juu yake.

k.14 “watu wetu nao wajifunze kudumu katika matendo mema, kwa matumizi yaliyo lazima”. Inaonekana maneno hayo ni kwa Wakristo wa Krete juu ya kuwatunza Zena na Apolo, ili wawe tayari kuwapokea na kuwasafirisha vizuri watakapoondoka. Shabaha ni “wasiwe hawana matunda”. Kwao ilikuwa njia ya kuzaa matunda. Twazaa matunda tunapowahudumia wengine mahitaji yao. Katika Waraka huo mkazo umekuwa juu ya waumini kutenda matendo mema (1:16; 2:7,14; 3:1,8).

k.15 Salaam za mwisho kwa Tito zilitoka kwa Paulo na wale wote waliokuwa pamoja naye. Wakati mwingine Paulo alijumlisha watu katika salaam zake kama alivyofanya hapa 1 Kor.16:20; 2 Kor.13:2; Flp.4:22. Wakati mwingine alitaja mmoja mmoja Rum. 16:21-23; Kol.4:10-14. Halafu Paulo alimwambia Tito awasalimie “wale watupendao katika Imani”. Kwa kuandika hivi ni kama Paulo amedokezea kwamba baadhi ya Wakristo wa Krete hawakuwa waaminifu kwake wala kwa Injili yake.

Kisha alifunga na baraka ya “neema na iwe pamoja nanyi nyote”.

MASWALI

Kwa sababu Waraka kwa Tito unafanana sana na Nyaraka za Timotheo nimeweka swali moja tu.

1. *Twawezaje kuyapamba mafundisho ya Mwokozi wetu Mungu?*

WARAKA KWA FILEMONI

YALIYOMO

UTANGULIZI

UFAFANUZI

1 1- 3 Salaam za Paulo
4- 7 Shukrani
8-14 Uhusiano wa Paulo na Onesimo
15-22 Ombi la Paulo kwa Filemoni
Ombi la kumwekea mahali tayari
23-25 Salaam za kuagana

UTANGULIZI

Waraka huu ni mfupi sana, una sura moja tu. Ni barua nzuri sana, imejaa upendo na neema. Yahusu watu watatu tu, Paulo mwandishi, aliyefungwa huko Rumi; Filemoni Mkristo mmoja wa Kanisa la Kolosai; na Onesimo, mtumwa wake aliyemtoroka na kwenda Rumi. Kwa hiyo ni barua ya kibinafsi kwa mtu binafsi.

UFAFANUZI

k.1-3 Salaam za Paulo
Paulo hakutaja Utume wake katika Waraka huo mfupi, kwa sababu ilikuwa barua ya kibinafsi kwa mtu mmoja Filemoni. Alimwandikia kama rafiki aliyetaka afanyiwe fadhili fulani. Alisema ni "mfungwa wa Yesu Kristo" mtu aliyeonja dhiki na mateso katika kumtumikia Kristo. Timotheo alikuwa pamoja naye wakati wa kuandika, alituma salaam zake.

Filemoni ni Mkristo, na inaonekana kwa maneno ya k.19b ni Paulo aliyemvuta kwa Kristo. Aliishi Kolosai na Wakristo walikutanika katika nyumba yake. Ni mtu aliyewasaidia Wakristo wenzake k.7b. Huenda Afia alikuwa mke wake na labda Arkipo alikuwa mwana wao, ila hatujui kuwa uhakika. Inaonekana alikuwa mhudumu katika shirika la Laodikia, mji uliokuwa karibu sana na Kolosai (Kol.4:16-17). Paulo aliweka pamoja Filemoni na Arkipo na kuwaita wajoli wake katika kazi ya Bwana, akitumia maneno "mpendwa wetu, mtenda kazi pamoja nasi" kwa Filemoni, na "askari mwenzetu" kwa Arkipo, neno

"askari" haina maana ya askari wa jeshi. Neema na amani ni baraka kubwa sana katika maisha ya Mkristo na daima Paulo alipenda kuzitaja katika salaam zake.

k.4-7 Shukrani
Paulo alimshukuru Mungu kwa ajili ya Filemoni na wenzake, akiwaombea kila wakati. Bila shaka alipokuwa kifungoni mawazo yake yalizungukia makanisa aliyoyapanda kila mahali, akiwafahamu waamini walioko katika kila shirika na kuwaombea mmoja mmoja. Alitambua uwezo mkuu wa Mungu katika kuwatunza hali wamezungukwa na umati wa watu wasioamini.

k.5: Filemoni alikuwa Mkristo safi aliyejulikana kwa imani yake na upendo wake kwa Kristo na kwa Wakristo wenzake.

k.6: Paulo aliomba kwamba hiyo imani ya Filemoni iliyotokeza upendo kwa Bwana na kwa watu wake iendelee kufanya kazi, ikue ili apate kujua zaidi na zaidi baraka za Mungu katika kutenda mema, ili azidi kumwamini Kristo na kumtii.

k.7: Paulo alifurahi sana kwa kuwa waamini waliburudishwa kwa msaada wa Filemoni, bila shaka kielelezo chake kiliwatia moyo, hata Paulo alisikia kufarajika kwa habari zake. Aliona ni ndugu yake hasa (k.16, 20).

k.8-14 Uhusiano wa Paulo na Onesimo
Kwanza twaona Paulo alimwita Onesimo "mtoto wangu niliyemzaa katika vifungo vyangu" Ni ajabu kuona Paulo akimwita hivyo. Kwa kweli neema ya Mungu ilikuwa imembadili sana. Zamani alikuwa Myahudi wa dhehebu la KiFarisayo, mwenye kujaa kiburi na majivuno na hapo alimwita Onesimo aliye Mmataifa, mtumwa, na mtu mbaya "mtoto wangu" (k.10) na "moyo wangu hasa" (k.12b). Katika Kol.3:11 aliandika "hapakuwa Myahudi wala Myunani, kutahiriwa wala kutokutahiriwa, mgeni wala mshenzi, mtumwa wala mwungwana, bali Kristo ni yote na katika yote". Maneno hayo hayakuwa maneno tu, yalifunulia moyo wake wa ndani. Aliishi kama alivyoamini.

Onesimo alimtoroka Filemoni akasafiri mpaka Rumi. Hatujui sababu zilizomfanya atoroke, labda alimwibia vitu fulani (k.18) au labda alitamani kuwa huru akifikiri ataweza kujificha katika Jiji kubwa la Rumi. Ilikuwa hatari sana kufanya alivyofanya kwa sababu katika siku zile watumwa walihesabiwa kama vyombo mikononi mwa mabwana wao walioweza kuwafanyia ukatili, kuwapiga sana, hata kuwachoma alama ya kuonyesha kwamba ni watoro, hata kuwaua. Hatujui ni kwa njia gani alipata kumfikia Paulo kifungoni, labda alianza kujuta na alifahamu kwamba Paulo alifahamiana na bwana wake Filemoni aliye Mkristo.

Twajua kwamba Onesimo alisaidiwa sana na Paulo, halafu akakaa naye kifungoni na kumhudumia kwa mahitaji yake. Paulo alimpenda sana na alitaka aendelee kukaa naye akisema "maana ni moyo wangu hasa" (k.12).

Lakini haikuwezekana Paulo aendelee kupokea huduma ya Onesimo, kwa sababu hakuwa wake, alikuwa mali ya Filemoni, na huyo Filemoni alikuwa ndugu mpendwa katika Kristo, atawezaje kumficha habari hizo? Ila swali kubwa ni "Filemoni atampokeaje?" Paulo alijua kwamba angaliweza kutumia mamlaka yake ya KiMitume na kumwagiza ampokee vizuri. Ila alichagua kumsihi kwa upendo akichochea huruma zake kwa kumkumbusha kwamba yeye ni mzee, tena ni mfungwa. Neno "mzee" laweza kubeba maana ya mjumbe (Efe.6:20; 2 Kor.5:20).

Paulo alionyesha unyenyekevu mkubwa, akitegemea shauri la Filemoni, kwa sababu alitaka Filemoni ampokee Onesimo kwa hiari na kwa furaha ili wema wake udhihirike wazi.

Jina "Onesimo" lilikuwa na maana "afaaye" na Paulo alisema kwamba zamani Onesimo "hakufaa" ili sasa ametimiza maana ya jina lake "bali sasa" badiliko limetokea katika moyo wa Onesimo. Alimfaa Paulo sana, pia atakapomrudia Filemoni atamfaa sana kwa kumtumikia kama mtumwa wake, ila tangu hapo atamtumikia kwa moyo na bidii (Kol.3:22-25). Kwake Paulo alikuwa "mwana" na kwake Filemoni "ndugu mpendwa katika Kristo".

Ni wazi kwamba ilimgharimia Paulo kumrudisha Onesimo ni kama alikuwa akituma sehemu ya nafsi yake mwenyewe. Paulo alidokezea kwamba kama Onesimo angalikaa angalikuwa badala ya Filemoni, kwa maana hata Filemoni alikuwa na deni kwa Paulo - deni la kiroho kwa baraka zote za rohoni alizozipata kutokana na huduma ya Paulo. Paulo hakuona ni vizuri yeye mwenyewe aamue kufuata jinsi alivyosikia bali afuate iliyo haki na halali. Filemoni akate shauri, kwa hiari.

k.15-22 Ombi la Paulo kwa Filemoni

k.15: Hapo Paulo aligusa jambo la Onesimo kurudi kwa bwana wake Filemoni. Paulo alitumia busara akisema "labda ndiyo sababu...." Aliona kwamba Mungu aliongoza mambo hayo yote. Iwapo Onesimo alitoroka kwa mapenzi yake mwenyewe Paulo alisema "alitengwa nawe kwa muda" kumbe Mungu alikuwa katika jambo hilo la ukaidi wa Onesimo. Kwa kimwili haikuonekana kuwa hivyo lakini kwa mawazo ya kiroho ndivyo ilivyokuwa, kwa sababu sasa watakuwa pamoja hata katika umilele.

k.16: Filemoni alikuwa amepotewa na mtumwa wake, ila sasa atampokea kama "ndugu mpendwa" kweli ataendelea kuwa mtumwa wake ila ataishi naye si kama mtumwa. Hatatendewa kama mtumwa na zaidi atampenda. Onesimo ni ndugu mpendwa wa Paulo na sasa ni zaidi kwa Filemoni. Kwa hiyo, hatua

kwa hatua Paulo alitayarisha mawazo ya Filemoni kumpokea kama ndugu mpendwa sana "katika mwili" katika uhusiano wa kibinadamu na "katika Bwana" katika uhusiano wa kiroho.

k.17-19: Hapo Paulo alitaja ombi lake waziwazi. Kama Filemoni na yeye ni washiriki kweli wa Imani basi Filemoni "ampokee Onesimo kama yeye mwenyewe". Paulo alijua kwamba Filemoni alikuwa amepata hasara, huenda alitoroka na mali, na ilikuwa haki apate kurudishiwa hasara hiyo. Paulo alijitoa kufanya hivyo "mimi nitalipa", ndipo alilinganisha deni hilo la Onesimo kwa Filemoni na deni la Filemoni kwake. Deni si la fedha au mali, bali ni deni la kiroho, kwa sababu kwa njia ya Paulo Filemoni alisikia Habari Njema ya Wokovu na kumpokea Kristo, kipawa cha thamani mno.

k.20: Kisha Paulo alitaja kitu alichotafuta hasa. Ikiwa Filemoni atampokea Onesimo kwa mikono miwili, kwa hiari yake na kwa furaha, basi Paulo alihesabu itakuwa faida katika Bwana, ataona Bwana amefanya kazi kwelikweli katika maisha ya Filemoni, na ataburudishwa katika Kristo, bila shaka atazidi kuona faida ya kufanya kazi ya Bwana potelea mbali amefungwa kwa ajili hiyo.

k.21: Paulo alitazamia kwamba Filemoni atamtii, hata kuzidi alivyomwambia. Afanye nini zaidi? huenda atampa Onesimo uhuru wake. Labda atamruhusu kukaa na Paulo. Ni vizuri kuweka lengo la juu mbele ya Wakristo.

k.22. Paulo alitazamia kufunguliwa na kusafiri mpaka Kolosai na kukaa na Filemoni. Ilikuwa kawaida ya siku zile kwa watu kupokea wageni bila shida yoyote.

k.23-25 Salaam za kuagana
Alituma salaama za Epafra aliyefungwa pamoja naye. Pia aliwataja Marko, Aristarko, Dema na Luka na kutuma salaam zao. Inaonekana walikuwa pamoja naye pale Rumi. Kisha akaufunga Waraka na "neema ya Bwana Yesu Kristo" akisema "roho zenu" Ni kwa Filemoni na wenzake. Kwa hiyo Paulo alikuwa na nia ya Kanisa la pale kushirikishwa barua hiyo iliyomhusu Filemoni kibinafsi.

MASWALI:

1. *Umejifunza nini kutokana na Waraka huo mfupi?*

WARAKA KWA WAEBRANIA

YALIYOMO

UTANGULIZI

(a) Mwandishi
(b) Walioandikiwa
(c) Tarehe ya kuandikwa
(d) Shabaha
(e) Mtindo

UFAFANUZI

1: 1-4 Mungu amesema neno lake la mwisho kwa njia ya Yesu Kristo
5-14 Yesu ni bora kuliko malaika

2: 1- 4 Hatari ya kutokumjali Mwana
5-9 Yesu atatukuzwa juu ya vyote
10-13 Kristo – kiongozi mkuu
14-18 Yesu – Kuhani wetu mkuu mwenye rehema

3: 1-6 Yesu ni mkuu kuliko Musa
7-19 Shauri na onyo juu ya kuwa waaminifu hadi mwisho

4: 1-16 Yesu ni mkuu kuliko Yoshua
1-11 Ipo ahadi ya raha
12-13 Uwezo wa Neno la Mungu
14-16 Yesu Kuhani Mkuu kuliko Haruni

5: 1-10 Sifa za Kuhani Mkuu
11-14 Ulegevu wa wale walioandikiwa

6: 1-8 Tatizo na hatari ya kutokukua kiroho na ya kuasi
9-12 Tumaini la mambo kuwa mazuri
13-20 Ahadi za Mungu ni imari na za kutegemewa kabisa

7: 1-28 Bwana Yesu ni Kuhani Mkuu kwa mfano wa Melkizedeki
1-10 Melkizedeki na Ibrahimu
11-25 Kristo na Haruni
26-28 Yesu – Kuhani Mkuu, Mtakatifu, Afaaye kabisa

8: 1-9:28 UBORA WA HUDUMA YA KRISTO

8: 1-6 Ubora wa Huduma ya Kristo
7-13 Yesu na Agano Jipya – Agano bora

9: 1-10 Maelezo ya Mahali Patakatifu na Huduma ya Makuhani
11-22 Uwezo mkuu wa Sadaka ya Kristo katika kutakasa
23-28 Sadaka ya Kristo ni ya namna pekee

10: 1-10 Kristo aliitoa dhabihu ya nafsi yake kwa hiari
11-18 Utimilifu na ukamilifu wa dhabihu ya Kristo
19-25 Faraja
26-31 Onyo kali
32-39 Mwito wa kuenenda kwa ushujaa

11: 1-40 Imani – mashujaa wa imani
1-3 Imani ni nini hasa?
4- 7 Imani ya Habili, Henoko, Nuhu
8-19 Imani ya Ibrahimu
20-22 Imani ya Isaka, Yakobo, Yusufu
23-29 Imani ya Musa
30-31 Imani ya Yoshua, Rahabu
32-40 Majumlisho ya Imani ya wengine na dhiki zitokanazo na imani

12: 1- 2 Kielezo chema cha imani ya Yesu
3-13 Marudi ya Baba kwa watoto wake
14-17 Maonyo juu ya kuikataa neema ya Mungu
18-29 Hofu iliyoandama na kutolewa kwa Agano la Kale na furaha ya Agano Jipya

13: 1- 6 Wito wa kuishi kwa upendano wa ndugu, usafi wa maisha, na kuridhika
7,17,24 Mashauri kuhusu viongozi
8-16 Imani ikazwe kwa Bwana Yesu, neema yake, na kudumu kwake
18,19,23 Mambo ya kuombewa
20-21 Baraka ya kuagana
22,24,25 Maneno ya kuufunga Waraka

UTANGULIZI

(a) Mwandishi

Mwandishi hakujitambulisha wala hatambuliki kwa hakika kwa mambo yaliyomo. Katika nakala zote za zamani hakuna jina. Hata hivyo, wasomaji wake walimfahamu, na wao wenyewe walikuwa kundi la waumini walioishi mahali fulani. Mwanzoni mwa barua hakuna salaam kutoka kwa mwandishi wala salaam kwa wale walioandikiwa. Ndani ya Waraka zimo ujumbe na salaam chache. Kwa hiyo, watu wamewaza watu mbalimbali kuwa mwandishi.

Kwa muda, Paulo alifikiriwa kuwa mwandishi, iwapo hakujitaja katika Waraka. Eusebio, mwandishi wa historia ya Kanisa aliandika kwamba Klementi wa Iskanderia alisema kwamba Paulo aliuandika kwa Kiebrania na Luka aliutafsiri kwa Kiyunani. Origen, mwandishi wa Kikristo katika karne ya tatu, aliutumia Waraka kana kwamba Paulo alikuwa mwandishi akisema kwamba kwa jumla Kanisa liliupokea kama ni wa Paulo ila kwa upande wake alikiri kwamba kama Kanisa limeupokea hivi ni vema, kwa sababu watu wa zamani wasingalisema hivi bila sababu, lakini kwa upande wake alikiri kwamba hakujua ni nani hasa aliye mwandishi, ila ni Mungu peke yake ambaye alijua. Lugha ya Waraka na mtindo wake sio wa Paulo kwa kulinganisha na maandishi yake mengine. Kiyunani cha Waraka ni safi sana. Kulibandikia jina la Paulo kulisaidia upokezi wake wa kuwekwa kwake katika Kanuni ya Vitabu vilivyokubalika kuwa Maandiko Matakatifu.

Mwandishi alijiweka katika jamii ya waumini wa kizazi cha pili walioipokea Injili kutoka kwa wale ambao walikuwa wamewajua waumini wa kwanza. Jambo hilo ni kinyume cha madai ya Paulo ya kuwa yeye aliipokea Injili moja kwa moja kwa ufunuo wa Yesu Kristo, wala si kwa mwanadamu awaye yote (Gal.1:11ku).

Kabla ya kuendelea ni vema kuona ni sifa gani zinazotakiwa kwa mtu kuwa mwandishi wa Waraka huo. Twajua mambo fulani juu yake kutoka Waraka wenyewe.

Tunajua alitoka katika jamii wa waumini wa kizazi cha pili ambao walipata kujua Injili kutoka wale walioipata kwa waumini wa kwanza waliomfahamu Bwana na kuwa mashahidi wa maisha yake. Pia walijaliwa kufanya miujiza na ishara kwa uwezo wa Roho Mtakatifu (Ebr.2:3-4). Pia alikuwa na mwelekeo wa kuwa mwalimu wa kufundisha maisha ya Kikristo na kujua sana Agano la Kale akilitumia tafsiri la Kiyunani lililoitwa Septuajinta. Alitumia Kiyunani safi. Alikuwa na moyo sana juu ya Imani ya Kikristo na alikuwa na mzigo juu ya wale waliotoka katika Imani ya Kiyahudi, ambao kwa ajili ya shida walizokuwa wakizipata walitaka kurudi nyuma. Hakuogopa majadiliano, ila majadiliano yake yalilenga kuwajenga waumini wa Kiyahudi katika imani ya Kikristo, na wakati wote aliweka onyo, au maneno ya kuwatia moyo, au kemeo katikati ya hoja

zake, kwa sababu alitambua kwamba ni muhimu kwa Mkristo kuyaweka mafundisho ya Kikristo katika maisha ya kila siku ili yasibaki mafundisho tu, wala yasiwe jambo la kichwa tu. Alijua habari za Timotheo (13:23) aliyekuwa angali hai na alimtaja Paulo. Yawezekana alikuwa amefungwa gerezani au alipona ugonjwa mkali (13:19).

Basi, kama mwandishi hakuwa Paulo, yupo nani ambaye alikuwa na sifa kama hizo za hapo juu, ambaye aliweza kuwa mwandishi? Majina mbalimbali yametolewa. Mmoja aliyependekezwa sana ni Barnaba. Tertullian alisema ni Barnaba. Twajua alikuwa rafiki na mfanyakazi pamoja na Paulo na Timotheo, ambao wote wawili wametajwa katika Waraka. Alikuwa Mlawi, kwa hiyo alijua sana Agano la Kale na mipango ya dhabihu, ibada, n.k. Alitoka Kipro, mahali pa kutumika Kiyunani safi. Waraka umeitwa „Neno la Faraja/Maonyo"; Barnaba pia aliitwa „Mwana wa Faraja" (Mdo.4:36; Ebr.13:22). Alipenda sana kuwafundisha Wakristo na alikuwa na kipawa cha kujihusisha vema na waumini wa Kiyahudi na Wayunani. Alifanya kazi sana na Paulo na wote wawili walikaa muda mrefu katika Kanisa la Antiokia wakiwafundisha waumini wapya (Mdo.11:23; 13:1).

Mwingine aliyependekezwa kuwa mwandishi ni Apollo, mtaalamu wa Agano la Kale, ambaye alipenda sana kulitumia katika kufundisha habari za Kristo. Alikuwa Mkristo wa Kiyahudi aliyetoka Iskanderia, halafu akaenda Efeso, ndipo akatumika katika Kanisa la Korintho na kudumu muda mrefu katika utumishi (1 Kor.3:4ku. Mdo.18:24ku. Tit.3:13). Ila jina lake halikupendekezwa mpaka baadaye sana.

Pamoja na hao, wengine ambao wamependekeza ni Sila, pia Petro, Aquila na hasa mkewe Priska.

Iliyopo ni kwamba hakuna jina moja ambalo limesimama peke yake na kudumu. Origen, baba mmoja wa Kanisa wa karne ya tatu alisema hivi „ni Mungu peke yake anayejua kwa hakika" na ni vema sisi nasi tuunge mkono maneno yake.

Jambo kubwa ni kwamba, ijapokuwa hatujui kwa hakika ni nani aliyeuandika Waraka huo, tunao uhakika wa umuhimu wa Waraka huo katika kuwekwa kwake katika Kanuni ya Vitabu vya Maandiko Matakatifu. Mafundisho yake ni mazuri sana, mtungo wake na mpango wake unaleta mwanga mkubwa juu ya upekee na ubora wa Yesu Kristo. Hoja ya mwandishi ndiyo hiyo, ya Yesu kuwa bora kabisa na kazi yake, cheo chake, na mambo yake yote kuwa bora kuliko yote ya dini ya Kiyahudi.

(b) Walioandikiwa

Waraka unaanza bila salaam kwa hiyo ni vigumu kujua kwa hakika ni akina nani walioandikiwa. Hata hivyo, kwa mambo yaliyomo, twaelekezwa kufikiri kwamba ni Wakristo wa Kiyahudi, waliokuwa kundi fulani au shirika fulani mahali fulani. Walijulikana kwa mwandishi aliyewapenda na kuwafahamu na kujua hali zao. Kwa sababu Waraka umejaa mambo ya Agano la Kale, hasa mipango ya ibada na desturi za dini ya Kiyahudi, mambo ya Ukuhani, dhabihu, n.k. yafikiriwa kwamba walikuwa waumini wenye asili ya Kiyahudi ambao kabla ya kuwa Wakristo waliabudu kwa desturi ya Kiyahudi. Mwandishi hataji desturi za kipagani. Alifuata mtindo wa Kiyahudi kwa jinsi alivyopanga hoja na majadiliano yake, iwapo aliandika kwa Kiyunani safi, maandishi yake yamekolea hali ya Kiyahudi.

Hao walioandikiwa waliishi wapi? Mawazo mbalimbali yametolewa. Wazo moja ni Yerusalemu au Palestina; wazo lingine ni Iskanderia, na lingine ni karibu na Kolosai katika Bonde la Lika katika jimbo la Asia, maana mengine yaliyotajwa yafanana na mambo yaliyomo katika Waraka kwa Wakolosai, pia Timotheo na Paulo wametajwa.

Wazo lingine lenye nguvu ni kwamba waliishi Italia. Sababu moja ya kufikiri hivi ni kwamba Klementi wa Rumi, mwandishi wa Kikristo aliishi pale na mwaka kama B.K.95 aliwaandikia Wakorintho barua na katika barua hiyo alidondoa mengi kutoka Waraka huo kwa Waebrania kana kwamba alikuwa na Waraka mbele yake alipokuwa akiandika. Katika 13:24 twakuta maneno „hao walio Italia wanawasalimu", maana yake, ama mwandishi yupo Italia naye anatoa salaam za watu walio pamoja naye; ama yupo mahali pengine na wako pamoja naye watu wa Italia ambao walijiunga naye katika kupeleka salaam.

Katika Warumi 16:5,14,15 tuna habari ya vikundi vitatu vya Wakristo waliokutana katika nyumba za wenzao. Yawezekana ni mojawapo wa vikundi hivi walioandikiwa.

Timotheo ametajwa (13:23) na tunajua kwamba Timotheo alihusika na Paulo wakati wa Paulo kufungwa Rumi na yawezekana Timotheo alikuwa amefungwa Rumi pia.

Kwa kujumlisha twaweza kusema kwamba wale walioandikiwa walikuwa Wakristo wa Kiyahudi waliopata imani yao ya Kikristo kutoka wale waliofundishwa na waumini wa kwanza kabisa waliomfahama Bwana Yesu. Wamekuwa Wakristo kwa muda mrefu (5:12) walikuwa wameokoka kweli, wamepewa nuru na kukionja kipawa cha mbinguni na kufanywa washirika wa Roho Mtakatifu na kulionja neno uri la Mungu n.k. (6:4,5; 10:32; 26-29). Baada ya kuongoka kwao walikuwa wamepita katika mateso makali wakinyanganywa mali zao na kuwa vichekesho kwa watu na hayo yote waliyapokea kwa furaha, nao waliwahurumia wafungwa (10:32-34). Viongozi wao wa kwanza walikuwa

wamekufa (13:7). Ila wakati huo wa Waraka kuandikwa hao waumini wamepoa kiroho, wamesimama bila kuendelea katika imani yao, badala ya kuwa waalimu kwa waumini wapya wao wenyewe walihitaji kufundishwa tena (5:11,12) ni kama wamekataa kuchukua shutumu kwa ajili ya Kristo, hawakuwa tayari kuachana na mambo ya Kiyahudi, hata walielekea kurudi kwenye imani yao ya kwanza ya Kiyahudi. Baadhi wameacha kukutana na wenzao (10:25). Pengine walikata tamaa walipoona shida zao zinaendelea, na kuona mateso yanawakabili tena, na Bwana Yesu hajarudi kama alivyoahidi. Kwa maneno ya 12:6;16; 13:4,5 inaonekana baadhi yao, huenda wachache, hawakuwa waaminifu katika ndoa, walikuwa na choyo, na walipenda mambo ya dunia kuliko mambo ya Mungu.

Kuna watu wanaofikiri kwamba tunayo mahubiri yaliyotolewa kwa kundi fulani na baadaye yalitumiwa kwa kundi lingine ambalo hali yao ilifanana na wale wa kwanza. Wafikiri hivyo kwa sababu neno „kusema" limetumiwa mara kwa mara – 2:5; 6:9; na 11:32. Kisha yaliwekwa katika hali ya Waraka kama tulio nao sasa.

(c) Tarehe ya kuandikwa

Hapo tena mawazo mbalimbali yametolewa. Kwa sababu hekalu la pale Yerusalemu halikutajwa yadhaniwa kwamba lilikuwa lingalipo na kwa sababu lilibomolewa B.K.70 tarehe iwe kabla ya B.K.7O. Timotheo alikuwa angali hai. Mwandishi ameandika kama mipango na ibada za Kiyahudi zilikuwa zikiendelea kama kawaida, na mambo hayo yote yalitoweka hekalu lilipobomolewa. Yawezekana mateso yanayotajwa ni yale yaliyotokea wakati wa Kaisari Nero B.K.64. Twaelekezwa kuwaza wakati kuwa kile cha kizazi cha pili cha waumini (k.2:3b). Mawazo ya wengi ni kwamba Waraka uliandikwa kati ya B.K.65-68.

Kama hekalu lilikuwa limeisha kubomolewa mwandishi asingalikuwa na kazi kubwa ya kuonyesha jinsi ya mipango ya dini ya Kiyahudi imekwisha, kwa sababu, kihistoria ndivyo ilivyokuwa baada ya B.K.70.

(d) Shabaha

Kama ambavyo tumeishataja, kufuatana na hali ya hao Wakristo walioandikiwa mwandishi alitaka kuwatia moyo na kuwaita kuvumilia, pamoja na kuwaonya juu ya hatari ya kurudi nyuma na kuacha imani ya Kikristo. Alilenga kuwajenga katika Imani yao kwa kuwaonyesha Ubora na Ukuu na Upekee wa Yesu Kristo na kuondoa mashaka yao juu ya Yesu kuwa Mwana wa Mungu. Waraka umejaa mashauri yaliyo kama dawa ya kuzitibu shida zao. (Taz,3:6,14; 4:14; 10:23 kuhusu kushika sana imani yao; 5:12; 10:36; 12:1 kuhusu kuvumilia kwa subira; na hitaji lao la kuwa na imani ili wawe na uhakika wa uzima ya milele 4:2,3; 6:12; 10:22:39; sura nzima ya 11 na 13:7)

(e) Mtindo
Mwandishi alipenda sana kufanya ulinganifu kati ya dini ya Kiyahudi na imani ya Kikristo. Alimlinganisha Yesu na malaika, na Musa; alilinganisha Ukuhani wa Bwana Yesu na ukuhani wa akina Haruni n.k. Alilinganisha dhabihu ya Yesu na dhabihu za wanyama zilizotolewa, n.k. Alipenda sana kutumia neno „ bora". Alijenga jambo moja juu ya lingine katika kushuhudia ubora wa Imani ya Kikristo na kuthibitisha kwamba dini ya Kikristo ni kamili na ya mwisho, hakuna neno lo lote la kuongezewa, kwa sababu Yesu ni Neno la mwisho, na kwa njia yake Mungu amejifunua kwa ukamilifu. Yesu ameangaza utukufu wa Mungu na kuzidhihirisha tabia zake njema. Kwa hiyo haiwaziki kwamba mtu aweza kumwacha Kristo na kurudia kwenye Uyahudi wake.

Katika Waraka huo tunayo mafundisho makubwa juu ya Yesu kuwa Kuhani wetu Mkuu na juu ya Ukuhani wake bora, na kiini cha Waraka ni sura za saba hadi kumi. Mwandishi ametilia mkazo juu ya Yesu kutimiza Sikukuu ya Upatanisha na kwa kifo chake kufanya Upatanisho Kamili kati ya Mungu na wanadamu, na kutokana na upatanisho huo njia iko wazi kwa mtu ye yote kumkaribia Mungu wakati wo wote na mahali po pote mradi anategemea hiyo kazi aliyofanya Yesu alipokufa Msalabani (4:16; 6:19,20; 7:25; 10:22; 12:22- 24).

UFAFANUZI

1: 1-4 Mungu amesema neno lake la mwisho kwa njia ya Yesu Kristo
Kama ambavyo tuliona katika Utangulizi mwandishi hakujitambulisha kwa wasomaji wake wale hakusema alikuwa akiwaandikia akina nani na mahali pao.

k. 1-2a Yesu ni mkuu kuliko manabii
Alianza mara moja kwa kumtaja Mungu na jinsi alivyojihusisha na taifa la Wayahudi hapo nyuma. Alisemaje? Alisema kwamba „Mungu alisema zamani na baba zetu". Kwa maneno hayo alionyesha kwamba upo uhusiano wa kweli kati ya ufunuo kwa baba zao na ufunuo ulioletwa na Yesu Kristo.
Ufunuo huo ulikuwaje? Ulikuwa kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi. Kwa maneno hayo twakumbuka huduma za malaika, torati, ndoto, viongozi kama akina Musa na Yoshua, matukio mbalimbali, makuhani na manabii, mipango ya ibada na dhabihu, katika zaburi n.k. Kwa njia hizo zote Mungu alisema akisema na Taifa lake.

Lakini ufunuo huo, ambao ulikuwa ufunuo halisi uliotoka kwa Mungu, ulikuwa „wa sehemu" na kwa „njia", kwa kadiri walivyoweza kuupokea. Kila sehemu na kila njia ilitoka kwa Mungu, nayo ilikuwa kweli na kufaa kwa wakati wake na katika mahali pake, na kila jambo liliwasaidia watu wa Mungu. Hakuna kosa

wala hakuna wazo la kufikiri kwamba sehemu au njia fulani haikuwa kweli, lakini ufunuo huo ulikuwa wa sehemu nyingi na kwa njia nyingi wala haukufikia upeo wa yote ambayo Mungu alitaka kusema nao, hata ikiwa yalijumlishwa pamoja hayakutosha kutoa ufunuo mtimilifu. Ulikuwa wa muda tu, mpaka uje ule ufunuo kamili, kwa hiyo, hayo yote *yalilenga* ule ufunuo kamili ulioletwa na Yesu Kristo. Ndipo twasoma „mwisho wa siku hizi Mungu amesema na sisi katika Mwana". Maana yake, Mwana ndiye kiini cha yote. Yeye amenafisisha ufunuo wa manabii n.k. wao walisema maneno, ila Mwana amesema kwa nafsi yake, kwa kuwa alikuwa Mungu aliyefanyika mwanadamu (1:2,3,5,8; 3:6; 4:14; 5:8; 7:3,18). Katika Yesu Kristo Mungu amejifunua kwa ukamilifu na utimilifu, ni Neno lake la mwisho, hana la kusema zaidi kwa wanadamu. Katika Yesu Kristo, wanadamu wamepewa yote wanayohitaji kwa kumjua na kumkaribia Mungu kwa njia ya upatanisho alioufanya Kristo, kusudi waishi maisha ya kumpendeza Mungu, yaani maisha matakatifu. Ijapokuwa Mungu hana la kusema zaidi, ila wanadamu, kwa upande wao, bado hawajaelewa huo ufunuo kwa ukamilifu. Hakuna neno lo lote la kuongeza kama fundisho jipya au ufunuo mpya, iliyobaki ni kwa wanadamu kuzidi kuufahamu huo ufunuo na kuuitikia jinsi iwapasavyo. „mwisho wa siku hizi" ni tangu Kristo kuja kwa mara ya kwanza mpaka sasa hadi atakaporudi (9:28; Mt,13:16-17). Yesu bado hajashika utawala juu ya ulimwengu wote. Atakaporudi ndipo ataushika usukani na kuwa Mfalme wa Wafalme na Bwana wa Mabwana na wakati huo falme za dunia hiyo zitawekwa kuwa Ufalme wake (Ufu.11:15).

Katika kusema na wanadamu kwa njia ya Kristo Mungu aliziba ufa mkubwa katika mawasiliano kati ya Yeye aliye Mtakatifu na wanadamu wenye dhambi. Upo uhusiano mkubwa kati ya Agano la Kale na Agano Jipya ambalo ni mwendelezo na matimizo ya Agano la Kale. Hakuna kukatika kati yao.

Bila shaka Mungu alisema na watu wa Mataifa mengine kwa njia nyingine, hasa katika uumbaji na dhamiri zao, ila hakujifunua kwao kama alivyojifunua kwa Taifa lake (Taz. Mdo.14:16,17: 17:23-31).

k. 2b-4 Sifa kuu za Mwana
Katika vifungu hivi tunazo sifa kuu za Mwana zinazomfanya awe amestahili kuwa „ufunuo kamili wa Mungu".

Sifa ya kwanza ni *„aliyemweka mrithi wa yote"* na *sifa ya pili* inayoandamana na hiyo ya kwanza ni *„kwa yeye aliufanya ulimwengu*".
Ni lini Yesu alipowekwa kuwa mrithi wa yote? Yawezekana ni wakati alipopaa na kuketi mkono wa kuume wa Mungu hali ameishafanya ukombozi wa ulimwengu. Au yawezekana aliwekwa mrithi wakati ule ule wa uamuzi kufanywa wa ulimwengu kuumbwa kwa njia yake, yaani, hata kabla ya yote kufanyika. Amekuwa mrithi kwa sababu yote yamefanyika kwa njia yake. „wa yote" ni nini hasa? Yafikiriwa kuwa uumbaji mzima na ndani yake mataifa yote (Zab.2:8) pamoja ya nyakati zote na ulimwengu katika hatua zake zote.

Yohana aliandika „vyote vilifanyika kwa huyo; wala pasipo yeye hakikufanyika cho chote kilichofanyika" (Yn.1:3). Pia katika Kol.1:16 twasoma „Kwa kuwa katika yeye vitu vyote viliumbwa, vilivyo mbinguni na vilivyo juu ya nchi, vinavyoonekana na visivyoonekana; ikiwa ni viti vya enzi, au usultani, au enzi, au mamlaka; vitu vyote viliumbwa kwa njia yake na kwa ajili yake". Hivyo Yesu ni mwanzo na mwisho wa uumbaji, atayarithi yote *aliyoyafanya*. Katika kuhojiana na Wayahudi Yesu alisema „Amin, amin, nawaambia, Yeye Ibrahimu asijakuwako, mimi niko" (Yn.8:58). Maneno hayo yalikuwa makubwa kwa Wayahudi waliomthamini sana Ibrahimu, baba wa taifa lao aliyeitwa na Mungu, kwa hiyo, dai hilo la Yesu lilikuwa dai kubwa sana. Yeye Mwana huitawala mienendo yote ya historia ya wanadamu, akiiongoza kwa mapenzi yake. Alipofanyika mwanadamu aliudai urithi wake (Mt.21:37ku. Ufu.11:15). Alikuwa muumba katika hatua zote zilizopita, hadi sasa, hata mpaka mwisho. Kwa hiyo, uhusiano wa Yesu na uumbaji ni katika kuwa Muumba, na Mhifadhi, na Mrithi wake.

k.3a Katika kifungu hicho tunazo sifa nyingine za Mwana. *Sifa ya tatu ni „kuwa mng"ao wa utukufu wake na chapa ya nafsi yake".* Maana yake ni kwamba katika Mwana utukufu wa Mungu uliangaza na kuonekana. Utukufu huo ni nini hasa? Ni utukufu wa tabia njema za Mungu, upendo na utakatifu wake, utu wema, haki na rehema zake. Hizo zote ziliangazwa katika maisha ya Yesu na hasa pale Msalabani, mahali pa kukutana kwa tabia hizo (Yn.17:1,4,5). Utukufu wa Mungu umetajwa katika Agano la Kale, kuhusu Kuwako Kwake, kama wakati wa Kutolewa kwa Torati penye Mlima Sinai. Pia kuhusu Ibada na mahali pake penye Hema ya Kukutania (Kut.24:15-17; 33:18-23; Law.9:5-6, 23). Yesu ni „utukufu wa Mungu" kimwili. *„chapa ya nafsi yake"* maana yake ni kwamba katika Yesu Mungu amedhihirishwa kwa ukamilifu, Mungi ni kama Yesu alivyomwonyesha, Yesu ni chapa yake, ni chapa halisi. Ni ukumbusho wa maneno ya Yesu kwa swali la Filipo „Bwana, utuonyeshe Baba" na Yesu alisema „Aliyeniona mimi amemwona Baba;"..."mimi ni ndani ya Baba na Baba yu ndani yangu" (Yn.14:8-10). Mfano ni mmoja, sura ni moja, ni mfano halisi na sura halisi, hamna tofauti isipokuwa katika Yesu kufanyika mwili. Kwa hali zote na tabia zote na mapenzi yote ni mamoja. Kwa hiyo, Mungu alifunuliwa kwa ukamilifu katika Yesu Kristo, Mwana wake. „Mimi na Baba tu umoja" (Yn.10:30; Yn.1:3; Kol.1;15,16; 2 Kor.4:4; Flp.2:6). Katika asili yake alikuwa Mungu kweli, ndipo alipofanyika mwili aliuangaza utukufu wa Mungu hali akiwa mwanadamu halisi.

k.3b *Sifa ya nne ni „akivichukua vyote kwa amri ya uweza wake"* maana yake ni kwamba Yeye Mwana ndiye yule anayeendeleza uumbaji wote uendelee katika mwenendo wake na katika kufuata sheria zake, akifanya hayo kwa amri yake kutokana na uwezo wake wa kuyatekeleza yote anayoamua juu yake. Kwa hiyo, sayari zote, jua na mwezi, bahari na vyote vilivyomo, milima na mabonde, miti na maua na ardhi na kila kitu vinaendeshwa na huyo Mwana. Ina maana kwamba zaidi ya kuubeba uumbaji anauendeleza na kuushikamanisha

(Kol.1:17) ondoa Yeye na yote huanguka na kuachana. Kwa hiyo, ulimwengu haukuumbwa halafu ukaachwa ujiendesha mwenyewe, kama saa iliyotiwa ufunguo halafu iachwe kuendelea peke yake. Kadiri ufahamu na ujuzi wetu juu ya uumbaji unavyokuwa na kwa kutokea kwa habari mpya zinazofunua maajabu ya uumbaji, ndipo twazidi kuutambua uwezo na ukuu na utukufu wa Mungu. Kutokana na jitahada za wanasayansi na wachunguzi wa mambo hayo, nyota mpya, sayari, na vitu vingi vinagunduliwa, twazidi kustaajabia sana uwezo, uadhama, na hekima ya Muumba wake. Kwa hiyo, uumbaji wote huongozwa hadi utakapoufikia mwisho wake katika mbingu mpya na dunia mpya. Wanasayansi, kutokana na shughuli zao za kutafuta majibu kuhusu jinsi vitu vilivyotengezwa na vilipata kuwepo n.k. hujikuta kwamba kwa kadiri wanavyoyapata majibu, ndipo maswali mengine huzuka, wala hamna mwisho katika utafiti wao.

k.3c *Sifa ya tano ni „akiisha kufanya utakaso wa dhambi"* Hapo tuna sifa juu ya kazi kubwa ya maana sana Yesu aliyoifanya alipokufa Msalabani, kazi ya kuwakomboa wenye dhambi, akizibeba dhambi na hatia na hukumu ya dhambi katika mwili wake (1 Pet. 1:18ku. 2:24; 3:18). Tuone ya kwamba hiyo kazi imeishafanyika „akiisha kufanya". Kazi nyingine, kama kuvichukua vyote kwa uweza wake, ni kazi zinazoendelea, ila hiyo ya kufanya utakaso ilifanyika mara moja tu, Yesu aliposulibiwa. Kazi hiyo haina haja ya kurudiwarudiwa. Katika kufanya utakaso Yesu alionyesha „utukufu wa upendo ulio tayari kuteswa na kuumizwa" kama tulivyoona hapo nyuma (Yn.17:1ku). Alifanya kwa moyo mkuu na kwa kujitoa kabisa na kwa kumwaga damu ya uhai wake. Kwa kazi hiyo ya ukombozi aliwaleta wanadamu kwa Mungu na kuwapasulia njia ya kumkaribia Mungu bila hofu, wala wasiwasi, wala kizuizi cho chote. Ilikuwapo njia moja tu ya kutatua tatizo kubwa la kutisha la „dhambi" na njia hiyo ilikuwa Kifo cha upatanisho cha Bwana Yesu. Yesu alistahili kufanya hiyo kazi ya utakaso kwa sababu ya uhusiano wake na Baba na uhusiano wake na uumbaji.

k.3d *Sifa ya sita* inayofuata ile ya kufanya utakaso ni „*aliketi mkono wa kuume wa Ukuu huko juu"*. Maneno „aliketi mkono.." yanaonesha kwamba kazi yake ya ukombozi ilitimizwa nayo ikakubalika na Baba kuwa dhabihi itoshayo kwa dhambi za ulimwengu wote. Katika Hema ya kukutania hakikuwepo kiti ili kuhani apumzike, jambo lililoashiria kwamba kazi zake hazikuisha. Dhabihu baada ya dhabihu ilitakiwa kutolewa, maana dhabihu zilizotolewa zilituliza tu, ila hakuziondoa dhambi. Zilikuwa za muda tu hadi Kuja kwa Kristo na kutolewa kwa dhabihu kamili. Jambo hilo lazungumziwa zaidi katika sura za baadaye. Kutokana na kazi hiyo kubwa Yesu amepewa heshima ya juu kabisa ipitayo heshima zote. (Flp.2:9ku. Efe,2:20,21; Zab.110; Lk.22:69).

Kwa hiyo, katika utangulizi huo mfupi Yesu ameonyeshwa kuwa Nabii kabisa, aliye mwenye mali yote na mrithi wa yote; Muumba asiyeumbwa, mwenye sura na chapa halisi ya Mungu; mwenye kuuendesha uumbaji mzima. Pia, Yesu ni Kuhani aliyetoa dhabihu itakasayo dhambi zote, na kuwa mshindi ashikaye

mahali pa heshima kuu juu ya uumbaji wake wote. Kutoka utangulizi huo unaomwadhimisha Yesu, mwandishi anaendelea kwa kuonyesha ukuu wake juu ya majina yote yenye heshima katika mawazo na maisha na utendaji katika dini ya Kiyahudi. Kuanzia 1:4-2:18 anamlinganisha Yesu na malaika na kuonyesha jinsi Yesu anavyowazidi kwa kila hali na kila jambo.

k.4 Kifungu hicho ni kama daraja ya kuunganisha sifa za „Mwana" na ushuhuda wa Maandiko unaoonyesha ubora na ukuu wa „Mwana" kwa kumlinganisha na malaika. Kabla ya kuendelea ni vema kutazama mafundisho ya Biblia juu ya malaika. Hao malaika ni nini hasa? Neno lenyewe lina maana ya „mjumbe". Wametajwa katika Agano la Kale na Agano Jipya. Inaonekana wako malaika wema na wako malaika wabaya, walioanguka. Walimtokea Ibrahimu na Sarai na kuwapa ahadi ya kumzaa mwana katika uzee wao, halafu wakati ule waliendelea na kumwokoa Lutu mikononi mwa watu wa Sodoma na Gomora kabla ya miji hiyo kuangamizwa (Mwa.18 na 19). Wametajwa kuwepo wakati wa Musa kupewa Torati (2:2; Mdo.7:53;Gal.3:19). Ni vigumu kuwa na uhakika juu ya habari hiyo, maana ilidhaniwa kwamba Musa alipewa Torati moja kwa moja kutoka kwa Mungu.

Mara kwa mara walileta ujumbe wa Mungu kwa mtu – Gideoni (Amu.6:11ku.) na mama wa Samsoni (Amu.13:3-5). Malaika alileta msaada kwa Eliya (1 Waf.19:5-7) na wakati mwingine pengine ni malaika aliyemtokea Yoshua kama jemadari ya vita (Yos.5:13-15) (2 Waf.6:17ku). Pia malaika ni walinzi (Zab.91:ll). Yakobo katika maoni ya ngazi aliona malaika wakipanda na kushuka juu yake (Mwa. 28:12). Katika Danieli malaika wamepewa majina, mmoja Gabrieli ambaye alimwelezea Danieli maana ya maono aliyoyapata (Dan.8:16ku. 9:21ku). Mikaeli aonekana kama malaika mlinzi wa Israeli (Dan.10:13,21; 12:1).

Katika Agano Jipya malaika Gabrieli alimtokea Zakaria na kumjulisha habari ya kuzaliwa kwa Yohana Mbatizaji (Lk.1:11ku) na tena Gabrieli alimtokea Mariamu na kumjulisha habari ya kuzaliwa kwa Yesu Kristo (Lk.1:26). Malaika alimtokea Yusufu na kumwambia amchukue Mariamu kuwa mkewe (Mt.1:20). Pia malaika aliwajulisha wachungaji habari ya kuzaliwa kwa Kristo ndipo walitokewa na jeshi la malaika (Lk.2:10,13). Malaika wametajwa kuwa walinzi wa watoto (Mt.18:10) na wa Petro na Yohana (Mdo.5:19ku. 12:7ku). Malaika akamwongoza Filipo Mwinjilisti (Mdo.8:26) na kumtokea Kornelio (Mdo.10:3) na Paulo katika safari ya kwenda Rumi (Mdo.27:23). Wameitwa „wana wa Mungu" katika Ayubu 38:7 wakifurahia uumbaji wa Mungu. Pengine hao waliotajwa katika Mwa.6:2 ni malaika wabaya. Yesu alitaja malaika kuwa wahusika katika hukumu ya mwisho (Mt.26:27; Mk.8:38; 13:27; Lk.12:8; 2 The.1:7). Malaika alimpiga Mfalme Herode, naye akafa (Mdo.12:23).

Katika maisha ya Bwana Yesu malaika walimtumikia mara baada ya majaribu yake, (Mt.4:11) ila hatuambiwa ni kwa njia gani walimhudumia, huenda walimtia

nguvu ya kimwili au kumletea chakula. Halafu pale Gethsemane alipokuwa katika dhiki kubwa wakati wa kumwomba Baba yake amwondolee „kikombe cha mateso" alihudumiwa na malaika (Lk.22:43). Askari walipokuja kumkamata Yesu alisema kwamba angaliweza kusaidiwa na majeshi ya malaika kama angalihitaji msaada wao (Mt.26:53).

Malaika wameitwa „wana wa Mungu" katika Mwanzo 6:2 (yadhaniwa walikuwa malaika wabaya) na katika Ayubu 1:6; 2:1; 38:7 wadhaniwa kuwa malaika wazuri. Mara zote hutajwa kwa jumla, hakuna aliyeitwa mwana wa Mungu peke yake. Imefikiriwa kuwa wameitwa hivyo kwa sababu wameumbwa na Mungu moja kwa moja kama Adamu, ambaye pia aliitwa mwana wa Mungu (Lk.3:38). Waliumbwa, hawakuwa wa milele.

Yadhaniwa Shetani alikuwa malaika mwenye uwezo mkuu aliyemwasi Muumba wake, ndipo alipoondolewa mahali pa juu akavuta kundi la malaika waliojiunga naye, nao wote walianguka (Isa.14:12-15; Eze.28:12-19; Mt.25:41; 2 Pet.2:4; Ufu.12:9).

Tutafikiri zaidi juu ya uhusiano wa malaika na waumini tutakapofika kwenye 1:14.

1:5-14 Yesu ni bora kuliko malaika

k.5 Hoja juu ya ukuu wa Yesu kuliko malaika unahusu „*Jina alilolirithi*" maana yake *cheo chake cha kuwa „Mwana wa Mungu*". Hao malaika walikuwa wajumbe wazuri sana, nao walitumiwa na Mungu kwa kazi maalum. Hata hivyo, walibaki ni wajumbe tu. Ila Yesu, kwa kuwa ni Mwana wa Mungu anawazidi kabisa. Hakuumbwa, na katika umilele alikuwa „Mwana". Alipozaliwa Mariamu aliambiwa ataitwa „Mwana wa Aliye juu" na „Mwana wa Mungu"(Lk.2:32,35). Yesu amelirithi Jina la Mwana kwa sababu ya mambo mawili makubwa: (I) alikuwa Mwana katika umilele kabla ya kuzaliwa mwanadamu (2) alikuwa Mwana kwa sababu ya Kufufuka kwake kutoka wafu hali akiwa Mwana wa Adamu (Rum.1:3-4; Mdo.13:33). Kwa hiyo, katika kusimamisha hoja yake mwandishi alidondoa maneno kutoka Zaburi 2:7, Zaburi ambayo ilikubalika kwamba yamhusu Masihi.

Halafu mwandishi alidondoa maneno kutoka 2 Sam.7:24 kuthibitisha hoja hiyo juu ya Jina bora la Mwana. Maneno hayo yalisemwa na Nabii Nathan kwa Mfalme Daudi nayo yalihusu kuzaliwa kwa mwana wake Sulemani. Ila pamoja na maana hiyo maneno hayo yalikuwa na maana kubwa zaidi iliyohusu Kuja kwa „Mwana mkubwa wa Daudi" yaani Masihi, ambaye kwa upande wa ubinadamu wake ataitwa „Mwana wa Daudi". Akiwa mwanadamu aliyefufuka kutoka kwa wafu Yesu alidai kuurithi huo ufalme wa Daudi na kwa sababu hiyo Baba amemwita „Mwanangu". *Hivyo jina la kuwa „Mwana wa Baba" ni jina kuu kupita jina lo lote ambalo malaika walipewa au waliweza kulidai*. Tazama swali

ambalo Yesu alilowauliza wakuu juma la mwisho la maisha yake. Wao walikuwa wamemshambulia na maswali yao wakitaka kumnasa ndipo yeye aliwashambulia na swali la maana sana kuhusu asili yake na „uana‟ wake‟ akilenga kuwaonyesha kwamba hata Daudi alijua kwamba „mwana‟ wake ndiye „bwana‟ wake mwenye asili katika Mungu na katika kufanyika mwanadamu atazaliwa katika ukoo wake (Mt.22:41; Zab.110). Katika umilele Mwana alikuwa pamoja na Baba katika uhusiano wa ukaribu kabisa, wakishirikiana katika Umoja wa Utatu Utakatifu; Baba, Mwana, Roho. Alipokuja duniani alipenda sana kulitumia jina „Mwana wa Adamu‟ (Dan.7:13-14). Hata hivyo, ijapokuwa hakutamka kwa wazi, kwa maneno na matendo yake alidai na kuonyesha kwamba Yeye ni Mwana wa Mungu. Neno hilo lilitawala mazungumzo yake na viongozi katika sura za Injili ya Yohana; (taz. Yn.5:19-25l 8:12ku. 31-58; 10:15ku. 11:40ku. 14:6ku. na mahali pengine pengi katika Yohana na Injili zingine). Hakuna wakati ambao Baba aliweza kusema Wewe si Mwanangu, ila siku ilifika ambayo kutokana na Kufufuka Kwake, katika kuwa mwanadamu wa utukufu, alipata cheo kipya cha kuwa mwanadamu aliyetukuzwa (Rum.8:29). Wakati wa ubatizo wake na wakati alipogeuka sura Mlimani, Baba alimtangazia kuwa „Mwana‟ wake (Mt.3:17; 17:5).

Kwa sababu mwandishi anatilia mkazo neno la ujumbe/upatanisho, Yesu ni bora kwa sababu ya cheo chake bora ya kuwa Mwana, hoja yake ni kwamba hata ujumbe unaouletwa na Mwana ni bora kabisa.

k.6 Hapo tena hoja ya mwandishi ni *Yesu ni mkuu kupita malaika kwa sababu Yeye anaabudiwa na malaika.*. Kama kawaida yake mwandishi alidondoa maneno kutoka Zab.97:7 ambayo pia yapo katika Kum.32:43. Maneno ni kutoka tafsiri la Septuajinta. Neno „tena‟ laweza kuwa na maana ya „sababu nyingine‟ kufuata sababu zilizotangulia. Au, yaweza kuhusu wakati wa jambo lenyewe. Swali ni „ni wakati gani‟ „aletapo mzaliwa wa kwanza ulimwenguni‟, Je! ni wakati wa kuzaliwa kwake; au wakati wa kufufuka kwake; au wakati wa Kuja kwake mara ya pili. Hapo, wataalamu huachana katika mawazo yao. Twajua kwamba alipozaliwa malaika walihusika (Lk.2:13ku). Na wakati alipofufuka kutoka wafu (Mt.28:2ku.Lk.24:2,23; Yn.20:12). Pia wametajwa kwamba watakuwepo pamoja na Yesu atakaporudi mara ya pili katika utukufu wa Baba (Mt.13:41ku. 24:29ku). Ni dhahiri kwamba daima wajibu mkubwa wa malaika ni kumwabudu kwa kuwa ni Mungu Mwana, mkuu wao. Kipaumbele chao cha kwanza ni kumtukuza na kumfanyia ibada wakati wote, ndiyo kazi yao muhimu kabisa na adhimisho yao ya kwanza.

Kuhusu maneno „mzaliwa wa kwanza‟ (12:23 ling. na Kol.1:15,18). Yeye ni mzaliwa wa kwanza kwa sababu ni Muumba na Mkombozi wa uumbaji wote naye atarudi tena ulimwenguni kwa uumbaji wake ili auingize katika utimilifu na ukamilifu wake. Alikuwa mzaliwa wa kwanza wa Baba kwa sababu kwa Yeye uumbaji ulifanyika pia Yeye ni mrithi wa yote. Ni mzaliwa wa kwanza kwa sababu alifufuka kutoka wafu wala hapatikani tena na mauti. Yu hai milele na

milele. Kwa hiyo, katika kusema hivi, mwandishi alitaka kuyanyosha mawazo ya Kiyahudi ambao huenda baadhi ya wasomaji wake walikuwa nayo. *Yule waliyemdhani kuwa chini ya malaika ni yule ambaye malaika humwabudu kama muumba wao.* Twajua kwamba malaika wametajwa mara kwa mara katika Kitabu cha Ufunuo, wakizungukia kiti cha enzi cha Mungu na cha Mwana Kondoo na kuongoza ibada kuu za pale (Ufu.5:11-12). Twapata picha ya jinsi Wayahudi walivyoelekea kuwaheshimu malaika kuliko ilivyokuwa sawa hata twasoma kwamba mara mbili Yohana mwandishi wa Kitabu cha Ufunuo alivutwa kumsujudu yule malaika aliyempa ujumbe, naye akakemewa (Ufu.19:9ku. 22:8,9).

k.7 Hapo mwandishi amedondoa maneno kutoka Zab.104:4 maneno yanayoonyesha *ukuu wa Mwana katika hali ya asili yake ya kutumikiwa na malaika.* Malaika ni watumishi wa Mungu wafanyao shughuli zao katika hali ya utumishi, wakifanana na upepo na moto. Yawezekana „upepo" na „moto" ni dalili za nguvu na uepesi wa kazi zao au pengine ni kuonyesha jinsi wanavyotokea na kutoweka bila kukaa. Utumishi wao ni wa muda, ila sivyo alivyo Mwana. *Yeye ni mkuu na bora kwa sababu yeye si mtumishi bali ni yule anayetumikiwa sawa na Mungu.*

k.8 Lafikiriwa Zaburi 45 ni wimbo kwa ndoa iliyotumika kwa arusi ya Mfalme. Wazo la k.7 juu ya Kristo kuwa Mungu anathibitishwa na maneno kutoka Zaburi 45:6-7. *Yesu ni mkuu wa kupita malaika kwa sababu anayo heshima iliyo kuu na bora. Tofauti na malaika Mwana ni wa milele, tena anamiliki kama Mfalme. Tena utawala wake ni bora kwa sababu anatawala kwa haki. Yeye huketi juu ya kiti cha enzi cha Mungu kama Mungu. Yeye ni Mfalme anayetawala milele na milele*, hakuna mwisho wa utawala wake, wala habadiliki katika hali yake. Kwa hiyo Yeye ni zaidi ya nabii anayesema na kuhani anayeokoa. Yeye ni Mfalme anayetawala. Pamoja na hayo utawala wake ni wa haki na adili.

k.9 Wazo kuhusu hali ya utawala wake linaendelea kwa kukaza *Yesu ni bora kupita malaika kwa sababu ya hali yake bora ya kutoa kielelezo chema cha uadilifu kupita malaika.* Yeye kwa hali ya asili anapenda haki na kuchukia maasi. Malaika wengine waliasi na kuanguka, ilitegemea uchaguzi wao, ila Mwana katika asili yake alipenda haki na kwa sababu hiyo Mungu alimfurahia sana na kumpaka mafuta ya furaha ya kipekee. Kwa hiyo, *Yesu ni mkuu na bora katika kutoa kielelezo bora cha uadilifu*.

Tukijumlisha vifungu 7 – 9 *Yesu ni bora* katika hali ya asili yake ya kuwa yule wa kutumikiwa kama Mungu. *Yeye ni bora* katika hali ya asili ya heshima yake ya kuketi kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu akitawala milele na milele. *Yeye ni bora* katika hali ya kuwa kielelezo bora cha kupenda haki na kuchukia uasi. Yeye ni mwadilifu kupita wote akishiriki tabia ya Mungu Mtakatifu. Hali hizo zimemwongoza Baba kumjalia shangwe na furaha kuu kupita mwingine awaye yote.

k.10-12 Hapo mwandishi ametaja Zab.102:25-27 kwa kuonyesha jinsi *Mwana alivyo mkuu kupita malaika kwa ajili ya kazi yake kuu na bora kuhusu Uumbaji.* Alishirikiana na Mungu katika kazi hiyo (1:2; Yn.1:3). Mbingu na nchi zitaharibika na kutoweka ila Mwana, Muumba wake haharibiki, wala hatoweki, Yeye hudumu milele na milele. Malaika ni viumbe, huenda walitanguliwa kuumbwa, hata hivyo, waliumbwa, tofauti na Mwana asiyeumbwa, anayeshiriki umilele pamoja na Mungu.

k.13 Halafu mwandishi aliyatumia maneno ya kwanza ya Zab,.110. Kwa maneno hayo *Yesu ni mkuu kuliko malaika kwa sababu amepewa mahali pa juu kabisa. Ameketishwa na Mungu kwenye mkono wake wa kuume, mahali pa heshima kuu*. Yuko pale katika hali ya kungojea wakati wa adui zake wote kuwekwa chini yake. Anazidi kukaa pale kwa amri ya Baba katika matumaini yenye uhakika ya ushindi kabisa. Pale msalabani alianza ushindi wake (Kol.2:15) ushindi unaoendelea hadi utakapofikia upeo wake katika upinzani wote na uadui wote kukomeshwa. Iwapo ameketishwa kwenye Kiti cha Enzi upinzani haujaisha bado, ila, Mungu ameamua utakomeshwa kabisa, kwa hiyo, hautadumu. Twaona ukuu wake kupita malaika katika picha ya mwisho ya malaika wote wakisujudu kwenye Kiti cha Enzi (Ufu.5:11-12; 1 Pet.3:22; Flp.2:10). Hakuna hata malaika ye yote ambaye amepewa mahali pa heshima kulingana na mahali pa Mwana. Ndiyo sababu Mungu amesema neno lake la mwisho katika Mwana.

k.14 Kwa njia ya swali mwandishi hutoboa wazi kazi na utumishi wa malaika. Wao hutumwa na Mungu ili wawahudumie waumini watakaoshiriki pamoja na Kristo katika utukufu wake. Malaika hupewa maagizo ya Mungu na kutumiwa naye katika kuwaletea waumini misaada mbalimbali. Malaika ni watumishi wa Mungu, si watumishi wetu, hata hivyo, utumishi wao ni kwa ajili yetu. Shughuli zao ni ulinzi (Zab.91:11) uongozi (Mwa.19:17) kutia moyo (Amu.6:12) kuokoa na shida (Mdo.12:7) kutia mwanga (Mt.2: 10-20) kutia nguvu (Lk.22:43) kukemea (Hes.22:32) na kadhalika. Mara nyingi hawaonekani wala hawatambulikani.

Maneno „watakaorithi wokovu" yanatuelekeza kuona kwamba ziko hatua tatu katika „wokovu". Hatua ya kwanza ni wakati wa kuamini – mtu kuokolewa na hatia ya dhambi. Kwa wakati wa sasa muumini huokolewa na nguvu za dhambi; na mwishowe ataokolewa mbali na kuwepo kwa dhambi. Kwa hiyo, muumini aweza kusema: „nimeokolewa"; „ninaokolewa"; „nitaokolewa".

MASWALI

Kwa maneno yako mwenyewe eleza sifa kuu za Bwana Yesu zilizotajwa katika sura hii.

Onyesha ni kwa hali gani zipi na kwa mambo gani Yesu ni mkuu kuliko malaika.

2:1-4 Hatari ya kutokumjali Mwana

Mwandishi anayo desturi ya kutoa hoja halafu kutoa mwito na kusihi au kutoa onyo au kuweka mwito na onyo pamoja kutokana na hayo aliyotangulia kusema akijenga juu yake. Amefanya hivyo mara kwa mara katika Waraka (taz.2:1-4; 3:12-19; 6:4-8; 10:26-31: 12:25-29). Hangoji mpaka amemaliza hoja yake, bali ameingiza onyo au mwito kati yake. Ndiyo sababu alianza kwa maneno „Kwa hiyo".

k.1 Maneno „Kwa hiyo" yahusu yale aliyokwisha kusema juu ya malaika. Amesisitiza ukuu wa Kristo kupita malaika na kutoa sababu zake. Katika sura ya kwanza tumeona kwamba Mwana ameketi katika kiti cha enzi cha Mungu, yuko mkono wake wa kuume, kwa kuambiwa na Baba aketi pale, naye anangojea mpaka adui zako wote wamekuwa chini ya miguu yake, maana yake, mpaka wameshindwa. Hivyo, ni dhahiri kwamba Mwana ni Neno la mwisho kutoka Mungu, katika Yeye Mungu amesema Neno lake la mwisho kwa wanadamu. Hakuna ufunuo au ujumbe mwingine kufuata ule wa Mwana.

Mwandishi hakuwa radhi kutoa mafundisho tu bali alikuwa na mzigo juu ya waumini kuishi maisha yaliyolingana na mafundisho ya imani yao katika Kristo. Kama ni hivyo waumini wameonywa juu ya ulegevu wao katika kumfuata Kristo. Wapaswa wafanye nini? Wameambiwa *kuyaangalia zaidi yale waliyosikia* ili wasije wakayakosa. Hao waumini, kama tulivyoona katika Utangulizi, walikuwa katika hatari ya kutokujali. Mwandishi alikuwa na moyo wa kiuchungaji na alikuwa na mzigo juu yao, alitaka watambue hatari waliyokuwa nayo wakiendelea na hali yao ya kutokutia maanani imani yao katika Kristo. Alikuwa akisema kwa waumini ambao hapo nyuma walikuwa wamemkubali Kristo ila sasa wako katika hatari ya kutaka kurudi kwenye dini yao ya asili ya Kiyahudi, pengine wamechoka na mateso na maudhi ya wenzao. Kwa vyo vyote wamepoa katika kuuona Uzuri wa Kristo.

k.2 Katika kifungu hicho mwandishi amelinganisha neno lililoletwa na malaika na neno lililoletwa na Kristo. Wayahudi waliamini kwamba malaika walikuwepo na kuhusika katika kuleta Torati kwa Musa. (Taz. Kum.33:2; Zab.68:17 – malaika hawatajwi kwa wazi ila ilimaanishwa kwamba ndio hao waliotajwa. Stefano na Paulo walisema wajumbe wa Torati walikuwa malaika Mdo.7:53; Gal.3:19). Kwa Torati kila kosa na uasi uliadhibiwa. Torati iliyoletwa na malaika ilikuwa na mamlaka na kila mtu aliwajibika kuitii. Kama ni hivyo, itakuwaje kwa Neno la Wokovu lililoletwa na Kristo, Mwana wa Mungu, ambaye yuko mkono wake wa kuume. Je! si mamlaka yake ni kubwa na ya kupita ile ya malaika? Watu hawakuchezea ujumbe wa malaika, kwa hiyo, Je! watu waudharau ujumbe wa wokovu ulioletwa na Kristo Mwenyewe? Haiwaziki wafanye hivyo. Itakuwaje wakifanya hivyo? Yawezekana mwandishi alikuwa akikumbuka uasi wa Waisraeli wakati wa kusafiri jangwani. Waliadhiwa kwa ukali (3:16ku).

k.3 Ndipo mwandishi aliuliza swali kubwa, la maana sana, „tutapataje kupona tusipojali wokovu mkuu namna hiii? Malaika walileta Torati; Yesu ameleta Wokovu. Tena wokovu „mkuu" wokovu wa kumwokoa mtu na dhambi zake na hukumu ya Mungu, na kumkirimia uzima wa milele. Kwa wokovu mtu hujaliwa ushirikiano wa kibinafsi, wa ukaribu sana, na Mungu.

Ndipo mwandishi aliendelea kuonyesha asili ya ujumbe wa wokovu walioletewa na kuuamini. Kwanza uliletwa na Yesu. Ni Yesu Mwenyewe aliyeuleta. Katika huduma yake hapo duniani alizunguka hapa na pale, vijijini na mijini akiwatangazia watu habari za Ufalme wa Mungu. Baadhi walimjali na kumwamini, baadhi kutokana na kumezwa na shughuli zao au kwa kutapanya nguvu zao katika mambo mengi walishindwa kujitoa kwa Kristo (Mk.4:20; Lk.6:46-48; Yn.4:50-53).

Halafu Yesu alikabidhi kazi ya kutangaza Habari Zake Njema, yaani Injili ya Wokovu kwa Mitume na wenzao ambao walikuwa wameandamana naye na *kutumwa naye* kwa kazi hiyo (Yn.14:26). Hao walikuwa mashahidi wa kuona. Hao walishuhudia kwa moyo mkuu na kwa ushujaa na kwa kuvumilia mateso, wakivuta watu kumwamini Kristo. Pamoja na kuwa mashahidi wao wenyewe walikuwa wameonja katika maisha yao uzuri na uwezo wa Kristo katika kuwasamehe dhambi zao na kuwatia nguvu ya Roho Mtakatifu na kuishi maisha mapya katika Kristo.

k.4 Halafu mwandishi alitaja jambo jingine. Kama hayo hayakutosha, basi pamoja na Yesu Mwenyewe, na Mitume na wenzao, hata Mungu Mwenyewe aliuthibitisha uhalisi wa ujumbe wao kwa kuwajalia uwezo wa kufanya miujiza na maajabu mbalimbali pia Roho Mtakatifu aliwapa waumini vipawa mbalimbali vilivyoboresha utumishi wao na maisha yao ya kiroho (1 Kor.12:7-11). Hayo yote yalionyesha kwamba Injili haikuwa na asili katika wanadamu, wala haikusimama peke yake bila Mungu na Roho Mtakatifu. Walivyofanya mitume na wenzao walifanywa kwa kuwezeshwa na Mungu na kwa jinsi Mungu, si wao, walivyotaka.

Kama ni hivyo, Je! wamwache Yesu na wokovu wake ambao wenzao waliowatangulia waliuthamini sana na kujitoa kabisa kwa ajili yake? Hakuna sababu za haki kwa ulegevu wao na kutokujali kwao. Ulikuwepo ushuhuda wa kutosha katika matukio ya historia ya kuwasaidia waendelee kuamini. Waliyohitaji ni kutia maanani imani yao na kuangalia sana mwenendo wao. Neno ambalo limetumika ni lile lililotumika kwa meli ambayo haikufungwa sawasawa kwenye kltuo chake, ndipo mwenye meli aliporudi alijikuta imeondoka mahali pake na kuchukuliwa na maji. Pia lilitumika kwa pete ambaye haikushika kidole cha mwanamke sawasawa kisha ikaondoka bila mwanamke kutambua kwamba imeondoka.

Lina maana kwamba jambo linatokea bila mtu kutambua kwamba linatokea, ni mfano wa kitu kuteleza au kutoweka. Waumini hawakukusudia kuasi ila kwa hali yao ya kutokujali wako katika hatari ya kujikuta kwamba wameipoteza imani yao bila kujua. Walielekea kuupenda ufunuo wa Agano la Kale na kuuacha ufunuo wa mwisho uliotoka kwa Mungu kwa njia ya Kristo. Ni upuuzi mkubwa wala haikueleweka kwa nini mtu apatwa na hali ya kutokujali huku ujumbe wenyewe ulileltwa na Kristo, Mwana wa Mungu, na kutangaziwa na wale walioandamana naye, huku Mungu akiyathibitisha mahubiri yao na ushuhuda wao, wala si hivyo tu, hata Roho alifanya kazi mioyoni mwa waumini na kuwahakikishia ukweli na uhalisi wa imani yao. Kwa jinsi mwandishi alivyoandika inaonekana yeye mwenyewe hakuwa miongoni mwa waumini wa kwanza bali alikuwa miongoni mwa wale waumini waliofuata, kama kizazi cha pili cha Kikristo sawa na wale walioandikiwa.

Hatari ni nini hasa? Kwa upande mmoja watapatwa na hasara kubwa sana, watapoteza imani yao katika Kristo na baraka zake zote. Lakini si hivyo tu, pamoja na hayo, watapatwa na adhabu (Mt.5.29=-30; 8:11-12; Yn..3:16-18; 36). Ikiwa wale waliokosa neno la malaika, hasa katika Torati, waliadhibiwa, si zaidi wale wasioljali neno la wokovu lililoletwa na Kristo, neno kuu la upendo mkuu wa Mungu katika kuwakomboa? Kwa mwandishi, hatarii hii ipo kweli, si mchezo wa maneno tu. Alitaka sana waendelee kuwa waaminifu kwa Kristo wasije wakamwasi.

Hilo lilikuwa onyo la kwanza, na mwandishi mara kwa mara aliweka maonyo kati ya hoja zake (3:7-4:13; 5:11-6:12; 10:19-39; 12:1-13:22).

2:5-9 Yesu atatukuzwa juu ya vyote

Katika vifungu vya kwanza vya Waraka mwandishi alimwonyesha Yesu kuwa Mungu Mwana aliyemfunulia Mungu kwa ukamilifu. Katika sehemu hiyo amemwonyesha Yesu kuwa mwanadamu halisi akimfunulia Mungu kwa ukamilifu.

Mwandishi bado angali akiandika kwa kukumbuka jinsi malaika walivyokuwa muhimu katika mawazo ya Wayahudi na ya wale anaowaandikia. Baadhi yao waliamini kwamba malaika ndio wajumbe wa kuleta neno la Mungu kwao na ya kuwa nyakati hizo zilikuwa chini ya uongozi wao wakiwaza Mikaeli kuwa kiongozi wao mkubwa. Pia walifikiri kwamba katika nyakati zijazo malaika watazidi kuhusika.

Katika vifungu hivi mwandishi ametumia maneno ya Zaburi 8:4-6; maneno yanayowahusu wanadamu (si maneno hasa ya kumhusu Kristo). Kifungu cha tatu na cha nne vya Zaburi hiyo vyasema juu ya udogo na unyonge wa wanadamu kwa kulingana na ukubwa na nguvu vinavyoonekana katika uumbaji „nikiziangalia mbingu zako, kazi ya vidole vyako, mwezi na nyota

ulizoziratibisha, mtu ni kitu gani hata umkumbuke, na binadamu hata umwangalie?"

Ndipo Zaburi inaendelea kwa kutaja ukubwa na heshima ya wanadamu katika mipango ya Mungu, „Umemfanya mdogo punde kuliko Mungu; Umemvika taji ya utukufu na heshima; Umemtawaza juu ya kazi za mikono yako; umevitia vitu vyote chini ya miguu yake". Kwa sasa, mwanadamu amefanyika kuwa „mdogo" kuliko malaika, lakini jambo hilo ni kwa muda tu, kutokana na uasi wa wanadamu, badala ya kutawala, wanadamu wameshindwa kutawala.Tangu mwanzo Mungu alikusudia wanadamu wawe juu ya uumbaji wote na baadaye kusudi hilo la Mungu litatimizwa (k.8b). Katika vifungu hivi tumepewa habari ya mambo mawili, unyonge wa wanadamu, na utukufu wa wanadamu utakaofuata huo unyonge wake. Kwa hiyo, ina maana kwamba, baadaye, wanadamu watakuwa juu ya malaika (1 Kor.6:3). Wanadamu waliumbwa ili wawe chini kidogo ya Mungu (katika Kiebrania neno linalotumika kwa wanadamu ni lile linalotumika kwa Mungu „elohim") waliumbwa katika mfano na sura yake, nao walipewa amri ya kuitiisha nchi, kutawala samaki na ndege na kile kiumbe chenye uhai n.k. (Mwa.1:27-29). Kwa kuasi kwao wanadamu walipoteza uwezo wa kutawala na kutiisha nao walipewa adhabu ya ardhi kulaaniwa n.k. (Mwa.3:17-19). Hayo yote yawahusu wanadamu na ni wanadamu ambao watakuwa „mabwana" katika ulimwengu ujao, si malaika, tena watakuwa mabwana wa malaika!.

k.9. k.8b chasema „sasa *bado hatujaona*" *halafu k.9a chasema „ila twamwona Yeye*" neno „twamwona" lina nguvu ya „twamwangalia sana". Yesu yu katikati ya historia ya wanadamu. Ameungana na wanadamu na katika kufanyika mwili amefananishwa na wanadamu walioanguka, huku akiwa tofauti nao. Kwa hiyo Yesu Kristo ana mahali pa maana sana katika hayo yote. Bila shaka Wakristo walioandikiwa walitatizwa na uhusiano kati ya malaika na Yesu hasa walipofikiri juu ya Yesu kufanyika mwili na kupatwa na maumivu na kuuawa. Ilikuwaje Yeye awe mjumbe aliye juu ya malaika? Mwandishi ameandika kwamba hata Yesu alikuwa chini ya malaika kwa *muda tu* tena *kwa kusudi maalumu* ya kuwaokoa wanadamu ili wanadamu waokolewe na unyonge wao na kuingia katika utukufu wao. Yesu, katika hali ya kuwa mwanadamu halisi, kwa kusudi, na kwa mapenzi ya Mungu, aliingia katika mambo ya wanadamu ili awarudishie kwenye hali ya kushinda badala ya kushindwa, ya kutawala badala ya kutawaliwa.

Yesu hakulindwa na shida na hatari za maisha ya wanadamu, hata alipatikana na mauti, sawa na wanadamu, na tofauti na malaika ambao hawafi. Alivikwa taji na utukufu ili aonje mauti kwa ajili ya kila mtu. Mungu alimpa hiyo taji alipomtoa ili afe kifo cha kufidia dhambi na kuwaokoa wanadamu. Mauti imekuwa kitu cha kutisha na wanadamu wote huishi chini ya wingu lake weusi. Yesu *alionja* mauti ya kimwili na kujua kufa kwa ujuzi wa kibinafsi na kwa njia hiyo amefananishwa na wanadamu kwa kupitia katika shida za mateso, dhiki,

kukataliwa, maumivu, n.k. Yeye alionja mauti katika hali yake mbaya, hali ya kusulibiwa kama mhalifu wa hali ya juu. Amefanya hayo kwa ajili ya kila mwanadamu ili asiwepo mtu ye yote atakayeionja mauti ya mwenye dhambi. Yeye ametoa sumu yake (1 Kor.15:55,56). Dhamiri ya mtu hutakaswa kwa kifo cha Kristo (9:14,28; 10:10). Neno „kuonja" linaashiria muda mfupi wa kufa kwake kwa sababu alifufuka kutoka wafu, lakini halipunguzi uchungu wake.

2:10-13 Yesu – kiongozi mkuu

Shabaha yake nzito ilikuwa kuwaleta wana wengi waufikilie utukufu, yaani wautimize lengo la kuumbwa kwao. Lilikuwa tendo lililoonyesha mzigo wa Mungu juu ya wana wake, hakuna njia iliyosababisha huzuni na uchungu wa moyo kwake kuliko hiyo, wala hakuna njia iliyomnyenyekeza sana kuliko hii. Yesu ni kiongozi wao na amestahili kuwa hivyo kwa sababu amejihusisha na kufananishwa na wanadamu kiasi cha kushiriki mateso, maumivu, na kifo. Mateso yalikuwa njia ya kumfanya afae na kumstahilisha awe kiongozi. Ilikuwa njia ya lazima. Neno „kukamilisha" halina maana kwamba Yesu hakuwa mkamilifu kabla ya kufanyika mwanadamu ila kwa njia ya kuishi maisha ya mwanadamu na kwa mateso na kufa kwake amehitimu na kuwa mkamilifu *zaidi*. Mfano wake ni mwalimu ambaye ni mwalimu kamili, amesomea ualimu, amepata cheti chake, aweza kuitwa mwalimu. Ndipo kwa kufanya hiyo kazi ya ualimu anahitimu na kuwa mwalimu kamili si kwa sababu anacho cheti cha ualimu tu bali kwa kufanya hiyo kazi. Yesu alijifunza kumtii Baba yake na kufanya mapenzi yake na kuyashinda majaribu yaliyompata n.k. (5:7ku.10:7,9). Wanadamu waliumbwa kwa shabaha ya kuwa mabwana wa uumbaji chini ya Mungu, ndipo kwa kuanguka, iwapo hawakushindwa kabisa, ni dhahiri kwamba hawawi mabwana wenye uwezo wa kutawala maisha yao na kushinda. Baadaye, hali hiyo itabadilika, nao wataingia hali ya kuwa mabwana wenye uwezo wa kutawala chini ya Mungu na pamoja na kiongozi wao, Mwokozi wao, Yesu Kristo, ndipo watakuwa kama walivyopaswa kuwa, si kwa kuwaza tu, wala si kwa kuamini tu, bali kwa ujuzi wa kibinafsi. Watayapata yote waliyoyakosa walipomwasi Mungu. Jambo hilo ladhihirisha upendo mkuu wa Mungu ambaye hakukata tamaa juu ya wanadamu. Mungu ndiye mwenye kuanza na mwenye kutimiza mwenendo huo wa kumrudishia wanadamu kwenye mahali pake pa heshima.

Watu walisikia shida katika kuutambua ukuu na utukufu wa Yesu kwa sababu aliishi maisha ya shida na kufa katika dhiki kubwa. Mwandishi alitaka kuwaonyesha kwamba maisha yake ya shida na kufa kwake katika dhiki vilidhihirisha utukufu na ukuu wa kweli na viliwezekana kwa neema ya Mungu.

k.11,12 Yesu hasikii haya kuwaita wanadamu „ndugu zake" (k.10 „wana"; k.11,12 „ndugu" k.13;11:16 „watoto") naye amekuwa radhi kujihusisha nasi kabisa na ile hali aliyoonyesha alipofanyika mwanadamu na kuishi maisha ya wanadamu bila kujihurumia, na alipokufa katika dhiki kubwa. Anaendelea kuwa

na hali hiyo hata sasa anapoishi katika utukufu wa mbinguni. Kwa hiyo Yeye ni tofauti na malaika ambao hawayajui wala hawayashiriki mambo ya kibinadamu. Kama kiongozi Yeye anawaongoza wanadamu katika safari yao ili wahitimu kama Yeye alivyohitimu katika kumtii Mungu na kufanya mapenzi yake na kuyashinda majaribu. Mwandishi alidondoa maneno kutoka Zaburi 22 na kutoka Isaya 8:17,18 kuonyesha jinsi Yesu alivyoshiriki nasi. Zaburi ya 22 inaanza na maneno ambayo Yesu aliyatumia alipokuwa msalabani, maneno ya kuonyesha taabu yake, ndipo Zaburi inamalizika na maneno ya ushindi wa mwenye haki ambaye mwishowe alimsifu Mungu. Na maneno ya Isaya ni juu ya Yesu kuwa yule aliyemtumaini Mungu hata katika dhiki zake. Alijikabidhi kwa Baba yake. Kwa sababu hizo Yeye amestahili kuwa Mwokozi na Kiongozi wetu naye yupo pamoja nasi katika shida zetu zote.

2:14-18 Yesu – Kuhani wetu mkuu mwenye rehema

Hapo mwandishi amemwonyesha Yesu kuwa Mkombozi mkuu ambaye ametuweka huru mbali na adui zetu kubwa za dhambi, mauti, na Shetani. Alikuja kutenganeza mfarakano kati yetu na Mungu. Ilimpasa apambane na adui za dhambi na mauti na Shetani na kuzishinda. Alikuja kuharibu kazi za Shetani na kutuweka uhuru mbali na nguvu za dhambi na Shetani na hofu ya mauti. Katika kupambana na adui hizo ilimpasa afanyike mwili na kuushiriki ubinadamu wetu, pasipo kufanyika mwanadamu asingaliweza kuwa mkombozi wetu. Dhambi ni doa katika utu wetu, twahitaji kutakaswa nayo (1:3) Dhambi ni adui, inaharibu, ni nguvu ya ndani inayotuzuia tusiweze kufanya yanayotupasa au tunayopenda. Yesu alifanya suluhu kwa dhambi zetu. Mauti iliingia maisha ya wanadamu moja baada ya mwanadamu kufanya dhambi (Mwa.2:17; 3:3-4; Rum.5:12; 6:23; 1 Kor.15:21, 56). Yesu kwa kufa kwake ametoa sumu yake na iwapo wanadamu wanaendelea kufa, hofu yake imeondolewa, na mwishowe mauti haitakuwepo. Shetani ameshindwa katika hali ya kufungwa. Ni kama mbwa mkali ambaye angali hai na angali ni mkali, ila kwa sababu amefungwa hawezi kumdhuru mtu isipokuwa mtu husogee karibu yake na kumjali (Yak.4:7). Yesu alitoa tahadhari juu yake akisema ni mwongo, mwuaji, mwizi na mdanganyaji na sisi twapasa kuwa na tahadhari juu yake (Mt.4:1-11; 13:10; 16:23).

Tulianza kuwekwa huru tangu Yesu alipozaliwa na kuuchukua ubinadamu wetu. Yesu zaidi ya kushiriki damu na mwili alishiriki mambo yetu yote. Kwa maisha yake matakatifu ya kufanya mapenzi ya Mungu kwa ukunjufu wa moyo na kwa kukataa dhambi iwapo alijaribiwa kufanya dhambi *kuliko* sisi tunavyojaribiwa. Mara nyingi sisi tunapojaribiwa tunashawishwa na tunaikubali, kwa hiyo, hatufikii upeo wa nguvu ya kujaribiwa kama yule asiyekubali kushawishwa. Nguvu ya jaribu inazidi kwa kadiri ambavyo mtu hulipinga. Tuliwekwa huru kwa sababu ya Yesu kuchukua ubinadamu wetu na kushiriki mambo yetu. Tuliwekwa huru kwa sababu ya Yesu kuyashinda majaribu yake yote na kuishi maisha yake yote bila kufanya dhambi na kwa sababu ya Yesu

kufanya mapenzi ya Mungu kwa ukamilifu. Halafu tuliwekwa huru kwa sababu ya Yesu kuishiriki mauti yetu, mauti ya wenye dhambi, akichukua adhabu yake mwilini wake na kutuweka uhuru mbali na hukumu na hatia ya dhambi. Hivyo, Shetani hawezi kutushtaki kwa Mungu, ameipoteza kazi hiyo kwa wote wanaomkubali Kristo.

Kwa upande wetu Yesu ni kuhani wetu mkuu, mwenye rehema, aweza kuondoa hofu zetu za mauti na hukumu na mambo ya mbeleni, aweza kutuhurumia kwa maisha yetu ya nyuma akitusamehe dhambi zetu, na kutuweka huru na hisia zetu zinazotushtaki kuwa na hatia, na kutuhakikishia msamaha wa Mungu, naye anatujalia maisha mapya.

Yesu hakuja kuwasaidia malaika, kwa sababu malaika hawapatikani na shida za maisha kama sisi, hawajui jambo la mauti, maana hawafi, wala hawateswi kama sisi. Sisi twalemewa na shida mbalimbali, twahofu, twasikia udhaifu, twasikia kushindwa. Habari njema ni kwamba Yesu aweza kujihusisha nasi na kutuhurumia na kusogea karibu nasi hali akifahamu jinsi tunavyojisikia, anajiweka mahali petu ili atusaidie na kutushindia. Anapenda kutuita „ndugu zake".

Yesu ni kuhani mkuu, mwaminifu katika mambo ya Mungu. Yesu alionyesha uaminifu na utii wake kwa Mungu, pia alionyesha uaminifu wake kwetu akituthibitishia upendo wake wa ajabu. Yeye ni wa kutegemewa kabisa nasi twaweza kujua kwamba Yeye yu pamoja nasi katika mambo yetu yote, majaribu yetu, dhiki na shida zetu. Yu pamoja nasi katika hali ya kusikia kama ambavyo mtu anavyojisikia wakati wa shida na mateso na majaribu. Pia yu pamoja nasi katika hali ya kutia nguvu, ya kutusaidia, ya kutuonyesha jinsi ya kuyakabili yale tunayoyapata. Yu pamoja nasi kututia nguvu (7:16,25; 1 Kor.10:13).

MASWALI

Kwa nini mwandishi ametoa tahadhari wa waumini?

Zaburi iliyotumika hapa inatoa mafundisho gani kumhusu Yesu, na kuwahusu waumini?

Ni mambo gani yanayomstahilisha Yesu kuwa Kuhani wetu mkuu?

3:1-6 Yesu ni mkuu kuliko Musa

Twaweza kusema Yesu ni Mkuu kuliko yeye aliyekuwa mkuu, kwa sababu katika Imani ya Kiyahudi na Taifa la Israeli hakuna aliyehesabiwa kuwa mkuu kumpita Musa na ndiye sababu ya mwandishi, baada ya kumwonyesha Yesu kuwa mkuu kuliko malaika aliendelea kwa kumwonyesha Yesu kuwa mkuu kuliko Musa.

Musa alikuwa mkuu kwa sababu ya mambo mbalimbali makubwa. Ilikuwa dhahiri kwamba Mungu alisema na watu wake kwa njia ya Musa. Aliitwa na kutumwa na Mungu kuwatoa Waisraeli katika utumwa wa Misri na alipambana na Farao kuhusu jambo hilo (Kut.3:1ku.). Aliwaongoza watu wake kuvuka Bahari ya Shamu na kupitia jangwani kwa miaka arobaini. Alipewa Amri kumi, na Mungu alisema naye uso kwa uso (Kut.5:1ku.14:10ku.19-20; Hes.12:6-8). Alipewa maagizo juu ya Ibada katika Israeli, dhabihu za kutolewa na Sikukuu za kuadhimishwa, na mipango ya Makuhani na Walawi n.k. (25-27). Alifanya yote kama alivyoagizwa.

Kwa hiyo, tunapoifikiria hoja ya mwandishi ya kuwa Yesu ni mkuu kuliko Musa, tukumbuke sababu za Wayahudi kumheshimu Musa kuwa kiongozi wao mkuu.

k.1-6 Maneno „kwa hiyo" ni kama daraja ya kutoka hoja ya Yesu kuwa mkuu kuliko malaika na kuingia hoja hiyo mpya ya Yesu kuwa mkuu kuliko Musa. Aliwasihi walioandikiwa akiwaita „ndugu watakatifu" na „wenye kushiriki mwito wa mbinguni". Ni ndugu kwa sababu Yesu hasikii haya kuwaita hivyo, kama ambavyo tuliona katika sura iliyotangulia (2:11,12). Tena ni „watakatifu" kwa sababu wamfuata Yeye aliye Mtakatifu ambaye anawaita ndugu, yule aliyeyashinda majaribu yake yote na kuhitimu maisha yake bila kufanya dhambi. Aliyatii mapenzi ya Mungu kwa furaha na moyo mkuu. Hivyo „ndugu zake" wapaswa wawe watakatifu kama Yeye alivyo. Pamoja na hayo ni watu walioitwa na Mungu kutoka mbinguni ambaye kusudi lake ni wafike Kwake mbinguni baada ya kumaliza safari yao ya hapa duniani (Efe.1:3-4)..

Kama alivyofanya katika 2:1-4 mwandishi anawasihi kumtafakari sana Yesu, yule ambaye kaika ubatizo wao walimkiri kuwa Mwokozi na Bwana wao. Neno lililotumika kwa „tafakari" lina nguvu, lina maana ya kumwaza kwa makini na kwa kumzingatia sana na kwa kumtambua vizuri. Huyo Yesu ametajwa kuwa „Mtume" na „Kuhani Mkuu". Ni mara ya kwanza ya mwandishi kumwita „Mtume" hapo nyuma amemwita „Kuhani Mkuu". Kama Musa alivyotumwa na Mungu, vivyo hivyo na Kristo alitumwa na Mungu mwenye utume maalum wa kuukomboa ulimwengu. Musa alitumwa kuwatoa Waisraeli watoke katika utumwa wa kimwili, ila Kristo alitumwa awatoe wanadamu wote, si Wayahudi tu, watolewe katika utumwa wa dhambi. Musa alisita alipotumwa, ila Yesu aliufurahia utume wake na kuukaribisha bila shida. Mwandishi alilitumia jina la Yesu akitaka kutilia mkazo ubinadamu wake.

k.2 Wote wawili, Yesu na Musa walikuwa waaminifu, ulinganifu hauwi kati ya aliye mwaminifu na asiye mwaminifu, la, wote wawili walikuwa waaminifu, na mwandishi hakutaja dosari yo yote katika uaminifu wa Musa. (Twajua dosari zilikuwepo ila hapo hazitajwi, mwandishi anataka kutilia mkazo uaminifu wa Musa). Pia wote wawili waliitwa na kutumwa na Mungu yule yule.

k.3ku. Tofauti iko wapi? Tofauti moja kubwa inayomwonyesha Yesu kuwa mkuu ni kwamba Musa alifanya kazi katika *nyumba „jsiyo yake"* akiwa *mtumishi katika nyumba hiyo ambayo ni* nyumba ya Mungu. Bali *Kristo ni mwenye nyumba, Yeye ndiye nyumba,* Yeye ni mjenzi wake aliyeibuni na kuamua jinsi jengo litakavyokuwa. Msanifu mjenzi ni yule mwenye uwezo wa kubuni na kupanga kila kitu jinsi itakavyokuwa. Katika mawazo yake, mwenye ustadi huo anao uwezo wa kuona jinsi nyumba itakavyokuwa. Jengo linalotokea ni matokeo ya mawazo yake, kwa njia ya jengo mawazo yake yaonekana wazi. Yesu ni mjenzi msanifu wa nyumba ya Mungu.

Mwandishi hakutaka kumshusha Musa kuhusu uaminifu wake, ila alipambanua kati ya vyeo vyao, Musa ni mtumishi, Yesu ni Mwana na Mjenzi wa nyumba.

Kwa hiyo, swali lililopo ni „nyumba ya Mungu" ni nini hasa? Wakati wa Musa bila shaka ilikuwa Taifa la Israeli pamoja na wazo la kuwa Hema ya Kukutania. Musa alipewa uongozi wa kila kitu cha kufanywa katika hiyo Hema, kwa sababu vyote vilikuwa vikiashiria mambo ya baadaye. Vilifundisha watu juu ya Mungu na Utakatifu wake, pia juu ya wanadamu kuwa wenye dhambi, na juu ya haja kubwa ya upatanisho kati ya Mungu Mtakatifu na mwenye dhambi. Hivyo Musa alipewa uongozi kamili wa kila kitu pamoja na habari ya sadaka za kutolewa, na wahudumu wake, na Sikukuu ya Upatanisho n.k. Hayo yote yalikuwa vivuli tu, vya muda tu, mpaka atakapokuja Kristo na kutimiza yote katika kufanya upatanisho halisi.

Pia twaweza kusema kwamba „nyumba ya Mungu" ni ulimwengu na vyote vilivyomo. Yesu alihusika katika uumbaji (Yn.1:3: Kol.1:16ku). Kwa hiyo, heshima yake ni kubwa sana wala si hivyo tu, Yeye ni *„mwana"* katika nyumba, Musa alikuwa mtumishi tu. Iko tofauti sana kati ya „mwana" na „mtumishi" katika nyumba. Mwana/Bwana anayo mamlaka katika nyumba yake, bali mtumishi siyo, yeye apaswa kufanya mapenzi ya bwana wa nyumba.

Musa aliashiria mambo ya baadaye yatakayopata matimizo yake katika Kristo. Mipango ya Ibada na sadaka na kadhalika, vyote vilikuwa vivuli kwa mambo ya baadaye, ambayo Kristo aliyatimiza alipokuja duniani. Kila kitu kilichoashiriwa katika mipango ya Ibada n.k. na kila amri vilitimizwa. Kwa mdomo wa Musa Mungu aliahidi kumtuma nabii mwingine atakayeleta ujumbe wake. Kristo alipokuja alisema kwamba alinena yote ambayo Baba alimpa kuyanena (Kum.18:18: Yn.14:24; 17:6,8,14,17). Njia zote za Musa na Yesu zilitoka kwa Mungu. Iliyotangulia ni Musa, ilikuwa ya Torati, ndipo Kristo alifuata akileta neema na kweli, kweli katika maana ya uhalisi (Yn.1:17).

k.6 Hasa, nyumba ni jamii ya watu wa Mungu. Mungu huishi ndani ya waumini kwa njia ya Roho Mtakatifu. Limekuwa kusudi la Mungu kuishi kati ya, na ndani ya, watu wake. Watu wake ni maskani yake (1 Kor.3:16; 6:19; Efe.2:22; Ufu.21:3; Yn.14:20; 17:22,23).

Kwa sababu Yesu ni mkuu kuliko Musa kwa hali zote na katika mambo yote mwandishi aliwasihi wale walioandikiwa walishike sana tumaini lao katika Kristo, wawe na ujasiri wa kudumu katika imani hiyo, hasa wakati kuteswa na imani yao kushambuliwa, wasiangalie nyuma na kutaka kurudi kwenye imani yao ya asili, ya Kiyahudi na kumtumaini Musa badala ya Kristo aliyewakomboa na dhambi zao. Kumwacha Kristo kwa Musa ni kuyaacha makubwa kwa madogo, na ni kuyaacha ya kudumu kwa mambo ya muda yanayopita. Ukweli wa imani yao utadhihirika katika uaminifu wao na kudumu kwao na katika kuendelea kumtumaini Kristo.

3:7-19 Shauri na onyo la kuwa waaminifu hadi mwisho

Tumeona ya kuwa mwandishi, ili awatie waumini moyo wa kudumu kuwa waaminifu kwa Kristo amewaonyesha ukuu na ubora wa Kristo akimlinganisha na Musa. Musa hakukosa katika uaminifu wake kwa Mungu, ila watu waliotoka Misri pamoja naye, wao walikosa imani kisha wakamwasi Mungu. Vivyo hivyo, Kristo ni wa kutegemewa kabisa na kuaminika, ila yawezekana wafuasi wake wafanane na watu wakati wa Musa, wapatwe na moyo wa kutokuamini kisha wakamwasi Kristo na kurudi nyuma.

Hivyo, mwandishi aliitumia Zaburi 95 kuonyesha hatari iliyopo kwa waumini wa „leo" wale walioandikiwa. Alitaka wautambue umuhimu wa kuishikilia sana imani yao katika Kristo, haidhuru wapatwe na vipingamizi mbalimbali. Aliwakumbusha juu ya mambo yaliyotokea wakati wa Musa. Watu waliondoka Misri kwa moyo mkuu, wakaanza safari yao ya kupitia jangwani mpaka nchi ya Kanaani, nchi ya „raha" yao, nchi ya starehe. Wakati walipokaribia kwenye mipaka ya kuingia Kanaani walisita, hawakuamini kwamba Mungu atawapa ile nchi, basi wakakataa shauri la Yoshua na Kalebu, wakayajali mashauri wa watu wengine 10 waliokwenda kuipeleleza nchi. Kwa sababu hiyo, Mungu aliwaacha wazunguke jangwani kama miaka 39 hivi. Mara kwa mara walipopata shida walianza kumnung"unikia Musa na kutaka kurudi Misri kwenye utumwa. (Taz. Kut.17:lku; Hes.20; Kum.6:16-17; Hes.14:22). Mungu aliwakasirisha na kutoa hukumu kali. Mwishowe katika wale wote waliotoka Misri chini ya uongozi wa Musa ni wawili tu walioingia Kanaani, Yoshua na Kalebu, wale ambao waliamini kwamba Mungu atawapa nchi, wakawashauri watu wasonge mbele na kuingia Kanaani.

Mwandishi alitaka kuwaonyesha waumini walioandikiwa kwamba, haitoshi kukata shauri na kumwamini Kristo kwa moyo, inayotakiwa ni kuendelea na kudumu katika kumtumaini Kristo wakati wa shida na mateso. Alikuwa na moyo wa kiuchungaji, akitaka kuwasaidia katika imani yao na safari yao ya kwenda mbinguni, hivyo aliwatahadharisha juu ya hatari waliyokuwa nayo.

Neno „leo" ni muhimu sana. Kielelezo alichotumia kiliwahusu watu wa zamani za kale, hata hivyo kiliwahusu wale walioandikiwa, maana ni Neno la Mungu na

ni Roho Mtakatifu ambaye bado angali akisema na watu wa Mungu kwa njia ya Zaburi hiyo. Alisema na jumla ya waumini pamoja na kwa kila mmoja wao (k.12) Kutokuamini ni kujitenga na Mungu aliye hai. Tangu zamani Wayahudi walifahamu kwamba Mungu ni Mmoja aliye Hai. Hao waliotoka Misri walifahamu hivyo kwa jinsi walivyotolewa Misri kwa maajabu mengi, hata hivyo, wakarudi nyuma. Waumini pia walikuwa wameonja nguvu za Kristo katika kuwatoa katika utumwa mwa dhambi, hata hivyo, hao pia, waweza kuteleza katika imani yao kiasi cha kumwasi Kristo. Ni onyo kubwa kwao, pia onyo hilo lahusu hata sisi wa leo.

k.13,14. Aliwapa shauri jema sana la kuwasaidia ili jambo hilo lisitokee. Njia ni kuonyana wao kwa wao, wasitegemee viongozi wao tu, bali kila Mkristo awe na mzigo juu ya Mkristo mwenzake, wasilegee katika kukutana ili katika ushirikiano wao wajengane. Wamekuwa washirika wa Kristo, ila wamepaswa waendelee na moyo ule waliokuwa nao walipoanza kuamini, kwa sababu, ni katika kudumu mpaka mwisho watakapoifikia raha yao.

k.15 Hapo tena twakuta neno „leo", inaonekana mwandishi aliwaza kwamba wamekaribia hali ya kuteleza kiasi cha kuelekea kuwa tayari kumwacha Kristo na kurudi kwenye dini yao ya asili, ya Kiyahudi.

k.16 Kwa mfululizo wa maswali aliwakumbusha na kutoboa wazi jinsi wale wote wa zamani waliotoka Misri hawakufika nchi ya Kanaani, isipokuwa Yoshua na Kalebu, watu wa imani, watu waliowashauri Waisraeli waendelee mbele na kuingia Kanaani. Hali ya „leo" hali ya „sasa" ni muhimu sana.

MASWALI
Ni kwa mambo gani Yesu ni mkuu kuliko Musa?

Mwandishi ametumia mfano wa Waisraeli, wakati wa Musa, kuwa njia ya kuwaonyo waumini. Kwa nini walihitaji kuonywa?

4:1-16 Yesu ni mkuu kuliko Yoshua

4:1-11 Ahadi ya raha ipo

Mwandishi anafuata hatua za Waisraeli katika historia yao ya kutoka utumwani. Hapo amefikia habari za Yoshua na jinsi ambavyo yeye aliinuliwa na Mungu kumfuata Musa na kuwaingiza Waisraeli katika nchi ya ahadi, nchi ya raha. Katika nchi hiyo watatulia, wataishi bila wasiwasi, wakimwabudu Mungu kwa jinsi walivyoambiwa na kuzishika Amri zake walizopewa. Yawezekana habari hii ya raha inadokezea raha ambayo ni zaidi ya kuingia Kanaani.
Mwandishi anajenga hoja yake juu ya jambo hilo, na katika kufanya hivyo inaonekana anawaza „raha" kwa njia mbalimbali, kihistoria, na kiroho.

Raha hiyo imefananishwa na raha ya sabato ya Mungu. Mungu alipomaliza kazi zake za uumbaji twasoma kwamba „akastarehe siku ya saba" akiifurahia kazi zake katika uumbaji (Mwa.2:1). Yesu naye, baada ya kazi yake ya ukombozi aliingia raha yake. Haina maana kwamba Mungu na Yesu hawafanyi kazi yo yote, la. Ni kama Mungu ametulia kwa sababu uumbaji unaendelea sawasawa, mfano wa makaniki ambaye ametengeneza mtambo na kuiachia ifanye kazi yake.

Maana ya raha kwa upande wa historia ya Waisraeli ni raha ya kufika na kuishi katika nchi ya ahadi.

k.1-2 Ahadi ya raha inayozungumzwa katika vifungu hivi bado ingaliko nayo ni ahadi ya kushikwa na watu. Ni raha kwa kila muumini. Walioandikwa waipokee kwa imani, wasiwe kama wale Waisraeli waliokosa kuingia Kanaana kwa sababu ya kutokuamini kwao, walinung"unika na kufanya dhambi bila kujali, iwapo walikuwa wametolewa utumwani kwa maajabu mengi ya Mungu. Iwapo walitoka Misri mioyo yao haikubadilika. Walikuwa na misaada mbalimbali, walikuwa na Hema ya Kukutania, walikuwa na dhabihu za kuwaashiria msamaha wa Mungu, walikuwa na Amri Kumi zilizowajulisha maadili waliyodaiwa na Mungu. Waliongozwa na wingu usiku na mchana. Musa na wenzake waliwapa ujumbe wa Mungu, hata hivyo, walikuwa na mioyo migumu. Na kwa sababu hiyo *wakakosa* kuingia Kanaani.

k.3-7 Lakini habari hiyo si juu ya Waisraeli tu. Inawahusu waumini wa leo, maana iko „raha" kwa watu wa Mungu. Ni raha ambayo Yesu anatoa katika Injili yake (Mt.11:28). Yesu ametoa ahadi ya kuwapumzisha wale wanaomjia, kwa kuwa watu huokolewa kwa kazi zake za ukombozi alizofanya pale Msalabani. Kwa kumpokea Yesu na wokovu wake tumewekwa huru na haja ya kutegemea mbinu na juhudi zetu, maana kwa njia ya kujitegemea hakuna mtu ye yote awezaye kujiokoa. Kwa kutubu na kumpokea Kristo mtu hupata raha nafsini mwake, aingizwe katika makusudi ya Mungu na humo ashiriki „raha ya Mungu". Wakati wa kuingia raha hiyo ni Sasa. Daudi alitaja jambo hilo, kwa hiyo, ni dhahiri kwamba raha inayozungumzwa ni zaidi ya ile ya kuingia Kanaani, maana wakati wa Daudi kusema maneno hayo Waisraeli wameishafika na kustarehe katika Kanaani (Yos.21:43-45; 22:4).

3:8ku. Basi, imesalia raha ya sabato kwa watu wa Mungu, raha kama ile ya Mungu. Ni raha ya „kustarehe katika kazi zake". Wokovu ni kipawa cha bure, cha neema, kutokana na ustahili wa Kristo si ustahili wetu. Mungu. Kristo amefanya yote yaliyohitajika ili mtu apate msamaha wa dhambi na uzima wa milele. Ni raha inayopatikana kwa imani. Kwa kawaida, wanadamu kwa sababu ya kiburi chake hupenda kuchanga kitu, yaani kufanya jambo fulani la kujistahilisha, lakini hali hii ni kinyume cha mapenzi ya Mungu na njia ya wokovu iliyowekwa kwa kila mwanadamu. Mungu humpokea kila mtu ambaye anampokea Mwana wake. Ila k.11 ni ukumbusho ya kuwa iwapo hatuokolewi

kwa matendo yetu mema au juhudi zetu, hata hivyo, twapaswa kuwa na bidii katika kumtumikia Mungu kwa furaha. Bidii si ile ya kutafuta kibali cha Mungu bali ni bidii ya shukrani kwa sababu tumeishakubalika na Mungu. Jambo hilo limewekwa wazi katika Efe.2:8-10; Flp.2.12-13; 4:13; Gal.2:20; Yn.15:5. Kwa hiyo, raha hii ni jambo la kiroho, ni raha ya imani katika Kristo.

4:12-13 Uwezo wa Neno la Mungu

Kisha mwandishi ametaja „Neno la Mungu" na sifa zake. Katika k.13 ameacha kusema juu ya Neno la Mungu na kusema juu ya Yule mwenye Neno na aliyemo katika Neno. Ni kama mamoja. Ameeleza Neno kuwa kitu kilicho hai, chenye uwezo wa kutoboa wazi viini vya mioyo yetu na kuyapambanua mawazo yetu na kuyahukumu. Ni Neno la Mungu lililo na uwezo wa kutufahamisha tulivyo hasa, kwa hiyo ni kiongozi cha kutegemewa sana. Neno la Mungu ni sawa na Mungu hai anayesema nasi katika Mwana wake. Twahitaji kulisoma kwa makini, na kulitia maanani, na kulitii. Neno la Mungu litatufunulia hatari ya kujitegemea na haja ya kumtegemea Mungu kwa kila kitu na kila hali. Lina nguvu ya kutimiza shabaha yake (Isa.55:10,11).

Kwa hiyo, hoja ya sura hii ni kwamba Mwana ni mkuu kuliko Yoshua na raha ya Yesu ni bora kuliko ile ya Yoshua ya kuwastarehesha Waisraeli katika Kanaani. Raha ya Yoshua ilikuwa ya kimwili, raha ya Yesu ni ya kiroho, kwa nafsi zetu, ni raha kamili. Bila imani katika Kristo mtu hawezi kujua hiyo raha katika ujuzi wa kibinafsi.

Katika sehemu hiyo, neno moja limerudiwa mara kwa mara, nalo ni „Jeo". Neno hilo linaweza kuhusu wakati wo wote ambalo jambo fulani limefungwa katika muda fulani na kwa sababu hiyo mtu hutakiwa kumtii Mungu katika muda huo, yaani katika „Jeo". Raha yetu inategemea utii wetu. Yapo mambo yanayodai utii wetu katika muda fulani na muda huo ukipita, basi nafasi ya utii inapita, na ikipita mtu hukosa „raha" nafsini mwake.

Kuanzia 4:14 hoja kubwa yahusu Ukuhani Mkuu wa Yesu, Mwana wa Mungu. Hoja hiyo inaendelea katika sura zinazofuata.

4:14-16 Yesu ni Kuhani Mkuu aliye Mkuu kuliko Haruni

k.14 Kifungu hicho chasema kwamba tunaye Kuhani Mkuu aliyeingia mbinguni.Yesu ndiye huyo Kuhani Mkuu aliyeyashinda majaribu yake yote na kutokana na ushindi wake amefika mahali bora, yaani ameingia mbinguni kwa Mungu, Baba yake. Ameitwa „mkuu" kwa sababu ya ushindi huo. Mwandishi amependa sana kulitumia jina la „Yesu" akiukaza ubinadamu wake, jambo mojawapo lililomstahilisha na kumfanya afae kuwa kuhani wetu. Pamoja na hayo,Yesu ni Kuhani Mkuu wa kipekee, kwa kuwa Yeye ni Mwana wa Mungu aliyetoka mbinguni. Mambo hayo mawili, ubinadamu wake, na uungu wake, yamemfanya awe Kuhani Mkuu wa kipekee. Haruni aliyekuwa kuhani mkuu

Makuhani

zamani za kale, wakati wa Waisraeli kutoka utumwani mwa Misri, alikuwa mwanadamu, na alitumika katika Hema ya Kukutania hapa duniani. Yesu afaa kuwa Kuhani wetu mkuu kwa sababu, katika maisha yake ya kibinadamu, alizionja taabu nyingi za aina mbalimbali. Alijua kucheka na kulia, kuhitaji mahitaji ya kimwili, kujaribiwa na dhambi. Alisikia ugumu wa kupingwa na kukataliwa, alichukiwa kiasi cha kuuawa. Maisha yake yote yalijaa majaribu. Alikuwa na nguvu na uwezo zaidi yetu, lakini viliongeza taabu zake. Yeye asiye na dhambi alistahimili na kudumu mwaminifu bila kufanya dhambi. Alisikia uvutiko mkali wa dhambi kuliko sisi ambao hatushindani na dhambi na kuyapinga majaribu mpaka mwisho, kama Yeye. Yeye aliyashinda yote, sisi hatuyashindi yote, ndiyo tofauti kati ya Kristo na sisi. Alifanya hayo kwa ajili yake na kwa ajili yetu, ili ushindi wake uwe ushindi wetu.

Waumini walioandikiwa waliitwa kuwa wakakamavu na kuishika na kuishuhudia imani yao na kuwa tayari kumkiri Kristo hata ikiwa watashtakiwa barazani. Mwandishi aliwakumbusha habari za Yesu mbele ya Liwali Pilato, alipoulizwa kwa kiapo kuukiri Umasihi wake na Uana wake, akakubali, hali akijua kwamba kwa kufanya hivyo, ni kama kutia sahihi kwenye cheti cha kuuawa kwake, kwa sababu, ilihesabiwa kufuru kudai kuwa Masihi, Mwana wa Mungu. Kuhani mkuu alimwapiza kwa kiapo akitafuta kupata neno la kumshtaki (Mt.26:63ku. 1 Tim.6:13).

k.15 Inawezekana mtu afikiri kwamba kwa sababu Yesu yupo mbinguni, mahali pa juu sana haitawezekana ajiweke mahali petu na kutuhurumia. Lakini sivyo ilivyo. Katika ulimwengu ulio kinyume chao, waumini wapaswa wasimwonee Kristo haya, wasiache imani yao wakati wa misukosuko au wakati wa mateso. Yesu Mwenyewe amejua katika ujuzi wa maisha yake ugumu wa kujaribiwa. Alijaribiwa kupita mwanadamu awaye yote akikutana na majaribu makali sana na kuyapinga kabisa. Kwa ye yote anayekubali majaribu ugumu wake unapungua, na kwa kiasi anachopinga ugumu unazidi. Yesu ameelewa yale yanayowapata na jinsi wanavyojisikia, Yeye ajua kwamba tu dhaifu, na kwa nguvu zetu hatuwezi kusimama imara. Jambo kubwa ni kwamba Yesu alipojaribiwa hakuanguka, hakufanya dhambi. Hata sisi, hakuna sababu ya sisi kuanguka au kufanya dhambi. Yesu ametoa kielelezo chema. Hatawaacha peke yao bila msaada.

Dhambi ni kizuizi kikubwa katika kushirikiana na Mungu. Ni kwa kutokufanya dhambi mtu aweza kupima ubaya wa dhambi.

k.16 Wito ni kukaribia kwa sababu ni kiti cha neema si kiti cha hukumu. Pamoja na kielelezo cha Yesu waumini wanayo misaada mikubwa; wana mahali pa kukimbilia na mtu wa kumkaribia wakati wa majaribu. Mahali ni „kiti cha neema" neno „kiti" linashiria kwamba ni mahali pa uwezo na mamlaka, mahali pa Mungu Mwenyewe. Pia ni mahali pa neema kutokana na dhabihu ya Kristo, alipoitoa nafsi yake kuwa fidia ya dhambi pale Msalabani. Pale twapewa rehema kwa dhambi za nyuma, msamaha, twaachiliwa kuhukumiwa iwapo twastahili kuhukumiwa. Pia twapata neema, twapewa baraka tele za Mungu kwa wakati huo wa sasa. Twahitaji rehema kwa yaliyopita na neema kwa yanayokuja. Waumini waliitwa kukikaribia hicho kiti cha neema kwa ujasiri, kusudi wajaliwe msaada wa Mungu wakati walipojaribiwa kumwacha Kristo na kuzirudia desturi zao katika dini ya Kiyahudi, yaani kuyarudia mambo ya Musa na Haruni na kumwacha Kristo. Wakifanya hivyo ni kumwacha Kuhani Mkuu, wa kipekee, mwenye uwezo, awezaye kuchukuana na udhaifu wao na kuwasaidia. Ni Kuhani Mkuu wa kipekee kwa sababu alikuwa Mungu Mwana aliyeshuka kutoka mbinguni na kurudi mbinguni baada ya kuupata ushindi wake. Haruni hakufanya hivyo. Yesu alizishinda nguvu za dhambi, za mauti, na za Shetani. Penye kiti cha neema waumini hukutana na Yesu, Kuhani Mkuu. Kuomba kunahitajika sana katika maisha ya Kikristo, lazima tumwendee Yesu na

kuupata msaada Kwake. Katika Agano la Kale makuhani waliwekwa na Mungu ili wawe kati ya Mungu Mtakatifu na watu. Waliwakilisha wanadamu kwa Mungu na Mungu kwa wanadamu, kama wapatanishi. Waliitwa kuwa watakatifu kama Mungu alivyo Mtakatifu. Huduma yao ilikuwa kutoa dhabihu za dhambi siku kwa siku na mwaka kwa mwaka.

MASWALI

1. Eleza aina za raha zinazotajwa katika sehemu hiyo. Raha kwa Mkristo ni raha ipi?

2. Andika vifungu vya k.12 na k13 kwa maneno yako mwenyewe.

5: 1-10 Sifa za Kuhani Mkuu

Katika sehemu hii mwandishi anaendelea na hoja yake juu ya ubora na ukuu wa Yesu na ukuhani wake kuliko ukuhani wa Haruni na wenzake.

k.1-4 Alieleza habari kuhusu kila kuhani mkuu. Kwanza, kila kuhani mkuu alichukuliwa kutoka jamii ya wanadamu, akiwa mwanadamu. Shabaha ilikuwa awe kati ya Mungu na wanadamu akiwawakilisha wanadamu kwa Mungu na kuwashughulikia, hasa katika mambo yamhusuyo Mungu. Kazi muhimu ya kila kuhani ilikuwa kutoa dhabihu kwa ajili ya dhambi za udhaifu na za kutokujua zilizofanywa na watu. (ling. Na Hes.15:30,31; Kum.17:12 hakuna msamaha kwa dhambi zilizofanya kwa kusudi na kwa dharau na fidhuli). Kwa sababu kuhani mkuu alitolewa katika wanadamu walio dhaifu ilimpasa atoe dhabihu kwa dhambi zake kabla ya kuzitoa kwa ajili ya wengine. Jambo hilo lilionyesha kwamba, iwapo mtu alichaguliwa na kuwekwa na Mungu kwa neema, hata hivyo alikuwa dhaifu.

Ilimbidi awe pole, mwenye tabia ya kuwahurumia watu, hali akitambua udhaifu wake and udhaifu wao, na jinsi ilivyo vigumu kuishi bila kukosa.

Kwa sababu kazi hiyo ni takatifu sana, mtu asithubutu kujiinua na kujiweka kuwa kuhani mkuu, **lazima awe ameitwa na kuwekwa na Mungu**, kama ambavyo zamani za kale Haruni alivyochaguliwa na kuwekwa na Mungu.

Kwa hiyo, yalikuwepo mambo mawili makubwa: kwanza, kwa upande wa wanadamu, budi kuhani mkuu atoke katika wanadamu wenzake ili aweze kujiweka mahali pao na kuwahurumia na kuchukuliana nao, maana hata yeye mwenyewe alijua jinsi alivyo dhaifu. Pili, kwa upande wa Mungu, budi kuhani mkuu awe amechaguliwa, na kuitwa, na kuwekwa na Mungu.

k.5ku. Ndipo mwandishi aliyachukua mambo hayo mawili na kuonyesha jinsi yalivyomhusu Kristo na ukuhani wake. Alianza na habari ya Yesu kuitwa na

kuwekwa na Mungu. Mwandishi alitumia maneno kutoka Zaburi 2 na Zaburi 110. Huyo Yesu aliyewekwa alikuwa Mwana wa Mungu, pia alikuwa Mfalme. Pamoja na hayo hakuwa na dhambi. Akiwa mwanadamu halisi aliishi bila kufanya dhambi iwapo alijaribiwa sana kupita wanadamu wengine wote. Kwa sababu hiyo, hakuwa na haja ya kutoa dhabihu kwa ajili yake mwenyewe. Akiwa kuhani mkuu alitoa dhabihu kwa ajili ya dhambi za wanadamu wengine wote. HivyoYesu hakuwa na upungufu wala kasoro yo yote katika ukuhani wake.

k.6b Ukuhani wa Yesu ulijengwa juu ya ukuhani wa Melkizedeki. Huyo Melkizedeki alikuwa nani? Aliishi wakati wa Ibrahimu (Mwa.14:1ku) akiwa kuhani na mfalme. Baadaye, nyakati za Musa na Haruni, Haruni alichaguliwa na Mungu na kuwekwa kuwa kuhani tu, hakuruhusiwa kuwa Mfalme pia. Nyakati za mwungano wa vyeo vya Ukuhani na Ufalme zilikuwa zimepita. Ndiyo sababu mojawapo ya kumwita Yesu kuhani mfano wa Melkizedeki maana Yesu alikuwa Kuhani Mkuu na Mfalme pia.. Halafu neno „milele" limetumika. Kwa nini? Melkizedeki alikuwa mwanadamu, ila Maandiko hayataji wazazi wake, wala asili yake, alionekana kama **yupo** tu (siyo kwamba hakuwa na wazazi n.k. ila mwandishi aliandika habari zake ili aweze kuwa *mfano wa ukuhani* wa Bwana Yesu. Hivyo, amekuwa *mfano* wa Yesu aliye wa milele. Tukumbuke kwamba mwandishi *aliandika* kwa mtindo wa marabi (waalimu wa Kiyahudi) kwa sababu alikuwa akiwaandikia Wayahudi waliozoea mtindo huo wa kuwaza. Tutarudi kumtafakaria Melkizedeki katika sura ya saba.

k.7ff. Baada ya kusema juu ya wito wa Yesu kuwa kuhani mkuu mwandishi aliendelea kuonyesha jinsi Yesu alivyolitimiza sharti lingine kuhusu ukuhani. Sharti hiyo ni juu ya kuwa na tabia ya kuchukuliana na udhaifu wa wanadamu na kuwahurumia na kuwafanyia kwa upole. Walioandikiwa walikumbushwa juu ya taabu za Yesu alipokuwa mwanadamu na kuishi hapa duniani kati ya wanadamu wengine. Alizionja dhiki na shida zilizozidi kawaida ya wanadamu kuzipata, hasa alipokaribia mwisho wa maisha yake. Katika Bustani ya Gethsemane alisikia dhiki kubwa alipokabili kifo chake cha msalabani, kifo cha kufanya fidia ya dhambi, wakati atakapohesabiwa mwenye dhambi na kufa kifo cha wenye dhambi na kuwa badala ya wenye dhambi, na kutwishwa dhambi zote za wanadamu. Katika Bustani ya Gethsemane alilia kwa Baba yake, aliomba sana, na kutokana na ujuzi huo wa kusononeka, alijifunza kumtii Baba na mapenzi yake. Si kana kwamba alikuwa hakumtii Mungu hapo nyuma, ila katika kukutana na mambo hayo magumu alizidi kujifunza kibinafsi ni nini kumtii Mungu. Hata msalabani, alizidi kujifunza huo utii. Alijulikana kama mtu aliyemcha Mungu. Hakuutumia uwezo wake wa kiMungu na kujiokoa bali alimtegemea Roho Mtakatifu na Neno la Mungu kumwongoza. Yawezekana tufikiri kwamba kwa sababu alikuwa Mwana hakuwa na haja ya kujifunza utii, lakini ilikuwa lazima kutokana na kuzaliwa mwanadamu. Kujifunza utii kulimstahilisha kuwa kiongozi wa wote watakaookolewa, maana hao nao wapaswa utii. Kwa sababu aliteswa aweza kuwahurumia wale wanaoteswa, na

bila shaka mwandishi aliandika hayo kwa ajili ya wale waliokuwa wamesikia shida kiasi cha kutaka kuiacha imani yao ya Kikristo na kurudi kwenye dini yao ya asili ya Kiyahudi, ili waepukane na dhiki na mateso. Alitaka wafahamu kwamba jaribio wanalolipata ni dogo kuliko lile lililompata Yesu (Isa.50:5-6). Tukumbuke kwamba Kuzaliwa kwa Yesu na Kibali chake cha kufanyika mwanadamu kulikuwa jambo la utii (10:7). Katika ujana wake alionyesha tabia ya utii (Lk.2:49, 52). (Ling. na Yn.17:4; Flp.2.8; Yn.4:34; 5:30; 6:38; Rum.15:3).

k.9,10 Maneno „alipokwisha kukamilishwa" hayana maana kwamba ulikuwepo wakati ambapo Yesu hakuwa kamili, la. Maana yake ni kwamba kutokana na ujuzi wa maisha alizidi kukomaa. Kwa mfano, mchungaji/pasta amekuwa mchungaji/pasta kamili siku ile anapoamriwa na Askofu, halafu, anapoendelea kufanya kazi ya mchungaji ya kuzitunza roho za watu, *azidi kujifunza kuwa mchungaji*, na kwa njia hiyo azidi kukamilishwa, ili awe amestahili kuitwa mchungaji/pasta. Amekuwa mchungaji kiutendaji si kwa cheo tu.

Amekuwa sababu ya wokovu kwa sababu ya ushindi wake wa kutoka wafu baada ya kufa na kutukuzwa kwake, wokovu wa milele kwa wote wanaomtii. Kama Yesu alivyopaswa utii na wokovu umepatikana kwa kutii kwake, hata sisi nasi twapaswa utii, na wokovu alioupata ni wetu kwa njia ya utii.

5:11-14 Ulegevu wa wale walioandikiwa

Katika sehemu hiyo mwandishi amewalaumu wale anaowaandikia kwa sababu iwapo wamekuwa waumini kwa muda mrefu hawajakua katika ujuzi wa imani ya Kikristo na katika kuishi maisha ya Kikristo. Mwanzoni walianza vizuri ila baadaye wamepoa na kulegea, kwa hiyo, badala ya kukomaa katika imani yao wamelegea.

k.11 Mwandishi angependa kuendelea katika kuwafundisha juu ya Melkizedeki na hasa juu ya uzuri na faida kubwa ya Ukuhani Mkuu wa Bwana Yesu. Katika k.11 ametaja shida yao kuwa uvivu wa kusikia, yaani hawataki kufundishwa, wamekuwa radhi na mambo ya kwanza kuhusu Imani ya Kikristo, ambayo mwandishi ameyaita „maziwa". Akiwa na mzigo juu ya roho zao alitamani sana kuwaelimisha mambo mengine yaliyo faida kwa maendeleo yao ya kiroho, hayo mengine ameyaita „nyama".

k.12 Hapo twajifunza wamekuwa Wakristo kwa muda mrefu. Kwa sababu ya uvivu wao wamekuwa waumini wasio na uwezo wa kutoa mafundisho kwa wengine. Bado wangali walihitaji msaada badala ya kuwa waumini wa kutoa msaada. Kutokuendelea katika ufahamu wa imani yao pamoja na kuwa na upungufu katika kupambanua yaliyowapasa kufanya katika maisha ya kila siku kumesababisha wafike kwenye hali ya hatari kwa roho zao. Hapo nyuma alikuwa amewaonya juu ya kutokuamini kwa Waisraeli walipopita jangwani, sasa hao wanaoandikiwa wamo katika hatari iyo hiyo.

k.13 Hawana udhuru. Kila muumini huhitaji „maziwa" yaani kuanza na mambo ya kwanza ya Kikristo. Kila mtoto azaliwapo hupewa „maziwa" ni kawaida, yanamfaa, vilevile na Mkristo, huanza kwa „maziwa". Lakini Je! Kama mtoto hakui, wazazi watawazaje? Si watawaza kwamba huyo mtoto wetu ni „mgonjwa", maana ni kanuni kwamba kila mtoto mdogo akue na azidi kukua. Mtoto akibaki na mikono mifupi au miguu mifupi, hata ikiwa anacho kiungo kimoja tu kilichopungua, wazazi watakuwa na mashaka juu ya mtoto.Ndivyo ilivyo kwa kila muumini. Kila chakula chafaa kwa wakati wake. Lazima Mkristo akue katika ufahamu wa imani yake na katika kuishi maisha yampasayo kama mfuasi wa Kristo. La, sivyo, ni kweli kabisa kwamba ana shida. Mwandishi haulaumu „uchanga" wa muumini wakati wa kwanza wa kuamini kwake, kitu anacholaumu ni kutokua kwake baadaye. „neno la haki" maneno hayo, huenda yahusu fundisho la kuhesabiwa haki kwa imani na jinsi mtu huletwa katika uhusiano mwema na Mungu kwa kuutegemea upatanisho alioufanya Yesu msalabani. Pia, habari ya kutenda haki, yaani kufanya mema ya kumpendeza Mungu baada ya kuhesabiwa haki kwa imani (Efe.2:8-10). Paulo alitumia mfano wa „maziwa" na „chakula kigumu" (1 Kor.3:1-2).

k.14 Muumini hukua kwa njia ya kujizoeza, budi awe na hamu ya kujua zaidi akitaka kufundishwa zaidi mpaka ameelewa zaidi, ndipo baadaye ajitoe kuwafundisha waumini wapya. Bila kujizoeza atashindwa kujua jinsi ya kutenda anapokutana na mambo yanayohitaji aamue la kufanya pia atakosa uwezo wa kuyapambanua kati ya mafundisho yaliyo kweli na mafundisho yasiyo kweli.

MASWALI

Eleza kazi za makuhani na tabia zinazohitajika kwa kufanya kazi ya ukuhani.

Onyesha jinsi Yesu alivyokuwa na tabia zilizohitajia ili awe Kuhani Mkuu afaaye.

Eleza hali za wale walioandikiwa.

6:1-8 Tatizo na hatari ya kutokukua kiroho

k.1-3 Mwandishi anaendelea na hoja yake juu ya hatari ya kutokukua kiroho, hatari iliyowakabili wale aliokuwa akiwaandikia. Mwisho wa sura ya tano alieleza jinsi alivyoshindwa kuwafundisha „chakula kigumu" kwa sababu walikuwa wangali wakitumia „maziwa" tu. Hayo yote kwa sababu walikuwa wavivu na walegevu katika kuongeza ufahamu wao wa mafundisho ya Kikristo pamoja na kushindwa kuishi maisha yaliyotakiwa.

Kitu alichotamani kuwafundisha kilihusu Ukuhani Ukuu wa Bwana Yesu, ukuhani uliokuwa wa mfano wa Melkizedeki, na jinsi Yesu, Mwana wa Mungu,

aliye Hai, aweza kuwa msaada mkubwa katika maisha yao ya kiroho. Neno hilo atalieleza zaidi baada ya sura hiyo ya sita.

Ni watu waliokwama katika mambo ya kwanza ya Imani ya Kikristo. Hayo mambo yalikuwa lazima kwa mtu aliyeongoka na kumwamini Kristo, *ni msingi imara ambao juu yake kila muumini alipaswa kujengwa juu yake*. Wamekuwa Wakristo wa muda mrefu, na bila shaka walianza vizuri, ila kosa lao wamebaki pale pale walipoanza. Mwandishi ameyataja mambo sita kama msingi wa kuanza maisha ya Kikristo. Kwanza ni jambo la toba, tangu mwanzo jambo hilo lilikuwa la kwanza kwa kila aliyetaka kumfuata Kristo. Yohana Mbatizaji alitayarisha njia ya Bwana Yesu kwa kutangaza neno la „tubuni" na kuwabatiza watu ubatizo wa toba. Ndipo Bwana Yesu alianza huduma yake na neno „tubuni". Maneno „kuzitubia kazi zisizo na hai" huenda maneno hayo yaliwalenga Wayahudi waliojitahidi kuishika Torati pamoja na sheria nyingi ndogondogo zilizoamriwa katika dini yao. Hizo zote hazimfikishi mtu kwenye uzima, pia mwisho wa dhambi ni mauti. Halafu jambo la pili lililotajwa ni „imani kwa Mungu". Wakati wote ujumbe wa Kikristo ulikuwa „tubuni, mmwaminini Kristo". Ni kumwamini Kristo katika hali ya kujitoa Kwake na kuingia katika ushirikiano mwema na Mungu. Mafundisho ya mabatizo – ubatizo wa Kikristo hasa ni mmoja, Wayahudi walizoea maosho mbalimbali. Labda baadhi yao walitatizwa kujua uhusiano uliopo kati ya ubatizo wa Yohana Mbatizaji na ubatizo wa Yesu. Mtu alibatizwa mara alipomkiri Kristo kuwa Mwokozi wake, ni neno lililoamriwa na Yesu (Mt.28:19). Kwa ubatizo muumini aliingizwa katika Kanisa, katika jamii ya waumini. Kumbe hao walioandikiwa bado wamekaa pale pale penye mambo hayo yaliyokuwa ya kwanza kabisa kwa kila mtu aliyeanza kumfuata Kristo. „Kuwekea mikono" kulifanywa kwa mambo mbalimbali – kwa kumpokea Roho Mt. (Mdo.8:17; 9:18; 10:47-48; 19;6) kwa uponyaji (Yak.5:14; Mdo.28:8) wakati wa kuchagua na kutuma watu kwa huduma fulani (Mdo.13:3). Jambo lingine la kimsingi ni „kufufuliwa wafu". Fundisho la ufufuo lilikuwa fundisho kubwa kutokana na Yesu kufufuka kutoka wafu. Katika dini ya Kiyahudi, Mafarisayo waliamini kwamba kuna ufufuo wa wafu mwisho wa mambo yote, lakini katika Imani ya Kikristo fundisho hilo ni kubwa kabisa, lilitajwa pamoja na Yesu kusulibiwa kuwa mambo makubwa katika Injili (1 Kor. 15:1-4). Hukumu ya milele ni jambo lingine ambalo waumini wapya walifundishwa. Hata katika dini ya Kiyahudi hukumu ilikuwepo. Yawezekana hao waumini walioandikiwa, ambao inaonekana wametoka katika dini ya Kiyahudi walikuwa bado wanashikilia baadhi ya mafundisho hayo kwa kuyawaza kama walivyozoea kuyawaza kabla ya kuwa Wakristo, bila kuongeza ufahamu wa mambo hayo katika mwanga wa Kristo.

Mwandishi anatamani sana kwamba, hao waumini, kwa msaada wa Mungu, wataache uvivu wao na kuwa na hamu ya kujifunza zaidi juu ya imani yao pamoja na kuzidi kuishi kulingana na hayo mafundisho.

k.4-8 Mambo yanayotajwa katika vifungu hivi yamewatatizwa Wakristo. Wengine wameuliza Je! Hao waliotajwa kuwa „waliokwisha kupewa nuru…." Walikuwa wameongoka kweli, au walikuwa wamejifanya kuwa wameongoka, au walioonekana katika jamii ya waumini kama wameongoka? Halafu wengine wawaza kwamba mwandishi aliyatumia maneno magumu ya kuwaonya kwa ukali ili afaulu kuwatisha kiasi cha kuwafanya wajirekebishe, ila hayo aliyoyasema juu ya isivyowezekana kutubu hayatatokea kwa kweli, ni maneno ya kitisho tu.

Mwandishi alianza sehemu hiyo kwa kueleza jinsi waumini walivyo; ni watu waliokwisha kupewa nuru….. na kukionja kipawa cha mbinguni……na kufanywa washirika wa Roho Mtakatifu…..na kulionja neno zuri la Mugu, na nguvu za zamani zijazo. Tunaposoma maneno hayo tunaona kwamba hayo ni maelezo mazuri ya waumini wa kweli. Mwandishi amesema kwa nguvu kwamba haiwezekani kwa hao watu wakimwacha Kristo na kuirudia imani yao ya Kiyahudi, wamrudie Kristo baadaye, wakatubu na kufanywa upya. Ina maana kwamba kumpa Kristo kisogo ni hatua ya mwisho isiyotenguka. Kwa nini ni hivyo? Hali ya mtu afanyaye jambo hilo ni baya, moyo wake umekuwa mgumu, rohoni mwake amekufa ganzi hata asiweze kujisikia, wala kubadilika. Yesu alisema juu ya kukufuru Roho Mtakatifu, dhambi isiyo na msamaha kwa sababu mtu hushindwa kutubu (Mt.12:21). Hali hiyo inafanana na hali ya Waisraeli jangwani (1 Kor.10:1-5). Ni dhambi gani inayosemwa? Ni dhambi ya uasi. Hao waumini wakimwacha Kristo kwa Musa, Haruni, n.k. yaani kwa dini ya Kiyahudi, watakuwa wamejiweka upande wa wale waliomsulibisha Bwana Yesu, wale Wayahudi waliomdharau Bwana Yesu kiasi cha kumtemea mate na kumlaani, na kumkatalia mbali. Jambo hili halitokei ghafula bali ni mwenendo wa muda mrefu. Mwandishi alianza kuwaonya katika sura ya pili 2:2ku. na tena katika sura ya tatu 3:12ku. Aliwaonyesha jinsi uasi ni kukosa kabisa kuwa na matumaini. Ni kufika katika hali ya kutokuweza kutubu.

Alitoboa wazi ni nini watakuwa wanafanya wakimwasi Kristo. Watakuwa wanavidharau vipawa vya Mungu; wanamsulibisha na kumfedhehi kwa wazi Mwana wa Mungu, yaani watafanana na wale waliomsulibisha Bwana Yesu; halafu wanazipoteza baraka za Mungu. Watafanana na nchi inayoinywa mvua halafu inatoa miiba na magugu ambayo yanachomwa moto baadaye badala ya kuzaa mboga kwa manufaa ya watu. Ni mwisho mbaya kabisa. Katika mfano wa mpanzi Yesu alisema juu ya mbegu iliyoanguka kwenye njia na nyingine kuanguka penye mwamba na nyingine penye migugu, ambazo hazizai matunda (Mt.13:8.9; 18-23; Ling. Na Mt.7:16, 21). Tunakumbushwa habari za Yuda Iskariote, na Dema (2 Tim.4:10), na katika Mdo.8;9,13-24 tuna habari za Simon Mchawi ambaye alikuwa na shida kubwa iwapo alikuwa amemwamini Kristo na kubatizwa. (2 Pet. 2:20-21).

Baadhi ya Wakristo huamini kwamba mtu aliyeongoka hawezi kurudi nyuma kiasi cha kupoteza wokovu wake (Yn.10:14,27-29; Rum.8:29,30; Efe.1:3-7) na

ya kwamba maneno hayo ya mwandishi yaliwahusu wale ambao *walionekana* katika jamii ya waumini ambao walikuwa hawajaokoka kweli. Ila kwa jinsi alivyosema katika k.4 ni vigumu kufikiri hivyo kwa sababu inasema „*waliokwisha kupewa nuru*"..n.k..

Katika sehemu hiyo kila muumini amepewa onyo kali kuhusu mwenendo wake wa Kikristo, budi sisi nasi tuwe na tahadhari katika maisha yetu. Jambo muhimu ni hali yetu ya sasa si jinsi tulivyookoka hapo nyuma. Twapaswa kuendelea na kukua kiroho.

6: 9-12 Tumaini la mambo kuwa mazuri

k.9 Hapo twaona mwandishi amebadilisha sauti yake, akitumia neno tamu „wapenzi" na kwa neno „lakini" ameacha kuyatumia maneno makali ya kuwaonya na kuonyesha kwamba iwapo ilimbidi awaonye, hata hivyo, angali anayo matumaini makubwa juu yao ya kwamba watalijali onyo lake, na kujirekebisha, ili yasiwapate yale aliyosema katika sehemu iliyotangulia. Yapo „mambo mazuri zaidi, na yaliyo ya wokovu".

Lipo jambo moja ambalo limemsaidia kuwawaza vizuri, nalo ni jinsi ambavyo hapo nyuma mpaka wakati huo wamekuwa watu waliowapenda waumini wenzao na kuwasaidia katika shida zao, huenda shida ya kukosa mahitaji ya lazima. Tukumbuke shirika hili la waumini walikuwa wameshambuliwa sana na adui za imani yao (10:32-34) na waliwahudumia na kuonyesha kwamba imani yao haikuwa ya midomo tu (Yk.2:26).

k.10 Mwandishi aliwaambia kwamba Mungu wao si dhalimu, ni Mungu wa haki, naye atayakumbuka hayo matendo mema na kuwapa thawabu yake. Katika kuwahudumia wenzao wamemhudumia Kristo (Mt.25:39,40) na kwa njia hiyo wamemshuhudia Kristo. Huduma yao imekuwa huduma inayoendelea, si ya mara moja. Mungu hakosi kutia maanani utumishi wa upendo, utumishi wa hali hiyo humtukuza Mungu.

k.11-12 Mwandishi ametumia habari hiyo kama kichochea cha kuwasihi waonyeshe bidii ile ile kwa upande wa imani na tumaini kama ambavyo wameonyesha katika upendo wa kuwahudumia wenzao. Alisema nao kwa jumla na kwa kila mmoja wao. Imani na matumaini huhitaji bidii. Wakikosa tumaini ndipo bidii itapungua, kwa hiyo, budi wawe na macho kwa yale mambo ambayo yatayapoza matumaini. Ni matumaini gani? Ni matumaini katika ahadi za Mungu juu ya ushindi wa mwisho.

6: 13-20 Ahadi za Mungu ni imara na za kutegemewa kabisa

k.13ku. Mwandishi alitumia mfano wa Ibrahimu ili awasaidie wasomaji wake kufahamu nguvu na uimara wa ahadi za Mungu. Zamani za kale Mungu alimsaidia Ibrahimu na kumtumainisha juu ya kupata mrithi, na nchi ya kukaa,

na wazao watakaotoka kwa huyo mrithi, na ya kwamba atakuwa sababu ya baraka kwa ulimwengu mzima. Ahadi hiyo ilitolewa katika Mwanzo 12:1-3 na kurudiwa katika 12:6-7, na baada ya muda mrefu Mwanzo 22:17. Ahadi hiyo ilimsaidia Ibrahimu kuvumilia na kusubiri katika matumaini ya matimizo ya hiyo hadi. Miaka 25 ilipita kati na Ibrahimu kupewa ahadi na ahadi kutimizwa, na katika muda huo, yeye na mkewe walizidi kuzeeka, Ibrahimu akiwa na miaka 100 Sara alipomzaa Isaka (Mwa.21:5; Rum.4:13ku).

Wanadamu hutumia kiapo wanapotaka kukaza ukweli wa ahadi zao. Kiapo hutumiwa katika mambo ya sheria kwa shabaha ya kutia nguvu maneno yanayosemwa na kuepa matumizi ya maneno ya uongo. Vilevile Mungu, ambaye kamwe hawezi kusema uongo, hata hivyo, alimthibitishia Ibrahimu ukweli wa ahadi yake kwa kuapa kwa nafsi yake. Hakuweza kuapa kwa kitu kingine au mtu mwingine, maana hakuna aliye mkuu kupita yeye. Kwa hiyo, kwa mambo mawili, ahadi na kiapo, Mungu alimhakikishia Ibrahimu juu ya kumpata mrithi, nchi, na kuwa baraka kwa ulimwengu. Kwa vyo vyote hakuweza kuubadili uamuzi wake, kwa hiyo, ahadi yake ilikuwa imara, haikuweza kutenguka.
Kwa njia hiyo ya kutoa ahadi Mungu huwatumainisha watu wake. Kwa hiyo, hao waumini, ambao kwa wakati huo walikuwa wakipita katika vipingamizi na mateso, budi waishikilie sana ahadi ya Mungu juu ya ushindi. Mbele yao ni kufika kwenye uzima wa milele, kwa hiyo, wakazane, wawe na bidii, wasitazame nyuma na kutaka kujisalimisha kwa kurudia imani yao ya kale, ya Kiyahudi.

Mwandishi ametumia mfano wa nanga ili awasaidie kutambua umuhimu wa ahadi na matumaini yaliyomo katika ahadi za Mungu. Nanga ina kazi njema ya kuishika meli isiyumbeyumbe. Katika misukosuko ya maisha hayo ni rahisi kwa roho zetu kuyumbayumba, twahitaji nanga inayotushika, nanga hiyo ni matumaini katika kutimiziwa ahadi za Mungu. Pamoja na mambo hayo mawili mazuri, ahadi na kiapo, tunaye Kuhani wetu Mkuu, Yesu ambaye ametangulia mbele yetu. Yeye ameishafika huko juu, hali ameyashinda magumu yote yaliyompata, na sasa anafanya huduma ya Kuhani Mkuu, akituwakilisha mbele za Mungu, na kutuombea na kutupatia neema ya kuvumilia.

MASWALI

1. *Ilikuwapo hatari gani mbele ya waumini walioelekea kurudi nyuma kiasi cha kumwasi Kristo?*

2. *Je! Hao walioandikiwa wameishafika hali ya kumwasi Kristo au bado? Toa sababu kwa jibu lako.*

3. *Wakristo walikuwa na msaada gani?*

7: 1-28 Bwana Yesu ni Kuhani Mkuu kwa mfano wa Melkizedeki

Mwandishi ameisha kudokezea habari hiyo katika 5:5,6,10 na 6:20 na katika sura hiyo anaeleza jambo hilo kwa kirefu. Shabaha yake ni kuonyesha ukuu na ubora wa Ukuhani wa Bwana Yesu kupita Ukuhani wa Haruni na WaLawi. Melkizedeki ni muhimu katika kufahamu namna ya ukuhani ukuu wa Bwana Yesu.

7:1-10 Melkizedeki na Ibrahimu

Ameanza kwa habari ya Melkizedeki na Abramu, habari hiyo imeandikwa katika Mwanzo 14.17-20. Lutu, ndugu yake Abramu alikuwa ametekwa wakati wa vita kati ya Wafalme kadha. Katika vita hiyo Abramu alikwenda kumwokoa Lutu na alipata ushindi mkubwa, akiwa na watu wachache, kama 318 tu. Mfalme wa Sodoma alitaka kumpa zawadi kwa ajili ya kuokolewa mikononi mwa wafalme wengine. Alipokuwa akirudi kutoka vitani Abramu alikutana na Melkizedeki. Huyo Melkizedeki alikuwa Mfalme wa Salemu na Kuhani wa Mungu aliye juu. Huyo alimhudumia Abramu kimwili na kumburudisha kwa kumpa mkate na divai (dhabihu haikutolewa) na kwa njia hiyo alitambua ushindi alioupata Abramu na kumshukuru Mungu kwa ajili yake. Ndipo Melkizedeki akambariki Abramu katika jina la Mungu aliye hai, na kwa upande wake Abramu akampa sehemu ya kumi ya vitu vyake, na kwa njia hiyo alimkiri Melkizedeki kuwa mkuu kuliko yeye. Maana ya jina lake ilikuwa Mfalme wa haki na mahali Salemu maana yake Amani. Pamoja na hayo, Melkizedeki alimbariki Mungu, yaani alimwabudu. Kwa hiyo, Melkizedeki alikuwa na vyeo viwili, Mfalme na Kuhani, na kwa maelezo ya jina na mahali, alikuwa Mfalme wa haki na amani. Abramu alikuwa na uhakika juu ya ukuu na mamlaka yake.

Kwa mtindo wa Kiyahudi walipotafuta maana ya jambo fulani walitegemea yasiyosemwa pamoja na yaliyosemwa, na hapo mwandishi ameleta maana kutoka kwa yale yasiyosemwa. Alionyesha kwamba katika Maandiko na katika tukio la kuonekana mara moja tu, tena kwa muda mfupi, bila kutajwa tena, Melkizedeki *alionekana kama* hana mwanzo wala mwisho, maana wazazi wake hawakutajwa, wala kuzaliwa kwake, wala kufariki kwake, (na hii katika kitabu cha Mwanzo kilicho na orodha nyingi za ukoo na kwa upande wa ukuhani ilikuwa lazima ya kuthibitisha ukoo). Melkizedeki ni kama „yupo" tu. Siyo kusema kwamba hakuwa mwanadamu, bila shaka alikuwa amezaliwa na baadaye alifariki dunia, *ila umuhimu wake ni katika jinsi alivyotokea na kuonekana katika Maandiko*. Jambo hilo lilikuwa na *lengo moja la maana sana*, la kumdhihirisha Kristo na Umilele wake. Melkizedeki alikuwa *mfano* wa Mwana wa Mungu, ila Yesu Kristo *alikuwa Mwana halisi*. Melkizedeki alikuwa *nakala halisi*, Yesu Kristo, si nakala bali mwana halisi wa kweli. Uhukani wa Kristo ni wa kudumu, ni wa milele, na ndiyo sababu Yeye hufaa kabisa kwa wanadamu wanaohitaji kuhani mkuu ambaye yupo wakati wo wote, ambaye wanaweza kumwendea mahali po pote walipo na wakati wo wote, bila kizuizi cho chote. Pia wahitaji Kuhani Mkuu mwenye *uwezo* wa kuwahudumia na kuwapatia

neema kila wanapoihitaji. Kristo huwapatia wamwaminio kipawa cha haki kutokana na kifo chake cha kuwa fidia ya dhambi, pamoja na kuwapatia wanadamu msamaha wa dhambi na kipawa cha uzima wa milele. Yeye huwapatia amani kwa Mungu kwa upatanisho alioufanya msalabani. Kwa upatanisho wake kila muumini huletwa katika uhusiano mwema na Mungu.

Melkizedeki ametajwa mara moja tena katika Agano la Kale. Kama miaka elfu baada ya Melkizedeki na Abramu kukutana, Daudi aliandika habari za Masihi na kusema kwamba Masihi atakuwa Kuhani kwa mfano wa Melkizedeki, pia alionyesha jinsi Masihi atakavyokuwa Mwana wa Mungu pamoja na kuwa Mwana wa Daudi kwa kuzaliwa kimwili katika ukoo wa Daudi. Yesu aliitumia Zaburi hiyo ya 110 alipojadiliana na viongozi alipokaribia kifo chake (Mt.22:41ku).

k. 4-10 Mwandishi aliendelea na hoja yake juu ya ukuu wa ukuhani wa Bwana Yesu kwa sababu ulifuata mfano wa Melkizedeki si wa Haruni na WaLawi. Abramu alikuwa mtu muhimu kabisa kwa upande wa taifa la Kiyahudi. Aliitwa na Mungu na kutokana na ahadi za Mungu alijaliwa kupata uzao, na nchi, na kuambiwa kwamba atakuwa sababu ya baraka kwa ulimwengu mzima. Mungu alimwambia kwamba uzao wake utakuwa kama mchanga wa bahari. Hata hivyo, alipokutana na Melizedeki ni Melkizedeki aliyeonekana ni mkuu. Jambo hilo lilidhihirishwa katika mambo kadha. Kwanza Melkizedeki alimbariki Abramu na kwa kawaida mkuu humbariki aliye chini yake. Pili, Abramu alimpa sehemu ya kumi ya nyara aliyopata katika ushindi wa vita. Tena Maandiko huwa kimya juu ya kufariki kwake Melkizedeki, alionekana kama yupo hai wakati wote (siyo kusema kwamba hakufariki, ila *alionekana kama hakufa).*

Ndipo mwandishi alifanya ulinganifu na ukuhani wa Haruni na WaLawi ambao ulikuwepo tangu wakati wa Musa. Lawi alikuwa mwana wa tatu wa Yakobo na Lea (Mwa.24:34). Hakuwa na historia nzuri (Mwa.34:25ku. 49:5-7) ila baadaye, wakati wa Musa, Haruni alipowapotosha Wana wa Israeli kwa kuwafanyia ndamu ya dhahabu, wakati Musa alipokuwa mlimani akiyapokea kwa Mungu mawe mawili yenye Amri Kumi, hao Walawi walijiweka upande wa Musa na kumsaidia katika kuitekeleza hukumu juu ya wale walioasi. Kabila nzima waliwekwa kuwa makuhani wa kuhudumia (Kut.32:26ku. Hes.3:6; 18:2; 35:1-5; Kum.10:8; 18:6ku). Hao Walawi waliipokea sehemu ya kumi ya mapato kutoka kwa Waisraeli wenzao, ila katika maelezo ya mwandishi, iwapo walikuwa wapokeaji, ilihesabiwa kwamba walikuwa watoaji wa sehemu ya kumi *wakifikiriwa kuwa katika viuno* mwa Abramu, Abramu alipomtolea Melkizedeki sehemu hiyo. Jambo hilo liliashiria kwamba Ukuhani wa WaLawi umepungua ule wa Melkizedeki, na ndiyo sababu Yesu hakuwa Kuhani kwa mfano wa Lawi, bali kwa mfano wa Melkizedeki. Walawi walipokezana huduma yao kizazi baada ya kizazi, lakini sivyo ilivyokuwa kwa Melkizedeki ambaye alionekana peke yake tu, bila kuwekwa na wanadamu na bila kutanguliwa au kufuatwa na wengine. Mungu *alitaka kuwafundisha* watu juu ya Ukuu wa ukuhani na umilele

wa Yesu. Katika taifa la Israeli Mungu aliamuru kwamba Makuhani watoke katika kabila la Lawi na Wafalme watoke katika kabila la Yuda, kwa hiyo, haikuwezekana mtu awe Kuhani na Mfalme. Lakini ndivyo alivyokuwa Melkizedeki na ndivyo alivyo Bwana Yesu. WaLawi hawakuwa wakuu kuliko wenzao, wote walikuwa ndugu, ila kwa upande wa sheria walipata kuwa makuhani. Abramu alijinyenyekea kwa Melkizedeki kwa furaha si kwa kuongozwa na sheria, huku amejaa nyara za ushindi wake. Huenda twaona mtindo huo wa kuwaza ni kigeni kwetu, ila wale walioandikiwa, wakiwa na malezi katika dini ya Kiyahudi, walizoea mtindo huo, nao wangalielewa vizuri yale yaliyosemwa na mwandishi.

7: 11-25 Kristo na Haruni

Katika sehemu hiyo mwandishi amesisitiza haja ya kuupata ukuhani mpya utakaowekwa badala ya ule wa Haruni na WaLawi, na badiliko katika ukuhani lilisababisha badiliko kwa Torati pia. Torati ilitolewa kuutegemeza Ukuhani, na mambo hayo mawili yalikuwa msingi wa dini ya Kiyahudi. Kwa Torati watu walipata kuutambua udhaifu wao wa kuwa wenye dhambi, ndipo watu walipata njia ya kusamehewa kwa njia ya dhabihu zilizotolewa na makuhani. Lakini dhabihu walizozitoa hazikuweza kuzitakasa dhamiri zao na kuwaleta mbele za Mungu Mtakatifu hasa. Hivyo, upungufu ulikuwapo, na kutokana na upungufu huo, daima dhabihu zilitakiwa kutolewa, mwaka baada ya mwaka, na kila kuhani alipokufa, ndipo mwingine aliwekwa mahali pake. Mipango hiyo yote iliwaelimisha watu juu ya Mungu kuwa Mtakatifu na jinsi dhambi ilivyo chukizo kwake, na iliwatazamisha watu kwa Kuja kwa Yule atakayetoa dhabihu kamili, ya kutosha, kuziondoa dhambi za watu, mara moja tu; na huyo alikuwa Kristo. Kwa hiyo, mpango huo mzima ulikuwa wa *muda tu*, mpaka hadi Kuhani Mkuu, awezaye kuwakamilisha watu ili wamkaribie Mungu kwa kweli na kushirikiana naye kibinafsi.

Yesu hakutoka katika kabila ya Lawi bali katika kabila ya Yuda, hivyo, kwa upande wa kibinadamu kamwe Yesu asingaliweza kuwa kuhani kwa mfano wa Haruni na WaLawi maana Torati ilisema kwamba kuhani lazima awe wa kabila ya Lawi. Yeremia alitabiri kwamba Mungu atafanya Agano Jipya na watu wake ndipo Agano la Kale litaondolewa kwa kuwa litakuwa limetimiza shaba yake (Yer.31:31ku). Yesu, usiku wa mwisho kabla ya Kufa alianzisha hilo Agano Jipya. Hivyo mpango mzima wa kale uliondolewa, neno lililokuwa ajabu kwa Wayahudi. Twakumbuka kwamba Stefano alihubiri jambo hilo na wakuu na wengine walimgeukia na kumpiga kwa mawe na kumwua (Mdo.6:9ku.- 7:1ku).

Kwa Kufufuka Kwake kutoka wafu Yesu amekuwa kuhani adumuye milele hali ameishinda mauti, na kwa sababu hiyo haiwezekani ukuhani wake ukomeshwe. Yeye ni Mwana wa Milele wa Baba (Ebr.1:10-12) na kwa Yeye ukamilifu umepatikana, ukamilifu ambao ulikosekana katika ukuhani wa Haruni na WaLawi. Kama ni hivyo ni upuzi mtupu kwa hao walioandikiwa kuwaza

kurudi kwenye dini yao ya asili na kwa mipango ya kale ambao imekwisha manufaa yake. Kila muumini huwa na Roho Mtakatifu kwa msaada wake, na dhamiri yake hutakaswa na damu ya Kristo.

k.20ku. Halafu mwandishi aliendelea kusisitiza ubora wa ukuhani wa Yesu. Makuhani wa KiLawi hawakuwekwa kwa kiapo, waliingia kwa kuzaliwa katika kabila la Lawi, walikubalika kuwa makuhani halali walipoweza kuuthibitisha ukoo wao. Ila Yesu aliwekwa kwa kiapo cha Mungu Mwenyewe, kiapo kilichomweka Kuhani kwa milele pasipo uwezekano wa kubadilishwa au kubatilishwa, maana kiapo kilikuwa cha Mungu Mwenyewe na kwa nafsi yake (taz. Zab.110:4). Hakuna kuhani mwingine awaye yote aliyewekwa kwa kiapo. Hapo tena twaona mkazo ni juu ya umilele wa ukuhani wa Yesu (k.3,17,21).

k.22 Kwa mara ya kwanza katika Waraka mwandishi ametaja jambo la agano, jambo ambalo atalisemea zaidi mbeleni. Yesu amekuwa mdhamini wa Agano lililo bora zaidi, Agano Jipya, Agano lililoanzishwa na Mungu Mwenyewe na kutiwa muhuri na damu ya Kristo, tena Agano la milele. Yesu **ni mdhamini wake sasa,** maana yake ni kwamba baraka za Agano zapatikana kwa jinsi zilivyoahidiwa.

k.23-24 Haidhuru kuhani alikuwa mzuri kiasi gani huduma yake ilikwisha wakati wa kufariki kwake, na yeye mwenyewe alihitaji kutoa dhabihu kwa ajili ya makosa yake kabla ya kuzitoa kwa dhambi za wengine. Sivyo ilivyo kwa Kristo, huduma yake huendelea bila kikoma, kwa vile Yeye Mwenyewe hana mwanzo wala mwisho, yu hai milele na milele. Pia Yeye Mwenyewe hahitaji kutoa dhabihu kwa ajili yake mwenyewe kwa sababu hakuwa na dhambi wala hakufanya dhambi iwapo alijaribiwa kiasi kikubwa kupita wanadamu wengine wote.

k.25 Hapo katika kifungu hicho twafika kwenye kiini kabisa cha ubora wa ukuhani wa Bwana Yesu. Yesu anao uwezo mkubwa kabisa wa kuwaokoa wenye dhambi, kwa sababu, baada ya kuwafia msalabani na kuwapatanisha na Mungu alifufuka kutoka kwa wafu na kuwa hai milele akiishi mahali pa juu kabisa. Huduma yake ni kuwaomboa watu kufuatana na mahitaji yao. Yeye huelewa kabisa shida na majaribu yanayowapata wanadamu, anajua ni nini ya kuishi katika ulimwengu huu unaompinga Mungu, na kwa sababu ameshinda dhambi, na Shetani, na mauti, anao uwezo usio na mpaka wa kutuokoa sisi wakati huo wa sasa. Lilikuwa neno kubwa kwa wale walioandikiwa waliojaribiwa kumwacha Kristo kwa sababu ya shida walizozipata. Yesu amejaa huruma, amejaa ufahamu wa mahitaji yetu, pia anao uwezo wa kukabili shida zetu na kutoa msaada unaolingana na mahitaji yetu.

7: 26-28 Yesu – Kuhani Mkuu, Mtakatifu, Afaaye kabisa

Hapo tunazo sifa kuu za kuhani wetu mkuu. Ni kuhani aliye mtakatifu, si kwa nje tu, bali kwa ndani pia. Makuhani walizoea kufuata sheria za maosho ya kuuondoa unajisi kwa kujisafisha kwa nje, unajisi walioupata kwa kugusa vitu fulani n.k. Yesu hakuwa na maovu yo yote, hata nukta moja, katika hali yake, katika mawazo yake, katika kunia kwake, na katika kufanya kwake. Kuna wema tu katika Yesu, hana waa lo lote. Alikuwa na uwezo wa kutokufanya dhambi.

„aliyetengwa na wakosaji" tusimaanishe kwamba Yesu aliishi mbali nasi, la, hata kidogo, alijulikana kuwa rafiki wa wenye dhambi na alishirikiana na kila aina ya watu, ila wakati wote alikuwa mwaminifu kwa Baba na mapenzi yake. Pamoja na sifa hizo Yesu ni wa juu kabisa, alitoka kwa Mungu, akarudi kwa Mungu, alikuwa kwa Mungu na alikuwa Mungu, alishirikiana na Mungu katika uumbaji, na kwa njia yake vitu vyote vilipata kuwako (Yn.1:1ku. Kol.1:16ku).

Pamoja na Kuhani Mkuu Mkamilifu Yeye ni Dhabihu Kuu Kamilifu, aliyetoa nafsi yake kuwa dhabihu ya dhambi. Hakuna kurudia kutoa dhabihu hiyo, imekubalika kuwa imetosha wakati wote kwa dhambi za ulimwengu wote. Aliye Kuhani wetu Mkuu na dhabihu daima kwa dhambi za ulimwengu wote, ni Mwana wa Milele wa Baba. Kwa sababu hiyo, walioandikiwa walihitaji kutia maanani hayo yote yaliyoelezwa kuhusu habari ya Yesu kuwa Kuhani Mkuu kwa mfano wa Melkizedeki, jambo ambalo mwandishi alikuwa akitamani sana kuwaelemisha juu yake (5:11,12).

MASWALI

Kristo na Melkizedeki walifanana katika mambo gani?

Kwa sababu gani Melkizedeki alionekana kuwa mkuu kuliko Ibrahimu?

Kwa njia zipi ukuhani wa Melkizedeki ulikuwa bora kuliko ule wa Haruni?

Uzuri wa Kristo unadhihirishwa katika mambo gani?

8:1 – 9:28 UBORA WA HUDUMA YA KRISTO

Kama ambavyo tumeona katika Waraka huo wote neno „bora" limetumika kila mara katika kumweleza Kristo, hasa kuhusu mambo yote muhimu yaliyokuwa katika dini ya Kiyahudi, hasa kwa sababu mwandishi alilenga kuwasaidia waumini walio na malezi katika dini hiyo. Ilionekana kwamba walitaka kuirudia dini yao ya kwanza, ili wayaepe mateso waliyoyapata kwa ajili ya kumfuata Kristo.

8:1-6 Ubora wa Huduma ya Kristo

k.1 Akitazama nyuma katika kuyajumlisha yaliyotangulia, mwandishi ametaja kwamba neno lililo kuu katika hayo yote ni „tunaye kuhani mkuu" ndipo alitaja kwamba huyo tuliye naye ameketi mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha Ukuu mbinguni. Alitumia neno „Ukuu" ili avute watu kuwaza jinsi Mungu alivyo na utukufu na mwenye adhama kuu. Yesu siye huyo Mwenye Ukuu ila yupo upande wake wa kuume. Katika uhusiano wa Utatu Mungu Baba ndiye mwenye mamlaka ya mwisho. Yesu amepita makuhani wote wengine kwa sababu Yeye ni Mfalme mkuu pia yupo mahali pakuu, pa enzi, pa mamlaka, pamoja na Mungu Baba yake. Ni Kuhani Mkuu na Mfalme Mkuu. Tena ameketi, tofauti na makuhani ambao daima walikuwa wamesimama, dalili ya kuonyesha kwamba kazi zao, na dhabihu zao, hazikuwa na mwisho. Katika patakatifu hapakuwa kiti cha kukalia. Yesu kwa nafsi yake ni bora, akiwa Mwana wa Baba, mwenye kuushiriki Uungu wake.

k.2 Ndipo Yesu ameitwa „mhudumu wa patakatifu, na wa ile hema ya kweli, ambayo Bwana aliiweka wala si mwanadamu". Kama ambavyo amefanya tangu mwanzo, hapo mwandishi amefanya ulinganifu na hema ya kukutania na hekalu, mahali walipohudumia makuhani. Huduma ya Yesu inafanyika katika mahali halisi ya umilele, mahali ambapo huduma yake hutambulika na kuthibitishwa kuwa na uwezo wa utekelezaji. Huduma ya makuhani katika Israeli ilibanwa katika mahali fulani na wakati fulani wa hapa duniani. Huduma ya Yesu hufanyika huko mbinguni, tena, si huduma ya kutoa dhabihu ya dhambi, kwa sababu Yeyey ameishatoa dhabihu hapa duniani, alipokufa msalabani. Huduma yake ya sasa ni kuwahudumia wanadamu baraka zitokanazo na dhabihu aliyoitoa. Baraka za kuwajalia watu msamaha wa dhambi na neema ya kuishi maisha ya Kikristo, na hasa kuwaombea waumini kulingana na mahitaji yao (Rum.8:34; Yn.14:26). Mahali walipohudumia makuhani palikuwa „mfano" tu na „kivuli" tu vya mahali halisi pa huduma ya Yesu. Huenda neno „mahali" si neno lifaalo kueleza „mahali" pa huduma ya Yesu. Huenda ni afadhali kusema „uhalisi wa kweli wa umilele" kama Kituo Kikuu cha Vitu vyote vya mbinguni na vya duniani. Twaweza kusema kwamba ni mahali bora zaidi.

k.3 Akiendelea kufanya ulinganifu mwandishi ameonyesha kwamba kazi muhimu ya kuhani ilikuwa kutoa vipawa na dhabihu, akiwekwa kuwa kati ya watu na Mungu na kuwaleta karibu na Mungu. Yesu akiwa kuhani alihitaji kuwa na dhabihu ya kumtolea Mungu, ila kwa hali ya ukuhani uliokuwapo asingalikubalika kutoa hiyo dhabihu kwa sababu hakutoka katika kabila ya Lawi. Alihesabiwa ni mlei tu. Ila iliyopo ni kwamba ameishatoa, dhabihu bora kuliko dhabihu za wanyama n.k. dhabihu ya Nafsi yake. Alitoa hapo duniani, mara moja tu, dhabihu kamili, dhabihu ya kutosha kuzifidia dhambi za ulimwengu wote. Ndiyo sababu sasa amekaa pale juu. Kazi hiyo imekwisha. Huduma aliyo nayo sasa, si huduma ya kuendelea kutoa dhabihu, la! Bali ni

huduma ya kuwahudumia wanadamu faida zote zilizopatikana kwa Kifo chake cha Upatanisho.

Musa alipewa na Mungu ufunuo wa mipango yote itakayowasaidia Waisraeli kuwa watu wapendezao Mungu (Kut.25:40). Mipango yote, kama ya hema, na hali yake ya kuwa sehemu mbili, patakatifu na patakatifu pa patakatifu, na vyombo vyake, na mipango ya dhabihu mbalimbali za kutolewa, na kila kitu, hayo yote yalikuwa na shabaha ya *kuwafundisha* Waisraeli juu ya Utakatifu wa Mungu, na jinsi wakosaji wawezavyo kumkaribia Mungu na kujihusisha naye vema. Ni kama fundisho kubwa la kuwasaidia na kuwatayarisha kwa baadaye, kwa Kuja kwa Kristo. Musa hakubuni mipango hiyo, aliipata kwa Mungu Mwenyewe.

k.6 Kwa nini Yesu anafanya huduma iliyo bora zaidi? Ni kwa sababu anahudumia agano lililo bora, lenye ahadi zilizo bora. Halafu mwandishi anaendelea kusema juu ya agano hilo na ahadi zake.

8: 7-13 Yesu na Agano Jipya – Agano lililo bora

Hapo mwandishi amefanya ulinganifu na agano la kwanza, ambalo lilitoka na kufanywa na Mungu. Kila agano huwa na pande mbili, upande wa Mungu na upande wa wanadamu. Tunapolitafakiria jambo la agano, kwa kawaida katika maagano kati ya watu kila upande huwa sawa, ila sivyo ilivyo tunapolitafakaria agano kati ya Mungu na watu. Mungu, wakati wote aweza kutimiza upande wake, hata iliposhindikana lile la kwanza aliweza kulitengeneza lingine jipya.

k.7 Katika Agano la kwanza shida ilitokea kwa sababu ya udhaifu wa wanadamu walioshindwa kuutimiza wajibu wao katika hilo Agano. Upungufu ulionekana katika mambo mawili, la kwanza, Agano lenyewe halikuwa na uwezo wa kuwezesha watu kuyatimiza matakwa yake. La pili, lilishindikana kwa sababu watu walikosa uwezo wa kuyatii maagizo yake. Twaweza kulifananisha Agano la Kwanza na ubao unaonekana njiani. Ubao huwa mzuri sana, unamwelekeza msafiri katika njia iendayo mahali anapotaka kwenda, tena mara kwa mara humjulisha ni kilometa ngapi ya kusafiri mpaka kufika mahali pale. Shida ya ubao ni katika kukosa nguvu ya kumwezesha msafiri afike mahali pale. Hata mtu aweza kuukasirikia huo ubao, ikiwa hana mafuta ya kutosha kumaliza safari yake, au ikiwa mtu amechoka sana hata hana nguvu ya kumaliza safiri yake n.k. Ndivyo ilivyokuwa Agano la Kwanza, Amri Kumi ni nzuri kabisa, zinayafunua mapenzi ya Mungu kwa maisha yetu, nazo *zadumu kuwa mwelekezo mzuri kwa maisha ya wanadamu.* Ziliandikwa na Mungu kwenye mbao za mawe na Musa alishuka mlimani na mbao hizo na kuwajulisha Waisraeli habari zake (Taz. Kut.19:4ku). Kwa sababu mbili za upungufu zilizotajwa hapa juu, Torati kukosa uwezo wa kumsaidia mtu kuzitimiza amri zake na watu kukosa uwezo wa kuyatimiza matakwa yake, lilihitajika Agano Jipya, lenye uwezo mpya na lenye nguvu ya kuwasaidia watu.

NdipoYesu akaja na kulitengeneza hilo Agano Jipya kwa kumwaga damu yake msalabani. Usiku ule kabla ya Kufa Kwake Yesu alitamka wazi habari ya hilo Agano Jipya (Mt.26:27-28; Kut.24:8). Maagano yote mawili yalitiwa muhuri na damu, moja kwa damu ya wanyame, la pili, kwa damu ya Mwana wa Mungu.

k.9ku. Kabla ya kufanya Agano na Israeli Mungu alikuwa amelifanya Agano na Abramu (Mwa.12:1ku). Msingi wa Agano hilo ulikuwa ahadi ya Mungu na imani ya Abramu. Hilo la Musa lilijengwa juu ya Torati na madai ya Utii kwa maagizo yake.

k.10ku. Nabii Yeremia alitabiri habari ya kuja kwa hilo Agano Jipya. Wakati alipotabiri habari hiyo taifa la Israeli lilikuwa limekwisha kwenda utumwani huko Babeli kwa sababu ya uasi wao. Lilibaki taifa la Yuda ambalo hali yake pia ilitia wasiwasi sana kwamba, hata taifa hilo, lisipoutengeneza mwenendo wake litapatikana na hukumu kama ile iliyopata taifa la Israeli. Kwa miaka arobaini Yeremia aliwatangazia watu hatari iliyokuwa ikiwakabili, ila watu hawakutaka kumsikiliza, wakamwudhi sana, huku wakiendelea katika njia zao mbovu. Katika giza la siku zake Yeremia alitazama mbele kwa wakati wa siku mpya kupumbazuka, wakati ambapo Mungu atajiingiza katika historia ya ulimwengu huu na kumleta Masihi, Mwana wake. Huyo ndiye atalitengeneza Agano Jipya, Agano lenye uwezo, litakalowaleta watu kwenye uhusiano mpya na Mungu wao.

Yeremia alitaja mambo makuu matatu yatakayotokea kwa kufanyika hilo Agano Jipya. Mungu ataziweka sheria zake mioyoni mwa wanadamu, zitakuwa ndani ya mtu, si nje yake, kama zile zilizoandikwa kwenye mawe. Agano litakuwa la kiroho si la andiko, andiko liliua kwa sababu lilimwambia la kufanya au kutokufanya bila kumwezesha kulitii. Kwa neema yake na kwa msaada wa Roho Mtakatifu, watu watasikia kama „joto" mioyoni mwao, nao watasikia msukumo wa ndani wa kumpenda Mungu nao watakuwa na nia ya kumpendeza, na kwa Roho watamwita Mungu „Baba" wala hawatamwaza tena kama Hakimu.

Jambo la pili, watu hawatahitaji kufundishwa habari za Mungu, kwa sababu kila mtu ataweza kumjua Mungu kwa kibinafsi, ataweza kujihusisha naye vema kwa njia ya Yesu Kristo. Kwa hiyo, pamoja na kuguswa katika mioyo yao wataguswa katika fahamu zao. Tena hawatakuwapo watu walio bora kuliko wenzao, mdogo kwa mkubwa, mwanamke kwa mwanaume, maskini kwa tajari, mtumwa na aliye huru, tofauti hizo zinazoleta matengano katika watu na kusababisha ubaguzi zitaondolewa katika Kristo, wote watakuwa sawa mbele zake (Gal.3:28).

Jambo la tatu katika hilo Agano Jipya ni msamaha kamili wa dhambi. Mungu atazifuta dhambi zote kwa sababu ya kifo cha upatanisho cha Yesu msalabani. Kwa sababu Mungu hana udhaifu wa usahaulifu, ameamua kwa nafsi yake

kwamba, *hatazikumbuka dhambi zetu tena*. Tutasamehewa kabisa kabisa. Haitakuwepo haja ya kumwendea kuhani na kutoa kondoo au mbuzi kila wakati. Ni mwisho wa mipango yote ya dhabihu iliyowekwa katika Agano la Kale kwa watu kusamehewa dhambi.

Hivyo, kwa sababu Kristo ameishafika na kulitengeneza hilo Agano Jipya, lile la kale limezeeka, nalo tayari kutoweka. Kwa hiyo, ni upuzi kabisa kwa hao walioandikiwa kutaka kurudi kwenye mipango ya kale. Tukumbuke ya kuwa, wakati alipokuwa akiwaandikia, mipango ya Agano la Kale ilikuwa ingaliendelea. Kama Waraka uliandikwa kabla ya B.K.70 Hekalu lilikuwa bado halijaangushwa.

MASWALI

1. Kwa nini Agano Jipya ililofanyika na Yesu ni bora kuliko Agano la Kale?

9:1-10 Maelezo ya Mahali Patakatifu na Huduma ya Makuhani

k. 1-5 Katika vifungu hivi vya kwanza mwandishi ametaja vifaa mbalimbali vilivyokuwamo katika Hema ya Kukutania, akifuata mfano wa hema ya kwanza iliyokuwa jangwani, kabla ya kujengwa kwa Hekalu wakati wa Waisraeli kuwa wamekaa katika nchi ya Kanaani kwa muda. Hema iliwekwa mahali palipoitwa Shiloh mara baada ya kuingia Kanaani (taz. Kutoka 25 na 26 kwa habari ya Hema na vitu vyake).

Ijapokuwa mipango hiyo yote ilielekea mwisho wake, kwa sababu kazi yake haikuhitajika baada ya Kuja kwa Kristo na Kufanyika Agano Jipya, hata hivyo, mwandishi aliona vema kutoa maelezo juu yake, akiamini kwamba kwa kufafanua kila kitu na maana yake mwanga mkuu utaangazwa juu ya Yesu na Agano lake Jipya na Huduma yake katika „mahali" halisi, yaani kule juu mbinguni. Alijua kwamba Musa alipoambiwa kufanya yote kwa jinsi alivyoambiwa, alikuwa amefunuliwa kweli za msingi zilizohusu Ibada ya Mungu. Katika mipango ya vitu vya dunia hii kweli za milele zilifunuliwa, ni kama Mungu alikuwa akiwafundisha watu wa kale kwa njia ya vitu hivi vikiwa kama picha. Mifano hiyo ilifaa kwa muda mpaka uje uhalisi wake yaani Kristo.

Zamani zile Hema ya Kukutania ilikuwa na sehemu tatu. Uwanja uliotumiwa kwa huduma ya makuhani, nao waliingia mle ndani kwa mlango mmoja. Hapo palikuwapo madhabahu ya dhahabu na juu yake zilitolewa dhabihu na sadaka zilizoletwa na Waisraeli.

Ndipo mle ndani ya uwanja lilikuwapo jengo lenye sehemu mbili. Sehemu ya kwanza iliitwa „Patakatifu". Ndani yake ilikuwepo Sahani yenye maji ya Maosho, hapo makuhani walinawa mikono n.k. ili wawe „safi" kwa huduma yao. Pamoja na Sahani ya Maosho, kilikuwapo Kinari cha Taa chenye vitawi saba,

kilichotengenezwa na dhahabu. Pia Meza yenye Mikate wa Onyesho ilikuwapo na madhabahu ya dhahabu ya kufukiza uvumba. Katika k.4 mwandishi amesema kwamba hiyo madhabahu ilikuwemo katika Patakatifu pa Patakatifu, ila hasa ilikuwa katika Patakatifu karibu na mahali pa kuingia kwenye Patakatifu pa Patakatifu. Pazia lilitenga mahali pa Patakatifu na mahali pa Patakatifu pa Patakatifu.

Katika Patakatifu pa Patakatifu Sanduku la Agano lilikuwemo, nalo lilifunikwa na dhahabu na funiko hilo liliitwa Kiti cha Rehema. Juu yake, upande wa kushoto na upande wa kulia Makerubi yaliyochongwa kwa dhahabu yalikuwepo, nyuso zao zilielekea kutazama Kiti cha Rehema na ile damu ya sadaka iliyowekwa juu ya Kiti hicho. Kisha Mwanga wa Utukufu ulioitwa Shekina uliangaza juu ya Kiti cha Rehema, Mwanga huo ulidhihirisha Kuwepo kwa Mungu.

Katika Sanduku la Agano, mbao mbili za Amri Kumi, zilizoandikwa na kidole cha Mungu zilikuwemo, zikishuhudia Torati iliyodai utii, ishara ya Mungu kutawala ulimwengu wote kwa uadilifu na haki (Kut.32:15). Juu yake Kiti cha Rehema kilishuhudia jinsi ambavyo Mungu amejaa huruma na nia ya kuwasamehe watu wake dhambi zao. Damu iliyowekwa juu ya Kiti cha Rehema ilionyesha jinsi ambavyo Madai ya Torati yemetulizwa kwa sadaka ya kumwaga damu. Pia, mle ndani ya Sanduka ilikuwemo kopu ya mana iliyoshuhudia uhifadhi na uaminifu wa Mungu katika kuwatunza watu wake wakati wote wa kusafiri jangwani (Kut.16:32). Pamoja na vitu hivi Fimbo ya Haruni iliyochipuka ilikuwemo, hiyo ilishuhudia uwezo mkuu wa Mungu katika kuwatoa watu wake utumwani (Hes.17:8-10). Madhabahu ya kufukiza uvumba ilishuhudia Uadhamu na Utukufu wa Mungu Mtakatifu, aliyestahili kuabudiwa na watu wake.

Wakati wa kusafiri jangwani, kila walipopiga kambi, waliisimamia hiyo Hema ya Kukutania kati ya Mahema yao. Mahema yao yaliwekwa kila upande, mahema ya makabila matatu kwa kila upande. Jambo hilo lilishuhudia umuhimu wa Ibada ya Mungu katika maisha ya Taifa zima.

k.6-10 Baada ya kueleza juu ya mahali na vifaa vya ibada mwandishi aliendelea na maelezo juu ya kazi za hao makuhani, na huduma kubwa ya kuhani mkuu, katika mahali palipoelezwa hapo juu.

k.6 Kwa upande wa makuhani na mahali palipoitwa Patakatifu, hao walifanya huduma yao kila wakati, wakitengeneza Taa na kubadili Mikate ya Onyesho na kutoa dhabihu zilizoletwa na Wana wa Israeli na kufikiza uvumba kwenye madhabahu ya kufukiza. Kila siku walifanya huduma ya namna hizo.

k.7 Kwa upande wa Kuhani Mkuu na mahali palipoitwa Patakatifu pa Patakatifu taratibu ilikuwa tofauti sana. Kwanza kabisa, ni Kuhani Mkuu, peke yake,

aliyeruhusiwa kuingia mle ndani. Pili, hakwenda mara kwa mara, ila mara moja kwa mwaka, siku nyingine zote hakuruhusiwa kuingia. Siku ya kuingia iliitwa Sikukuu ya Upatanisho (Law.16:1). Tatu, wanyama kadha walioamriwa walichinjwa ndipo Kuhani Mkuu aliingia mle ndani akichukua damu yake kwa ajili ya dhambi zake na za Waisraeli, hasa kwa dhambi za kutokujua, inaonekana kwamba haikuwepo sadaka kwa ajili ya dhambi zilizofanya kwa kusudi. Twaweza kujumlisha jambo hilo kwa kutazama jinsi ambavyo neno *moja* limetumiwa: mahali palikuwa *pamoja tu* (Patakatifu pa Patakatifu); mhusika alikuwa *mtu mmoja tu (*kuhani mkuu)*;* wakati ulikuwa *mara moja tu* (Sikukuu ya Upatanisho)*;* na njia ilikuwa *moja tu (*ya kuchukua damu ya mnyama).

k.8 Ndipo mwandishi alisema kwamba kwa mambo hayo Roho Mtakatifu alikuwa akiwafundisha watu kwamba njia kamili ya kumkaribia Mungu ilikuwa bado haijapatikana, ilikuwa kwa muda tu mpaka atakapokuja Kristo. Kwa sababu mipango hiyo ilirudiwa-rudiwa kila mwaka ilikuwa wazi kwamba haikuwa kamili.

k.9-10 Udhaifu ulionekana katika dhamiri za watu zilizoendelea kuwashtaki. Kila wakati walikuwa wakisubiri Sikukuu ya Upatanisho, ilipopita moja waliingojea nyingine ya mwaka uliofuata, na iliendelea hivyo mwaka baada ya mwaka. Haukupatikana utakaso wa ndani, wala amani na Mungu, yote yalikuwa ya nje tu, haikuwa na uwezo wa kugusa mioyo na dhamiri za watu. Kila kitu kilisema „Bado, bado, bado!". Faida yake ilikuwa katika kuwatayarisha watu kwa Kuja kwa Kristo na kwa kutolewa Dhabihu ya Nafsi yake itakayotosha kuondoa dhambi kwa hakika.

9:11-22 Uwezo mkuu wa sadaka ya Kristo katika kutakasa

Mwandishi aliendelea na kawaida yake ya kufanya ulinganifu kati ya Agano la Kale na upungufu wake na Agano Jipya lenye uwezo lililofanywa na Kristo.

k.11 Kuja kwa Kristo kulifanya mabadiliko makubwa, kulileta „mambo mema yatakayokuwapo". Akilinganisha na Hema, mahali palipofanyika Ibada katika Israeli, alionyesha kwamba Yesu alifanya huduma yake mahali halisi, mahali pasipofanyika kwa mikono ya wanadamu, mahali pa kiroho, yaani mbele za Mungu Mwenyewe. Ni wapi huo „uhalisi" ambao Hema ilikuwa mfano wake? Uhalisi ulikuwa Usoni mwa Mungu Mwenyewe (Mk.14:58; Mdo.7:48; Isa.57:15). Si mahali hasa. Yesu alipozungumza na Mwanamke Msamaria alisema kwamba yapasa Ibada ifanywe kwa roho na kweli (Yn.4:21,23). Mbinguni ni pakuu na pakamilifu kuliko Hema. Dalili iliyoonyesha kwamba dhabihu ya Yesu imekubalika na Mungu ni kwa Pazia la Hekalu kupasuliwa kutoka juu wakati wa Kufa Kwake (Mt.27:51).

k.12 Halafu mwandishi alionyesha ubora wa sadaka ya Kristo. Hapo nyuma damu ya mbuzi na kondoo n.k. ilimwagika, nyingi sana, kila siku, kila mwaka. Ila Kristo alimwaga damu yake mara moja tu, akiwa Mwana Kondoo halisi (Yn.1:29,35) ilikuwa damu ya Mwana wa Mungu aliyefanyika mwanadamu, damu ya mwanadamu mmoja tu, ambaye hakuwa na doa, wala mawaa, wala kosoro yo yote, wala upungufu wo wote katika maisha yake. Alikufa mara moja tu, hata hivyo, kifo chake kilitosha kuwa dhabihu kwa dhambi za ulimwengu wote, kwa dhambi zilizokwisha kufanyika na kwa dhambi ambazo hazijafanyika bado, maana ilikuwa dhabihu yenye matokeo yadumuyo hata milele. Katika mpango wa ibada katika Israeli sadaka nyingi za aina mbalimbali zilitolewa, kila siku, pamoja na zile zilizotolewa katika Sikukuu ya Upatanisho (Law.16:11,15, 21,22; ng"ombe na mbuzi; Hes.19 „ng"ombe mke mwekundu – majivu yake)
Kwa dhabihu ya nafsi yake Yesu alitupatia ukombozi wa milele na kwa njia yake watu hufunguliwa pingu za dhambi na kuwekwa huru mbali na hukumu na nguvu ya dhambi iliyomo katika utu wetu. Hivyo, kila amwaminiye Kristo na Kifo Chake, wapata msamaha kamili wa dhambi zake na usalama wa roho yake.

Neno „ukombozi" linatukumbusha habari za soko la watumwa, mahali walipoletwa watumwa, ili wauzwe na watu wapate kuwanunua. Mtumwa hakuwekwa uhuru ila alibadilishwa bwana wake. Vivyo hivyo, wanadamu walio watumwa wa dhambi kwa ukombozi wa Yesu wamepata Bwana mpya, wana nafasi ya kubadili bwana wao mbaya „dhambi" kwa bwana mwingine mzuri „Kristo".

Kwa sababu ya maisha yake makamilifu Yesu aliingia mbele za Mungu. Pia aliingia mbele za Mungu kwa ajili yetu kwa sababu ya kifo chake kwa ajili ya dhambi zetu. Ni wakili wetu. Alitoa fidia kubwa mno, gharama ya nafsi yake, hamna fidia izidiyo hiyo aliyoitoa Kristo, fidia ya nafsi yake. Kwa hiyo, hakuna shaka yo yote juu ya utoshelevu wake wa kutakasa dhambi. Alipoingia mbele za Mungu hakuichukua damu ya Kifo Chake mfano wa Kuhani Mkuu aliyeichukua damu ya mnyama, la, ila aliingia *kwa sababu ya* kifo chake. Alikufa hapa duniani, na mara dhabihu yake ilikubalika na Baba yake, jambo lililoshuhudiwa katika pazia la hekalu kupasuka kutoka juu, wakati ule ule wa kufa kwake.

k.13-14 Kwa sadaka zilizotolewa chini ya mpango wa Agano la Kale watu walipata kutakaswa na uchafu wa mwili, waliondolewa unajisi ili waendelee kumwabudu Mungu, ila hawakupata amani katika dhamiri zao, kwa sababu waliendelea kutoa dhabihu kila wakati, dalili ya kuwa utakaso kamili haujapatikana bado. Mara Sikukuu ya Upatanisho (Law.16) ilipopita, watu waliingojea ile ya mwaka ujao. Ni tofauti sana na Dhabihu ya Kristo, Yeye alitoa nafsi yake kwa Mungu, kwa njia ya Roho Mtakatifu, (Isa.42:1ku) na kwa sababu hiyo watu hutakaswa dhamiri zao, na kusikia amani na Mungu mioyoni mwao (Rum.5:1,2). Kwa ndani wanasikia msukumo wa kumtumikia Mungu kwa furaha badala ya kufanya matendo mafuu, yaani matendo ya dhambi

pamoja na matendo bure, yale yasiyo na matunda. Wanyama walichukuliwa bila wao kukubali, na bila wao kufahamu yanatokea nini, ila Kristo alifanya kwa hiari yake mwenyewe, na kwa kufahamu kabisa kazi anayofanya, kazi ya ukombozi. Mara kwa mara alitoa habari za Kufa Kwake mapema kabla ya kutokea kwake, na usiku ule kabla ya kufa, kwa kusudi maalum, alivichukua mkate na divai na kutamka wazi „hii ndiyo damu yangu ya agano, imwagikayo kwa ajili ya wengi kwa ondoleo la dhambi" (Mt.26:28).

Waumini wamepata uwezo wa kumtumikia Mungu kwa kiroho, katika „uhalisi" usioonekana (Efe.2:6; 1 Kor.6:17). Kwa Roho wamwita Mungu „Baba" (Rum.8:15,16) wakijua kwamba njia imekuwa wazi ya kumkaribia Mungu kama Baba bila wasiwasi. Kwa sababu ya imani yao wanafanya matendo mema kwa furaha wakipenda kumtumikia Mungu (Efe.2:8-10).

k.15 Kwa sababu ya dhabihu ya Nafsi yake Yesu amekuwa daraja kati ya Mungu na wanadamu, kwanza, akiwa Mungu na Mwanadamu, pili, kwa kuondoa dhambi iliyokuwa kizuizi kilichomzuia Mungu Mtakatifu asishiriki na wenye dhambi. Msingi wa huduma yake ya kuwa mjumbe wa Agano Jipya ni katika kutoa Nafsi yake kuwa fidia ya dhambi, naye amekuwa badala ya Musa aliyekuwa mjumbe wa Agano la Kale (Gal.3:19ku). Waisraeli walizoea kuwa na wajumbe, kama malaika, na kuhani mkuu, na katika Agano Jipya, Kristo amekuwa mjumbe mkuu na bora kupita hao wote. Kwa kifo chake dhambi zote zilizofanyika wakati wa Agano la Kale zimeondolewa na wote wanaoitika wito wa Mungu wameahidiwa urithi wa uzima wa milele. Hata watu walioishi kabla ya Kristo waliishiriki ahadi hii, Injili ilihubiriwa kwao katika mipango iliyowekwa (4:2) ila ilikuwa kwamba baraka hazikupatikana mpaka Kristo alipokuja na kufanya ukombozi. Yesu, katika kuwa Mjumbe bora ameonyesha upendo wa ajabu sana, ametoa maisha yake kiasi cha kumwaga damu yake katika kufa ili watu wapate ondoleo la dhambi zao na kipawa cha uzima wa milele. Ahadi ya urithi wa milele ni kwa wenye dhambi, wasio na kitu cho chote cha kuwastahilisha mbele za Mungu, nao wameitwa na Mungu kuishiriki hiyo ahadi ya urithi wa milele. Ahadi hiyo ina uhakika, imeahidiwa na Mungu asiyeweza kusema uongo, tena ameahidi kwa kiapo. Tena ni ya milele, haiwezi kutoweka au kuondolewa kwa njia yo yote, maana Mungu ni mdhamini wake, na „mali" ya urithi ni baraka zote zilizopatikana kwa Kifo cha Yesu, baraka ya kuhesabiwa haki na kusamehewa dhambi kwa sasa; uzima wa milele baadaye, pamoja na neema ya kushinda dhambi katika maisha ya sasa; na kushirikiana na Mungu kibinafsi na kumtumikia kwa furaha. Kristo kama mjumbe wa Agano Jipya hutujalia mambo hayo yote, Yeye ni kama msimamizi wa mirathi.

k.16ku. Katika sehemu hiyo mwandishi amesisitiza lazima kabisa ya kuwepo kwa kifo cha kumwaga damu. Katika Agano la Kale, Agano lilitengenezwa kwa kumwagika kwa damu ya wanyama; na katika Agano Jipya kwa damu ya Kristo kumwagika. Katika kuzungumzia Agano hapo mwandishi ametumia maana ya Wosia. Ni desturi ya wanadamu wengi kufanya Wosia na kwa njia yake kutaja

wale wa kurithi mali yao. Ila watu hawawezi kupata sehemu ya urithi mpaka amekufa yule aliyefanya Wosia. Ndipo ataja yule au wale wa kusimamia Wosia, ambao wataangalia kwamba mali inagawiwa kufuata mapenzi yake jinsi yalivyoandikwa katika hati ya Wosia. Hao hufanya kazi mara kitokeapo kifo cha yule mtu. Kristo ni mwenye kufanya Hati ya Wosia na mwenye kutekeleza maagizo yake, akiwa hai baada ya Kufa. Amekuwa wote wawili, mwenye kufanya Hati na mwenye kutekeleza maagizo yake baada ya Kifo Chake kama vile alivyokuwa Kuhani Mkuu wa kutoa sadaka na Sadaka aliyoitoa Kuhani Mkuu. Hivyo, tuna hakika ya kushirikishwa baraka zote alizotupatia kwa Kifo Chake.

Kwa njia ya damu nyingi za wanyama kumwagika Mungu alikuwa akiwafundisha watu uzito wa dhambi na jinsi isivyowezekana kushirikiana naye bila kutolewa kwa dhabihu zilizoamriwa. Kwa kumwagika kwa damu ya Kristo neno hilo limethibitishwa kabisa, ni kifo cha kumwagika damu tu, tena ya Mwana wake, kilicho na uwezo wa kuondoa dhambi. Dhambi huleta mauti (Eze,18:4; Rum.6:23). Hati ya Wosia haina nguvu yo yote mpaka yule aliyeifanya amekufa.

k.18ku Mwandishi ameeleza jinsi ilivyokuwa wakati wa Agano la Kale. Mungu alipofanya Agano na Abramu, agano hilo lilitengenezwa kwa kutolewa kwa sadaka (Mwa.15:1-18) na Agano na Wana wa Israeli pia lilitengezwa kwa kutolewa sadaka zilizoamriwa (Kut.24:1-8). Twasoma kwamba watu wenyewe walinyunyiziwa damu, pamoja na Kitabu cha Agano, na hema, na vyombo vyote vya ibada. Hakuna kitu kilichohesabiwa kuwa „safi" bila kuwa na alama ya damu (Law.8:15,19; 16:14-16). Kwa kunyunyiziwa damu, watu wenyewe walihesabiwa watu wa Agano na washiriki wake, ndipo waliweza kuzishiriki baraka zake, ambazo zilikuwa za muda tu, na bila nguvu ya kusafisha dhamiri zao.

9:23-28 Sadaka ya Kristo ni ya namna pekee

Mwandishi ameendelea na mafundisho juu ya sadaka ya Kristo na upekee wake. Amesisitiza mambo matatu: damu ya Kristo ilikuwa bora kupita damu ya wanyama iliyomwagika, iwapo damu nyingi ya wanyama ilimwagika. Kwa sababu hiyo matokeo yake ni bora, yazidiyo matokeo yote yaliyopatikana kwa sadaka za wanyama. Pamoja na hayo, Kuhani Mkuu, aliingia katika Patakatifu pa Patakatifu, mahali palipotengenezwa na mikono ya wanadamu, ila Yesu aliingia mbinguni, usoni pa Mungu. Tena, tofauti na Kuhani Mkuu ambaye baada ya kuingia ilimpasa atoke tena mpaka uje mwaka mwingine, ndipo aingie na kutoka tena. Yesu yupo usoni pa Mungu sikuzote. Yupo pale, si kwa ajili yake, bali kwa ajili yetu, ili atupatie ushirikiano mwema na Mungu, ushirikiano udumuo, naye anatuhudumia baraka za Agano alilolifanya. Baada ya Musa kupewa uongozi juu ya kutengeneza Hema na vifaa vyake na mipango yake, yeye hakuweza kuingia mle ndani ya Hema. Ilikuwa wajibu wa

Kuhani Mkuu tu. Agano na Waisraeli lilipotengenezwa na dhabihu zilitolewa ndipo Musa, Haruni, Nadabu, na Abihu na watu sabini miongoni mwa wazee, „wakamwona Mungu wa Israeli" (Kut.24:9ku) nao wakashirikiana naye. Kisha Musa aliitwa kupanda mlimani ili apate mbao mbili za sheria za kuwafundisha Waisraeli. Tangu hapo hatusikii tena habari ya mtu ye yote ya „kumwona"Mungu.

Tunaposoma kwamba Yesu aliingia patakatifu halisi, yaani mbinguni, tusifikiri kwamba alikwenda na bakuli ya damu yake, kama Kuhani Mkuu alivyofanya na damu ya wanyama, la! Mara damu yake ilipomwagika pale Msalabani, upatanisho mkamilifu ulifanyika, sadaka yake ilikubalika mbele za Mungu, na kushuhudiwa katika Pazia la Hekalu kupasuka kutoka juu. Watu wa kale walisubiri sana kwa Kuhani Mkuu kutokea hali yu hai, nao walipomwona walifurahi sana, wakijua kwamba Mungu amewakubali. Yesu alifufuliwa kutoka watu na kwa sababu hiyo tunao uhakika wa sadaka yake kukubalika juu mbinguni. Halafu mwandishi amesisitiza kwamba Yesu ametoa sadaka kamili, mara moja tu, hana haja ya kuirudia, wala hairudiwi, kwa sababu ilikuwa ya nafsi yake. Sivyo ilivyokuwa kwa kuhani mkuu. Tusisahua kwamba, mkazo ni juu ya sadaka ya Yesu, mkazo huo ni kwa sababu sadaka ilikuwa kwa ajili yetu. Yeye Mwenyewe alikuwa Mungu kamili na Mwandamu kamili, asiyekuwa na dhambi, wala kujua, wala kufanya dhambi.

k.26 Mwandishi amesema kwamba Yesu alitokea „katika utimilifu wa nyakati" neno ambalo Paulo alisema katika Wagalatia 4:4 na Petro katika 1 Petro 1:20. Iwapo mwandishi amesema sana juu ya Kuhani Mkuu na Sikukuu ya Upatanisho, ni vema tukumbuke kwamba, hata kila siku makuhani walitoa sadaka za dhambi na za aina mbalimbali, wakihudumia penye madhabaha iliyokuwa katika Patakatifu.

Maneno „azitangue dhambi" ni maneno muhimu yanayoonyesha kwamba Yesu amefanya kazi kubwa sana, amefanya dhambi isiwe na nguvu yo yote tena (1 Kor.15:55ku) (Isa.53:12; 1 Pet.2:24) na kwa sababu hiyo, wanadamu wanao uwezo wa kushinda dhambi maishani mwao.

Katika kusubiri kwa muda mrefu ndipo kumtuma Kristo Mungu alikuwa amewapatia wanadamu muda mrefu sana wa kujifunza kwamba hawawezi kujiokoa wenyewe, ama kwa kufuata dini zao mbalimbali, ama kwa kufuata elimu na filosofia mbalimbali, ama kwa jitahada zao na bidii zao; ama kwa mbinu zao mbalimbali. Njia hizo zote hazikufaulu. Katika Kuja kwa Yesu na kwa kazi yake ya ukombozi tumefikishwa kwenye „nyakati za mwisho" kwa sababu Mungu hana zaidi la kufanya kwa ajili yetu, maana, sasa kwa Kifo cha Yesu, njia imekuwa wazi kwa mtu ye yote, wakati wo wote, kumkaribia Mungu bila kizuizi cho chote, hali akitegemea Kifo cha Yesu.

k.27-28 Kila mwanadamu anakufa kwa mara moja tu, kamwe harudi tena duniani. Ndipo hukumu ya Mungu inamngojea. Lakini sivyo ilivyo kwa Kristo. Alikufa mara moja ili kwa Kifo Chake awakomboe wanadamu; akarudi juu kule alikotoka, na kutoka pale anawahudumia watu baraka za ukombozi wake. Kisha atarudi tena duniani. Kufanya nini? Kuwachukua wale wanaomsubiri, wale wote waliomtumaini kwa wokovu, ili wapate matimizo ya ukombozi wao, yaani miili yao kukombolewa. Kwa sasa, roho za waumini zimeokolewa, ila bado miili yao ni dhaifu, ndipo Kristo atakapotokea, watajaliwa miili mipya, miili ya ufufuo, miili yenye uwezo mpya, miili itakayofaa kwa maisha katika uzima wa milele (1 Kor.15:51ku. Rum.8:23). Wakati wa kuokolewa utakuwa umepita, ni wakati wa matimizo ya wokovu kwa wale waliomweka tumaini lao katika Kristo. Jambo hilo ni kwa wote „wamtazamio".

MASWALI

1. Eleza ubora wa sadaka ya Kristo na kuonyesha upekee wake.

10:1-10 Kristo alitoa dhabihu ya nafsi yake kwa hiari

Katika vifungu vinne vya kwanza mwandishi amejumlisha hoja yake juu ya Ubora wa dhabihu ya Kristo.

k.1a Kama kawaida yake ya kulinganisha, ameonyesha kwamba dhabihu na sadaka na mipango kuhusu Sikukuu ya Upatanisho n.k. hayo yote yalikuwa „kivuli" tu, si kitu chenyewe, na kwa sababu yalikuwa kivuli tu yaliashiria kile kitu halisi, ambacho ni Kristo na dhabihu yake moja iliyotosha kuondoa dhambi. Kile „kivuli" cha mipango katika Agano la Kale kilitoa picha nzuri na sawa nacho kilieleza vizuri dhabihu ya Kristo iliyotolewa mara moja. Bila ishara watu wasingalielekezwa na mpata Kristo na bila kivuli wasingalimtambua Kristo na kuelewa Yeye na kazi yake. Tofauti moja ni kwamba aliyeitoa dhabihu hiyo kamili ni Kristo, akiwa dhabihu pamoja na Kuhani Mkuu aliyeitoa hiyo dhabihu. Mfano mzuri ni wa mtu anayeichukua picha ya mkewe mfukoni mwake, ni picha iliyo sawa, ya mkewe, lakini si mkewe hasa, maana hawezi kuzungumza naye, wala kushirikiana naye, na mkewe wa picha hawezi kumpikia n.k. kwa kuwa ni picha tu. Ndivyo ilivyokuwa mipango iliyoamriwa na Torati, ilitoka kwa Mungu aliyempasha Musa habari zake alipokuwa mlimani. Mipango hiyo haikuwa bure, ilikuwa na kazi maalum ya kufundisha na kutayarisha kwa Kristo, ila yenyewe haikuweza kuyatimiza mambo yaliyoashiriwa.

k.1b-2 Halafu mwandishi alisisitiza kwamba kama dhabihu zile za zamani zingaliweza kuondoa dhambi zisingalitakiwa kutolewa kila mwaka. Zilikuwa dhaifu, hazikuweza kuzigusa dhamiri za waabudio na kuzitakasa, kwa kuwa, kama wangalisikia wamesafika kwa ndani wasingalisikia haja ya kurudia kutoa sadaka tena.

k.3 Kila mwaka watu walikumbuka dhambi zao, kila Sikukuu ya Upatanisho ilishuhudia kwamba Dhabihu zilizotolewa mwaka uliopita hazikutosha. Walifahamu nafsini mwao kwamba dhamiri zao ziliendelea kuwashtaki na ya kwamba walihitaji sadaka zitolewe tena. Mungu pia alitulizwa na dhabihu zilizotolewa, ila bado hazikumridhisha kabisa, kwa hiyo, dhabihu zitolewe tena na tena, maana dhambi bado haijaondolewa mbele zake. Dhabihu zilikuwa kama kitulizo tu, mpaka kuja kwa Kristo na dhabihu yake kamili.

k.4 Kwa maneno ya kifungu hicho mwandishi amesema wazi kabisa kwamba haikuwezekana damu ya wanyama iondoe dhambi. Hao wanyama walichukuliwa tu, bila kibali chao, na bila wao kufahamu sababu ya kuchinjwa kwao, kwa hiyo, haiwaziki kwamba damu yao ina uwezo wa kuondoa dhambi. Je! Itawezaje wanyama wasiojua maadili, wala mambo ya mema na mabaya, waondoe dhambi. Dhambi ni kitu kihusikacho na maadili. Je! Mungu mwadilifu atawezaje kukubali kitu kisicho na hali yo yote ya uadilifu? Je! Kitu cha kimwili chaweza kuondoa kitu kihusikacho na nafsi na roho ya mtu? La! Sivyo! Hakuna usikilizano au ushirikiano kati ya mtoa sadaka na sadaka yenyewe.

Ila jambo muhimu kabisa ni kwamba watu walifundishwa kwa njia hiyo ya damu nyingi za wanyama wengi kumwagika kila siku na kila mwaka, daima. Walifundishwa kwamba dhambi ni jambo zito sana machoni mwa Mungu na dhambi haipatilizwi mpaka uhai umetolewa mpaka kufa. Hapo nyuma, wakati wa Agano la Kale, upatilizo wa muda ulipatikana kwa njia ya uhai wa wanyama wengi sana kutolewa mpaka kufa, Ndipo Agano Jipya lilitengenezwa kwa njia ya uhai wa mmoja, Mwanadamu Yesu Kristo, asiyekuwa na dhambi, kutoa uhai wake mpaka kufa, ili awe fidia ya wenye dhambi (Mk.10:45), ndipo dhambi ilipatilizwa kabisa.

k.5-7 Hapo mwandishi ameyatumia maneno kutoka Zaburi 40:6-8 ili atoboe wazi hali bora ya dhabihu ya Kristo. Mungu alimwekea mwili, mwili wa mwanadamu, kwa kusudi la kufanya mapenzi yake. Kristo alikuja ili afanye mapenzi ya Mungu, yaani, amtii Mungu katika mambo yote. Kwa hiari yake mwenyewe, na kwa kutaka, na kwa moyo mkuu, Yesu alijitoa kufanya mapenzi ya Baba yake. Aliishi maisha matakatifu, hakufanya dhambi, iwapo alijaribiwa sawa hata kupita wanadamu wengine wote. Twakumbuke taabu yake katika Gethsemane alipofikia upeo wa mwenendo wa kumtii Baba na kukaribia Kifo chake Msalabani. Alijaribiwa sana sana asimtii Baba yake. Alihitaji mwili kwa kujitoa kwake tangu kuzaliwa kwake na ni katika mwili wa kibinadamu alimtii Mungu wakati wote. Kwa sababu hakuwa na dhambi, wala kufanya dhambi, alistahili kutoa dhabihu ya nafsi yake na kutoa uhai wake katika kufa ili afidie dhambi. Zamani za kale, wanyama waliotolewa kwa sadaka, budi wasiwe na madoa au mawaa, tena wasiwe wamezeeka, au kupatwa na ajali n.k. lazima wawe wanyama walio wazuri sana katika kundi.

k.7 „ndipo niliposema, Tazama, nimekuja (katika gombo la chuo nimeandikiwa) Niyafanye mapenzi yako, Mungu". Maneno hayo ya Zaburi yanaonyesha jinsi Yesu katika umilele, alijitoa kufanya mapenzi ya Mungu. Alikubali kufanyika mwanadamu. Alijua kwamba Maandiko yalimhusu Yeye na kusema juu ya Kifo chake. Kwa mfano Isaya alitaja Mwana-Kondoo na Mtumishi Ateswaye (Isa.53). Hivyo, Kifo chake hakikuwa ajali, wala bahati mbaya, bali yalikuwa mapenzi ya Mungu.

k.8,9 Huenda kifungu hicho chatatanisha kinaposema kwamba dhabihu na matoleo n.k. Mungu hakuzitaka wala kupendezwa nao. Maana hayo yote yaliamriwa na Torati iliyotoka kwa Mungu. Imekuwaje Mungu hakuzitaka wala kupendezwa nazo? Kwa sababu hazikuweza kuchukua nafasi ya utii. Thamani ya dhabihu n.k. ilihusu fundisho lake. Mara kwa mara katika Agano la Kale, ubora wa utii kuliko kutoa dhabihu umeonyeshwa. Sauli aliposhindwa kumtii Mungu, Nabii Samweli alimwambia wazi kwamba kutii ni bora….(1 Sam.15:11ku). Nabii Isaya aliwaambia Waisraeli jinsi ambavyo Mungu alikuwa amekinai matendo yao ya dini, kama kuadhimisha Sikukuu, na kutoa dhabihu; afadhali wangalirekibisha maisha yao (Isa.1:11ku). Hosea na Amosi walisema vivyo hivyo, pia Micah (Mic.6:6-8). Mungu alitaka dhabihu ya moyo, ya mtu kutoa maisha yake kufanya mapenzi yake kwa furaha (Zab.51.16-19).

Katika Kuja kwa Kristo na kazi yake mipango yote ya kale imeondolewa, imekwisha kazi yake, na kwa sababu ni mwisho wa Agano la Kale, ni mwanzo wa Agano Jipya. Moja limeondoka ili liingie la Pili lililo bora, lenye uwezo.
Kwa jinsi alivyojitoa maisha yake yote kufanya mapenzi ya Mungu kwa moyo na kwa jinsi alivyojitoa uhai wake katika kufa, hata kufa kwa kusulibiwa, kama mhalifu wa hali ya juu, twatambua uzito wa dhambi, na gharama kubwa iliyotolewa katika kutuokoa na kututakasa (Isa.50:4ku) Amefanya zaidi ya kuondolea hatia, ametufanya kuwa safi machoni mwa Mungu.

Kwa hiyo, twajifunza kwamba dhabihu peke yake hazikutosha, wakati wote, hata wakati wa mipango ya kale Mungu alikuwa akitazama hali ya moyo na nia ya mtu, bila hali njema ya kutubu na kumpenda Mungu zile ibada zilikuwa tupu. Ila hatuwezi kusema kwamba hazikuwa na thamani yo yote ama Yesu asingalikuwa na haja ya kutoa thabihu ya nafsi yake, maana ni wazi kwamba maisha yake yote yalikuwa mema na ya kumpendeza Mungu.

k.10 Hapo mwandishi amesema wazi kwamba kwa utii wa Bwana Yesu katika maisha yake yote hata mpaka kutoa uhai wake katika kufa, wanadamu wamepata utakaso, utakaso kamili, utakaso unaoendelea kufanya kazi yake na kumwezesha mtu adumu kuwa mtakatifu akiishi kwa imani katika Kristo (1 Kor.1:30). Kwa Kifo cha Yesu mtu amefanywa kuwa anastahili kuingia mbele za Mungu na kumwabudu kama Mungu atakavyo (Yn.4:23,24).

10:11-18 Utimilifu na ukamilifu wa Dhabihu ya Kristo

k.11,12. Hapo mwandishi ameonyesha tofauti kubwa kati ya dhabihu zilizotolewa na makuhani na dhabihu moja iliyotolewa na Kristo. Ametoboa wazi tofauti hiyo kwa maneno machache „kila kuhani *husimama* kila siku akitoa dhabihu zile zile mara nyingi, ambazo haziwezi kabisa kuondoa dhambi". Makuhani walikuwa na shughuli nyingi, penye hema ya kukutania na baadaye, katika hekalu, daima hao makuhani walikuwa na kazi nyingi, hata hawakuweza kupumzika, hawakuweza kuketi na kupumzika kidogo, maana dhabihu zilitolewa mara nyingi. Tena dhabihu hizo hazikuweza kuondoa dhambi, hasa walileta kumbukumbu la dhambi (k.3). Kuhani alipomaliza kutoa moja alijitayarisha kutoa nyingine. Sivyo ilivyokuwa kwa Kristo, Kuhani Mkuu. Yeye, mara baada ya kutoa sadaka ya nafsi yake, pale Msalabani, akapaa juu na *kuketi mkono wa kuume wa Mungu,* mahali pa mamlaka penye heshima kubwa. Pale Msalabani, alilia „Imekwisha" akionyesha ukamilifu wa dhabihu ya nafsi yake. Ilitosha kabisa kuondoa dhambi na ilipata kibali cha Mungu kuwa hivyo.

k.13 Tangu hapo Yesu anafanya nini? Yesu atarudi tena na hapo kati anangojea mpaka adui zake wote wamekubali kwamba Yeye amewashinda. Ni ukumbusho wa maneno ya Zab.110:1; Zaburi iliyosema juu ya Kuhani Mkuu ambaye atafanana na Melkizedeki. Pamoja na hayo anawahudumia wanaomwamini neema wanayohitaji kwa maisha ya Kikristo. Anawapatia faida zote zilizomo katika hilo Agano Jipya, hasa msamaha wa dhambi na ngvu ya kushinda majaribu. Ila hana haja tena ya kutoa dhabihu yo yote kwa ajili ya dhambi.

Dhabihu yake ina matokeo ambayo hudumu milele, ina nguvu kabisa ya kuwakamilisha wale wote wanaomtumaini Kristo na Kifo Chake. Katika k.10 twasoma „tumepata utakaso" na hapo twasoma „wanaotakaswa" kama kazi hiyo bado ingali ikiendelea kufanyika. Jambo limetendekea, waumini wametakaswa na dhabihu ya Kristo, nao wanaendelea kutakaswa kwa sababu wangalimo ulimwenguni na kupatwa na majaribu mengi na vipingamizi vingi. Kila siku wazidi kushinda dhambi na kuishi maisha yanayodaiwa na Mungu wao aliye Mtakatifu (Tit.2:14; Ebr.2:10-11). Wamewekwa kando, ndiyo maana ya utakaso, ili wampendeze Mungu katika kumwabudu na kumtumikia.

k.15-18 Kisha mwandishi afunga sehemu hiyo yote kwa kurudia kutaja tena habari ya Agano Jipya jinsi nabii Yeremia alivyotabiri juu yake (Yer.31:31-34). Alikuwa amelitaja hapo nyuma (8:10ku). Pale mkazo wake ulikuwa juu ya Upya wake, hapo mkazo wake ni juu ya Ukamilifu wake. Aliona ya kuwa Roho Mtakatifu alikuwa amemwongoza Yeremia katika utabiri wake na sasa utabiri huo umetimizwa. Agano Jipya limetengenezwa na Yesu Kristo na baraka zake kubwa ni kwamba sheria za Mungu zinaandikwa mioyoni mwa watu na katika nia zao. Kwa hiyo, badiliko kubwa ni kwamba Agano Jipya lafanya kazi mioyoni

mwa watu, lile la Kale lilikuwa nje ya watu, sheria ziliandikwa kwenye mbao za mawe. Kwa msaada wa Roho Mtakatifu watu watajua ndani ya nafsi zao sheria za Mungu, wala si hivyo tu, watakuwa na nia na uwezo wa kuzitimiza (Mdo.1:8; Efe.3:16). Pamoja na hayo, jambo kubwa sana ni watu kusamehewa dhambi zao kabisa kabisa. Kwa dhabihu za zamani, dhambi ilikumbukwa (k.3) kwa dhabihu ya Kristo dhambi inaondolewa na kusahauliwa na Mungu, si kwa sababu ya udhaifu wa kusahau, bali kwa uamuzi wa kutokukumbuka. Kama tusomavyo katika Zab.103:12 na Isa.1:18 dhambi inawekwa mbali nasi kabisa.

Kama ni hivyo, hamna haja tena ya dhabihu au toleo lo lote kwa ajili ya dhambi. Nyingine haitakiwi, haitafanya kazi yo yote; tena ikitolewa itaonyesha dharau kwa ile iliyofanyika na Kristo. Ipo njia moja ya kumwendea Mungu, iliyo na manufaa na uwezo kufanya kitu kwa wanadamu, nayo ni Kristo na Kifo Chake.

Mambo hayo yote hutufundisha utakatifu wa Mungu, na ubaya wa dhambi, na haja yetu ya kutakaswa. Pia twajifunza kwamba kila mwanadamu, baada ya kufa, ataitwa kutoa habari zake mbele za huyo Mungu Mtakatifu ambaye katika upendo wake mkubwa alimtoa Yesu ili tupate msamaha na utakaso. Kisha twajifunza kwamba Kristo aliyekuja mara ya kwanza atakuja tena ili aukamilishe wokovu wa wale wote wanaomtazamia, ndipo miili yetu itakombolewa na kutolewa katika unyonge wake (Rum.8:23). Hivyo, twaona umuhimu na ulazima wa Upatanisho uliofanyika na Yesu pale Msalabani.

10:19-25 Faraja

Katika 13.22 mwandishi alieleza andiko lake la waraka huu kuwa „neno hilo lenye maonyo" kwa sababu alikuwa akiwaandikia Wakristo waliohitaji kufundishwa, kutiwa moyo na kuonywa. Baadhi yao walivutwa kurudi kwenye imani ya Kiyahudi, kwa sababu ya mateso na shida walizozipata katika kumfuata Kristo. Waandishi wa Agano Jipya walizoea kutoa mafundisho halafu kutoa mwongozo wa kuwasaidia waumini ili wayatekeleze hayo mafundisho katika maisha ya kila siku, wakiunganisha na mafundisho na maadili katika maisha ya Kikristo. Huyo mwandishi wa Waraka huu alikuwa na mzigo sana juu ya wale aliokuwa akiwaandikia.

Hapo nyuma amewakumbusha juu ya kazi kubwa sana ambayo Yesu amefanya kwa ajili yao, akiwa Kuhani Mkuu aliyeitoa dhabihu ya Nafsi yake na kufa kwa ajili ya kufanya upatanisho kati ya Mungu na wenye dhambi. Pia amewafundisha juu ya kazi kubwa ambayo Yesu angali akiendelea kufanya. Akiwa Kuhani Mkuu anaendelea kufanya huduma yake, mbele za Mungu Mwenyewe, akiwawakilisha wanadamu na kuwapatia nafasi ya kuingia mbele za Mungu, hali wakiitegemea dhabihu yake. Kristo ni mjumbe wa Agano Jipya na kwa sababu hiyo anawahudumia waumini baraka zote zilizopatikana kwa Agano alilolifanya.

k.19 „Basi" neno hilo ni kama daraja kati ya mafundisho yaliyotangulia na mashauri juu ya utekelezaji wake katika maisha ya kila siku.
Kwanza amezitaja fadhili mbili walizo nazo. Moja ni „ujasiri wa kupaingia patakatifu kwa damu ya Yesu"; nyingine ni „kuwa na kuhani mkuu juu ya nyumba ya Mungu". „Tuna ujasiri wa kuingia…" yaani waumini waweza kumkaribia Mungu na kuzungumza naye bila wasiwasi wo wote na bila kizuizi cho chote. Yesu aliingia mbele za Mungu, na waumini waweza kuingia mbele za Mungu, yaani wana haki kabisa kufanya hivyo kwa sababu ya Yesu mtangulizi wao. Ni fadhili kubwa sana kuwa na nafasi ya kumwomba Mungu, wakati wo wote, bila kumpitia mtu ye yote, kwa sharti moja tu, la kumwamini Kristo na kukubali kwamba amefanya yote yaliyotakiwa kufungua njia hiyo, twaingia kwa „damu ya Kristo" yaani kwa Kifo Chake. Ni njia mpya ambayo haikuwepo hapo nyuma. Kwa maelezo katika sura zilizotangulia tumeona jinsi njia ilivyobanwa kwa watu wote isipokuwa kwa mtu mmoja tu, tena hata kwa yeye ilikuwa kwa mara moja katika mwaka tu, tena katika mahali pamoja palipoamriwa tu. Sasa njia ni kwa ye yote anayemwamini Kristo; kwa wakati wo wote, na kwa mahali po pote, ndiyo sababu imeitwa njia mpya. Tena imeitwa njia hai, kwa sababu yule aliyeipasua yu Hai, iwapo alikufa kama dhabihu, alifufuka kutoka wafu, hakubaki kuwa mfu kama wala wanyama waliochinjwa walivyobaki. Pazia lilizuia watu wasiingie ndani ya Patakatifu pa Patakatifu, sasa kwa „kupasuliwa kwa mwili wa Yesu pale Msalabani" njia ya kumwendea Mungu imekuwa wazi. Siku ile Yesu alipokufa pazia la hekalu lilipasuka kutoka juu, kama ishara ya kutangaza kwamba njia imekuwa wazi, ni kama kusema **karibu**! Bila shaka makuhani waliokuwemo hekaluni siku ile waliogopa sana.

k.21 „na kuwa na kuhani mkuu juu ya nyumba ya Mungu" Huyu Kuhani Mkuu, Yesu Kristo ana mamlaka, yeye ni „juu ya" nyumba ya Mungu. Yafikirwa kwamba maana ya nyumba ya Mungu ni jamii ya waumini. Kuhani Mkuu tuliye naye ametuhakikishia ruhusa ya kuingia mbele za Mungu ili tumwabudu, na kumwomba. Yesu anao uwezo na madaraka ya kuongoza mambo ya watu wake, pia Yeye yu hai ili atuombee daima (7:25). Kwa sababu Yeye yu mbele za Mungu daima waumini wanao uwezo wa kuisha maisha ya kiroho na kushirikiana na Mungu.

Halafu baada ya kutaja fadhili za waumini, ndipo wajibu zao tatu zimetajwa. k.22 „na tukaribie…." k.23 „na tulishike…." k.24 „tukaangaliane sisi kwa sisi…".

k.22 Wajibu wa kwanza kwa hao Wakristo katika kuitikia fadhili walizojaliwa ni kumkaribia Mungu, wawe na ujasiri wa kumwendea, washike nafasi kubwa ambayo sasa ipo kwa ajili yao, wawe na mazoea ya kumwabudu na kumshukuru na kumwomba. Fadhili hiyo ni ya ajabu, imepatikana kwa Kujitoa kwa Yesu. Yesu alitoa maisha yake yote kila siku hata mpaka alipojitoa kabisa katika Kufa kuwa fidia ya dhambi na baada ya Kufufuka kwake anaendelea kujitoa na kutumikia, akiwa mjumbe na mdhamini wa Agano Jipya, pamoja na

kuwaombea watu wake kwa Baba yake. Basi waitumie nafasi hiyo. Wapaswa wawe na hali gani? Wawe na ujasiri, wasiogope kumwendea Mungu, wasiwe walegevu, wasifikiri kwamba hawafai, maana ni Yesu aliyestahili ambaye anawastahilisha. Hali nyingine ni kuwa na moyo wa kweli, wawe wanyofu wakitamani sana kutafuta ile neema itakayowawezesha kufanya mapenzi ya Mungu. Hali nyingine ni kuwa na utimilifu wa imani, yaani wategemee kabisa ule upatanisho alioufanya Yesu, wajue kwa hakika kwamba Yesu amewapasulia njia, na kwa imani katika Yeye wawe wanamwendea Mungu na kumpa shukrani zao na kumweleza mahitaji yao. Macho yao yamkazie Yesu, Kuhani Mkuu. Halafu mwandishi ametaja habari za usafi wa moyo na kuoshwa mwili. Yaani usafi wa ndani na usafi wa nje. Kwa damu ya Kristo dhamiri zao zimetakaswa na mioyo yao imesafika, kwa hiyo, wanapomkaribia Mungu wawe na ujasiri wa kujua kwamba Mungu huwapokea kwa sababu wametakaswa na damu, yaani sadaka ya Kristo. Kuoshwa mwili, inaonekana maneno hayo yanahusu ubatizo, kwa kuwa mtu hukiri imani ya ndani kwa tendo la nje la kubatizwa, ubatizo ukiwa ishari ya nje ya kuithibitisha imani ya ndani.

k.23 Wajibu wa pili ni „na tulishike sana ungamo la tumaini letu, lisigeuke". Wajibu huo umejengwa juu ya uaminifu wa Mungu aliyeahidi kuwalinda wale walio Wake. Jambo lingine kubwa ni tumaini. Waumini wamepewa ahadi mbalimbali za kuwatumainisha juu ya maisha ya sasa na ya baadaye. Kwa hiyo, waumini wamewajibika kuziamini ahadi hizo na kulishika tumaini lao (1 Yn.3:1-4). Mkristo hutumaini kwamba Yeye aliyeanza kazi njema ndani yake ataimaliza (Flp.1:6). Potelea mbali apatwe na vipingamizi na shida gani, Mkristo awe na tumaini kwamba haidhuru atapatwa na nini, mwishowe atashinda na kufika kwenye uzima wa milele. Hili lilikuwa jambo kubwa kwa hao walioandikiwa ambao walishambuliwa kwa sababu ya kumfuata Kristo. Wawe na uhakika juu ya uaminifu wa Mungu aliyewaita.

k.24 Ndipo wajibu wao wa tatu ni „tukaangaliane sisi kwa sisi na kuhimizana katika upendo na kazi nzuri". Katika maisha ya Kikristo, mambo matatu ni makubwa, imani, tumaini, na upendo, na kama isemavyo katika 1 Kor.13:13 pendo ndilo neno lililo kuu. Lazima wapendane, na katika kupendana wawe na mzigo juu ya kila Mkristo mwenzao. Hasa katika kukusanyika pamoja, wasilegee. Inaonekana baadhi yao wameacha kuihudhuria mikutano yao, hatujui sababu zao, labda walikuwa na kiburi na kujiona kwamba wanayo nguvu ya kutosha kuishi maisha ya Kikristo bila kukutana na wenzao. Labda walifikiri kwamba wakikutana watavuta usikivu wa watawala na kupata shida, au pengine wamepoa kwa sababu walifikiri kwamba Bwana Yesu atarudi na kumbe amekawia. Mwandishi hakusema sababu zao ila ni wazi kwamba aliziona kuwa hazitoshi. Kwa nini wakutane? Jambo moja ni kuhimizana katika upendo na kazi nzuri, yaani watieni moyo, kama kuchokozana ili waziamshe nia za wenzao kusudi waonyeshe upendo kiutendaji na kufanya matendo mema. Wasidai kuwa Wakristo bila kuishi kama Wakristo. Halafu mwandishi ametaja „waonyane" yaani upendo wao usiwe laini bali uwe na nguvu ya

kuwaonya wale ambao walihitaji kuyarekebisha maisha yao. Mwandishi amesema kwamba wazidi kufanya hivi „kwa kadiri mwonavyo siku ile kuwa inakaribia". Ni siku ipi inayokaribia? Wengi hufikiri kwamba ni siku ya Kurudi kwa Bwana Yesu, kwa sababu, zamani zile wengi walidhani kwamba Kristo atarudi mapema. Baadaye mawazo kama hayo yalipoa walipoona ya kuwa Kristo hajarudi bado. Wazo lingine ni kwamba siku ile ni siku ya kujaribiwa sana, wakati serikali itakapochukua hatua ya kuwatesa Wakristo. Haidhuru ilikuwa siku gani, iliyotakiwa ni wao kujiweka tayari kwa ajili yake kwa kupendana na kukutana, kusaidiana na kushauriana, kuonyana na kutiana moyo, ili wasilegee na kupoa kisha wakarudi nyuma.

10:26-31 Onyo kali

Mwandishi anaendelea kuonyesha uhusiano uliopo kati ya „kujua" na „kufanya" yaani kuyatekeleza mafundisho makubwa ya Kikristo katika maisha ya kila siku. Katika Waraka huo mzima mwandishi amekuwa na desturi ya kutoa maonyo mara kwa mara: taz, 2:1ku; 3:17ku. 5:11ku. na mara kwa mara amewasihi wawe na tahadhari sana 3:12; 4:1,11. Kwa hiyo, hapo tena, amewaonya kwa ukali juu ya hatari ya kuasi. Ni kama anataka kuamsha ndani yao utambuzi wa hatari waliyo nayo katika kulegea na kutokujali, kabla hawajafika kwenye hatua ile ya kufanya mioyo yao kuwa migumu hata wasiweze kujirekibisha.

k.26 Inaonekana jambo linalozungumzwa hapo si lile la Mkristo dhaifu ambaye ameteleza kidogo, au amefanya dhambi bila kutambua ni dhambi, bali ni hali ya Mkristo ambaye amejua kweli za Mungu nafsini mwake wala si kwa kichwa tu, hali ametiwa nuru kwa msaada wa Roho Mtakatifu. Mtu huyo yu katika hali mbaya sana, ya hatari kabisa, kwa sababu hakuna njia ya uponyaji, kwa sababu, hakuna dhabihu nyingine iliyopo kwa kumsamehe dhambi zake ikiwa amemdharau Kristo na Kufa Kwake kwa dhambi zake.

k.27-28 Imembakia nini mtu wa namna hiyo? Imebaki hukumu kali ya Mungu aliye Hai. Tazama ni kwa „wao wapingao" yaani kwa wale ambao wamempa kisogo Kristo na kumwasi. Wamejitenga na Kristo, pengine wameisha kurudi kwenye dini ya Kiyahudi (1 Yn.2:19). Halafu mwandishi ametaja hukumu iliyowapata waasi chini ya Agano la Kale. Ikiwa uasi wao ulithibitishwa na mashahidi wawili au watatu, basi waliuawa bila huruma, kwa hiyo, swali ni kwamba, Je! Hao wanaoliasi Agano Jipya lililofanyika na Yesu wameistahili hukumu gani? Si hukumu inayozidi ile ya zamani? (Kum.16:6ku. 17:2ku). Ni wazi kwamba jambo linalozungumzwa halihusu tendo moja bali hali iliyochaguliwa na kukazwa.

k.29 Hapo mwandishi ameweka wazi mambo matatu makubwa ambayo hao wapinzani wameyafanya.

i. „wamemkanyaga Mwana wa Mungu" yaani wamekataa, tena, kwa kusudi, kuamini kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu. Neno „kanyaga" ni neno gumu la kuonyesha kwamba mtu amekataa kwa kusudi, si kwa bahati mbaya au kwa kutokuelewa.

ii. „wamehesabu damu ya agano waliyotakaswa kwayo kuwa ni kitu ovyo" ni ile damu iliyoitakasa dhamiri zao, damu ya Kristo iliyomwagika Msalabani, iliyo na nguvu ya kutakasa mtu na dhambi zake. Sasa damu hiyo imekuwa kwao kitu ovyo, haina maana yo yote, wameidharau sana. Damu hiyo, yaani dhabihu ya Kristo, ilikuwa muhimu kabisa katika mtu kupatanishwa na Mungu na kusamehewa dhambi zake na kuletwa kwenye uhusiano mwema na Mungu. Kama mtu ameidharau hiyo sadaka ya Kristo, atapata wapi kitu kingine cha kuondoa dhambi zake?

iii. „na kumfanyia jeuri Roho wa neema" Ni kwa kazi ya Roho Mtakatifu mtu husaidiwa kumfahamu Kristo na wokovu wake, na kufanywa upya na kufanywa kuwa mtoto wa Mungu, mwenye kibali chake. Kwa Roho mtu huletwa kwenye uhusiano mwema na Mungu na kwa neema apata nguvu ya kuishi maisha ya Kikristo. Kwa hiyo, mtu akiichezea neema hii na kuidharau kabisa, hata kumdhihaki Roho wa Mungu, huyo mtu amejiweka mbali na msaada (Yn.14:26; 16:8,13). Ni mfano wa mgonjwa anayekataa mashauri na dawa za daktari. Ni nani atakayemsaidia kuelewa ugonjwa wake na kumpatia dawa za kutumia n.k.?

k.30-31 Kisha mwandishi amefunga onyo lake kale kwa kutumia Maandiko kuhusu Mungu na hukumu yake (Kum.32:35ku. 33:27ku. Amo.3:1,2). Ni Mungu mwenye kupatiliza kisasi, ni Mungu atakeyewalipa watu kwa uasi wao. Mungu yu hai, kwa hiyo, si jambo rahisi kuanguka mikononi mwake. Ila twakumbuka Mwana Mpotevu alipenda kuanguka mikononi mwa Baba yake aliporudi nyumbani na kutubu maovu yake (Lk.15:20). Hata Daudi zamani, alipotambua kwamba ameiasi amri ya Mungu alimrudia Mungu (2 Sam.24:24).
Kuasi ni zaidi ya kuvunja amri kadha bali ni *kuuvunja uhusiano*, jambo zito. Kukutana na Mungu aliye Hai, Mtukufu, Mtakatifu, ni jambo la kutisha, tusipokuwa na imani ya kweli katika Yesu Kristo.

10:32-39 Mwito wa kuenenda kwa ushujaa

Mwandishi, kama ilivyokuwa desturi yake, baada ya kutoa onyo, alitoa mwito wa kuwatia moyo wa kudumu akitumaini kwamba baada ya kuonywa watayapokea maonyo yake na kujirekebisha, maana hakutaka kuendelea kusemasema juu ya mambo yaliyomtia yeye wasiwasi na yaliyowatisha wao juu ya hatari ya hukumu ya Mungu (5:11-6:8).

k.32-35 Jambo la kwanza, aliwashauri wakumbuke jinsi walivyoishi siku zile za kwanza walipoanza kumwamini Kristo. Waliishije! Waliishi maisha ya ajabu

sana. Inaonekana waliteswa sana na kudharauliwa. Hawakuzijali dhihaka za watu, hata waliposhtumiwa hadharani mwa watu na kuonewa mashaka na kushtakiwa kwa uongo. Walifurahi waliponyanganywa mali zao, kama Bwana Yesu alivyofundisha wafuasi wake. Walihesabu mali ya dunia hii si kitu kwa sababu ya kuwa na mali ya maana sana, wakiwa na Kristo na kibali cha Mungu na msaada mkubwa wa Roho. Basi, walifurahi sana wala hawakuzisikitikia hasara walizozipata. Mtu asiye Mkristo hana budi kuvumilia shida anazopata ila hatazifurahia, ataziona kuwa ni bure tu. Tena, wakati ambapo wao wenyewe waliachiliwa kuteswa, huku wenzao waliteswa, waliwahurumia na kushirikiana nao wakitembelea wale waliofungwa gerezani, bila kujali hatari ya kukamatwa. Waliwapenda na kuonyesha huruma, na kuwasaidia kwa mali zao na kuwatunza familia zao. Iwapo hatujui mambo hayo yalitokea wapi, kama Rumi, au penginepo, liko wazo la kufikiri kwamba yawezekana ni wakari wa Kaisari Klaudio ambaye alipokuwa Kaisari huko Rumi kama B.K.4l aliwabana Wakristo sana na sheria kali, na baadaye twajua aliwafukuza waondoke Rumi.

k.35-36 Mwandishi aliwaambia wazi kwamba wasiutupe ujasiri wao, wakumbuke jinsi walivyokuwa mwanzoni kwa sababu ni katika kudumu waumini wanaonyesha uhalisi na ukweli wa imani yao. Ni wale wadumuo *mpaka mwisho* ambao wataokolewa. Ipo thawabu ya milele kwa wale wanaodumu. Jambo wanalohitaji ni kuvumilia mpaka Kristo atakaporudi au mpaka atakapokuja kuwachukua wakati wa kufa kwao na kuwapokea Kwake. Wakristo wapaswa kuamini kwamba Kurudi kwa Kristo ku karibu wakati wote. Mungu ameahidi kwamba Kristo atarudi (Mdo.3:19,20; 1 The.1:10; Ebr.6:12). Walianza maisha ya Kikristo kwa imani na maisha hayo yaendelezwa kwa imani, na kwa imani Mkristo atamaliza safari yake.

k.37-40 Kisha mwandishi alidondoa maneno kutoka Hab.2:3-4 juu ya umuhimu wa imani kwa yule aliyehesabiwa haki kwa imani. Yampasa aishi kwa imani hata anapoteswa au kupata shida kwa sababu ya imani yake. Kusitasita hakumpendeza Mungu hata kidogo. Mwandishi ametumaini kwamba wale anaowaandikia watayajali maonyo aliyowapa pamoja na mwito mwema wa kuwatia moyo. Bila shaka wakikumbuka hali yao ya kwanza na jinsi walivyovumilia mengi, tena kwa furaha, haiwaziki kwamba watashindwa kuendelea. Mwandishi hajakata tamaa juu yao.

MASWALI

Eleza tofauti zilizpo kati ya sadaka ya wanyama na sadaka ya Kristo?

Kwa nini dhabihu ya Kristo ni kamili?

Wakristo hutiwa moyo wa kudumu kuwa waaminifu kwa faraja ya Mungu. Faraja hiyo ni ya namna gani?

Kwa nini kila mara mwandishi alikuwa anawaonya waumini walioandikiwa?

11: 1-40 IMANI – MASHUJAA WA IMANI

Sura hii isomwe katika mwanga wa yote yaliyotangulia. Sura iliyotangulia ilimalizika na maneno „tumo miongoni mwa hao walio na imani ya kutuokoa roho zetu" (10:39). Ni imani katika ahadi za Mungu, ni kumwamini Mungu na Neno lake. Waraka ulianza „Mungu alisema zamani na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi, mwisho wa siku hizi amesema na sisi katika Mwana" (1:1,2) likiwa neno lake la mwisho. Halafu mwandishi alipitia katika historia yao akionyesha jinsi Mungu alivyosema nao kwa njia nyingi akisisitiza kwamba Mwana ni bora kuliko hao wote waliotangulia kama Musa, Yoshua, n.k. pia dhabihu yake ni bora na ukuhani wake ni bora. Kwa hiyo, potelea mbali hapo nyuma watu walikuwa wamekuwa na imani gani, sasa wapaswa kumwamini Kristo na dhabihu yake kamili na ya kutosha kwa dhambi za ulimwengu wote.
Kwa wale waliokata shauri la kumwamini Kristo, budi waendelee kuishi kwa imani, hamna njia nyingine.

11:1-3 Imani ni nini hasa?

Katika vifungu hivi mwandishi ameeleza wazi maana yake. Imani ni kitu imara, ni msingi halisi wa kutegemewa na kujenga juu yake. Imani **si** wazo au dhanio fulani. Ni kumwamini Mungu na ahadi zake na neno lake, ni kutia maanani ufunuo wa Mungu, jinsi ulivyo katika Maandiko. Ni kuamini kwamba Mungu hufanya kazi katika historia ya wanadamu akiwa Yule anayeshika usukani na kuongoza mambo yanayotokea. Kuhusu mambo ya mbele ni kuwa na uhakika juu yake, mfano wa hati ya kumiliki, si ardhi, bali utukufu wa uzima wa milele katika maisha yajayo. Kwa macho yetu ya kimwili tunaona yaliyopo na kwa macho ya kiroho, ya imani, twaona yale yaliyo mbele ambayo Mungu amewaahidi waumini. Ni kuwa na hakika kwamba ndivyo itakavyokuwa. Mfano wake ni wa hakimu aliye na hakika juu ya kesi iliyo mbele yake. Ni kuwa na ujasiri wa kutenda mambo kuhusu kesi tunayojua kwamba kwa hakika haitaanguka kortini. Ni kumwamini Mungu na ahadi zake bila wasiwasi wo wote. Kwa hiyo, waumini wasiishi kwa kuangalia mambo jinsi yalivyo kwa sasa, kwa sababu, ya sasa hupita, waumini ni watu wanaosafiri katika ulimwengu huu na kuwa na tumaini „kufika nyumbani" kwa makao ya milele, kwa Mungu. Yaliyo mbele ni bora kuliko ya sasa.
Pamoja na hayo imani yahusu maisha ya sasa, waumini wapaswa kuwaza juu ya mambo yanayotokea katika wakati wao na kuyachunguza na kuyapima na kutambua ni nini ambayo Mungu anafanya na kuvumilia magumu yanayowapata.

k.2 Mwandishi amejaza sura hii na habari za wale walioishi zamani ambao kwa imani walitenda matendo makuu na kuyasababisha matukio makuu. Alianza na wale walioishi kabla ya Gharika ndipo Nuhu, halafu na wengine walioishi baada ya Gharika. Hao wote waliamini ujumbe na ahadi za Mungu kwao.

k.3 Kifungu hicho chasema juu ya Mungu na uumbaji wake. Kwa sababu hakuna aliyekuwepo wakati wa Mungu kuumba ulimwengu na vitu vyake (Mwa.1:1) hakuna njia ya kujua jinsi umbaji ulivyotokea. Ila Mungu amefunua habari zake katika Mwanzo, sura ya 1 na ya 2. Hivyo inampasa mtu aamini kwamba uumbaji ulitokea kwa Neno lake. Mara saba Mungu alisema na vitu mbalimbali vilitokea, vikaonekana, ambavyo kabla ya Mungu kutoa Neno lake havikuwepo wala havikuonekana. Ni neno la kuaminika. Sayansi yaweza kueleza jinsi vitu vinavyofanya kazi yake n.k. lakini haiwezi kueleza chanzo chake. Kwa hiyo, twaamini kwamba Mungu Yuko, naye ni asili ya vitu vyote.

11:4-7 Imani ya Habili, Henoko, Nuhu

Wa kwanza kutajwa ni Habili, na mwandishi amemlinganisha na ndugu yake Kaini. Hao walikuwa wa kwanza kuzaliwa. Habili alikuwa mchungaji na Kaini alikuwa mkulima. Kwa imani Habili alimtolea Mungu dhabihu iliyo bora kuliko Kaini, kwa hiyo, alishuhudiwa kuwa ana haki. Twaona imani na haki zimeunganishwa pamoja. Jambo ilihusu ibada. Sadaka haikuitwa sadaka ya dhambi. Kutokana na maneno ya Mwa.4:4ku.shida haikuhusu aina ya sadaka, ya Habili, mnyama; na ya Kaini, mazao ya ardhi; hasa ilihusu hali ya maisha yao, Kaini aliambiwa wazi „kama ukitenda vyema, hutapata kibali? Usipotenda vyema dhambi iko, inakuotea mlangani, nayo inakutamani wewe, walakini yapasa uishinde" (ling.1 Yoh.3:12). Mungu hakuwa na upendeleo alipomkubali Habili na sadaka yake. Habili alikuwa na moyo mzuri na nia njema, alitaka kumpendeza Mungu na kwa shukrani alimtolea Mungu sadaka nzuri „wazao wa kwanza wa wanyama wake na sehemu zilizonona za wanyama". Kwa nini Habili alikuwa na tabia hiyo? Ni kwa sababu alimwamini Mungu na kumtegemea katika maisha yake na kujua kwamba Mungu ni mwema. Ila Kaini hakujali, moyo wake haukuwa mnyofu mbele za Mungu. Kisha akamwua ndugu yake, akimwonea wivu kwa kuwa ndugu yake alipata kibali cha Mungu, kibali ambacho yeye mwenyewe angalikuwa nacho, kama angalikuwa na hali ile ya ndugu yake. „jjapokuwa amekufa, angali akinena" maana yake ni kwamba kwa njia hiyo aliishuhudia imani yake akimtolea Mungu sadaka nzuri, iliyomgharimu wanyama wazuri wa kundi lake, tena alifanya kwa furaha na shukrani. Tena alikuwa tayari kwa Mungu kumpatia haki yake (Mwa.4:10; Ebr.12:24). Ni ukumbusho wa sadaka ya Kristo iliyo bora kupita ile ya Habili.

k.5 Halafu mwandishi amemtaja Henoko, mtu aliyeishi kabla ya Gharika. Hatuna habari kwamba kwa miaka ya kwanza ya maisha yake alimpenda Mungu, ila alipofikia umri wa miaka 65 alimzaa mwana na kumpa jina Methusela, na tangu hapo kwa miaka mia tatu Maandiko yasema kwamba „akaenda na Mungu" (Mwa.5:22ku) yaani alimpendeza Mungu. Katika Yuda l:14:15 inaonekana alitoa unabii, pengine juu ya Gharika itakayokuja Mungu atakapowahukumu watu waovu wasipotengeneza mienendo yao. Maneno „kutembea na Mungu" huleta wazo la kushirikiana vema na Mungu, kuwa na uhusiano mzuri naye, kumpenda na kumtii. Henoko aliishi maisha yake kwa

imani, akitia maanani maneno ya Mungu. Nia yake ilipatana na nia ya Mungu. Kisha Henoko hakufa kama kawaida ya wanadamu, siku moja Mungu alimchukua na hakuonekana hapa duniani tena.

Jambo kubwa linalowahusu hao wawili, Habili na Henoko, ni imani yao, waliishi na kufanya walivyofanya kwa imani. Matendo yao na maisha yao yalikuwa matokeo ya kumwamini Mungu, wakitia maanani Neno lake na mapenzi yake.

k.6 Hapo mwandishi ametilia mkazo neno „imani" akionyesha jinsi imani ni msingi wa mambo yote. Kwanza kabisa, lazima mtu aamini kwamba Mungu yuko na ya kwamba mtu akimwendea Mungu atapewa thawabu na Mungu. Imani ni jambo linalompendeza Mungu na kwa imani mtu huhesabiwa kuwa na haki, yaani kuwa na uhusiano mwema na Mungu. Bila imani mtu huwa na kiburi cha kujitegemea na kujiona kwamba hana haja ya Mungu, hata aweza kuwaza kwamba hakuna Mungu, au kwamba Mungu hana la kumsaidia. Hali hiyo ni chukizo kwa Mungu. Katika uumbaji mtu huelekezwa kuona kwamba yuko Muumba asiyeonekana aliye nyuma ya vitu vyote vinavyoonekana. Tunapotazama uumbaji twaona utaratibu mzuri, twaona vitu vizuri vinavyoonyesha uzuri wa Muumba wake, twautambua uwezo wake mkubwa unaoendesha vitu vyote na kuiona hekima ya ajabu. Katika sura za kwanza za Kitabu cha Mwanzo twaambiwa jinsi ulimwengu na viumbe vyake vilivyotokea, kwa Mungu kusema „na iwe… ikawa" (Ebr.1:1-3; Zab.33:6,9; Zab.139).

k.7 Halafu mwandishi amemtaja Nuhu ambaye amejulikana sana kwa sababu ya tendo lake la kuiunda safina kabla ya kutokea kwa Gharika. Kwa nini aliiunda safina? Yeye na familia yake waliishi maili mia moja mbali na bahari, tena safina ilikuwa kubwa kuzidi mahitaji ya familia yake. Sababu kuu ni imani yake. Alikuwa mcha Mungu wakati wa watu wengine wote kuwa waasi, kwa hiyo haikuwa rahisi awe mwaminifu kwa Mungu. Hata hivyo, alitembea na Mungu na kuisikiliza sauti yake. Ndipo Mungu alimfunulia jambo la ajabu, alimwambia kwamba mbeleni ataleta hukumu juu ya waasi na kuwaangamiza kwa njia ya Gharika. Wakati wa kuambiwa, hazikuwepo dalili zo zote za Kuja kwa Gharika, wala haikutokea kwa miaka mia na ishirini. Hata hivyo, Nuhu akamwamini Mungu juu ya habari hiyo, akaanza kuandaa kwa ajili yake ili familia yake waokolewe, pamoja na ye yote atakayemcha Mungu kama yeye na kujiunga naye katika shughuli hiyo kubwa ya kuijenga safina. Hakikuwepo kitu cho chote kilichoonekana kilichomsaidia Nuhu ila ule ujumbe aliopewa na Mungu tu.

Habari hizo ni katika Mwanzo sura za 6, 7, na 8. Nuhu alianza kukata miti, na kuvikusanya vifaa, na kutayarisha kiwanja katika nchi kavu, ndipo polepole aliijenga hiyo safina. Pamoja na kujenga Nuhu aliwapasha watu habari za kuja kwa gharika. Bila shaka walikuwa na maulizo mengi, unafanyaje? Pia walimdhihaki na kumcheka, na kumpinga. Lakini yeye aliyavumilia hayo yote

huku akiendelea kujenga. Muda ulikuwa mrefu sana kati ya kuambiwa habari za gharika na gharika kufika, muda wa miaka mia na ishirini. Katika muda huo wote hakusita wala hakuchoka, kwa imani alidumu mwaminifu. Ni kama aliiona gharika iwapo ilikuwa bado haijatokea. Ni wa kwanza kuitwa mwenye haki (Mwa.6:9) na tunaona kwamba kuamini na kutii kunakwenda pamoja. Safina ilipokuwa tayari, Mungu alimwita aingie ndani yake pamoja na familia yake, jumla yao watu wanane, hakuna hata mmoja mwingine ambaye alivutwa kumwamini Mungu wakati huo wote, huku mtumishi wake ameonyesha imani na utii wa ajabu sana. Kwa hiyo, yeye kwa shughuli zake aliuhukumu ulimwengu kuwa na makosa. Kisha safina ilijaa wanyama na ndege n.k.!! Yesu alitumia siku za Nuhu kuwa mfano wa siku zitakazotangulia kurudi kwake. Watu watawapinga watu wa Mungu na kuwadharau (Mt.24:27-29; Lk.17:26ku). Matokeo ya imani ya Nuhu ni yeye na familia kuokolewa; watu wengine kushuhudiwa na kuonywa juu ya maisha yao, na yeye kuhesabiwa haki na kupata kibali cha Mungu na kushirikiana naye vema (1 Pet.3:20; 2 Pet.2:5).

11:8-19 Imani ya Abrahimu

Ibrahimu amewazidi wengi katika kuishi kwa imani na kumtegemea Mungu na kujenga maisha yake kwa kulitii Neno la Mungu kwake, hata ameitwa „baba" wa waumini. Habari ya Ibrahimu inapatikana Mwanzo 11:27 – 25:11.

k.8-12 Mungu alipomwita Ibrahimu kwa mara ya kwanza alikuwa akiishi katika Uru wa Wakaldayo pamoja na familia yake (Mwa.11:31; Yos.24:2; Mdo.7:2-5). Kwa imani aliondoka nyumbani asijue mahali pa kwenda maana Mungu hakusema kwa wazi ni wapi aende. Mwanzoni hakuambiwa juu ya urithi, alipoondoka alikuwa bado hajaahidiwa cho chote, kwa hiyo, hakuna kitu cha kumvuta, maana ahadi ya urithi ilitolewa baadaye kama zawadi ya utii wake (Mwa.13:14ku. I5:18; 17:8). Katika safari yao yeye na familia yake walifika Harani, na hapo baba yake Tera akafariki dunia. Kisha Mungu akamwita tena aondoke na kusafiri mpaka nchi ya ahadi.

Ni jambo gumu kwa mtu kuacha nchi yake na mambo ambayo ameyazoea na kuanza maisha mapya na mageni kwake. Ni dhahiri kwamba katika Uru walikuwa na maisha mazuri, ya furaha na amani na mafanikio. Uru ulikuwa na ustaarabu na maendeleo ya hali ya juu katika siku zile na sehemu ile. Historia imeshuhudia habari zake. Ibrahimu alionyesha ujasiri mkubwa akiwa tayari kuacha nyuma maisha ya Uru na mazoea yake mazuri akijitoa kwa maisha mageni, ambayo pengine yatakuwa magumu, maisha ambayo hana habari juu yake.

Alipofika katika nchi ya Kanaani aliishi humo kama mgeni na msafiri, akipita hapa na pale, na kuishi katika hema. Hakuwa na sehemu yo yote ya nchi ambayo ilikuwa mali yake isipokuwa kiwanja cha maziko alichokinunua kutoka kwa wenyeji kwa kumzika mkewe alipofariki (Mwa.23:6). Hata mwana wake na

mjukuu wake waliishi katika mahema. Hawakujaribu kufanya nchi ya ahadi kuwa nchi yao. Kwa nini waliishi hivyo? Jibu ni kwamba Ibrahimu alikuwa akiutazamia mji ulio bora, mji uliobuniwa na kutengenezwa na Mungu, mji wa kukaa milele. Kwa hiyo, alikuwa radhi na maisha yake ya Kanaani, hali akijua kwamba kuna mema zaidi yanayomngojea baadaye. Wangaliweza kurudi makwao, lakini walivumilia hali wakisubiri kufika kwenye ule mji wa Mungu. Hii ndiyo sababu Mungu hakuona haya kuitwa Mungu wao. Waisraeli walizoea kusema „Mungu wa Ibrahimu na Isaka na Yakobo" hata Yesu alilitumia jina hilo (Mt.22:32). Neno hilo lilifaa wale walioandikiwa kwa sababu walikuwa wakiitwa kuondoka katika dini yao ya asili, ya Kiyahudi, na kuvunja uhusiano wao na mazoea yao ya hapa nyuma, ili wapate kuishi kwa imani katika Kristo.

k.11 Vipi imani ya Sara? Mwanzoni alipoambiwa atamzaa mtoto katika uzee wake, akacheka, si kwa furaha, bali kwa kuona mashaka, na Mungu akamkemea. Alipozaliwa Isaka akafurahi, furaha ya kweli, kwa sababu ya Mungu kumtimizia ahadi yake (Mwa.18:12,13,15; 21:6). Wataalamu waona kwamba maneno ambayo yametafsiriwa „alipokea uwezo wa kuwa na mimba" si tafsiri kamili, kwa sababu neno ambalo limetumika lahusu uwezo wa mwanamume kutia mbegu si ya mwanamke kuipokea. Hata hivyo, inaonekana kwamba Sara mwenyewe alifika kwenye hatua ya kumwamini Mungu kwa sababu wote wawili, yeye pamoja na mumewe waliweza kumzaa Isaka, kama isemavyo katika k.12. Miili yao ilikuwa kama imekufa ila imani yao ilikua hai na imara. Ila si wakati wote Ibrahimu aliamini kwamba atampata mwana kwa Sarai. Polepole katika shida zilizompata alifika hatua hiyo, imani yake haikutokea moja kwa moja.

k.12 ling. na Rum.4:19,20. Ibrahimu alikuwa mzee sana wa kukaribia umri wa miaka mia na mke wake alikaribia umri wa miaka tisini, jambo hilo la kuchukua mimba lilipotokea. Ni dhahiri kwamba Ibrahimu alizingatia sana vile vizuizi vilivyokuwepo vya kuwazuia wasipate mtoto, yaani hali yake na hali ya mke wake kimwili, jinsi isivyowezekana kabisa wao wazae mtoto. Hakuwa mjinga, wala hakufumba macho, asiyaone hayo yote. Alijua kabisa kwamba hakuna uwezekano, wala hakuna matumaini yo yote, hata hivyo, kinyume chake, alithubutu kumwamini Mungu, kwa sababu ni Mungu aliyetoa ahadi, ahadi iliyomhusu Sara si mwanamke mwingine. Kimwili walikuwa wafu, ila kiroho walikuwa hai kwa Mungu kwa njia ya imani, na Mungu, kwa upande wake, alikuwa mwaminifu kwa zile ahadi zake kwao.

k.13-16 Hapo mwandishi ametuonyesha kwamba ijapokuwa Ibrahimu na Sara walimwamini Mungu na kuishi katika nchi ya ahadi, hata hivyo, waliishi kama wageni na wasafiri, kama watu wanaotazamia mji ulio bora, makao yao ya mbinguni, na kwa sababu hiyo, waliishi kama watu ambao walihesabu kwamba bado hawajafika kwenye makao ya kukaa na kudumu. Walionyesha subira nyingi wakiwa radhi kungojea ya baadaye. Walitambua kwamba mambo ya dunia hii hupita na kutoweka wala si ya kutegemewa. Ahadi ilibaki mioyoni

mwao nalo litatimizwa kwa ukamilifu katika maisha ya baadaye. Jambo hilo ni kielelezo kwa sisi Wakristo, kwa sababu, sisi pia twakiri kwamba tu wasafiri hapo duniani, tu wageni, kwetu ni mbinguni, ila mara nyingi, maisha tunayoishi hayashuhudii jambo hilo. Mara nyingi, twaishi kama watu wa kukaa hapa kwa muda mrefu. Twazitumia fedha zetu kwa vitu ambavyo si lazima kwa maisha yetu ya kila siku, huku wengi katika ulimwengu huu wanakufa kwa njaa na mabaa mbalimbali. Je! Mtu anayehama nyumba fulani, anafanyaje? Je anatumia pesa nyingi katika kuitengeneza? Sidhani. Yeye aishi katika matazamio makubwa katika nyumba anayoihamia, hajali ile anayoiacha. Kwa kielelezo chake Ibrahimu hukemea maisha ya raha na kujipenda ambayo wengi wetu huyatafuta. Walishi kwa imani na kufa kwa imani, bila kuona matimizo ya ahadi walizopewa, ila walizikaribisha kwa mbali. Walikuwa wageni na wapitaji (Flp.3:20; 1 Pet.1:17; 2:11). Vizazi vingi vitapita mpaka wazao wao watakapoishi Kanaani kama ni nchi yao.

k.17-19 Habari hii ni katika Mwanzo 22:1-14
k.17 Baada ya kuzaliwa na kukua kwa Isaka, Ibrahimu alipewa mtihani mkali sana kwa imani yake. Aliitwa na Mungu aende mahali fulani na kumtoa Isaka kuwa dhabihu. Ni nini katika mawazo ya Mungu ambayo yamfanya amwombe Ibrahimu amchinje yule yule mwenye kuendeleza „wazao wa imani"? Bila shaka neno hilo lilimtatiza Ibrahimu sana. Katika kumtii Mungu na agizo lake Je! atoe mwana wake mpendwa anayempenda sana? Tena, atoe yule yule ambaye Mungu Mwenyewe amewawezesha kumzaa. Ni katika yeye tu, peke yake, ambaye ahadi ya kurithi inaendelea kusimama. Ni nani atakayeirithi nchi, kama akimtoa huyo? Isaka hajaoa bado, wala hana watoto! Ajabu ni kwamba Ibrahimu hakusita wala kubisha. Kwa uzito wa moyo akafunga safari na
kwenda pamoja na Isaka na vitu vilivyohitajika, kisu, moto, kamba, kuni, vyote tayari kumchinja. Kwa nini aliweza kumtii Mungu katika jambo hilo gumu kabisa? Kwa sababu aliamini kwamba hata akimchinja Mungu atapata njia ya kumrudisha, hata aweza kumfufua kutoka wafu, ili makusudi ya Mungu katika kumwita yeye na kumjalia mtoto, yaaendelee, hayawezi kuanguka chini. Dakika ya mwisho Mungu akamzuia asimchinje, na ilihesabiwa kana kwamba amempata kutoka wafu. Mtu mmoja amesema kwamba imani iliunda kweli ya Ufufuo. Tumaini la Ibrahimu lilidumu katika Mungu na Neno lake, si katika mtoto aliyezaliwa kutokana na imani na utii wake. Ingalikuwa rahisi sana aanze kumtegemea Isaka zaidi ya Mungu, lakini haikuwa hivyo. Alifika kwenye upeo wa imani na utii. Hakuweka mpaka katika kiasi cha utii wake wala katika uwezo wa Mungu. Ibrahimu aliishi kwa imani na kufa kwa imani, ila haina maana kwamba hakuwa na kosa wala kasoro wala upungufu, la, ila alimpenda Mungu na kumtegemea (Mwa.15:1). Kwake Neno la Mungu lilikuwa muhimu, lenye nguvu, lenye mamlaka, na kwa sababu hiyo, alilitia maanani maishani mwake.

Katika habari hiyo ni vema tutazame imani ya Isaka, wakati huo alikuwa mtu mzima. Alimwamini baba yake kabisa, hakutoroka, wala hakupigana naye,

akakubali kulazwa juu ya kuni na kufungwa kamba n.k. Hivyo, imetupasa kuwa na imani kama Isaka alivyokuwa nayo pamoja kufuata kielelezo cha Ibrahimu.

11:20-22 Imani ya Isaka, Yakobo, Yusufu

Katika vifungu hivi vichache mwandishi ametaja habari za watu watatu; Isaka, Yakobo, na Yusufu. Ijapokuwa angaliweza kutaja mambo mengi mbalimbali kuhusu kila mmoja na imani yake, hata hivyo, alichagua machache, na machache hayo yalihusu wakati walipoelekea kufa.

Isaka: Kumhusu Isaka ametaja jambo la Isaka kuwabariki watoto wake wawili, Yakobo na Esau waliozaliwa mapacha. Kwa imani Isaka alitambua tabia zao na jinsi watakavyohusika katika mipango ya Mungu na kwa sababu hiyo wakai wa kutoa baraka alimtanguliza Yakobo mdogo iwapo Esau alikuwa wa kwanza kuzaliwa. Jambo la baraka ya wazazi lilikuwa muhimu sana katika maisha yao, kwa sababu baraka ilihusika na urithi wa baadaye. Baraka aliyotoa Isaka imeandikwa baada ya maneno „sasa mimi nimekuwa mzee, wala sijui siku ya kufa kwangu" (Mwa. 27:2) na baraka yenyewe ni katika Mwa.27:28,29,39,40. Alikuwa mzee, dhaifu, na kipofu, hata hivyo, kwa imani aliweza kutazama mbele baada ya kufa kwake na kuona ukuu wa wana wake.

Tukisoma Mwanzo 27 kwa juujuu inaonekana kwamba Yakobo alipata hiyo baraka kwa ujanja na kwa hila kuliko kuipata kwa utambuzi wa ndani wa baba yake Isaka, hata hivyo, Mungu alimruhusu Yakobo kufanya jinsi alivyotaka kulingana na tabia yake. Hakufanya vizuri kwa baba, aliongozwa vibaya na mama, alikuwa na wivu mkubwa kwa ndugu yake Esau. Hata hivyo, Mungu alimsaidia, na kumbariki, si kwa sababu alistahili kusaidiwa bali kwa sababu alihitaji sana msaada huo. Maishani mwake wote Isaka aliishi kama msafiri na mgeni katika nchi ya Kanaani, hakuwa na sehemu yo yote ambayo aliweza kudai kuwa yake ila katika kuwabariki wana wake, kwa imani, alitazama mbele na kukabidhi baraka kwa kizazi kijacho akiona kwamba watu wengine watawatumikia wazao wa hao wana wake na baadaye mataifa watawaheshimu.

Yakobo: Yakobo aliishi maisha ya fujo, hakujitawala. Mwisho wa maisha yake alimwona mwana wake Yusufu kuwa mkuu katika nchi ya Misri, akiwa wa pili kwa Farao. Alitoa baraka ya pekee alipokaribia mwisho wa maisha yake (Mwa.47:27-30). Baraka yenyewe imeandikwa katika Mwa.48:9-22. Yusufu hakupendezwa na baba yake alipouweka mkono wake wa kuume juu ya kichwa cha Efraimu mdogo na kuuweka mkono wa kushoto juu ya Manase, mzaliwa wa kwanza. Ila Yakobo alikuwa amefanya kwa kusudi, maana, kwa imani, aliona kwamba, mbeleni Efraimu atamzidi Manase. Alijua kwa hakika Mungu hatakosa kuwasaidia, nao watafanikiwa na kupata nchi. Alifanya katika hali ya kumwabudu Mungu akiiegemea fimbo yake hali alikuwa amezeeka

sana. Mwisho wa maisha yake Yakobo alitambua ujinga wake katika kutumia hila na kupanga mambo bila kumjali Mungu.

Yusufu: Yusufu aliishi katika nchi ya Kanaani nchi ya ahadi kwa miaka 17 tu, ndipo akauzwa na ndugu zake, akapelekwa kuwa mtumwa huko Misri. Ndugu zake walimwonea wivu sana kwa sababu alikuwa mdogo na kupendelewa sana na baba yao. Huko Misri baada ya kupitia kwenye shida nyingi, kwa msaada wa Mungu wake, ambaye alimtumaini katika magumu yote aliyoyapata, alipandishwa cheo na kuwa wa pili kwa Farao. Aliheshimika sana, iwapo alikuwa mgeni, si mwenyeji. Hata hivyo, yeye hakusahau asili yake na nchi yake. Wakati wa njaa katika nchi ya Kanaani aliwahifadhi ndugu zake waliokuja Misri wakitafuta chakula. Pia alijaliwa kumwona baba yake, Yakobo, katika uzee wake. Yusufu alipokaribia kumaliza maisha yake, hali ameishi katika nchi ya Misri karibu maisha yake yote, alitoa agizo kwamba, maiti yake ihifadhiwe, kisha, baada ya miaka mingi, yaani baada ya miaka mia nne, mifupi yake iende huko Kanaani, wakati ndugu zake watakapokombolewa kutoka utumwani mwa Misri (Mwa.50:22-26). Ni jambo la ajabu kuona kwamba, kwa imani, alijua hakika kwamba ndugu zake watarudi makwao. Kusudi tumaini hilo lidumu kati yao kwa muda huo mrefu, wasije wakasahau walipotoka, alitoa agizo juu ya mifupa yake kuwa ukumbusho kwao na kuwa njia ya kuyachochea matumaini ya kukombolewa na kutoka Misri na kurudi makwao ambayo ni Kanaani nchi waliyoahidiwa na Mungu (Mwa.50:4-26). Neno hilo lilitimizwa baada ya miaka mia nne. Walipoondoka Misri chini ya uongozi wa Musa waliichukua mifupa yake (Kut.13:19) ndipo baada ya kufika Kanaani mifupa ilizikwa kama alivyoagiza (Yos.24:32).

Tukijumlisha habari za hao watatu, kwa kila mmoja jambo moja limetajwa, jambo ambalo lilihusu imani inayotazama mbele kwa mambo ya baadaye, ambayo bado hayajatokea, pia mambo ambayo dalili za kutokea kwake hazikuonekana.

Hao watatu, walipotazama mbele, baada ya kufa kwao, walikuwa na matumaini makubwa kuhusu mambo ya baadaye, kwa sababu, kwa imani, walikuwa na uhakika kwamba Mungu wao, yule ambaye amewaongoza katika maisha yao, ataendelea kuwaongoza wazao wao baada yao. Walimwamini Mungu. Hawakuwa waota ndoto wa mchana, wala wenye matamanio, la „waliona" kwa imani, waliona mambo halisi. Wote watatu walikufa bila kutimiziwa ahadi ya Mungu kuhusu nchi ya ahadi na kuwa taifa kubwa. Isaka aliishi kama msafiri na mgeni katika nchi ya ahadi. Yakobo alihamia Misri wakati wa njaa, akafa Misri. (Yusufu alimrudisha nyumbani na kumzika huko katika nchi ya ahadi Mwa.49.30-50:6). Yusufu isipokuwa kwa miaka kumi na saba ya maisha yake aliishi maisha yake yote huko Misri, nchi isiyo yake, akafa huko. Hata hivyo, hao wote walikufa bila kukata tamaa juu ya ahadi za Mungu, walitumaini kwamba Mungu atazitimiza ahadi zake kwa wazao wao, baada ya kuondoka kwao.

11:23-29 Imani ya Musa (ling. Mdo.7:20-44)
Musa alikuwa mkuu katika historia ya watu wa Mungu. Yeye sawa na Ibrahimu alisifiwa sana, Ibrahimu akiwa „baba" wa taifa na Musa „mkombozi" yule ambaye chini ya mkono hodari wa Mungu aliwakomboa kutoka utumwani mwa Misri. Pia alijulikana sana kuwa yule aliyepokea Torati kutoka kwa Mungu na kuwapa.Yapo mambo matano makubwa ambayo yametajwa kuhusu imani yake.

k.23 Kabla ya kutoa habari za imani ya Musa, Mwandishi ameanza kwa kutaja imani ya wazazi wake Amramu na Yokebedi (Kut.6:20). Musa alizaliwa wakati wa dhiki kubwa kwa Waisraeli, waliokuwa watumwa katika nchi ya Misri. Farao, Mfalme wa Misri, aliogopa sana alipotambua kwamba hao Waebrania wanazidi kuwa wengi, akahofu sana kwamba watapata nguvu ndipo watafanya fujo na kutoroka. Hivyo alitoa agizo kwamba watoto wote wa kiume wauawe wakati wa kuzaliwa (Kut.1:15ku). Kwa imani wazazi walimficha kitoto chao Musa kwa muda wa miezi mitatu ndipo wakamweka katika kisafina cha manyasi na kukiweka majini kando ya mto. Huko umbu lake Miriamu akakaa pale na kutazama yatakayotokea. Kwa nini walifanya hivi? Twasoma kwamba walifanya „kwa imani". Walipomtazama kitoto chao, jinsi alivyoonekana kuwa mzuri, walijisikia kwamba huyo ni wa pekee na ya kwamba huenda Mungu anayo makusudi juu yake. Kama Waebrania wenzao, bila shaka waliishi katika tumaini la kukombolewa na kurudi makwao kama Ibrahimu alivyotaja zamani za kale (Mwa.15:13). Walikuwa na ujasiri wakitenda tendo lililokuwa kinyume cha amri ya Farao, tendo lililohatarisha maisha yao. Ajabu ni kwamba kwa imani maisha ya Musa ilihifadhiwa, tena kwa njia ya ajabu, binti wa yule aliyetoa amri ya kuwaua watoto ndiye aliyemtoa majini na kumchukua kuwa mtoto wake! Ajabu lingine ni kwamba mama wa Musa alipewa nafasi ya kumlea kwa ajili ya binti Farao, na bila shaka katika muda huo Musa alipata kujua kwamba yeye ni Mwebrania, mmojawapo wa taifa lililoteuliwa na Mungu.
k.24-26 Mama alipomaliza kumlea Musa akaenda kuishi katika jumba la kifalme, na pale alielimishwa katika elimu yote ya WaMisri, akawa hodari katika mambo mengi (Mdo.7:22). Aliishi bila kujua shida yo yote ya maisha ya kawaida, alikula na kuvaa vizuri n.k. Huko, nje ya jumba la kifalme, Waebrania wenzake walitumikishwa vibaya sana wakifanya kazi za shokoa za kujenga majumba makubwa n.k. Alipokuwa mtu mzima ilimbidi Musa achague kati ya kuhesabiwa mtoto wa binti Farao au ajihesabu ni Mwebrania, kama alivyo hasa, na kujihusianisha nao. Uchaguzi huo ulikuwa mgumu kabisa kwake,
maana ni kuchagua kati ya maisha ya raha na heshima na maisha ya shida na mashutumu. Kwa imani, alichagua kuitwa Mwebrania na kukataa mazuri yote ya KiMisri. Kwa nini alikataa kuitwa mwana wa binti Farao? Kwa sababu, alitambua kwamba ijapokuwa maisha ya sasa ni mazuri lakini ni ya muda, afadhali akubali mateso pamoja na watu wake, kwa sababu hao ndiyo watu walioteuliwa na Mungu, na Mungu yu upande wao. Jaribu ambalo lingaliweza kumpata ni kufikiri kwamba akiwa katika jumba la Mfalme na kuwa karibu na

Farao, atapata nafasi ya kuwasaidia watu wake ili wapunguziwe shida zao, hata pengine nafasi ya kumshauri Farao awaruhusu warudi makwao. Lakini alilishinda jaribio hilo, akaamua kuondokae katika nyumba ya Mfalme na kuungojea uongozi wa Mungu kuhusu njia ya kuwasaidia watu wake.

Katika uchaguzi huo Musa alikuwa amejiweka upande wa watu wake walio watumwa, walioteswa, waliodharauliwa, ambao pia ni watu walioteuliwa na Mungu. Kwa imani alichagua kukataa maisha ya raha na ya heshima, ili ashiriki mateso na dharau za watu wake. Ilihitaji imani kufanya hivyo, kwa sababu watu wake walikuwa wameonewa kwa muda mrefu na njia ya kutoroka utumwani mwao haikuonekana, ni kwa imani ya kumtegemea Mungu na uwezo wake, na ahadi zake za zamani. Alijua kwamba, kwa vyovyote, katika wakati ulioamriwa na Mungu, watafaulu kuondoka. Ni ajabu kwamba alitambua kwamba kushtumiwa kwa ajili ya Kristo ni utajiri upitao utajiri wote wa Misri (tukumbuke kwamba Kristo alikuwa bado hajaja ulimwenguni wakati huo, hata hivyo, alihusianishwa na matukio hayo – Yn.8:56; 1 Kor.10:4). Mwandishi alisisitiza habari hiyo kwa sababu alikuwa akiwaandikia Wakristo wa Kiebrania ambao walikabili mateso na mashtumu kwa ajili ya kuwa Wakristo, nao walijaribiwa sana kuiacha imani yao na kurudi kwenye dini yao ya asili ya Kiyahudi.

k.27 Imani ya Musa ilitilia makali kuona kwake, maana katika kifungu hicho mwandishi ametuambia siri ya uchaguzi wa Musa. „Alistahimili kama amwonaye yeye asiyeonekana". Kwa imani alimwona Mungu na Kristo wake (Kut.2:14ku). Kuhusu kuondoka kwake katika nyumba ya Kifalme, Je! Alikimbia kwa kumwogopa Farao na hasira yake? Tukumbuke habari ya kumpiga Mmisri na kumwua, ndipo siku ya pili yake akawakuta Waebrania wawili wakigombana akajiingiza na kumkemea yule aliyemdhulumu mwenzake. Yule mtu aliyekemewa akasema „ni nani aliyekuweka wewe kuwa mkuu wetu na mwamuzi juu yetu?" ndipo akataja habari ya Mmisri aliyeuawa. Musa aliogopa alipofahamu habari hiyo inajulikana, kisha Farao akapata habari, alitambua kwamba Musa ni hatari kwake, akataka kumwua. Musa akaondoka na kwenda kuishi katika nchi ya Midiani, akakaa huko muda mrefu, hadi alipoitwa na Mungu kwa kazi ya kuwakomboa watu wake (Kut.2:11 – 3:1ku). Lazima Musa angoje mpaka wakati ulipoamriwa na Mungu na kwa njia zilizoruhusiwa na Mungu, si kwa hasira na uuaji. Je! Musa alifanya uchaguzi „kwa imani" (k.24,27) au „kwa hofu" (Kut.2:13-15). Ijapokuwa alisikia hofu, hata hivyo, alikuwa tayari kutulia na kuishi jangwani kwa muda mrefu mpaka Mungu atakapomwongoza kurudi kwa Farao na kushindana naye mpaka Farao atakapowaruhusu waondoke nchini.

k.28 Jambo jingine linaloonyesha imani ya Musa lilihusu wakati wa baadaye, baada ya kushindana na Farao juu ya kuwaruhusu watu wake kurudi makwao. Baada ya mapigo makubwa, yaliyomfanya Farao mara nyingine kukubali waondoke, ndipo pigo lilipopoa akakataa tena. Kisha Mungu alimwongoza

Musa kufanya jambo la pekee. Waisraeli wote waiandae Pasaka, wachinje mwana kondoo au mbuzi na kuitia damu yake kwenye miimo ya milango na vizingiti vya juu vya nyumba zao, ndipo wale chakula hali wamesimama na kuwa tayari kabisa kuondoka usiku. Tendo hilo lilikuwa geni kabisa, tendo la kuwagharamia wanyama, na katika kaida za dini lililkuwa mpya kwao (Kut. 12:1ku). Hukumu kali kabisa iliwapata WaMisri, maana hao hawakuiweka damu kwenye nyumba zao, na kwa sababu hiyo, malaika alipopita juu ya nyumba zote za Misri, mzaliwa wa kwanza aliyekuwemo ndani aliuawa ila malaika alipoiona damu kwenye milango akapita juu bila kumwua mzaliwa wa kwanza. Ndipo Farao na wakuu wakaja wakamwomba Musa aondoke pamoja na watu wake. Musa alionyesha imani kwa mambo mawili, la kwanza kwa kufuata maagizo ya Mungu juu ya kufanya Pasaka na pili, kwa sababu alimwamini na kulitegemea Neno lake juu ya hatari kubwa inayokaribia, bila kujua matokeo yake.

k.29 Jambo lingine lililoonyesha imani ya Musa lilitokea baada ya Musa na watu wake kuwa wameondoka nchini. Wakakuta kizuizi kikubwa katika safari yao, wakafika kwa Bahari ya Shamu. Lazima waende mbele, hawana njia ya kwenda penginepo. WaMisri, hali wakidhani kwamba watawapata, walikuwa wamewafuata kwa farasi na magari yao. Ilihitaji imani kubwa kwa Musa kuwaongoza watu wake kwenda mbele kwa Bahari huku wanayaona maji yake tu. Akawaagiza wasimame na kuona matendo makuu ya Mungu, na kumbe, walipotazama nyuma, WaMisri wako wamewafuata. Mbele ni maji, nyuma ni WaMisri. Watu waliogopa sana na kumlaumu Musa, wakaona afadhali wangalikaa Misri na kumtumikia Farao. Ni Musa, peke yake aliyekuwa na imani walipokuwa ukingoni mwa maji. Baada ya kusikia amri ya Mungu ya kwenda mbele, Musa akaiinua fimbo yake na kuunyosha mkono wake juu ya bahara, nayo ikagawanyika, na njia ilipatikana kwa watu kupita kati ya bahari. WaMisri walipojaribu kuwafuata, wakachelewa, maji yakarudi na kuwaua (Kut.14:5ku). Ilihitaji imani thabiti kufanya kama Musa alivyofanya siku ile.

Mwandishi ameacha kuandika habari nyingine za Musa, hakutaja habari yo yote kuhusu muda mrefu wa Waisraeli kuishi jangwani katika safari ya kurudi Kanaani nchi waliyoahidiwa na Mungu, katika muda huo watu kwa jumla hawakuamini.

11:30-31 Imani ya Yoshua na Rahabu

k.30-31 Hakuna habari juu ya miaka arobaini baada ya watu kuondoka Misri mpaka walipokuwa tayari kuingia nchi ya ahadi. Katika vifungu hivi viwili matukio mawili yametajwa. Kwanza, habari za kuta za Yeriko kuanguka (Yos.6:1-20). Mwandishi amesema kwamba zilianguka kwa sababu ya imani ya Waisraeli. Mji ulilindwa sana, ulionekana kama mji usioshindika. Mungu alimwambia Yoshua wazunguke mji kwa siku sita hali wameongozwa na makuhani waliopiga tarumbeta. Kwa ujasiri wa kuamini kwamba Mungu

atawashindia walifanya kama Yoshua alivyowaagiza kulingana na agizo la Mungu. Kisha, siku ya saba, walipozunguka, kuta zikaanguka, na watu waliingia na kuwaua wenyeji wa Yeriko. Habari hizo ni katika kitabu cha Yoshua, sura ya tano.

Halafu jambo lingine limetajwa nalo ni imani ya Rahabu. Bila shaka watu walishtuka kuona kwamba imani yake imesifiwa, maana Rahabu alikuwa Mmtaifa, tena kahabu, maisha yake hayakuwa mazuri. Ila yeye alikuwa amesikia habari za Waisraeli na jinsi ambavyo hapo nyuma Mungu wao alikuwa amewashindia, jinsi walivyovuka Bahari ya Shamu na kutoroka Misri. Kwa hiyo, aliposikia habari ya kuwa Waisraeli walikuwa tayari kuvuka Mto.Yordani na kuukaribia Yeriko, alijua kwa hakika kwamba Waisraeli watafaulu kuushinda mji wa Yeriko uliodhaniwa kwamba haushindiki. Wapelelezi wawili walifika Yeriko kwa siri ili wapate kujua hali ya mji na kandokando yake, na hali ya wenyeji. Habari hii imeandikiwa katika Yoshua 2. Basi Rahabu aliwakaribisha hao wawili na kuwaambia jinsi alivyoamini na alipatana nao, kwa upande wake yeye atawahifadhi na kuwapa nafasi ya kutoroka na kurudi makwao kwa usalama, na wao kwa upande wao, watamlinda wakati wa kuja kuuteka mji. Aliwapa ishara ya uzi nyekundi itakayowekwa dirishani ili nyumba yake itambulike. Rahabu alikuwa na imani jasiri, wenyeji hawakuwa tayari kuamini kwamba mji wao utatekwa, ila yeye, kinyume chao, ndivyo alivyoamini (Yak.2:11).

11:32-40 Majumlisho ya wengine wa Imani na dhiki zitokanazo na imani

Mwandishi ametambua ya kwamba haiwezekani kuandika habari za watu wengine wote walioonyesha imani kwa njia ya matendo yao. Ametaja kwa pamoja watu sita, baadhi yao, wanne, walikuwa Waamuzi ambao waliishi baada ya Waisraeli kuwa wamekaa kwa muda katika nchi ya ahadi na kabla ya Mungu kuwaruhusu kuwa na mfalme. Zilikuwa nyakati za fujo, nyakati za kila mtu kuamua mambo yake mwenyewe (Amu.17.6). Samweli alikuwa mwamuzi na nabii na Daudi aliwekwa kuwa mfalme. Pia, matendo yao yaliyoonyesha imani yao yamejumlishwa. Twakumbuka Danieli na wakati alipowekwa katika tanuru ya moto na moto wake haukumgusa na tena alipowekwa kwa simba nao walifumba vinywa vyao wasimle (3:20ku. 6:16ku). Katika vita wengine walikuwa hodari sana (1 Sam.14:14; 2 Waf.11ku). Hata wanawake, kwa imani, walipokea kutoka wafu, wafu wao (1 Waf.17:24; 2 Waf.48ku).

Ijapokuwa hao watu walisifiwa kwa imani tusifikiri kwamba hawakuwa na kasoro, walikuwa na udhaifu mbalimbali, hata hivyo, imani yao ilishinda udhaifu waliokuwa nao, hata wakawa hodari kwa kufanya jinsi Mungu alivyowataka. Gideoni alikuwa na hofu, Baraka alisitasita, Samsoni alifanya kwa mzaha,Yeftha alitoa kiapo kwa haraka, bila kufikiri.

Daudi alikuwa mtaminifu na Samweli hakufanya kwa uangalifu. Hao wote walisifiwa na Mungu kwa ajili ya imani yao iliyokuwa msingi wa matendo yao hodari.

k.35-38 Pamoja na matendo hao, kwa imani, hao watu walivumilia shida na mateso mbalimbali, mapigo, dhihaka, kufungwa gerezani, hata baadhi waliuawa. Wengine walikosa mahitaji na wengine walifukuzwa na kuishi kwa shida nyikani na milimani, mapangoni na mashimoni. Mwandishi ameandika kwamba „ulimwengu haukustahili kuwa nao". Machoni mwa wanadamu walionekana kuwa wamekosa heshima, ila machoni mwa Mungu wameheshimika sana.

k.39-40 Katika maisha yao ya hapa duniani walipata shida na kukosa heshima na walikufa bila kutimiziwa kwa ukamilifu ahadi za Mungu. Kwa sababu hiyo liko jambo kubwa la maana sana mbele yao nalo ni kuitimiziwa ahadi hizo, ila hawawezi kuzirithi mpaka wengine watakaoishi baada yao watafaulu katika kuishi maisha ya imani, ndipo wote kwa pamoja watazawadiwa katika maisha ya baadaye.

MASWALI

Toa mfano unaoonyesha imani ni nini hasa (mfano wa kawaida).

Chagua kati ya Ibrahimu na Musa na kuonyesha jinsi walivyoishi kwa imani.

12:1-2 Kielelezo chema cha Imani ya Yesu

Baada ya kutaja watu walioishi zamani za kale waliokuwa hodari katika kumwamini Mungu na kutenda matendo makuu kutokana na imani yao, mwandishi ameweka mbele za wasomaji wake Yesu Kristo ambaye alipofanyika mwanadamu aliishi maisha yake katika hali ya kumwamini na kumtegemea Baba yake katika mambo yote. Yesu ndiye kielelezo chema cha kufuatwa, hao wengine huwatia moyo waumini waliopo sasa ila hasa ni Yesu anayetoa mfano mkubwa wa kufuatwa.

Kama ambavyo tumeona, mara kwa mara, ilimbidi mwandishi awaonye wasomaji wake juu ya kudumu kuwa mwaminifu katika maisha yao ya Kikristo, hasa kwa sababu walikuwa wakikatishwa tamaa kwa magumu na mateso waliyopata kwa ajili ya imani yao. Wasomaji walielekea kutaka kurudi kwenye imani yao ya kwanza ya Kiyahudi, ili waepuke mateso na dhiki zao.

k.1 Hapo mwandishi amechora picha ya kiwanja cha michezo na wapiga mbio katika mashindano. Hao washindani wapaswa waweke kando kila kitu ambacho kingewazuia wasipige mbio vizuri. Tungeshangaa kuona mpiga mbio hali amevaa koti kubwa la nje, au kuwa amebeba mzigo mzito mgongoni n.k.

Kila mpiga mbio wa kweli huweka kando kila kizuizi kusudi akimbie vizuri. Pia mpiga mbio ajiweke huru na vitu ambavyo havina msaada kwake, huangalie uzito wake pia hufanya mazoezi ya kimwili ili kwa vyovyote awe amejitayarisha vizuri kwa mashindano yaliyo mbele yake.

Hao wapiga mbio huzungukwa na mashahidi. Kwa kawaida watu huhudhuria mashindano ya michezo mbalimbali, hao ni watazamaji, kazi yao ni kuwatia moyo hao wachezaji. Ila mashahidi waliotajwa hapo na mwandishi hawawi watazamaji, bali ni mashahidi. Wao waliotangulia katika mashindano ya imani, waliotajwa katika sura ya 11, si watazamaji wa hao wa sasa, bali ni mashahidi. Kama ni mashahidi, washuhudia nini hasa? Washuhudia hao wa sasa kwamba *upo uwezekano wa kushinda katika mashindano ya imani*. Ni kama wako, hai, wakipiga sauti za kutia moyo hao wa sasa.

Kila muumini anatakiwa aweke kando kila kizuizi, yaani kila kitu kisichomsaidia katika mashindano ya imani. Katika maisha yetu yapo mengine ambayo si dhambi hasa, ila kwa muumini ni mambo yasiyomjenga katika imani, si msaada kwake. Kila muumini atafakari sana juu ya maisha yake, na kuacha kila hali na kila jambo lisilomfaa. Pengine kwa mtu fulani litakuwa jambo fulani na kwa mwingine jambo lingine, kila muumini akate shauri hali akijua ni nini hasa ambayo inamzuia katika mwenendo wa Kikristo.

„dhambi ile ituzingaye kwa upesi" ni nini dhambi hiyo? Yawezekana ni hali ya kutokuamini, yaani kutotia maanani Neno la Mungu, au kutoa udhuru kwa dhambi fulani, au kufikiri kwamba hakuna haja ya kuyajali marudi ya Mungu na hukumu yake. Ni rahisi sana kwa Mkristo kunaswa katika dhambi fulani, kwa hiyo, daima awe na tahadhari katika maisha yake.

Wale walioandikiwa wamo katika safu ya watu waliomtegemea Mungu tangu zamani za kale, na sisi, tunaosoma maelezo hayo wamo katika safu hiyo, sote tumo katika mashindano ya imani. Kama ilivyokuwa kwa watu wa kale hata kwa walioandikiwa, hata kwa sisi wa leo, twaitwa kujitoa kabisa kumfuata Kristo. Yapo mengi ya kuuvuta usikivu wetu, hasa katika dunia ya sasa, imejaa mengi sana, mazuri kwa mabaya, yanayoweza kupoza nia yetu ya kumfuata Kristo. Lazima tuweke kando matakwa yetu mengi, hata matakwa mazuri. Swali kubwa kwa kila mtu anayeishi duniani lahusu shabaha ya kuumbwa kwake. Ni kwa kila mtu haidhuru anamkubali Mungu na Kuwepo Kwake au siyo. Swali ni „Kwa nini tupo hapa duniani?" Tupo kwa kusudi moja la kufanya mapenzi ya Mungu. Ni vema tutambue kwamba mashindano ya imani ni mfano wa shindano la mbio la marathani (Mbio za masafu marefu) si shindano la mbio la kilometa mia moja au mbili tu. Shindano hilo ni majaribio ya ustahamilivu, hivyo, tujiandae kukimbia kwa muda mrefu. Mwandishi amesema „tupige mbio kwa saburi" mambo mawili yawiana – tupige mbio na kwa saburi. Kwa kawaida, mtu anayepiga mbio afanye kwa haraka si kwa saburi.

k.2 Liko jambo moja kubwa litakalotusaidia katika mashindano ya imani yetu nalo ni „kumtazama Yesu" yaani ni kumkazia macho (2:9; 3.1: 4:14,16). Kwa nini tumtazame Yesu. Ni kwa sababu Yesu aliishi maisha ya imani na kupata ushindi. Tangu mwanzo mpaka mwisho wa maisha yake alimtegemea Baba yake, alimtii na kufanya mapenzi yake, kwa moyo na kwa kutaka, akitafuta kumpendeza katika yote. Alipatwa na vipingamizi, chuki na dharau za watu na mwishowe alikataliwa na kuuawa. Haikuwa rahisi akubali kuwa dhabihu ya dhambi na kuuawa kwa kumwaga damu yake msalabani, hata hivyo alimtegemea Baba na kuamini kwamba Baba atampitishia katika hayo magumu yote. Yesu ndiye kielelezo chema cha imani na Yeye ndiye sababu kila muumini ameitwa kumkazia macho, kumzingatia, ili atiwe moyo katika mashindano ya imani yaliyo mbele yake.

„mwenye kuanzisha na mwenye kutimiza imani yetu". Yesu ameunda shindano hilo la imani. Yesu anajua hakika kwamba imani inatakiwa. Pamoja na kutoa kielelezo Yesu anatutia nguvu (Efe.3:16; Flp.4:13). Yuko mbele za Baba ili atuombee na kutupatia mahitaji yetu ya kiroho. Yesu ni mfano wa imani iliyojaribiwa kabisa, mpaka upeo. Kwa hiyo, mashauri kwa wale walioandikiwa ni „wasikate tamaa mapema" „wasilegee mpaka wamemaliza shindano"waendelee kusimama, wasianguke, hadi wamepita utepe wa kumaliza shindano".

„kwa ajili ya furaha iliyowekwa mbele yake" Ni furaha gani inayosemwa? Ni zaidi ya furaha ya binafsi ya kurudi salama kwa Baba na kuwekwa mbali na shida. Ni furaha ya kuleta wana wengi kwa utukufu. Ni furaha ya kuona na kutusaidia sisi wa leo, ili sisi nasi, tushinde. Yatupasa kuvumilia mengi kama Yeye alivyofanya, na mwishowe tutashiriki katika utukufu wake. Hapo twafunuliwa siri ya ushindi wake, alikuwa akitazama mbele, baada ya Msalaba na kujua kwamba, Yeye atakaribishwa na Baba yake, ila, si hivyo tu, bali na wote watakaokanyaga nyayo zake za imani watakaribishwa na Baba yake katika makao ya milele. Neno hilo lilikuwa kubwa kwa wale walioandikiwa, kwa sababu, hao walikuwa wameanza kukata tamaa, waliwaza kurudi kwenye dini yao ya asili ya Kiyahudi, ili waepukane na mateso na magumu waliyokuwa wakiyapata katika kumfuata Kristo. Wakimkazia macho Kristo, yale mengine yaliyokuwa yakiuvuta usikivu wao yatatoweka.

12: 3-13 Marudi ya Baba kwa watoto wake

Mwandishi aliendelea kuwalenga wasomaji wake na kuwasaidia kuelewa mapingamizi yao, kwanza kwa kuyalinganisha na yale yaliyompita Kristo, ndipo kuelekeza mawazo yao ili wayawaze kama marudi ya Baba anayewapenda sana watoto wake.

k.3-4 Watakapolinganisha mateso yao na yale yaliyompata Kristo watatambua kwamba ya Kristo yalizidi sana sana ya kwao, maana Kristo alimwaga damu

yake katika kukataa kufanya dhambi na kumwasi Baba yake. Ijapokuwa wamepatwa na shida bado hawajaitwa kufa kwa ajili ya Kristo. Yesu aliyastahamili yote yaliyotupwa Kwake, vita yake ilikuwa kali sana, hata hivyo, alidumu mwaminifu kwa Baba na mapenzi yake. Vivyo hivyo, na hao waumini waliojaribiwa sana kuacha imani yao ili wayaepe mapingamizi, vilevile wapaswa wayastahamili hayo yote na kudumu waaminifu kwa Kristo. Watasaidiwa kwa kumtafakari sana Kristo.

k.5ku. Lipo jambo lingine litakalowasaidia. Yawezekana kwamba wamekuwa na maulizo mengi kuhusu mateso yao; Je! kwa nini Mungu anaruhusu tupate shida za namna hiyo? Je! Tumekuwa na kasoro gani eti! Tupate shida hizo? Je! Mungu anatafuta kutuadhibu kwa njia hiyo? La, hata kidogo. Mateso yao na magumu yanayowapata ni dalili ya upendo wa Mungu kwa hao walio watoto wake. Ni dalili ya kuwathibitisha kuwa watoto wake halisi. Ni njia ambayo kwayo Mungu huwarudi kwa shabaha ya kuwatayarisha kwa kuishi naye milele na milele. Ni njia ya kuwafundisha kujiweka zaidi na zaidi kwa Mungu na mapenzi yake. Kwa hiyo wameitwa kuyajali hayo marudi, kuyathamini, na kuyavumilia. Hayo marudi ni dalili ya uthamani wao machoni mwa Baba yao wa mbinguni. Wanaporudiwa kwa njia ya magumu yanayowapata, (ingalau yanatoka kwa watu wengine, si Mungu anayeyatuma) wahesabu kwamba Baba anawafanyia kama watoto, kwa hiyo, wayapokee kama ndivyo ilivyo.

Aliwakumbusha juu ya baba zao wa kimwili. Wazazi huwarudi watoto wao, pengine katika kuwarudi wanafanya makosa, au huenda shabaha yao si njema, hata hivyo, ni kwa faida ya mtoto. Mungu amejaa hekima, ajua kabisa ni nini yaliyo faida yetu, si kwa sasa hivi tu, hata kwa baadaye, na lengo lake ni kwa sisi kuushiriki utakatifu wake. Wakipokea katika lengo hilo watatiwa nguvu na kuzaa matunda ya haki na amani. Marudi yana maumivu, ni kitu cha huzuni, ila wajue kwamba shabaha yake ni njema na mwisho wake ni furaha (Rum.5:3-4; Yak.1:3-4; 1 Pet.1:7). Mwalimu mmoja wa michezo alisema hivi „nawalazimisha watu kufanya yale wasiyoyataka kuyafanya ili wahitimu na kuwa kama sikuzote walivyotaka kuwa".

k.12,13 Kisha mwandishi amewasihi waumini walioandikiwa wakaze mwendo, wasaidieni, hasa wale walio dhaifu, wasiwe kikwazo, wala wasiweke kikwazo kwa wengine, kusudi kwa pamoja waendelee kuwa waaminifu kwa Kristo potelea mbali wakutane na mapingamizi gani.

12:14-17 Maonyo juu ya kuikataa neema ya Mungu

k.14 Hapo mwandishi amewaonya juu ya mambo mawili yaliyo muhimu katika maisha ya Kikristo. Jambo la kwanza lahusu maisha yao wao kwa wao katika shirika zao pamoja na hali ya kila muumini kwa mwenzake. Ni jambo la amani. Amewashauri wawe na bidii, watafute sana kuishi kwa amani, wawe wepesi wa kutengeneza jambo lolote linapozuka linaloharibu amani kati yao (Mt.5:9;

Rum.12:18). Kamwe Mkristo asiwe chanzo cha ugomvi au mashindano. Jambo la pili lahusu maisha ya muumini mbele za Mungu, apaswa awe na hali ya utakatifu, yaani awe amejiweka wakfu ili aishi maisha yanayompendeza Mungu (Mt.5:8). Bila utakatifu mtu hawezi kumwona Mungu, ama sasa katika maisha yake ya kiroho, na zaidi, baadaye Kristo atakaporudi tena. Kwa kuishi maisha ya utakatifu mtu huhitaji neema ya Mungu, awe na uhusiano ulio hai na Bwana Yesu, haina maana kwamba awe anashikilia amri mbalimbali tu, akifanya hivyo atafanana na Mafarisayo.

k.15 Ilimbidi kila muumini awe na mzigo juu ya wenzake ndipo ataweza kutambua ikiwa mwingine ameanza kupoa au kurudi nyuma. Maneno „shina la uchungu" ni ukumbusho wa Kum.29:8-19 hasa k.18. Bila kuwa na mzigo ni rahisi kwa wengi kuambukizwa, kwa hiyo, wawe wepesi wa kutengeneza shida yoyote inayozuka katika shirika zao. Twajua kwamba mizizi ya magugu mengine inakwenda chini sana, na ni vigumu kuitoa ikiwa imepata nguvu na kukua.

k.16-17 Ndipo mwandishi alikumbuka habari za Esau aliyeishi zamani sana. Amemwita mwasherati, na hatujui alikuwa na maana gani alipomwita hivyo, kwa sababu katika habari zake hatusomi habari ya namna hiyo. Ni dhahiri kwamba hakumcha Mungu kwa vile hakujali urithi wake wa mzaliwa wa kwanza ambao ndani yake alirithi ahadi za Mungu. Badala yake alitaka kutuliza njaa ya mara moja, kitu kidogo sana kwa kulingana na kitu kikubwa cha ahadi za Mungu. Baadaye alipotafuta baraka iliyoandamana na urithi, baba yake hakuwa tayari kumpa (Mwa.25:28ku; 27:39). Habari ya Esau ilitoa fundisho kubwa na onyo kali kwa hao waumini, wakiacha imani ya Kikristo na kurudi kwenye imani ya Kiyahudi, watakuwa wamefanana na Esau, aliyehesabu chakula, kitu cha muda tu, ni bora kuliko ahadi za Mungu zinazoendelea. Inawezekana wachague maisha ya raha ya sasa na katika kuchagua wakose raha ya milele. Uchaguzi mwingine hautanguki, lile tunalochagua, ndivyo linavyodumu kuwa. Walikuwa wamepewa onyo la namna hiyo hapo nyuma (3:12).

12:18-29 Hofu iliyoandama na kutolewa kwa Agano la Kale na furaha ya Agano Jipya

Hapo mwandishi amelinganisha mambo ya Agano la Kale na ya Agano Jipya. Alianza kwa kutaja vitiisho vilivyokuwepo wakati wa kutolewa Agano la Kale pale Mlima Sinai. Kila jambo lililonyesha pengo kubwa kati ya Mungu na wanadamu. Aliwakumbusha mambo yaliyotokea wakati ule (Kut.19:16-19; 20:18-21), moto; giza; tufani; mlio wa baragumu na sauti ya kipekee, sauti ya Mungu iliyosema na watu. Watu waliogopa sana, hata waliomba sauti hiyo isiseme nao, ila iseme na Musa ndipo Musa alete habari zake. Mlima wote na kandokando yake na kila kitu kilijaa utakatifu wa Mungu na mtu au mnyama

yeyote aliyeugusa aliuawa. Hata Musa, mtumishi wa Mungu aliyechaguliwa kuwaongoza Waisraeli aliogopa na kutetemeka.

Katika Agano Jipya, yaani Injili mambo huwa tofauti sana. Alitaja baraka za waumini. Wameufikilia mlima Sayuni na mji wa Mungu aliye hai, Yerusalemu wa mbinguni (Gal.4:26 Flp.3:20; Ufu.21:1). Maana yake ni kwamba walipookolewa walikutana na Mungu aliye hai, kwa njia ya kushirikiana na Kristo kibinafsi. Katika Kristo wameishafika kwenye mji wa milele, mji udumuo, mji ambao Abrahimu aliutafuta (11:10,16). Tayari wamekuwa raia wa mbinguni. Jeshi kubwa la malaika huwahudumia (1:14; Kum.33:2; Dan.7:2; Lk.2:13; Ufu.5:1).Yawezekana „mkutano mkuu wa Kanisa la wazaliwa wa kwanza" ni ushirika mzima wa watakatifu; Kanisa ni mwili wa Kristo, na washiriki wa Mwili huo washiriki jina la wazaliwa wa kwanza kama Kristo aitwavyo (Kol.1:18; Rum.8:29) nao ni warithi wa Mungu na warithi pamoja na Kristo (Rum.8:17).

Wamefika kwa „Mungu, mwamuzi wa watu wote". Waumini wasimama mbele za Mungu, mwamuzi, bila hofu kwa sababu Yesu alihukumiwa kwa dhambi zao, na kila atubuye na kumwamini Kristo na kifo chake cha Msalaba kilicho fidia ya dhambi zao, huachiliwa, hahukumiwi kwa dhambi zake (Rum.8:1; Yn.5:24).
Ina maana gani „roho za watu wenye haki waliokamilika"? huenda hao ni waumini walioishi kabla ya Kristo (11:40). Yafikiriwa ni hao kwa sababu ni roho zao ambazo zimetajwa, si miili yao ambayo inangojea ufufuo wa mwisho.

Pia waumini wamefika kwa Yesu, mjumbe wa Agano Jipya na damu ya kunyunyiziwa inenayo mema kuliko ile ya Habili. Kwa damu yake Yesu amewapatia waumini ondoleo kamili la dhambi, msamaha kamili (1 Pet.1:19). Mungu aliahidi kwamba katika Agano Jipya hakuna kumbukumbu la dhambi (Yer.31:31-34). Sivyo ilivyokuwa katika Agano la Kale, ijapokuwa dhabihu za kusamehe dhambi zilikuwepo, hata dhabihu zenyewe zilizotolewa kila wakati zilikuwa kumbukumbu kwamba ondoleo kamili la dhambi bado halijapatikana (Ebr.10:1-4).
Damu ya Habili ililia kutoka ardhini ikitaka kulipizwa, bali damu ya Kristo iliyomwagika Msalabani si damu ya kulipiza bali ya kusamehe.

Tukijumlisha baraka hizo za Agano Jipya mwandishi anataka kuwaonyesha hao waumini kwamba kwa njia ya kushirikiana na Yesu ni kama wameishafika kwenye mji wa milele nao wanao majeshi ya malaika tayari kuwahudumia. Wako pamoja na umati mkubwa wa waumini wa tangu zamani za kale, nao wako mbele ya „mwamuzi wa watu wote", wamo katika kundi kubwa la wote waliohesabiwa haki na kukamilishwa na Yesu, mhudumu wa Agano hilo Jipya, kwa kuwa damu yake hunena habari za kutakaswa dhambi na kusamehewa.

Kwa hiyo, haiwaziki kwamba hao wenye baraka hizo wanataka kurudi kuwa chini ya Agano la Kale liletalo hofu, kwa sababu wale waishio chini ya Torati

hudaiwa kushika sheria zake zote na kukosa kushika huleta hukumu, wala haiwezekani mtu azishike kwa ukamilifu.

MASWALI

1. *Kwa nini waumini waliitwa kumtazama na kumtafakari Yesu?*

2. *Kwa nini Mungu anarudi waumini wake, toa sababu zake na shabaha yake?*

Sura 13: Katika sura hii mwandishi ametoa mashauri mbalimbali na kuwasihi waumini waishi maisha kiutendaji yanayopatana na Ukristo wao.

13:1-6 Wito wa kuishi kwa upendano wa ndugu; usafi wa maisha; na kuridhika

k.1 Jambo kubwa la kwanza ni upendano wa ndugu kama Bwana Yesu alivyofundisha kuwa alama hasa ya wafuasi wake (Yn.13:35). Waumini ni washiriki katika familia moja ya Mungu. Haidhuru ni wa kabila au rika au hali gani, kila muumini ameingiwa kushiriki pamoja na wenzake katika maisha ya Kristo.

k.2 Katika kupendana wamewajibika kuwakaribisha wageni, kuwafadhili, kuwaingiza katika shirika zao, wasiishi kwa ubaguzi na kwa kuwapenda watu kadha na kutowajali wengine. Neno la ukaribishaji lilikuwa kubwa kwa Wakristo wakati ule. Wakristo walifundisha kuwakaribisha waumini wenzao waliosafiri n.k. maana ilikuwa vigumu kupata mahali pa usalama pa kukaa, hoteli nyingi zilitumiwa na makahaba na wizi n.k. Huenda maneno „wengine wamewakaribisha malaika pasipo kujua" ni ukumbusho wa Ibrahimu alipowakaribisha wale wasafiri watatu (Mwa. 18:1ku) na habari za Gideoni na Manoah (Amu.6 na 13) (1 Tim.3:2; Tit.1:8; Mt.25:35ku. Rum.12:13; 1 Pet.4:9).

k.3 Wenzao wengine walikuwa wamefungwa na wengine walikuwa wamedhulumiwa, yawezekana kwa ajili ya imani yao katika Kristo. Katika kuwakumbuka wajiweka mahali pao kimawazo na kuwafanyia kiutendaji kufuatana na mahitaji yao, pengine kwa kuwatembelea, pengine kwa kuwapatika mahitaji yao, yaani wazingatia ni nini hasa ambacho kitawasaidia, na bila shaka walihitaji maombi (1 Kor.12:26).

k.4 Jambo lingine ni usafi wa maisha. Mwandishi alitilia mkazo uthamani wa ndoa na usafi wa maisha. Huenda wengine walikuwa wakifundisha kwamba si vizuri kuoa, ni afadhali kukaa bila kuoa (1 Tim.4:3) wakifundisha mambo ya mwili ni maovu. Katika kusema juu ya ndoa mwandishi alijua kwamba ndoa ni jambo la maana sana katika maisha ya wanadamu, nalo linahitaji kila aliyeoa na aliyeolewa kufanya juhudi kuitunza ndoa yake. Ni kama agano kati ya watu

wawili tofauti, ni zaidi ya miili yao kuungana hata nafsi zao huungana pia (1 Kor.6:16-18).

k.5-6 Jambo lingine ni kuridhika na kumtegemea Mungu. Mtu akipenda fedha anaonyesha kwamba amekosa imani katika uaminifu wa Mungu kumtunza. Jambo kubwa ni uhusiano wetu wa Mungu si vitu tulivyo navyo (1 Tim.6:6-8; Mt.6:31-33). Choyo huleta hali ya kutokuridhika. Mungu ametuahidi kwamba hatatupungukia wala hatatuacha. Pengine wengine waliogopa mateso na kuhofu itakuwaje wakifungwa au kunyang"anywa mali zao au kunyima kazi n.k.

13:7, 17, 24 Mashauri kuhusu viongozi

Viongozi wametajwa katika vifungu vitatu, k.7; k.17; na k.24.
k.7 Inaonekana hao wanaotajwa hapa ni wale waliotangulia na sasa wamefariki dunia. Yawapasa waumini wawakumbuke kama wale waliowapa Neno la Mungu (2:3,4). Katika kuwakumbuka wachunguze mwisho wa mwenendo wao; ina maana gani „mwisho wa mwenendo wao" Je! Waliuawa kwa imani yao? Hatujui. Kwa vyovyote ina maana kwamba walimaliza vizuri safari yao, waliishi kwa imani, na walikufa katika tumaini la uzima wa milele, na kwa sababu hiyo walioandikiwa wameitwa kuiiga imani yao.

13:8-16 Imani ikazwe kwa Bwana Yesu, neema yake, na kudumu kwake

Zaidi ya kuwakumbuka hao ambao wamemaliza maisha yao hapo duniani, waumini wawe watiifu kwa Yesu Kristo ambaye yupo wakati wote, alikuwapo, yupo, tena atakuwapo milele na milele, wala habadiliki (1:12; Zab.102:27). Tumaini lao liwe katika Yeye hasa, viongozi huja na kuondoka na wale waliotangulia waliwasaidia na kuwafundisha habari za Kristo walizozipata kwa wale walioandamana na Yesu, hata hivyo, hasa imani yao iwe katika Kristo Aliye Hai, ambaye daima yu mbele za Mungu akiwaombea (7:24,25).

k.9 Watu kadha walikuwa wakijaribu kuipotosha imani yao wakileta mafundisho mageni yasiyopatana na Injili walioipokea. Inaonekana mafundisho hayo yalihusu maagizo juu ya kula au kutokula vyakula fulani, mafundisho ambayo hayakufaidi watu (Kol.16-23; 1 Kor.8:8; Rum.14:17; 1 Tim.4:3). Ni neema inayoimarisha mioyo wa waumini, si chakula kadha.

k.10ku. Maneno „tuna madhabahu" yana maana gani? Kwa Wakristo madhabahu ni Msalaba wa Kristo, mahali ambapo Kristo alipotoa dhabihu moja, itoshayo, kwa dhambi za ulimwengu wote. Wakristo hawana haja tena ya madhabahu au dhabihu au makuhani. Yawezekana wengine waliwadhihaki kwa vile hawakuwa na vitu vya namna hiyo. Walijaribiwa kurudi kwenye dini yao ya Kiyahudi ili waepe dhihaka na mateso, ila wakifanya hivyo hawatakuwa na sehemu wala kuzishiriki baraka za Kristo na Msalaba wake. Yesu alisulibiwa nje ya kuta za Yerusalemu, dalili ya kukataliwa na watu wake; vivyo hivyo, wafuasi wake wapaswa wayashiriki mashutumu yake. Wale wanaokaa katika

dini ya Kiyahudi na kuihudumia hema hawashiriki faida ipatikanayo kwa ile dhabihu moja ya Kristo yenye thamani kuliko dhabihu zote za wanyama. Wakristo ni watu wasio na „mji wao" hapa duniani, ni wasafiri, wafanane na Ibrahimu na wote wenye imani (11:10; 13ku). Katika Agano la Kale makuhani waliruhusiwa kula nyama ya wanyama waliotolewa kwa dhabihu mbalimbali ila hawakuruhusiwa kula nyama ya wanayama waliotolewa kuwa dhabihu ya dhambi Sikukuu ya Upatanisho (Lawi.4:12; 16:27). Hivyo, wale wanaoishi kwa kanuni za Agano la Kale kuhusu dhabihu hawawezi kushiriki baraka za dhabihi ya dhambi iliyotolewa pale Msalabani na Kristo, dhabihu halisi yenye uwezo wa kuondoa dhambi. Ni kwa dhabihu hiyo ya Kristo mtu hupata msamaha wa dhambi na kipawa cha uzima wa milele.

k.15,16 Ijapokuwa Wakristo hawatoi dhabihu za wanyama, hata hivyo, wanatoa dhabihu. Dhabihu gani? Dhabihu zao ni kumsifu Mungu daima, kumkiri mbele za watu, kutenda mema na kushirikiana. Wamshukuru Mungu sana kwa wokovu wao, kwa Kifo cha Yesu kilichowapatia msamaha wa dhambi na kipawa cha uzima wa milele. Wanaonyesha shukrani zao kiutendaji katika kutenda mema, ndiyo shabaha ya kuokolewa kwao (Efe.2:8-10).

13:18, 19, 23 Mambo ya kuombewa

Viongozi wanaotajwa hapa ni wale waliowafuata wale waliotajwa katika k.7. Wapo wakati ule mwandishi alipokuwa akiwaandikia hao waumini. Anawashaur waumini kuwatii na kuwanyenyekea, kwa sababu wana wajibu mzito wa kuzitunza roho za waumini na baadaye wataitwa kutoa hesabu ya kazi yao mbele za Mungu. Neno lililotumika kwa kutii ina maana ya kushawishi na kuvuta. Kama wanafanya usimamizi wao vizuri, katika kicho cha Bwana, waumini hawatakuwa na sababu ya kusikia shida katika kuwatii na kuwanyenyekea. Furaha ya viongoi imo mikononi mwa waumini. Kama viongozi wmewajibika kuwaongoza vizuri, vivyo hivyo, na waumini wamewajibika kuyapokea mafundisho yao na kuyatia maanani na kuyatimiza katika maisha ya kila siku, kwa sababu mafundisho ya viongozi wazuri yanatoka katika Neno la Mungu. Viongozi wanaoongozi waumini wasiotaka kutoa kiroho, watu wasio na mzigo juu ya kuishi kwa kulingana na imani yao, huwahuzunisha viongozi. Viongozi wa kweli hatawali kwa nguvu ya kulazimisha kama watawala wa dunia hii, waongoze kama Bwana Yesu alivyosema kwa Mitume (Mk.10:42,43) na kama akina Paulo na Petro na Yohana walivyosema baadaye (2 Kor.1:24; 1 Pet.5:3; 3 Yoh.9,10).

13:20-21 Baraka ya kuagana

k.18-19 Jambo moja kubwa katika maisha ya Kikristo ni maombi, hasa kuombeeni. Mara nyingi katika Agano Jipya nyaraka zinasisitiza jambo hilo. Mwandishi anasikia haja ya kuombewa na wale anaowaandikia. Yawezekana wengine wamemlaumu kwa vile alivyowaonya juu ya hali yao ya kutaka kurudi kwenye dini ya Kiyahudi. Yeye mwenyewe anayo dhamiri njema, amekuwa na

mzigo juu ya waumini hao, ametimiza wajibu wake kwao katika kuwaandikia barua hiyo yednye maonyo na kwa upande wake lengo lake ni kuishi maisha yake sawasawa na imani yake. Pamoja na kutaka yeye na wao kuombeeni analo jambo moja la binafsi analotaka waliombee, nalo ni yeye kurudi kwao mapema. Ni wazi kwamba anawapenda na anataka kushirikiana nao kwa ukaribu.

Ndipo yeye alikuwa akiwaombea kwa Mungu. Ombi lake ni zuri sana, na kuhusu wao kwa msaada wa Mungu kukamilika ili wafanye mapenzi ya Mungu ili Mungu Mwenyewe apendezwe na kutukuzwa. Tutazama maneno aliyoyatumia katika ombi lake kwa Mungu. Kwanza kabisa amwita Mungu „Mungu wa amani" ukumbusho wa hali ya Mungu aliye asili ya amani, mpenda amani, aliyepatanisha wanadamu, wenye dhambi, na Nafsi yake aliye Mtakatifu. (Rum.5:1; Efe.2:14-17; Kol.1:20). Yesu alikuwa njia ya upatanisho huo alipokufa Msalabani kama dhabihu ya dhambi, akimwaga damu yake kwa msamaha wa dhambi. Mungu alimfufua kutoka wafu kwa nguvu na kutia muhuri yake kwenye Agano Jipya, damu ya milele. Yesu ameitwa „mchungaji mkuu wa kondoo" maneno yanayosisitiza huruma ya Mungu na utunzaji mzuri wa Yesu aliyejaa huruma kwa wanadamu. Ni Mungu anayeokoa, na Mungu mwenye nguvu, ni Mungu mwenye kujaa huruma; Mungu aliye mwaminifu kwa Agano lake, amefungana kabisa na watu wake; Mungu mwenye msaada anayeweza kuwakamilisha waumini ili watende mema na kutimiza mapenzi yake, Yeye Mwenyewe akifanya kazi ndani yake na kuwatengeneza kwa kuponya shida zao na kuwapa vipawa kwa shabaha hiyo, ili mwishowe wampendeze na kumtukuza. Ni hapa tu, katika Waraka mzima, ambalo neno la Yesu kufufuka limetajwa, hasa Waraka umesisitizwa kule Kutukuzwa kwa Yesu mbele za Baba na kufanya kazi ya Kuhani Mkuu mbele zake akitupatia baraka zote zitokanazo na Kifo Chake.

13:22, 24-25 Maneno ya kuufunga Waraka

Kama desturi yake katika Waraka huo anawasihi tena kuupokea waraka huo ambao anauita „neno hili lenye maonyo". Ni barua kutoka mtu mwenye moyo wa kiuchungaji, na andiko lake linaonyesha mzigo wake juu yao na sababu yake ya kutoa maonyo kwao. Waraka umejaa theologia ila hasa usifikiriwi kuwa hati ya theologia.

Halafu anawapasha habari za Timotheo, bila shaka huyo Timotheo ni yule aliyekuwa mjoli wa Paulo. Inaonekana alikuwa amefungwa ila hatuna habari za kufungwa kwake na wapi alipofungwa na sababu yake hasa. Habari njema ni kwambe amefunguliwa na mwandishi alitaka kumleta pamoja naye atakapokuja kwao karibuni hivi, ikiwa atamfikia kabla ya kuondoka kwake.

k.24 Hapo twaona umuhimu wa kushirikiana. Inaonekana barua yenyewe ilikwenda kwa shirika kadha, si kwa viongozi fulani. Mwandishi anataka viongozi wote na waumini wote wasalimiwe, mkazo ni juu ya wote kusalimiwa.

Watakatifu wote ni waumini wote, katika Nyaraka ni neno linalotumika kwa waumini, si neno kwa watu wachache wa pekee. „Hao wa Italia" huenda ni wale ambao asili yao ni Italia, kwa sababu hatujui hasa mwandishi alikuwa wapi alipoandika barua hiyo, wala hatujui kwa hakika walioandikiwa waliishi wapi.

k.25 Neema ndiyo asili ya mambo yote (2:9; 4:16; 10:29;, 12:15,28; 13:9) na mwandishi amefunga waraka wake na neno hilo. Neema ni fadhili ya Mungu katika Kristo.

MASWALI

1. Mwandishi aliwapa waumini mashauri na mausia gani?

2. Alisemaje kuhusu viongozi?

INSHA *(Kuhusu Waraka mzima)*

Andika insha ya kuonyesha ni mambo gani makuu ambayo umeyajifunza kutoka Waraka

Andika insha kumhusu Kristo na upekee wa Nafsi yake, upekee wa huduma yake na upekee wa dhabihu yake
Umepata msaada gani kwa maisha yako ya kiroho?

UFAFANUZI WA WARAKA WA YAKOBO

YALIYOMO

UTANGULIZI

a) Mwandishi
b) Walioandikiwa
c) Tarehe ya Kuandikwa
d) Sababu ya Kuandikwa
e) Umuhimu wa Waraka Kwetu Sisi

UFAFANUZI

1: 1 Salaam zake
2-11 Majaribu na hekima ya kuyakabili
12-18 Kuvumilia majaribu
19-25 Umuhimu wa Neno la Mungu
26-27 Dini iliyo safi

2: 1-8 Onyo juu ya upendeleo
9-13 Sheria ya Kifalme na ya Uhuru
14-26 Imani ya kweli na ile isiyo kweli

3: 1-12 Kutawala ulimi
13-18 Hekima ya kidunia na hekima itokayo kwa Mungu

4: 1- 5 Onyo juu ya choyo na kupenda dunia
6-10 Kumkaribia Mungu kwa unyenyekevu
11-12 Onyo juu ya kusingiziana
13-17 Onyo juu ya kupanga maisha bila kumjali Mungu

5: 1- 6 Onyo juu ya choyo na udhalimu
7-12 Haja ya kuvumilia
13-18 Uwezo wa maombi mbalimbali
19-20 Kumrejeza ndugu aliyepotea

UTANGULIZI

a) Mwandishi

Katika Agano Jipya wako watatu au zaidi wenye jina la Yakobo. Wawili wao wametajwa katika orodha za Mitume zilizomo katika Injili ya Mathayo, Marko, na Luka. Mmoja ni Yakobo, Mwana wa Zebedayo aliyekuwa ndugu wa Mtume Yohana. Pia Yakobo wa Alfayo ametajwa katika orodha hizo, ila hamna habari zaidi juu yake.
Katika hao wawili aliyejulikana zaidi ni Yakobo, mwana wa Zebedayo. Yakobo wa Alfayo hatajwi isipokuwa katika jumla ya Mitume 12 au Thenashara kama walivyoitwa mara kwa mara.

Yakobo wa Zebedayo alikuwa wa kwanza katika Mitume kuuawa kwa imani yake, taz. Matendo 12. kama B.K.44. Kwa hiyo, ni vigumu kufikiri kwamba yeye ndiye mwandishi wa kitabu hicho.

Kwa kuwa hatuna habari yoyote juu ya Yakobo wa Alfayo ni vigumu kufikiri yeye ndiye mwandishi, ila hatuwezi kusema hivyo kwa uhakika.

Ila, kuna Yakobo mwingine, ndugu yake Bwana Yesu, ambaye hudhaniwa na wengi kuwa mwandishi. Tunazo habari mbalimbali juu yake, na habari hizo zinatuongoza kufikiri yeye ndiye mwandishi wa kitabu hicho.

Wakati wa Huduma yake Bwana Yesu ndugu zake hawakumwamini taz. Yn.7:2,5. Yesu alimtokea Yakobo baada ya Kufufuka Kwake (1 Kor.15:7) na yeye pamoja na ndugu zake wengine walikuwapo kabla ya Pentekoste wakimsubiri Roho Mtakatifu, pamoja na Mitume, wanawake, na mamaye Yesu. (Matendo 1:14).

Yakobo alionekana kuwa Mwenye Kiti katika Baraza Kuu la Kanisa lililofanyika Yerusalemu, kama B.K.49. Baraza hilo lilikuwa la maana sana kuhusu maendeleo ya Injili hasa kati ya WaMataifa. Baadhi ya waumini wa Kiyahudi walitaka kuwalazimisha waumini wa KiMataifa watahiriwe na kushika Torati, na mashindano makali yalitokea. Uamuzi ulitolewa na Baraza hilo na uamuzi huo uliwaruhusu Wakristo wa KiMataifa wapokelewe kwa kubatizwa bila kutahiriwa.

Kwa hiyo, huyo Yakobo, ndugu yake Bwana Yesu, alikuwa na heshima na cheo katika Kanisa la Yerusalemu. Tukichunguza tabia yake alionekana mtu mtaratibu sana, mtu wa kutegemewa na Wayahudi wenzake, aliye na uzoefu mkubwa katika Agano la Kale. Vilevile alikuwa na mzigo juu ya Wakristo kuishi maisha safi yapatanayo na imani yao, akizingatia sana mafundisho ya Bwana Yesu katika Hotuba ya Mlimani.

Yusufu (Josephus) Mwandishi wa Historia ya Kiyahudi alisema kwamba Yakobo aliuawa kama B.K.62 hivi.

b) Walioandikiwa

Tukiangalia Sura ya kwanza na kifungu cha kwanza Yakobo ametumia maneno hayo „kwa kabila 12 zilizotawanyika". Kuna maelezo mawili kuhusu maneno hayo. Ama „kabila 12 zilizotawanyika" ni lugha ya kueleza shirika za Wakristo wa Kiyahudi waliokuwa hapa na pale. Ikiwa ni hivyo Yakobo alikuwa akiwalenga Wayahudi wenzake waliogeuka kuwa Wakristo. Ama alikuwa na maana ya Kanisa Zima duniani, akitumia lugha ya Agano la Kale kwa Watu Wapya wa Mungu waliokuwa wameingia katika urithi wa Watu wa Mungu wa Zamani, yaani Israeli ya Kale.

Kwa sababu Yakobo alikuwa Myahudi na kuwaza kama Myahudi, hali amekolea kabisa mafundisho ya Agano la Kale, si ajabu atumie lugha hiyo ya „kabila 12 zilizotawanyika" kueleza Kanisa Zima na waumini wote. Kwa hiyo alikuwa akiwalenga Wakristo wote, Wayahudi kwa Wamataifa, akihesabu kwamba Mungu bado angali akiwakusanya watu Kwake kama alivyofanya zamani, na Watu wa Mungu wanaendelea katika Kanisa la Kristo. Hata Paulo aliwaza na kufundisha vivyo hivyo, na Petro pia katika Nyaraka zake.

Yawezekana aliuandika Waraka ili usomwe katika makanisa siku ya Jumapili, labda yote yalisomwa mara moja na kurudiwa Jumapili nyingine. Tena watu wameona kwamba ni rahisi kuugawa Waraka katika sehemu mbili; Sura ya 1 na ya 2 zina vifungu 53 na sura ya 3 hadi 5 zina vifungu 55. Hakuna shida yoyote kwa upande wa kuanzia au kwa upande wa kumalizia katika kusoma sehemu zote mbili kwa wakati tofauti.

c) Tarehe Ya Kuandikwa

Wataalamu wengi huwaza kwamba Waraka huu uliandikwa mapema kama B.K.50. Ikiwa ni hivyo Waraka ni mmojawapo wa zile za kwanza kuandikwa.

d) Sababu ya Kuandikwa

Tunapousoma Waraka huu hatuoni dalili ya kuwepo shida fulani kubwa au tatizo kubwa lililomsukuma Yakobo auandike Waraka huu, kama, kwa mfano, ilivyokuwa wakati wa Paulo kuwaandikia Wagalatia na Wakorintho. Hata hivyo, katika hali yake kuwa na uongozi katika Kanisa la Yerusalemu, na kujua hali ya makanisa mbalimbali, alitambua kwamba ipo hatari kubwa kwa Wakristo kukosa kuishi kama ilivyowapasa kulingana na imani yao. Katika Waraka huo Yakobo hasemi juu ya toba na kumwamini Kristo; hasemi juu ya Msalaba na Ukombozi wa Kristo. Alijua wale anaowaandikia wamekwisha kukubali hayo yote.

e) Umuhimu wa Waraka Kwetu Sisi

Mkazo ni juu ya kutenda na kuishi maisha ya Kikristo na Waraka unatoa uongozi mzuri kwa Mkristo yeyote, wa wakati wowote, na wa mahali popote. Waraka huo unagusa mambo kama Majaribu, na jinsi ya kupambana nayo; Hekima; umuhimu wa Neno la Mungu na Maombi. Ametaja dhambi na makosa mbalimbali kama upendeleo, dhambi za ulimi na usemi, tabia ya kupenda dunia, tabia ya ugomvi na mashindano, ya kusengenya ndugu na kumhukumu, kupanga maisha bila kumjali Mungu. Pia ametaja hatari ya utajiri kwa wenye mali ambao hujaribiwa kutumia mali yao vibaya. Hivyo, Waraka huo unao msaada mkubwa kwa maisha yetu ya Kikristo.

Kwa kukaza sana matendo yetu Je! amepunguza fundisho la kuhesabiwa haki kwa imani na kuokolewa kwa neema peke yake? Hasa tukilinganisha na Waraka kwa Wagalatia na jinsi Paulo alivyosisitiza sana neno la Imani. Paulo alikuwa akihojiana juu ya wokovu, na njia ambayo kwayo wokovu unapatikana, kwa hiyo alikaza sana kwamba wokovu hauji kwa matendo yetu wala kwa kustahili kwetu, bali kwa kumwamini Kristo tu.

Yakobo alikuwa akihojiana juu ya Imani ya kweli, akionyesha njia ya kupima ukweli wa imani inayookoa. Kwake imani ya mtu hutambulikana katika maisha yake - kama Yesu alivyosema „kwa matunda yao mtawatambua" (Mt.7:16). Lazima imani iwe hai, ifanye kazi, itokeze matendo, izae matunda. Ni rahisi kwa mtu kudai kuwa na imani, ila tutajuaje madai yake ni kweli? Jibu la Yakobo ni, “tazama maisha yake”. Imani na matendo vinawiana kabisa, imani inayokosa matendo, si imani!

UFAFANUZI

1:1 Salaam zake

Katika salaam zake Yakobo amejieleza kuwa “mtumwa wa Mungu na wa Bwana Yesu Kristo”. Hakudai cheo chochote au uongozi au mamlaka yoyote. Watumishi wote wa mwanzoni walipenda sana kujidhili na kujiita „watumwa" wakimweka Bwana Yesu sawa na Mungu.

Kama ambavyo tumeona katika utangulizi kuhusu Walioandikiwa, wao wameitwa „kabila kumi na mbili waliotawanyika". Ni Kanisa Zima ambalo limeenea mahali pengi katika ulimwengu ulio kinyume chake. Mungu amekusanya Kwake watu wa kabila mbalimbali (tusifikiri ni Israeli, wale kabila kumi na mbili tu) na mwisho wa mambo yote, Yesu atakapokuja, tutakusanyika Kwake. (Yak.5:7 na 1 The.4:17).

1:2-11 Majaribu na Hekima ya kuyakabili

Akiwa ulimwenguni Mkristo atakutana na majaribu, na hayo majaribu yataipima

imani yake. Shida na dhiki na magumu ya maisha huja, tukipenda, tusipende, lazima tuzikabili. Tutazikabili kwa njia gani na kwa mawazo gani? Yakobo amesema neno la ajabu sana; amesema „hesabuni ni furaha tupu, mkiangukia katika majaribu mbalimbali" Kwa hiyo, itikio letu ni kuyakaribisha kwa furaha. Swali la kujiuliza ni „kwa nini?" Kwa sababu ni njia ya kukuza imani yetu na kuitia nguvu. Imani yetu itadhihirishwa kuwa ya kweli. Mungu atatumia mambo hayo yasiyo mazuri kwa makusudi mema ya kuleta faida katika maisha yetu ya kiroho. Mkristo atakua na kukomaa, Mkristo atajifunza subira na atakamilika kiroho.

Ni kitu gani hasa kitakachotusaidia kuwaza hivyo juu ya majaribu na kuitikia vema kwa kuyakaribisha kwa furaha? Kitu kinachohitajika ni Hekima.

Tutapataje hiyo hekima? k.5. Ni kipawa ambacho Mungu humpa mtu anayemwomba bila shaka. Atakayeipata ni mtu mwenye nia safi, aliye na lengo moja tu, huyo atapewa na Mungu, kwa sababu Mungu hupenda sana tuwe na hekima katika maisha yetu, maana kwa msaada wa hekima tutazidi kutambua na kutimiza mapenzi yake. Kwa hekima ya kibinadamu tusingefikiri kwamba yatupasa kukaribisha dhiki na magumu ya maisha kwa furaha!!

Twaona jinsi Yakobo alivyokumbuka sana mafundisho ya Bwana Yesu: Kuhusu kuomba kwa imani pasipo shaka linganisha na Mathayo 17:20: 21:21-22 na Marko 11:23-24.

Katika 1:9-11 Yakobo ametoa mfano wa hekima na jinsi itakavyowasaidia watu wa hali mbalimbali katika maisha yao. Mtu maskini au mtu asiye na cheo, ni rahisi asikie kukwazwa na hali yake - lakini, akiwa Mkristo mwenye hekima itokayo juu atatambua kwamba hata yeye anacho cheo kikubwa sana, ni mtoto wa Mungu na mrithi pamoja na Kristo. Kwa sababu hiyo hataisikitikia hali yake.

Vilevile tajiri, kwa hekima itokayo juu atamsifu Mungu kwamba ameshushwa asiutegemee utajiri wake. Alipomjia Kristo Msalabani ilimbidi aje Kwake kama mwombaji na mhitaji asiye na kitu cha kuchangia kwa ukombozi wake. Kwa hiyo, maskini na tajiri, wataupata ushindi kwa kujua namna ya kuwaza juu ya hali zao tofauti, na ujuzi huo wataipata kwa hekima ambayo Mungu atawapa wanapomwomba pasipo shaka.

1:12-18 Kuvumilia majaribu

Katika sehemu hiyo Yakobo aliendelea kusema juu ya Majaribu, ila katika sehemu hiyo majaribu ni tofauti na yale ya sehemu ya kwanza. Katika sehemu ya kwanza yalikuwa aina ya shida, dhiki, na magumu ya maisha hayo, yanayotujia kwa sababu tupo duniani na hayo hayana budi kutujia mara kwa mara.

Katika k.12 Yakobo ametaja uheri wa mtu anayestahimili majaribu yake, kwa sababu mwisho wake ni uzima wa milele.

Kuanzia kifungu cha 13 Yakobo ametaja kujaribiwa kwa maovu kutokana na tamaa zetu za ndani. Amesema wazi kwamba majaribu hayo kamwe hayatoki kwa Mungu. Shauri lake ni tofauti sana na hapo nyuma. Pale tulishauriwa tuyakaribishe kwa furaha, tena kwa njia yake, imani yetu itakuzwa na kukomaa. Lakini sivyo ilivyo kwa majaribu anayozungumzia katika sehemu hiyo ya pili. Hayo ya pili yaweza kutudanganya, na kusababisha dhambi, ambayo mwisho wake ni mauti. Yatupasa kuyapinga hayo, kukataa kabisa tamaa zetu mbaya zinapoinuka ndani yetu. Kwa hiyo Majaribu ya aina ya kwanza huleta faida kubwa katika maisha yetu ya kiroho, ila, yale ya aina ya pili, tukiyakubali huleta hasara kubwa kiroho. Kwa hiyo itikio letu ni tofauti. Katika k.16 Yakobo ametoa onyo juu ya kudanganywa, twahitaji hekima ya Mungu kuyapambanua mambo hayo ya majaribu. Tukumbuke ya kuwa iwapo tumezaliwa kwa mara ya pili bado utu wa kale ungalimo ndani yetu, hivyo tuwe macho juu yake ili usiinuke. Tukilisha utu mpya huo utakuwa na nguvu, utaushinda ule wa kale. Tukilisha ule wa kale huo utakuwa na nguvu na kuzuia utu mpya usitawale maisha yetu.

k.17 Mungu ni Mpaji Mwema kabisa, Yeye hutoa Mema tu. Vipawa vyake vyote ni vyema, na kamili, na kufaa kabisa shabaha yake. Yeye Mungu Mpaji hana hila yoyote ndani yake, hana shabaha zilizofichwa katika Kutoa Kwake. Kila baraka hutokana na Wema Wake usio na kigeugeu, Yeye halegei wala hakati tamaa Mt.7:11. Hata katika miendo ya jua na mwezi kivuli chatokea, mwezi hupatwa, n.k. bali sivyo ilivyo kwa Mungu, Muumba wetu. Yeye ni nuru, wala giza lolote hamna ndani yake (1 Yoh.1:5).

k.18 Katika vipawa vyake vyote kipawa kilicho Bora ni Uzazi mpya, yaani kuzaliwa kwa mara ya pili na kufanywa kuwa Mtoto wa Mungu. Huo Uzazi bora unatokana na Kutaka Kwake Mungu Mwenyewe. Haongozwi wala kutawaliwa na lolote la upande wetu, Yu Huru. Pia unatokana kwa njia ya Neno lake. Twashirikishwa uzima wa milele kwa njia ya Neno la Kweli (Yn.1:12-13; 3:3-6; 1 Pet. 1:3, 23). Shabaha ya Uzazi Mpya ni kufanya sisi kuwa mali Yake, ili tujiweke wakfu kwa Mungu. Mfano wake ni jinsi Waisraeli walivyomletea Mungu malimbuko ya mavuno yao, sisi Wakristo ni malimbuko ya viumbe vyake.

1:19-25 Umuhimu wa Neno la Mungu

Je! Mkristo awezaye kukua na kukomaa kiroho? Katika sehemu iliyotangulia tumeona ya kuwa Yakobo alifundisha kwamba majaribu, (kama dhiki na magumu n.k.) yakikaribishwa kwa furaha ni njia mojawapo ya kuikuza imani ya mtu. Vilevile, majaribu (yatokanayo na tamaa zetu mbaya) yakipingwa ni njia nyingine ya kukua kiroho. Halafu Yakobo alitaja jambo la hekima iliyo kipawa

cha Mungu kuwa msaada kwa Mkristo kupambana na hali mbalimbali na kuziitikia vema, kusudi mtu akue kiroho.

Hasa Mkristo huhitaji msaada wa Neno la Mungu ambalo kwalo alizaliwa kwa mara ya pili. Neno la Mungu litamwongoza katika maisha ya Kikristo. Hivyo, Yakobo ameshauri mambo kadha kuhusu jinsi impasavyo Mkristo kulitumia Neno la Mungu.

Katika k.19 ameshauriwa awe mwepesi wa kulisikia; (Lk.8:18; 11:28; Mk. 4:9). Katika k.21 ameshauri kwamba mtu alipokee Neno kwa upole, na ajinyenyekee chini yake na kulijali. Pia alipokee katika hali ya maisha yake kuwa yametayarishwa kama shamba liwekwavyo tayari kwa kulimwa kabla ya mbegu kupandwa ndani yake. Katika k.22 Yakobo ametaja wajibu wa kulitii Neno na kulitekeleza ki-maisha.

Pamoja na hayo, Yakobo ameshauri mengine ili mtu akue kiroho. Mtu awe mzito wa kusema, asiwe mwepesi wa kutoa maoni yake, kwa sababu maoni yetu hayatakiwi kila wakati, ila ni kiburi chetu kinachotufanya kufikiri ni vema tuseme. Afadhali tutoe nafasi kwa Neno kuzungumza na sisi badala ya kuingia majadiliano marefu na kulitafiti sana.

Jambo jingine ambalo Yakobo ameshauri ni kwamba tusiwe mwepesi wa kukasirika (Mit.29:22).

Shabaha ya kulisikia Neno ni utendaji wa Neno, uheri si katika kulisikia bali katika kulitenda.

1:25: „sheria kamilifu iliyo na uhuru" - yaani Neno la Mungu, tusiwaze ni Agano la Kale tu. Yakobo ameliita „sheria" kwa sababu ni „mwongozo" kwa maisha ya Kikristo. Kwa kulitenda twapata baraka ya kuwekwa huru. Tusiwe wasikiaji wa muda tu, bali tudumu katika kulisikia na kulitenda.

1:26-27 Dini iliyo safi

Yakobo amekaza mambo matatu muhimu katika maisha ya Mkristo. Kwanza ni utawala wa ulimi. Amekwisha kugusa habari ya ulimi katika k.19 na aliendelea kusema juu yake tena katika sura ya tatu.

Mkazo wake wa pili ni kuhusu uangalizi wa wahitaji na wasio na msaada, tuwe na mzigo juu ya wajane na yatima n.k. (Zab. 68:5). Katika sura ya pili Yakobo amesema zaidi juu ya hilo.

Mkazo wake wa tatu ni usafi wa maisha, tusichafuliwe na dunia inayotuzunguka (1 Yoh.2:15-17 na 3:3)

MASWALI

1. *Twajifunza nini kutokana na Majaribu yanayotajwa katika 1:1-12?*
2. *Kwa nini yanaitwa "majaribu"?*
3. *Yakobo ameshauri tufanye nini na majaribu ya aina hiyo?*
4. *Tukifuata mashauri ya Yakobo itakuwaje kwa imani yetu?*
5. *Tunahitaji nini kutoka kwa Mungu itakayotusaidia kuitika vema? Bila kitu hiki, kwa kawaida, tungeitikaje?*
6. *Ziko tofauti gani kati ya majaribu ya kwanza na yale yaliyopo 1:13-18?*
7. *Tuwe na itikio gani kwa hayo, aina ya pili?*
8. *Itatokea nini kwa imani yetu ikiwa tutafuata mashauri ya Yakobo?*
9. *Kwa nini Neno la Mungu ni muhimu sana kwa Mkristo?*
10. *Kwa sababu ya umuhimu wake Yakobo ametoa uongozi juu yake Taja mambo kadha ambayo ametushauri.*
11. *Yakobo ametaja mambo matatu ya lazima katika "dini ya kweli". Kwa nini alichagua mambo hayo? Unakubaliana naye?*

2:1-8 Onyo juu ya Upendeleo

Kwa kweli Yakobo aligusa sana matendo yetu, hata hivyo, asili ya matendo yetu ni Imani tuliyo nayo katika Bwana Yesu kama alivyoandika katika k.1. Alimwita Bwana Yesu, Bwana wa utukufu na Yakobo aliona kwamba Utukufu wa Yesu ulidhihirika katika maisha na matendo yake. Aliona ya kuwa Yesu Kristo hakuwa na upendeleo wowote wa watu, kwa hiyo yawapasa wafuasi wake, vilevile, wasiwe na upendeleo wa watu. Kwa kutaja habari za upendeleo inaonekana ametambua ya kuwa upendeleo umeingia katika maisha ya Wakristo na ya Kanisa.

Upendeleo ni kosa kubwa. Ni kinyume cha imani ya Kikristo kwa watu kupokelewa tofauti wakati wa kwenda kusali na katika mikutano ya Kikristo, kwa sababu ya hali zao za kimwili, mavazi, cheo, n.k.

Kwanza ni kosa la kuwa na vipimo viwili, na hilo ni kinyume cha imani yetu. Pia ni kufanana na ulimwengu katika kupima watu kwa kutazama hali zao za nje, mavazi yao, sura zao (1 Sam.16:7). Ni kutokufanana na Mungu wetu na Bwana wetu. Mungu amejiita Mungu wa wajane na yatima. Bwana Yesu alifurahi sana kushirikiana na wanyonge na wasiopendwa na watu. Alifurahi kuwa mtumishi, alijifanya kama hakuwa na cheo wala hali. Kwa Kujidhili Kwake Mungu alimkuza mno na kumpa Jina lipitalo kila jina (Flp.2:7-11; Ebr.2:9). Tunafuata kielelezo cha Yesu kwa namna gani tunapobagua kati ya watu na kuwakaribisha tofauti katika makanisa yetu? Je! tunawabembeleza eti tupate pesa?

Upendeleo unakana kanuni ya wokovu wetu, kwa sababu Mungu ameonyesha huruma yake, si kwa uzuri wetu, bali kwa unyonge wetu. Potelea mbali tuwe na hali gani, sote tu wenye dhambi, na wokovu ni kipawa cha Mungu tusichostahili. Twaupata wokovu kwa kumwamini Yesu Kristo na Kifo Chake msalabani.

Wote wanaomjia Msalabani wamjia na mikono mitupu „sina cha mkononi" (1 Kor.1:16, 26-29).

Halafu Yakobo amesema kwamba ni wenye mali na cheo ambao mara nyingi huwaonea Wakristo k.6.

2:9-13 Sheria ya Kifalme na ya Uhuru

Yakobo aliendelea na habari ya upendeleo na kutaja Sheria ya Kifalme na Sheria ya Uhuru. Sheria ya Kifalme ni Sheria ya Mfalme wetu Yesu Kristo ambayo ni Upendo. Tukipendelea watu twaivunja sheria hiyo ya upendo, maana hatuwezi kupenda jirani tukiwa na upendeleo. Katika Ufalme wake Yesu huongoza na kutawala yote kwa sheria ya upendo (Mk.12:28-33; Rumi 13:8-10; Gal.5:14). Mungu aliwapa Waisraeli Sheria zake walipokuwa kwenye Mlima wa Sinai, baada ya wao kukombolewa kutoka utumwani (Kut.3:12). Sheria hizo hazikuwa ngazi ya kupanda na kustahili ukombozi wao, maana walikuwa wamekwisha kutolewa Misri, bali zilikuwa mwongozo kwa maisha ya wale waliokombolewa. Sheria ni Ufunuo wa tabia ya Mungu. Mungu ni Mmoja, Sheria nayo ina umoja, haiwezekani kuchagua kati ya sheria ipi ya kushika na ipi ya kutokushika. Mtu huwa mkosaji akiivunja moja tu hali ameshika zote zingine. Sheria ni Sheria ya Uhuru kwa sababu kutokana na kazi ya Kristo Msalabani tunashirikishwa uwezo wa kuzishika, uwezo ambao hapo nyuma hatukuwa nao maana tulikuwa watumwa wa dhambi bila uwezo. Uwezo huo umetuweka huru ili tushike sheria kwa kutaka na kwa moyo. Kwa mfano, sheria „usiibe" imegeuzwa kuwa si amri kali bali ahadi ya kuwa „sitaiba"kutokana na huo uwezo ninaojaliwa na Yesu.

Mkristo ni mtu aliyehurumiwa sana na Mungu, naye hushuhudia hali hiyo kwa kuwahurumia wengine. Si kana kwamba Mungu atatuhurumia kwa sababu tumewahurumia wengine, la, sivyo, ila ni njia ya kushuhudia kuhurumiwa kwetu. Tunapoonyesha upendeleo kwa matajiri na wenye vyeo tumekosea neno la huruma kwa kuacha kando wanyonge na wasio na msaada.

Kila mwanadamu huhitaji huruma za Mungu na hasa anapokabili Siku ya Mwisho ya Hukumu. Ikiwa tumekwisha kukubali huruma za Mungu katika kutuokoa ni vema tuzidi kuwahurumia wengine.

2:14-26 Imani ya Kweli na ile isiyo Kweli

Huenda walikuwepo Wakristo waliokataa kwamba Sheria ina sehemu yoyote

katika maisha yao, walidai wamewekwa huru, wameokolewa kwa neema bila nyongeza yoyote. Hata hivyo tutawezaje kutambua wale walio na Imani safi na wale ambao hudai kuwa na Imani, lakini maisha yao yana mambo yasiyopatana na madai yao.

Yakobo ametoboa wazi kwamba ipo imani ya kweli, na ipo imani isiyoweza kuhesabiwa kuwa imani, kwa sababu imekosa kuzaa matendo k.18. Katika k.14 na k.16 ametaja imani isiyofaa na k.17 imani iliyokufa, na k.20 imani isiyo na kazi. Ni imani ya maneno tu, isiyo na matendo k.14, 17,18, 20, 26 na imebaki kuwa madai ya mtu tu k.14, 26.

Katika k.14 Yakobo aliuliza swali kali “Je! imani ya namna hii yaweza kumwokoa?” Bila shaka jibu ni la, hata kidogo.

Ni wazi kwamba Yakobo alijua kwa hakika kwamba imani ni lazima, pia itangulie (1:3,6; 2:2, 23; 5:15). Katika kukaza matokeo ya imani amefanana na Bwana Yesu aliyefundisha kwamba imani ya kweli itatambulikana kwa matunda katika maisha (Mt.7:16-20). Kinyume cha wengine ambao hufikiri Yakobo amefundisha Kuokolewa kwa Matendo, ni dhahiri msingi wake ni Imani, ila alichunguza juu ya ule ukweli wa imani, si kwa upande wa mafundisho au theologia bali kwa upande wa utendaji.

Ametoa mifano minne, miwili juu ya imani isiyofaa na miwili juu ya imani ifaayo.

Mfano wa kwanza ni juu ya imani isiyofaa: k.15-17. Picha ni ya mtu na jirani yake mwenye shida ya kupungukiwa na riziki. Yule mtu alitoa shauri jema kwa jirani yake, maana kwa maneno yake alionyesha huruma; ila alikosa kufanya jambo lolote la kumsaidia, hakumpa nguo wala chakula, kwa hiyo yule jirani akabaki katika hali yake ya shida. Imani ya huyo mtu haikuwa hai, haikuzaa matunda, haikufaa kitu.

Mfano wa pili pia inahusu imani isiyofaa, ila katika mfano huo ni kati ya mtu na Mungu wake k.18-20. Yakobo amesema kwamba hata mashetani wanajua na kuamini Mungu yuko, lakini imani hii haiwasaidii kitu, wamebaki katika hali ya kutetemeka na kuogopa, hawabadili mwenendo wao, bado ni wapinzani wa yule wanaomwamini kuwa yuko. Hata sisi twaweza kuwa na imani kichwani isiyoleta mabadiliko yoyote maishani mwetu.

Katika k.21-26 Yakobo ametoa mifano miwili ya imani ya kweli. Mfano wa kwanza k.21-24 unamhusu Ibrahimu, imani yake ilifanya kazi k.22 na kwa matendo yake imani yake ilikamilika. Katika sura ya kwanza na vifungu vya 3 na 4 Yakobo alisema kwamba imani ya mtu hupimwa na kujaribiwa na kwa njia hiyo hukamilishwa. Katika Mwanzo 15:6 twasoma Ibrahimu alimwamini Mungu na kwa sababu hiyo alihesabiwa haki. Katika Mwanzo 22:1 imani yake ilipimwa vikali sana alipoitwa na Mungu kumtoa Isaka kuwa dhabihu. Yeye hakusita,

akamtii Mungu na kwa njia hiyo imani yake ilikamilishwa (Mwa.22:12 na Ebr.11:17-19). Kwa hiyo ukweli wa imani yake ulithibitishwa.

Halafu Yakobo ametoa mfano mwingine wa imani ifaayo. Rahabu alionyesha ukweli wa imani yake alipowakaribisha na kuwahifadhi wale wageni waliomjia. Aliwasaidia kwa mahitaji yao, aliwaficha darini hata aliweka maisha yake hatarini kwa ajili yao. Kwa imani alifahamu Waisraeli wataushinda mji wa Yeriko, akajiandaa kwa kupatana na hao wageni, matendo yake yalilingana na imani yake.

Je! Yakobo alikuwa akipinga mafundisho ya Paulo juu ya kuhesabiwa haki kwa imani peke yake, hasa jinsi alivyokaza katika Waraka kwa Wagalatia na kwa Warumi?

La, hoja zao ni tofauti.

Paulo alitaka kuonyesha jinsi mtu anavyoupata wokovu. Njia ya kuupata wokovu ni kwa kumwamini Kristo tu na kazi yake ya upatanisho alioufanya Msalabani.

Yakobo alitaka kutoboa wazi imani ya kweli ni imani gani. Kwa hiyo alikaza kwamba lazima imani iwe hai, izae matunda, iwe na matendo. Hakufundisha mtu ataokolewa kwa matendo. Mara nyingi ametumia neno la imani. Tutatambuaje imani ya kweli inayomwokoa mtu? Kwa matunda yatokanayo kwa imani yake. Imani inayobaki kama wazo la mtu au ukiri wake haina faida (Mt.22:1-14 na Ufu.19:8). Tumeokolewa ili tuzae matendo mema (Efe.2:8-10).

MASWALI

1. *Je! Jambo la "upendeleo" latuhusu sisi Wakristo wa leo?*
2. *Je!"Upendeleo" upo katika makanisa ya leo? Eleza.*
3. *Toa sababu za kuonyesha jinsi upendeleo ni "dhambi" na kuwa kinyume cha imani ya Kikristo.*
4. *Ni nini iliyo Sheria ya Kifalme?*
5. *Je! Yampasa Mkristo aishike?*
6. *Kwa nini Sheria imeitwa ya "Uhuru"? Eleza maana yake*
7. *Yakobo alifundisha nini juu ya uhusiano kati ya imani na matendo?*
8. *Je! alimpinga Paulo na mkazo wake juu ya imani? Je! alitaka kuweka matendo badala ya imani kuwa kitu muhimu? Lengo lake hasa lilikuwa nini?*

3:1-12 Kutawala Ulimi

Yakobo amekwisha kutaja habari za ulimi 1:26; 2:12. Katika 1:19 aliunganisha jambo la kuzaliwa upya na jambo la kusema na kufundisha umuhimu wa ulimi katika dini iliyo safi 1:26.

Yawezekana Wakristo walikuwa wakiithamini sana kazi ya kuhubiri na kushuhudia. Mara nyingi twafikiri Mkristo apaswa kutoa ushuhuda wa maneno mara baada ya kukata shauri la kumpokea Kristo, hata, pengine twawapa kazi ya kuhubiri Neno kabla hawajapata ujuzi wa maisha ya kiroho na ya Maandiko.

Mara nyingi hatujali dhambi za usemi, wala kufikiri kwamba ukosefu katika kunena ni dhambi. Ni vema tukumbuke ya kuwa Biblia inasema sana juu ya usemi wetu na matumizi ya maneno.

k.1 „msiwe waalimu wengi" kwa nini? ni neno ambalo tusingefikiri lisemwe, maana haja kubwa ipo ya mafundisho. Chombo cha mwalimu ni ulimi. Mwalimu ana nafasi kubwa na tele za kuongoza mawazo na maisha ya watu. Kuna majaribu mengi, na ni rahisi kukosa. Kwa sababu mwalimu anagusa maisha ya watu, lazima, aangalie sana mafundisho yake na matumizi ya maneno katika kufundisha. Kwa sababu mwalimu aweza kufanya makubwa na kuleta baraka nyingi ila kwa upande wa pili aweza kusababisha shida nyingi, ndiyo sababu hukumu yake itakuwa kubwa.

Si kana kwamba Yakobo alitaka Mkristo awe na ulimi ulionyamaa, La! sivyo. Yeye alitaka Mkristo awe na ulimi uliotawaliwa. Yeye hakuwa kinyume cha watu kuhubiri na kushuhudia n.k. ila hakupenda Wakristo wawe wepesi wa kusema na kuthamini kazi hizo zaidi. Mkristo anapotawala ulimi wake anamtukuza Bwana wake vizuri.

Katika k.2 alisema neno kubwa "mtu asiyejikwaa katika kunena huyo ni mtu mkamilifu awezaye kuuzuia na mwili wake wote". Aliona ya kuwa utawala wa maisha unatokana na utawala wa ulimi. Mtu atawalaye ulimi wake amepata nguvu ya kuzitawala tamaa zote zingine.

k.2-4 Yakobo alitoa mfano wa farasi, na mfano wa usukani wa merikebu. Lijamu hutumika kutawala farasi - lijamu ni kitu kidogo sana kulingana na farasi: Usukani ni kitu kidogo sana kulingana na merikebu: Ajabu ni kwamba vitu hivi vidogo vyaweza kutawala na kuongoza vitu vikubwa. Farasi ni mnyama mwenye nguvu nyingi, lakini huongozwa na lijamu tu. Merikebu ni kitu kikubwa, hata hivyo huongozwa na usukani tu.

Vilevile katika viungo vyetu ulimi ni kiungo kidogo, hata hivyo ulimi hufanya makubwa, kwa hiyo ulimi ni ufunguo wa nguvu za mtu. Tutakubaliana ni kweli

tukiwaza hotuba za wana siasa, na mahubiri ya mapasta na wainjilisti. Serikali zimepinduliwa, maisha ya watu yamepinduliwa kwa njia hiyo.

k.5-6 Nguvu ya ulimi hasa unaelekea maovu, ni kama nguvu ya moto. Yakobo umetumia mfano wa moto na msitu unaowashwa na moto mdogo sana, hata moto ya kiberiti tu. Moto huenea kwa haraka mno na kusababisha hasara kubwa.

Tabia ya ulimi ni uovu: na ulimi umo ndani ya miili yetu kama kiungo kimojawapo. Ni kama ndani yetu uovu umepata mjumbe au mteteaje wake, na kuweka kikao chake ndani yetu. Katika k.6 twakuta maneno “nao ulimi ni moto; ule ulimwengu wa uovu, ule ulimi, umewekwa katika viungo vyetu”. Katika Maandiko „ulimwengu" una maana ya kujumlisha yote yaliyo kinyume cha Mungu.

Pia Yakobo alisema ulimi unanajisi mwili wote, ni kama maovu yetu yapitia kwa njia ya ulimi, hata tunajisemea na kujitetea mashauri ya kufanya dhambi.

„mfulizo wa maumbile" Ni vigumu kujua hasa Yakobo alikuwa na maana gani kwa kutumia lugha hiyo. Labda aliwaza ya kuwa ulimi unaendelea na kazi yake tangu mwanzo hadi mwisho wa maisha yetu. Tunapozeeka tunaacha dhambi zingine, lakini siyo za ulimi.

„nao huwashwa moto na Jehanum" Ulimi ni rafiki wa Shetani, Shetani huutumia sana kwa kutekeleza shabaha yake ya kumpinga Mungu. Hata mashauri mengine yaonekana ni mazuri, kumbe sivyo, tukikumbuka jinsi Petro alivyojaribu kumshauri Bwana Yesu asiende Msalabani (Mt.16:22).

Wakati wa Pentekoste, Roho wa Mungu alishuka na ndimi za Mitume na wenzao ziliguswa ili ziwe vyombo vya kumshuhudia Kristo (Mdo.2:11, Isa.6:7).

k.7-8a Yakobo aliendelea na mafundisho yake makali kuhusu ulimi. Alisema, ulimi haufuguki, ni kitu ambacho kimemshinda mwanadamu. Wanadamu wamefaulu kufuga wanyama na viumbe wengi sana, lakini hakuna awezaye kuufuga ulimi kwa nguvu zake mwenyewe. Kwa hiyo Mkristo anayeutawala ulimi wake anatoa ushuhuda mkali, kwa sababu, hali hiyo haielezeki nje ya nguvu ya Mungu - „bali ulimi hakuna awezaye kuufuga"

k.8b-11 Yakobo alizidi kusema juu ya ulimi. Ulimi hautulii, ghafula huamka na kujitokeza, bila kutazamiwa. Pia ni sumu kama sumu ya nyoka, sumu iletayo mauti. Sumu inayouharibu uhusiano kati ya mtu na mtu, hata ndani ya nyumba. Bila shaka Yakobo alikumbuka Bwana Yesu Mwenyewe - Yn.7:46 “Hajanena kamwe mtu yeyote kama huyu anavyonena”; Luka 4:22 “Wakiyastaajabia maneno ya neema yaliyotoka kinywani mwake” Isaya alisema alama ya Mtumishi Ateswaye itakuwa “hana hila ulimini mwake” (Isa.53:9).

Isaya mwenyewe alipoitwa na Mungu alijishuhudia dhambi yake kwa kukiri uchafu wa ulimi wake, ndipo alitakaswa midomoni (Isa.6:1ku).

Ulimi unao unafiki mkubwa wa kuwa na mambo mawili yasiyopatana. Twaweza kuwalaani wanadamu, huko tunamhimidi Mungu. Yakobo alisema chemchemi haitoi maji matamu na maji machungu katika jicho moja, wala haiwapasa wanadamu kutoa maneno mabaya na maneno mazuri katika ulimi mmoja. Mara nyingi mabaya yanayashinda mazuri na kukumbukwa zaidi. Ni rahisi kufuta baraka za ibada yetu tunapotoka nje na kusema vibaya, kusengenya, n.k.

Ulimi ni kioo cha moyo wa ndani (Mt.12:34-37; 15:18-20).

3:13-18 Hekima ya kidunia na hekima itokayo kwa Mungu

Yakobo amekwisha kusema juu ya hekima na jinsi tunavyohitaji hekima ya Mungu na utayari wa Mungu kutupatia hiyo hekima tukimwomba bila kusitasita I:5ku.Hekima itatusaidia kutambua umuhimu wa kuenenda vema tukiishi kwa kumpendeza Mungu.

Hekima si neno geni kwa watu wa Mungu. Katika Agano la Kale vitabu kama Ayubu, Mithali, na Mhubiri, vilikaza umuhimu wa kuwa na hekima. Kwa hekima ya Mungu Mkristo atayakabili mambo yote ya maisha kwa tabia zinazompendeza Mungu. Atakuwa mpole kama Bwana wake (Mt.11:29:53; Rum.12:3; Efe.4:1). Atatafuta amani na atataka kuwa na maisha safi.

Baadhi ya watu huona ni hekima kugombana na watu, na kujiona na kuwa na mabega ya kujisukuma, kuwaonea wivu wengine, n.k. lakini hekima ya namna hiyo haitoki kwa Mungu, bali kwa Shetani. Ndipo Yakobo aliorodhesha sifa za hekima itokayo juu kwa Mungu, nazo ni: usafi, amani, upole; utayari wa kusikiliza mashauri ya watu, rehema, matunda mema. Hekima itokayo juu kwa Mungu haina fitina wala unafiki. Orodha hiyo hutusaidia kujipima ili tuone kama sisi wenyewe tunayo hekima hiyo ya Mungu.

Kuanzia sura ya nne hadi sura ya tano, kifungu cha sita, Yakobo ametoa maonyo juu ya hali na tabia za ki-dunia na jinsi Mkristo awezavyo kuzishinda. Mwisho wa sura ya tatu tulipewa sifa za hekima itokayo kwa Mungu, na mkazo ulikuwa juu ya kuishi kwa amani na upole bila fitina na unafiki.

MASWALI

1. *Zungumzia alivyosema Yakobo juu ya hatari ya ulimi. Je! unakubaliana naye? Umejifunza nini kutokana na alivyosema? Tutawezaje kuzitawala ndimi zetu?*
2. *Eleza tofauti zilizopo kati ya hekima ya dunia na hekima ya Mungu?*

4:1-5 Onyo juu ya choyo na kupenda dunia

"urafiki wa dunia" Mwanzoni wa sura ya nne badala ya amani twakuta habari za "vita na mapigano". Vita ipo kwa Mkristo kwa sababu yeye ni adui si rafiki wa dunia hii mbovu. Urafiki na dunia huugusa uhusiano wetu na Mungu na uhusiano wetu na wengine na kuuharibu.

Neno "tamaa" limetajwa katika k.1 na k.3. Kiini cha kupenda dunia au kuwa na urafiki na dunia ni kujipenda na kutamani vitu kwa ajili ya faida yetu wenyewe. Hivyo twamwonea mtu wivu, na kupigana naye, hata mwishowe wengine wamekuwa tayari kumwua mtu ili wajipatie kitu fulani. Huenda kitu kinachotaminiwa si kitu kibaya ila sababu ya kukitaka ni mbaya. Twakumbuka jinsi Kaini alivyomwonea Habili ndugu yake wivu kisha akamwua (Mwa. 4); pia Daudi alimtamani mke wa Uria, akapanga Uria auawe vitani ili awe na mkewe (2 Sam.11); Mfalme Ahabu alitamani sana shamba la mzibabu la Nabothi, akamwua (1 Waf.21). Yesu aliweka chuki sawa na uaji. (Mt.5:21) Taz. 1 Yoh.3:15.

Hali hiyo hugusa sana uhusiano wetu na Mungu. k.2-5. Tunao uhuru wa ajabu mbele za Mungu kumwomba kile tunachohitaji. Yeye ni Mpaji mkarimu sana (Zab.84:11; Rumi 8:32). Lakini tunapoomba kwa kujifaidi wenyewe tu Yeye hawi tayari kutupa k.3.

Yakobo anatufundisha ya kuwa "urafiki na dunia" ni jambo baya sana. Ameuita "uzinzi". Sisi ni mali ya Mungu, pia sisi ni Bibi Arusi wa Bwana Yesu, maana, Yeye amefanya agano nasi. Tukipenda vitu vya wengine na kuwa tayari kuwafanyia vibaya ili tuvipate, ni wazi kwamba upendo wetu kwa Kristo si upendo wa kweli, tumeisha kuipa dunia na vitu vyake utiifu wetu.

Ushirikiano wetu na Mungu unaharibika k.4. Tumepata amani na Mungu kwa kupatanishwa na Kristo alipokufa Msalabani, (Rum 5:10; Kol.1:10). Tunapojipenda, na tunapowachukia wengine, amani huondoka moyoni, na badala ya kuwa na urafiki na Mungu tumekuwa adui wake.

k.5 Tunavunja moyo wa Mungu, sawa na mtu aliyempenda fulani, halafu akamwacha kwa mwingine. Mungu anatutamani kwa hamu kubwa sana, hata anasikia wivu juu yetu, ule wivu mzuri mfano wa wivu wa mume kwa mkewe. Itakuwa ajabu kwa mtu anayempenda mke wake kama hatasikia wivu akiona mwingine ameingia kati yao. Mungu hutaka tumpende kwa mioyo yetu yote na kuwa mwaminifu kwake wakati wote. Anaumizwa tunapokosa kumrudishia upendo. (Taz. Kut. 20:5; 34:14; Kum.4:24; 5:29; 6:15. Eze39:25; Yoe. 2:18; Zek.1:14; 2:8).

Mawazo ya utangulizi kuhusu 4:6 - 5:6. Yakobo ameendelea kusema juu ya makosa mengine kuhusu urafiki na dunia. Katika kuwaza kwetu tunakosa

kuwa na ufahamu wa kweli, maana tunaporuhusu tamaa ya vitu n.k. twadhani kwamba matimizo ya hizo tamaa ndiyo jambo kubwa la kwanza katika maisha yetu.
Vivyo hivyo twakosa katika kuwaza “vitu” tukidhani ya kuwa viko kwa ajili ya faida yetu tu.

Pia twakosa kutia maanani uhusiano wetu na watu, ikiwa tu tayari kutokuwajali hata kuwafanyia vibaya wakiwa kati yetu na kile kitu tunachotamani.

Zaidi twakosa juu ya uhusiano wetu na Mungu, kwa sababu hali hizo ni kinyume chake na mapenzi yake.

Katika sehemu hiyo Yakobo ametuita tuyaondoe malawama hayo. Katika 4:6- 10 ametuita kutembea pamoja na Mungu, na kwa kufanya hivyo tutasikia raha nafsini mwetu na hamu ya “kutamani vitu” itatulizwa.

Katika 4:11-12 ametushauri juu ya uhusiano wetu na wengine. Yatupasa kunyenyekea na kukataa mazungumzo ya kiburi na dharau ambayo kwayo tunawahukumu wengine.

Katika 4:13-17 Yakobo ametaja haja ya kuwa na nia mpya, tuache kiburi cha kujitegemea kwa kufanya mipango yetu bila kumweka Mungu nafasi ya kutuongoza wakati wa kupanga.

Katika 5:1-6 Yakobo amesema tujihadhari na tamaa ya vitu na mali kwa sababu tunavyoviwaza na kuvishughulikia tunajifunua hali yetu halisi ya kupenda dunia. Sehemu hiyo ya 4:6 - 5:6 imejaa maagizo na wajibu 4:7 “mtiini Mungu”; 4:8 “mkaribieni Mungu”; “itakaseni mioyo”; 4:11 “msisingiziane”; 4:15; “semeni Bwana akipenda tutakuwa hai na kufanya hii na hii”.

Kwa mashauri hayo twajifunza kwamba tu vitani, hakuna utakatifu wa mara moja, na si rahisi tupate ushindi. Ila katika 4:6a tumefunuliwa siri ya ushindi na utakatifu “hutujalia neema iliyozidi”. Tunapojitanguliza badala ya kumruhusu Mungu atangulie katika maisha yetu hatuupoteza wokovu tuliojaliwa kama kipawa. Mungu huitika kwa kuzidi kutujalia neema, Yeye hakubali kushindwa na hali zetu. Kwa hiyo iwapo kwa mkazo wa utendaji tungedhani Yakobo anafundisha kwamba twaweza kujitengeneza, lakini sivyo ilivyo, yeye amefahamu kwamba neema ya Mungu inahitajika, na neema hiyo haina mwisho, uvumilivu wa Mungu hauna kikomo, wala Mungu hachoki. Daima neema yake huwahi mahitaji yetu.

Turudia hayo malawama ya sehemu hiyo na kuyachunguza zaidi:

4:6b-10 Kumkaribia Mungu kwa unyenyekevu

Tusiwe na kiburi mbele zake Mungu. Neema ni kipawa chake kwa wanyenyekevu. Unyenyekevu ni tabia ambayo Mungu hupendezwa nayo na mwenye tabia hiyo atakwezwa na Mungu. Kiburi ni kinyume chake, naye anakichukia, na mwenye kiburi atashushwa.

k.7 Ni wajibu wetu kumtii Mungu kwa nia ya ndani na kwa matendo ya nje, ndipo itajulikana kwamba tu watu wake wa kweli. Tunampomtii Mungu tunampinga Shetani, ni njia maalum ya kumpinga na kumfukuza katika maisha yetu.

k.8 “mkaribieni Mungu naye atawakaribia ninyi” Ni wajibu wetu kumkaribia Mungu na kutafuta kushirikiana naye. Ni kama amri na ahadi zimefungamanishwa, ila ni amri inayotangulia. Tunamkaribia Mungu kwa njia gani: hasa katika maombi na utulivu; katika kusoma Biblia; katika ibada; pia katika kupenda kuzungumza habari zake na wengine n.k.
k.8b. Tukitaka kumkaribia Mungu twapaswa kuuondoa uchafu wa maisha yetu na wa nia zetu za ndani. Katika sura ya kwanza na k.7 alitaja habari ya kuwa na nia mbili, kutokulenga jambo moja. Hata Bwana Yesu alisema juu ya hali hiyo katika Mathayo 6:24 Yakobo ameagiza “takaseni mikono yenu, yaani matendo yenu, na kuisafisha mioyo yenu, enye wenye nia mbili”. Hakutaja Roho Mtakatifu, aliandika kama ni kazi ya muumini mwenyewe kuondoa mabaya katika maisha yake na kuingiza Neno la Mungu; ling. na 1:21.

Yakobo alisema kwa uzito, aliona kwamba Wakristo wasiotenda kufuatana na imani yao wanahitaji kutubu kwa kweli, kujidhili mbele za Mungu kwa huzuni na kuombeleza na kulia.

4:11-12 Onyo juu ya kusingiziana

Tusisingiziane, kwa sababu ipo hatari ya kuwahukumu wengine ambayo ni kazi ya Mungu peke yake. Tusitie mashaka juu ya tabia au nia ya mtu mwingine. Tena hata ikiwa kuna kweli ndani yake, siyo kusema tuna ruksa ya kusema juu yake, potelea mbali. Ni vigumu kusemea jambo fulani lisilo zuri bila dharau, na hivyo, twaingia hatari ya kujikuza na kumshusha mwingine kwa kuupunguza uzuri wake.

Tukumbuke kwamba akiwa Mkristo ni mwenzetu, ni ndugu, ni sawa na sisi, ni mrithi wa wokovu mmoja ambaye ametakaswa na damu ya Kristo kama sisi. Hakuna aliyeokolewa kutokana na kustahili kwake ila kwa Kupenda Kwake Mungu Mwenyewe. Sote tu wenye dhambi ambao kwa uwezo wetu wenyewe hatukuweza kujiokoa.

Ikiwa yule mtu ni jirani yetu tunawajibika kumtunza na kumhudumia ki- uchungaji. Akianguka ni juu yetu kumwinua badala ya kumhukumu.

Yakobo amefundisha kwamba yule anayemsingizia Mkristo mwenzake anakosa juu ya sheria. Sheria ipi? huenda Yakobo alikuwa akiwaza Sheria ya Ki-falme, (2:8) sheria ya kupenda jirani kama mwenyewe.

Kwa masingizio mtu huivunja sheria; tena huihukumu sheria na kupunguza thamani yake, akihesabu haki yake ya kusema inazidi ile ya sheria. Ameihukumu sheria badala ya kuifanya na hivyo ameasi mamlaka ya sheria.

Kwa nini Yakobo amesema juu ya Sheria. Ni kwa sababu Sheria ilitolewa na Mungu, ni ufunuo wa tabia zake. Ni kama tabia zake zimewekwa katika hali ya sheria, na kuwa maagizo kwa wanadamu. Msingi wa hukumu ni sheria zake. Yeye Mungu ni Mmoja na sheria mbalimbali zina umoja. Kwa hiyo tunapoasi au kutokujali sheria ni sawa na kumwasi au kutokumjali Mungu. Kwa hiyo, uhusiano wetu na wengine ni kioo kinachoonyesha uhusiano wetu na Mungu pia. Tukiwa na shida na wengine, ni dalili ya kuwa ipo shida kati yetu na Mungu pia. Mwenye uwezo wa kuokoa au kuangamiza ni Mungu k.12. Yeye alitoa sheria, na ni Yeye atakayehukumu, kwa hiyo, si kazi yetu kumhukumu mtu mwingine. Yakobo alimaliza sehemu hiyo kwa kuuliza swali kali “u nani wewe?” Jibu la Mkristo ni “mimi ni mwenye dhambi asiyestahili mbele za Mungu; nimepata kibali cha Mungu kwa sababu Kristo alikufa kwa ajili yangu”. Kama ni hivyo nitawezaje kumgeukia mwingine na kumhukumu?

4:13-17 Onyo juu ya kupanga maisha yetu bila kumjali Mungu

Hali ya kujidhania na kujitegemea kwa upande wa kupanga maisha yetu ni kosa. Neno hilo lahusu “leo” na “kesho” na “mwaka ujao”. Ni lile dhana la kufikiri kwamba nitakuwa hai na nitakuwa na uwezo wa kufanya ninavyotaka kama “bwana” wa maisha yangu.

Ni dhana la kuamini kwamba nikikata shauri la kufanya jambo fulani hakika litafanyika. Ni dhana la kufikiri mashauri ninayokata na yale ninayokusudia, kwa mfano, kufanya biashara na kupata faida n.k. yatatokea. Hayo yote ni kama kawaida ya wanadamu, jinsi wanavyoishi, ila mbele za Mungu hali hiyo imejaa kiburi. Ni kuishi kama tunayo haki ya kuwa hai, na kukata mashauri, na kuwa na uwezo wa kufaulu.

Yakobo amepinga wazo la kudhania kwamba maisha ya mtu ni yake tu. Ni nini itakayotusaidia kuzipinga hali hizo?

Katika k.14 ametaja “kutokujua kwetu”. Katika ujinga mtu hupanga mambo kwa mwaka kesho, huku hajui la kesho!!! Katika udhaifu wetu wa kibinadamu, sisi hatujui kwa hakika mambo yatakayotokea katika dakika mbili mbele licha ya siku mbili, au miaka miwili. Twakumbuka mfano wa Bwana Yesu kuhusu tajiri mjinga (Lk. 12:16-21).

Halafu Yakobo amefananisha udhaifu wa maisha yetu kwa maneno “ninyi ni mvuke” k.14; kama mvuke sisi sio wa kudumu, sisi hatuwezi kustahimili upepo mkali, na tunapotoweka duniani, hatuonekani tena hapo duniani.

Yakobo hakufundisha kwamba ni vibaya kupanga mambo, la hata kidogo. Ila alikaza ya kwamba tuna haja ya kumtanguliza Mungu na kujua kwamba uwezekano wote hutoka Kwake. Uhai wetu umo mkononi mwake, nguvu za mwili na nguvu za akili, pamoja na matukio mbalimbali katika mazingira yetu humtegemea Mungu. Kwa hiyo iliyopo ni sisi kusema “Bwana akipenda, tutakuwa hai na kufanya hivi na hivi”. Ni vizuri kutazama mbele na kuwa na mipango na malengo yetu, hali tunamruhusu Mungu kuwa kati yake na kuutegemea uongozi wake.
k.15 Hatuna hakika juu ya kuwapo kwetu “kesho”. “Wakati” ni kitu kinachoendelea, mfano wa mstari ulio na mwanzo na mwisho. “Wakati” si duara isiyo na mwanzo wala mwisho. Tuna haja ya kuwaza “mwisho wa mambo yote” na kuandaa tayari kwa mwisho huo.

k.16 Mungu anahesabu hali ya kupanga mambo bila kumjali ni kujisifu na kujivuna; ni jambo baya machoni mwake, naye analichukia.

k.17 Ni juu yetu kufanya mema, na wote wasiofanya mema hali wanafahamu ni wajibu yao wamefanya dhambi. Kwa hiyo ipo dhambi ya “kutokutenda” na “kutokukumbuka” hata Bwana Yesu alisema hivyo katika Mfano alioutoa kuhusu Hukumu ya mwisho (Mt. 25:31ku).

MASWALI

1. *Kwa nini Yakobo amesema tamaa ya vitu na hali ya kupenda dunia ni “uzinzi”?*
2. *Hali hiyo inagusaje uhusiano wetu na watu?*
3. *Hali hiyo inagusaje uhusiano wetu na Mungu?*
4. *Mungu anasikiaje tunapopenda vitu na dunia kuliko Yeye?*
5. *Yakobo ametoa mashauri mbalimbali 4:6-10: taja mashauri yake?*
6. *Kuna hatari gani katika kusengenya?*
7. *Kwa nini ni vizuri kusema (kama WaAfrika wengi husema) “Bwana akipenda”. Tukisema maneno hayo kwa kweli, tunakiri nini juu ya maisha yetu? juu ya uwezo wetu? na juu ya Mungu?*

5:1-6 Onyo juu ya choyo na udhalimu

Katika sehemu hiyo Yakobo ametoa maonyo juu ya udhalimu wa wenye mali. Ni neno kwa matajiri k.l wanaojaribiwa sana kwa upande wa mali; ila tusifikiri ni neno kwao tu. Tabia ya choyo haimo katika matajiri na wenye mali tu. Sote twavuta kutamani hata ikiwa hatuna mali.

Choyo huonekana katika hali mbalimbali. Kwanza katika “kujiwekea akiba”. Lugha ya “kuoza” na “kuliwa na nondo” na “kutu” yahusu vitu vilivyowekwa kwa “akiba” Chakula kisichotumiwa kwa wakati wake; nguo zisizovaliwa kwa muda; fedha zisizotumiwa n.k. Lakini swali linazuka “kwa nini watu hujiwekea akiba, kwa nini hawatumii vitu vyao?”. Yakobo ametaja “siku za mwisho” Je! alikuwa na maana kwamba anayejiwekea akiba amepoa katika tumaini la Kurudi kwa Bwana Yesu? Amesahau ni wajibu wake kuvitumia vitu vyake kwa kuueneza Ufalme wake, tukikumbuka mfano wa Bwana Yesu juu ya kutumia talanta tulizopewa; (Mt. 25:25; Lk. 19:20). Hata sasa tumo katika siku za mwisho, hizo zilianza Yesu Alipokuja kwa mara ya Kwanza na zitakwisha Atakaporudi kwa mara ya pili.

Katika sehemu hiyo Yakobo ametaja kitu kingine kuhusu choyo. Mwenye choyo hujaribiwa kuwadhalimu watu, kupunja ndugu yake kwa sababu ya tamaa ya fedha na mali. Mara nyingi matajiri wamedhulumu watu, si kwa kuiba bali kwa kuwalipa mishahara midogo, kuwa wanyimavu kwao, kutokuwa na huruma kwa hali za wafanya kazi wao. Yakobo alisema kwa ukali kwamba, vilio vya walimaji na wavunaji vimeingia masikioni mwa Bwana wa Majeshi. Udhalimu na choyo vimepiga kelele, na Bwana atawahukumu wahusika. Kwa kumpunja mtu na kumdhulumu mtu twafanya kinyume cha ukiri wetu wa Kikristo wa kuwa wafuasi wa Mungu, Baba yetu aliye mkarimu mno. Tumekuwa “wana” tusiofanana na Baba yetu.

Halafu Yakobo aliendelea kwa kutaja dalili nyingine ya choyo, ambayo ni “kujifurahisha katika anasa”. Ni kuuthamini utajiri kuwa kitu cha kuutumia kwa raha yake tu. Yakobo alitumia lugha ya ajabu, amefananisha watu wa namna hiyo kama wanyama walionenepa tayari kwa siku ya machinjo. Siku ya machinjo ni siku ya Hukumu ya Bwana Yesu. Ni afadhali kuwa mnyama aliyekonda katika siku hiyo!!! Ikiwa tumetumia vitu na mali yetu kwa kujifurahisha tu, na kwa faida yetu tu na hasa ikiwa tumewadhulumu wengine katika kupata hiyo mali, basi itakuwa vigumu sana kwa Bwana Yesu kutukaribisha kwenye makao yake ya milele. Twakumbuka ya kuwa Yeye, mwenye mali zote alikubali kuwa maskini kwa ajili yetu ili sisi tuwe matajiri katika mambo ya kiroho (2 Kor.8:9).

Mwishowe Yakobo alionyesha ya kuwa mwenye choyo ni mtu aliye na nia mbili. Katika k.6 ametaja habari za kumwua mwenye haki na mwenye haki hashindani naye. Hapo twakumbushwa kielelezo cha Bwana Yesu aliyeuzwa na Yuda Iskariote, mmojawapo wa Mitume wake (Yn. 12:5-6). Ni kama kuchagua kati ya Yesu na fedha. Tukichagua fedha twaachana na Yesu. Hata Yesu alisema wazi “hamwezi kutumikia mabwana wawili, Mungu na mali”. Kiini cha kupenda dunia ni kujipenda mwenyewe.

5:7-12 Haja ya Kuvumilia

Yakobo alitaka waumini waishi katika mwanga wa Kuja Kwake Bwana Yesu mara ya pili. Hivyo, wahitaji kuvumilia, mfano wa mkulima ambaye baada ya kupanda mbegu zake hungojea mvua na kusubiri mpaka mimea imekua na kukomaa, ndipo ataweza kuvuna. Mwanzoni wa Waraka Yakobo alitufundisha kwamba tutakutana na matatizo na shida, na Mungu atazitumia ili imani yetu ipate kukuzwa na kutimilika kwa kuvumilia magumu tunayoyakuta katika maisha yetu. Lazima tuikaze mioyo yetu kwa Mungu, tusiwe na nia mbili, wala tusisitesite katika imani yetu. Tujiandae maisha kwa kukutana na Bwana wetu. Halafu Yakobo ataja habari za kunung'unikiana kuwa kitu kisichotupasa. Tumeona kwamba Yakobo ametaja sana shida za ulimi, na kosa moja la ulimi ni kunung'unika, dalili ya mawazo mabaya moyoni. Manung'uniko hupoza uhusiano mzuri kati ya watu, ni kama kumwagalia mtu maji baridi, tena Wakristo wengi hawajatambua ni jambo lisilo zuri.

k.10-12 Yakobo ametukumbusha kielelezo cha manabii waliovumilia mateso makali. Wameitwa heri. Mfano mmoja ni Ayubu; na ni vema tujue ya kuwa mwisho wao walirehemiwa na Bwana. Twaitwa kukifuata kielelezo chao na kutiwa moyo ili sisi nasi tuvumilie mpaka mwisho. Mungu hujifunua kwa watumishi wavumilivu, kama alivyofanya kwa Ayubu ambaye alishuhudia kwamba alipata kumjua Mungu zaidi sana (Ayu.42:5).

Tunahitaji kuangalia maneno yetu, hatuna haja ya kutumia kiapo, neno la kweli latosha peke yake bila nyongeza ya maneno kama “haki ya Bwana” n.k. Mkristo atamani sana kusema iliyo kweli, ajulikane kama mtu wa kweli, ili akisema “ndiyo” itakubalika ni “ndiyo” na akisema “siyo” ikubalike ni “siyo” Mapambo ya maneno mengi hayatakiwi. Kwa kuangalia maneno yetu tutaepa hukumu ya Mungu.

5:13-18 Uwezo wa Maombi mbalimbali

Yakobo ameeleza habari za maombi mbalimbali; maombi ya mtu binafsi; maombi ya wazee; maombi kwa wakati mbalimbali.

k.13 Mtu afanye nini anapopatikana na mabaya - aombe, kwa kusudi la kusimama imara na kujua njia ya kupita katika mabaya yaliyompata.

Mtu afanye nini anapokuwa na furaha? basi aimbe zaburi ya kumsifu Mungu.

Hivyo, kwa hali zote za maisha yake apate faida ya kiroho. Kwa kuomba wakati wa shida ataepa jaribu la kumnung'unikia Mungu. Kwa kuimba zaburi wakati ambapo mambo yanakwenda vizuri mtu katika raha yake ataepa mtego wa kulegea na kumsahau Mungu. Kila hali ina itikio lake litakalomfurahisha Mungu, ama ni kuomba ama ni kuimba. Twajifunza kumkimbilia Mungu katika hali

yoyote tuliyo nayo, maana Yeye ndiye Mwenye msaada kwa kila hali, na tunapokea yote kama ni mapenzi yake.

Je! nifanye nini ninapougua au wakati Mkristo mwenzetu anapokuwa hawezi. Shauri la Yakobo ni kwamba jambo hilo lahusu jamii ya waumini.

Mgonjwa mwenyewe awaite wazee, na wazee baada ya kuitwa, wamwombee na kumpaka mafuta katika Jina La Bwana. Kwa hiyo, katika mawazo ya Yakobo, iwepo huduma kwa wagonjwa katika makanisa, na huduma hiyo imo mikononi mwa wazee. Haionekani kuwa huduma ya mtu mmoja wa ki-pekee. Tena inaonekana kuwa huduma ya kanisa la palepale. Kwa kusema mgonjwa awaite wazee, huenda mkazo ni kwa mgonjwa kusikia anataka huduma hiyo. Ni kama huduma iwepo kwa wale wanaosikia kuitumia. Zaidi ya uponyaji wa mwili mtu atapata baraka ya kiroho, atasamehewa dhambi zake ikiwa amefanya dhambi. Pengine maana yake ni kwamba anapolala kitandani hali anaumwa atatambua ugonjwa wake umetokana na dhambi fulani; au anapojihoji atakumbuka dhambi fulani iliyotendeka hapo nyuma, ambayo alikuwa ameisahau, iwapo haikusababisha ugonjwa wake, ndipo ataitubu. Wazo lingine ni kwamba anapotulia na kutafakari maisha yake anatambua hawezi kuwa mzima asipopatanishwa na Mungu wake. Tunafahamu kwamba katika mtindo wa kuwaza kwao Wayahudi walizoea kuunganisha jambo la kuugua na dhambi. Sehemu hiyo inatukumbusha jinsi Yesu alivyomhudumia mgonjwa wa kupooza (Mt.9:2).

Kupakwa mafuta katika Jina la Bwana kutakuwa ishara kwa mgonjwa ya kuwa Roho Mtakatifu, Mpaji wa Uzima anafanya kazi kwa njia ya huduma hiyo. Ilitegemewa mgonjwa ataponywa. Kwa kulitumia Jina la Bwana ni ukiri kwamba ni Bwana tu, peke yake, awezaye kumponya. Kazi ya wazee ni kumwombea, na hasa katika habari hiyo mkazo ni kwamba ni huduma ya kuomba kuliko huduma ya uponyaji. Ni maombi ya imani itakayomwokoa (Ling. na Mt.18:19; 21:22; Yn.14:13). Imani ni kujiweka tayarl kwa mapenzi ya Mungu kutendeka na matokeo yahesabiwa hivyo.

k.16: Kwa upande wa uponyaji wa dhambi, Wakristo huwajibika kushirikiana na kusaidiana ili washinde dhambi zao. Ni jambo kubwa kumfunulia mwingine dhambi au udhaifu fulani tulio nao, na vilevile ni jambo zito kwa yule anayeshirikishwa. Kwa njia hiyo msaada utapatikana, maana itakuwa dhahiri kwamba, ndugu fulani kwa kweli anataka kushinda dhambi yake. Katika habari hiyo jambo la kuombeana ni la maana sana, isije mtu ashikwe na utafiti tu. Lengo ni “mpate kuponywa”.

k:16b-18: Maombi yana nguvu sana na husababisha matokeo makubwa. Maombi hufanya kazi, na ndiyo sababu Yakobo amesema “yafaa sana”, kuna nguvu ya utekelezaji ndani yake. Yakobo ametaja kuomba kwake mwenye haki, pia kuomba kwa bidii. Maombi ambayo Mungu husikiliza ni maombi ya

mtu wa Mungu, ambayo amekaza moyo wake kwa Mungu, na nia yake ni kumpendeza Mungu. Si kwamba hana dhambi, la! (k.17) ila huyo mtu ana nia ya kufanya mapenzi ya Mungu.

Yakobo ameleta mbele yetu kielelezo cha Nabii Eliya, ambaye ameelezwa kuwa “mwanadamu mwenye tabia moja na sisi” maana yake hakuwa mtu wa ajabu, ila alifanana na sisi. Hata hivyo aliomba jambo la ajabu, mvua isinywe kwa muda wa miaka mitatu na miezi sita; halafu baada ya muda huo, aliomba ili mvua irudi, ikarudi. Mungu alijiunga na maombi ya Eliya, maana ni Mungu peke yake awezaye kuleta au kuzuia mvua. Katika kuomba Mungu na mwanadamu hukutana!! Aliomba kwa bidii, maana yake alijitoa kwa kuomba, alitegemea njia hiyo tu, hakutumia mbinu zingine. Tena shabaha ya kuomba kwake ilikuwa kwamba watu watambue Kuwepo Kwake Mungu na makosa yao ya kumwasi.

5:19-20 Kumrejeza ndugu aliyepotea

Yakobo amefunga Waraka wake kwa kuendelea na jambo la kusaidiana kimaisha. Hasa amegusa habari ya ndugu fulani ambaye amerudi nyuma katika maisha yake ya Kikristo. Je! tumwache katika kosa lake; au vipi? Yakobo ameshauri kwamba tujitahidi kumrejeza, maana ni neno muhimu sana. Tukifaulu roho ya yule mtu itaokolewa na mauti ya milele, pia dhambi zake zitafunikwa, naye atatoka katika njia ya kupotea. Yakobo hakusema kwamba kazi hiyo ni ya wachungaji au wazee, ni kazi ya muumini yeyote aliye na mzigo juu ya mwenzake.

Mara nyingi katika Waraka huo tumekumbushwa maneno na matendo ya Bwana Yesu Mwenyewe, ni kama Yakobo alikuwa amekolea sana sana habari za Yesu na kuziweka kuwa msingi wa maisha na mafundisho yake.

Sidhani kuna Waraka mwingine uliojaa mwongozo wa jinsi ya kuishi maisha ya Kikristo kuliko Waraka huo. Ni msaada mkubwa kwa upande wa kutenda kwetu, na umegusa maeneo mengi katika maisha yetu.

Waraka ulikoma kwa ghafula. Yakobo hakutoa salaam za kuagana na wasomaji wake. Alitaka ubaki mawazoni mwao wajibu wao wa kushirikiana na kusaidiana na kuombeana.

MASWALI

1. *Kutokana na choyo mtu humfanyia nini mwenzake?*
2. *Yakobo ametaja mambo kadha yaliyo dalili za choyo. Eleza mambo hayo.*
3. *Bwana Yesu alisema nini juu ya mali?*
4. *Kwa nini tunahitaji uvumilivu katika maisha yetu?*
5. *Taja aina mbalimbali za maombi. Kwa nini maombi yana nguvu na kusababisha matokeo makubwa? Ni tabia na hali zipi ambazo zinamfanya Mungu ajibu maombi ya mtu?*

KWA JUMLA

Waraka huu wa Yakobo umekusaidiaje?